# KOZI YA UINJILISTI YA WANAFUNZI WA YESU

Masomo - 48

TOLEO LILILOFUPISHWA
NA KITABU CHA KAZI

na Don W. Krow
Pamoja na Andrew Wommack

Copyright © 2016 Andrew Wommack
Ruhusa imetolewa kutoa nakala au kuchapisha kwa ajili ya madhumuni ya kufundisha wanafunzi wa Yesu katika sharti kuwa kitasambazwa bure bila gharama.

Andrew Wommack Ministries
P.O. Box 3333
Colorado Springs, CO 80934-3333
www.awmi.net

Mpaka iwe imeonyeshwa, nukuu zote za maandiko zimechukuliwa kutoka kwenye tafsiri ya Biblia ya King James.

Jina la Kwanza la Kitabu: Kozi ya Uinjilisti ya Uanafunzi wa Yesu Masomo - 48
© 2016
Andrew Wommack Ministries – Europe
PO Box 4392, Walsall, WS1 9AR, England
www.awme.net

ISBN: 978-1-910984-20-8
Item Code: SW417

Jina la Kwanza la Kitabu: Kozi ya Uinjilisti ya Uanafunzi wa Yesu Masomo - 48

# YALIYOMO

## DARAJA 1


| | | |
|---|---|---|
| 1 | UZIMA WA MILELE | 3 |
| 2 | WOKOVU KWA NEEMA | 8 |
| 3 | HAKI KWA NEEMA | 15 |
| 4 | MAHUSIANO NA MUNGU | 19 |
| 5 | ASILI YA MUNGU | 25 |
| 6 | TOBA | 31 |
| 7 | KUJITOA | 39 |
| 8 | UBATIZO WA MAJI | 45 |
| 9 | UTAMBULISHO KATIKA KRISTO (Sehemu 1) | 50 |
| 10 | UTAMBULISHO KATIKA KRISTO (Sehemu 2) | 56 |
| 11 | NINI KINACHOTOKEA PALE MKRISTO ANAPOTENDA DHAMBI? | 61 |
| 12 | UAMINIFU WA NENO LA MUNGU | 65 |
| 13 | MUNGU HANA HATIA | 71 |
| 14 | NGUVU YA MAISHA YALIYOJAZWA NA ROHO | 76 |
| 15 | JINSI YA KUMPOKEA ROHO MTAKATIFU | 81 |
| 16 | FAIDA ZA KUNENA KWA LUGHA | 87 |


## DARAJA 2


| | | |
|---|---|---|
| 1 | UBINAFSI: The Source of All Grief | 95 |
| 2 | JINSI YA KULITAFAKARI NENO LA MUNGU | 101 |
| 3 | KUFANYA UPYA NIA | 105 |
| 4 | UMUHIMU WA KANISA LA KRISTO | 111 |
| 5 | UKOMBOZI | 119 |
| 6 | MAMLAKA YA MUUMINI | 125 |
| 7 | UPONYAJI KATIKA MSAMAHA | 132 |
| 8 | VIZUIZI VYA UPONYAJI | 139 |
| 9 | KUSAMEHE WENGINE | 146 |
| 10 | NDOA (Sehemu 1) | 153 |
| 11 | NDOA (Sehemu 2) | 159 |
| 12 | AINA YA UPENDO WA MUNGU (Sehemu 1) | 167 |
| 13 | AINA YA UPENDO WA MUNGU (Sehemu 2) | 174 |
| 14 | FEDHA (Sehemu 1) | 180 |
| 15 | FEDHA (Sehemu 2) | 186 |
| 16 | NINI CHA KUFANYA INAPOONEKANA MAOMBI YAKO HAYA JAJIBIWA | 191 |


## DARAJA 3


| | | |
|---|---|---|
| 1 | MTIRIRIKO WA KIUNGU | 199 |
| 2 | KUTUMIA KARAMA KUHUDUMU | 205 |
| 3 | MIUJIZA HUMTUKUZA MUNGU | 214 |
| 4 | NGUVU YA MAHUSIANO YA KIMUNGU | 222 |
| 5 | MATESO | 227 |
| 6 | MFALME NA UFALME WAKE | 233 |
| 7 | KITU CHA MSINGI CHA IMANI IOKOAYO | 243 |
| 8 | MATUMIZI SAHIHI YA SHERIA YA MUNGU | 247 |
| 9 | SI CHINI YA SHERIA, BALI CHINI YA NEEMA | 254 |
| 10 | HAKUNA TENA HATIA YA DHAMBI | 261 |
| 11 | MIMI NAPENDWA, MIMI NI MZURI | 269 |
| 12 | TUNDA LA WOKOVU (Sehemu 1) | 275 |
| 13 | TUNDA LA WOKOVU (Sehemu 2) | 281 |
| 14 | WITO WA KUWA MFUASI WA YESU | 287 |
| 15 | JINSI YA KUTUMIA USHUHUDA WAKO | 295 |
| 16 | KUTUMIA KARAMA ZA KILA MTU ILI KUFANYA WANAFUNZI | 303 |

# KOZI YA UINJILISTI YA UANAFUNZI WA YESU

# DARAJA 1

Ruhusa imetolewa kutoa nakala au kuchapisha kwa ajili ya madhumuni ya kufundisha wanafunzi wa Yesu katika sharti kuwa kitasambazwa bure bila gharama.

DARAJA 1

# SOMO 1
# UZIMA WA MILELE

*Na Andrew Wommack*

Moja ya kifungu cha maandiko kinachofahamika sana ni Yohana 3:16. Inaonekana ya kuwa kila mtu anaufahamu mstari huo toka akiwa na umri mdogo, Lakini bado ninaamini umekuwa haueleweki na umetumika vibaya. Yohana 3:16 inasema, *"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kwamba kila amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele."*

Kidesturi, andiko hili limekuwa likitumika kufundisha ya kuwa Yesu alikuja na akafa kwa ajili ya dhambi zetu ili kwamba tusiangamie. Kama hili lilivyo kweli, mstari huu unasema ya kuwa madhumuni halisi ya Yesu kuja hapa ulimwenguni na kufa kwa ajili yetu ilikuwa ili tuwe na uzima wa milele. Ilitokea tu kuwa dhambi zetu zilikuw ani kizuizi ambacho kilisimama kati yetu na uzima huu wa milele.

Ni kweli ya kuwa Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, Na ni kweli kuwa ikiwa kama tutamwamini Yesu, hatutaangamia, lakini kuna ya zaidi kwenye Injili kuliko hayo. Ujumbe halisi wa Injili ni ya kuwa Mungu anataka kukupa uzima wa milele. Sasa acha nielezee hilo.

Usiku kabla ya kusulubiwa kwake, Yesu alikuwa akiomba, Na Akasema hivi, *"Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo Uliyemtuma"* (Yohana 17:3).

Hii inasema ya kuwa uzima wa milele ni kumjua Baba, Mungu wa pekee wa kweli, na kumjua Yesu Kristo, aliyemtuma. Hivyo ndivyo uzima wa milele ulivyo. Watu wengi wanafikiria ya kuwa uzima wa milele ni kuishi. Vyema, kil amtu anaishi milele. Ni uelewa mbaya kufikiria kuwa mtu anapokufa haendelei kuwepo. Roho na nafsi vinarudi kwa Mungu. Mwili unaoza kaburini. Ukweli ni kuwa, kila mtu ambaye ameshawahi kuishi kwenye uso wa dunia ataendelea kuishi katika hali ya roho. HIvyo kusema kuwa uzima wa milele ni kuishi milele siyo kweli yote – kila mtu anaishi milele. Mstari huu unaweka wazi kabisa ya kuwa uzima wa milele hapewi kila mtu.

Baadhi ya watu wangesema, *"Uzima wa milele ni kuishi milele mbinguni dhidi ya kuishi milele kuzimu."* Lakini uzima wa milele ni kile ambacho Yesu alisema katika Yohana 17:3 – kumjua Mungu na Yesu Kristo. Ni zaidi ya maarifa ya kiakili. Neno hili *"kujua"* linatumika kote katika maandiko kuelezea, uhusiano binafsi na wa ndani zaidi ambao unaweza kuwa nao.

Madhumuni halisi ya wokovu si kuishi milele mbinguni, kama ambavyo hilo litakuw a ni jambo kuu. Madhumuni halisi ya wokovu ni kuwa na uhusiano binafsi na wa ndani pamoja na Bwana Mungu. Kuna watu wengi ambao wamemlilia Mungu kwa ajili ya msamaha wa dhambi zao lakini hawajawahi kuwa na uhusiano wa ndani na Mungu kama ndiyo lengo lao.

Kwa kutokuelezea madhumuni halisi ya wokovu, hatuitendei haki Injili. Tunapowasilisha wokovu kama kitu ambacho kinashughulika tu na mambo ya kiroho ambayo yatatufaidisha tu katika siku zijazo, katika umilele, hatuwasaidii watu. Kuna baadhi ya watu ambao wanaishi katika kuzimu hiyo kwa sasa hapa duniani. Wengi wameshushwa moyo, wanaishi katika umasikini, wakipambana na migongano, kukataliwa, maumivu, ndoa zilizosh indwa. Watu wanajaribu tu kuishi siku hat asiku. Wanajaribu tu kuweka vichwa vyao juu ya maji. Kwa kuufanya wokovu kitu ambacho kinashughulika tu na maisha yajayo, Watu wengi hukataa kufanya uamuzi huo kwa sababu wanashughuli nyingi sana wakijaribu tu kuishi leo.

Ukweli ni kuwa sit u Yesu alikuja kuleta matokeo kwenye mustakabali wa uzima wetu ili kwamba tuweze kuishi milele mbinguni katika Baraka badala ya adhabu na laana ya kuzimu, lakini Yesu pia alikuja kutuokoa na dunia hii mbovu iliyoko sasa (Wagal. 1:4). Yesu alikuja kukupa urafiki wa karibu sana na uhusiano binafsi pamoja na Mungu baba leo.

Yesu alikuja kukurejesha kwenye uhusiano wa karibu, na wa binafsi pamoja Naye. Yesu anakupenda. Yesu anataka kukujua wewe binafsi. Yesu anataka kukupa ubora wa miasha ambao ni mkubwa kuliko chochote ambacho ungeweza kukipata kupitia chanzo kingine chochote..

Yesu aliiweka hivi katika Yohana 10:10: *"Mwivi* [akimzungumzia Shetani] *haji ila, aibe, na kuchinja na kuharibu: Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele"*. Mungu anataka kukupa uzima wa milele. Mungu anataka kukupa uzima tele, name naamini ya kuwa unauhitaji leo – ya kuwa unauhitaji. Kristo alikufa si tu ili akusamehe dhambi zako, bali akulete karibu naye. Ikiwa kama humjui Bwana, unhitaji Kumjua kwa madhumuni hayo. Ikiwa kama umeshaokoka, unahitaji kwenda zaidi tu ya kusamehewa dhambi zako na uingie kwenye uzima wa milele pamoja na Baba.

# UKWELI KUHUSU UZIMA WA MILELE

A. Madhumuni ya Injili ni uzima wa milele. (Yohana 3:16).

B. Uzima wa milele ni kumjua Mungu. (Yohana 17:3).

C. Kumjua Mungu ni uhusiano wa ndani. (1 Wakor. 6:16-17).

D. Uzima wa milele unapatikana sasa. (1 Yohana 5:12).

E. Mungu anataka uhusiano binafsi pamoja na wewe. (Ufu. 3:20).

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Yohana 3:16. Madhumuniya Mungu kumtuma Yesu ulimwenguni yalikuwa yapi? ______________________________
______________________________

2. Matumizi ya kibiblia ya neno "kumjua" ina maanisha kuwa na uhusiano wa ndani na binafsi na mtu (Mwa. 4:1). Soma Yohana 17:3. Uzima wa Milele ni nini, kufuatana na mstari huu? ______________________________
______________________________

3. Soma 1 Yohana 5:11-12. Kufuatana na mistari hii, Ni wakati gani uzima wa milele unaanza? ______________________________
______________________________

4. Soma Yohana 10:10. Ni aina gani ya uzima ambao Yesu alikuja kutupa? _
______________________________
______________________________

5. Elezea kwa maneno yako mwenyewe sifa au tabia za uzima wa milele.
______________________________
______________________________

6. Je unaamini ya kuwa Mungu alimtuma Mwanawe Yesu ulimwenguni ili afe kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, ili atupe sisi ambao tunaamini katika uzima wa milele?
______________________________

7. Je inaeleweka kwako ya kuwa uzima wa milele sit u urefu wa muda (umilele) bali ubora na utele wa uzima? ______________________________
______________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Yohana 3:16

"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."

### Mwanzo 4:1

"Adamu akamjua Hawa mkewe; naye akapata mimba, akamzaa Kaini,na akasema, Nimepata mtoto mwanamume kwa BWANA."

### Yohana 17:3

"Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma."

### 1 Yohana 5:11-12

"[11] Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe. [12] Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima."

### Yohana 10:10

"Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao."

# MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Yohana 3:16. Madhumuniya Mungu kumtuma Yesu ulimwenguni yalikuwa yapi? **Kuuokoa ulimwengu, kuwapa wale wote wanoamini katika Yesu Kristo uzima wa milele kwa kuondoa adhabu ya dhambi.**

2. Matumizi ya kibiblia ya neno "kumjua" ina maanisha kuwa na uhusiano wa ndani na binafsi na mtu (Mwa. 4:1). Soma Yohana 17:3. Uzima wa Milele ni nini, kufuatana na mstari huu? **Uzima wa milele ni kumjua Mungu na Yesu Kristo (si kimwili bali kwa undani na ukaribu zaidi).**

3. Soma 1 Yohana 5:11-12. Kufuatana na mistari hii, Ni wakati gani uzima wa milele unaanza? **Tunapompokea Mwana (Yesu Kristo) maishani mwetu.**

4. Soma Yohana 10:10. Ni aina gani ya uzima ambao Yesu alikuja kutupa? **Uzima tele!**

5. Elezea kwa maneno yako mwenyewe sifa au tabia za uzima wa milele. **Uzima wa tele life itakuwa ni kinyume ya kile alichokisema Yesu kuhusus mwivi alichokuja kukifanya.**

6. Je unaamini ya kuwa Mungu alimtuma Mwanawe Yesu ulimwenguni ili afe kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, ili atupe sisi ambao tunaamini katika uzima wa milele? **Ndiyo.**

7. Je inaeleweka kwako ya kuwa uzima wa milele sit u urefu wa muda (umilele) bali ubora na utele wa uzima? **Ndiyo.**

DARAJA 1

# SOMO LA 2
# WOKOVU KWA NEEMA

*Na Don Krow*

Yesu mara nyingi alitumia mifano, simulizi ambayo ilielezea kweli za kiroho. Luka 18:9-14 inaanza, "Akawaambia mfano huu watu waliojiamini ya kuwa wao ni wenye haki, wakiwadharau wengine." Yesu alikuwa akilenga kundi fulani: wale ambao walijiamini ya kuwa walikuwa ni wenye haki na wakawadharau wengine. Alitoa mfano huu kwa watu hawa ambao waliamini katika mambo waliyoyafanya. Tunaweza kuwaita wanaojihesabia haki, ndicho ambacho Yesu alikuwa akikizungumza pale aliposema wanawadharau watu wengine wote wakisema, "Mimi ni bora kuliko wewe!"

Katika mstari wa 10, Yesu anasema, "Watu wawili walipanda kwenda hekaluni kusali, mmoja Farisayo, wa pili mtoza ushuru." Tunaweza kusema katika lugha ya kisasa ya kuwa walikwenda kanisani kuomba, na moja alikuwa ni Farisayo. Farisayo alikuwa ni mtu wa dini sana. Neno hapa lina maanisha "yeye aliyetengwa", mtu ambaye alikuwa ni wa dini sana kiasi kwamba angesema, "Usininajisi! Usinisogelee karibu". Mimi si kama watu wengine! Mimi ni bora kuliko watu wengine!" Mtu mwengine ambaye Yesu alimtaja alikuwa ni mtoza ushuru. Watu hawa walikuwa ni watoza ushuru na walifahamika kuwa ni watu waovu sana, watu wenye dhambi ambao walidanganya na walikula rushwa. Walikusanya ushuru kwa njia yoyote ile ambayo wangeweza kutumia, walichukua fedha nyingi na kuziweka mifukoni mwao, na kuwapa baadhi ya fedha hizo serikali ya Warumi, hivyo hawakuwa watu waliopendwa na wenzao.

Habari inaendelea katika mstari wa 11, "Yule Farisayo akasimama akiomba hivi moyoni mwake; Ee Mungu, nakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine, wanyang'anyi, wadhalimu, wazinzi, wala kama huyu mtoza ushuru." Ninataka uone ya kuwa. Alikuwa akiomba kwa nani? Ukweli alikuwa akijiomba yeye mwenyewe ingawa alikuwa akisema "Mungu" na akitumia maneno sahihi. Mungu alikuwa hatambui maombi yake, na tutaona baadaye kwa nini hilo lilikuwa hivyo. Angalia ya kuwa aliomba, "Mungu, nina kushukuru kwa kuwa mimi siko kama watu wengine wowote. Si mtenda dhambi. Si mnyanganyi, si mdhalimu, si mzinzi, wala si kama huyu mtoza ushuru." Farisayo huyu, mtu huyu wa dini, alisema, "Mimi si kama watu wengine. Si mtenda dhambi. Si mnyanganyi, si dhalimu, si mzinzi, na si kama mtoza

ushuru huyu ambaye amekuja kuomba." Unaona, aliwadharau wengine kwa kuwa alifikiria ya kuwa alikuwa bora kuliko wao.

Katika mstari wa 12, Farisayo alisema, "Mimi nafunga mara mbili kwa juma; hutoa zaka katika mapato yangu yote." Alikuwa akisema, "Angalia kile nina chokifanya?" Je unajua ina maana gani kufunga? Hasa ina maanisha kukaa bila kula.Alitoa fedha kwa Kanisa. Alikuwa ni moja wa wale watu ambao walisema, "Usinisumbue mimi! Ninaishi maisha mazuri! Ninatoa misaada! Ninatoa fedha kule kanisani!"

Halafu tunakuja kwa watoza ushuru katika mstari wa 13: "Lakini yule mtoza ushuru alisimama mbali, wala hakuthubutu hata kuinua macho yake mbinguni, bali alijipiga-piga kifua akisema, Ee Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhambi." Angalia lugha yake ya mwili: "alisimama mbali". Hakwenda hata mpaka kanisani. Alikuwa ana aibu sana kuhusus maisha yake na mambo ambayo ameyafanya kiasi kuwa akasimama mbali n ahata hakutazama juu, wala kunyanyua macho yake mbinguni, bali alipiga piga kifua chake. Biblia inapozungumza kuhusus kupiga piga kifua katika Agano la Kale, mara nyingi pia walichana mavazi yao,ambayo ilikuwa ni njia ya, "Nisamehe, Mungu, Kwa yale niliyoyafanya!" Ilikuwa ni ishara ya toba, moyo mkunjufu, na roho iliyovunjika, ambayo Mungu asingeidharau. Mtoza ushuru huyu, mtenda dhambi kama alivyokuwa, alimlilia Mungu na kuomba, "Mungu unirehemu, mimi ni mwenye dhambi!"

Mstari wa 14 unasema, "Nawaambia, mtu huyu alishuka kwenda nyumbani kwake amehesabiwa haki kuliko yule mwengine; kwa maana kila ajikwezaye atashushwa, naye ajishushaye atakwezwa." Mtoza ushuru alikwenda nyumbani akiwa amehesabiwa haki, akitangazwa kuwa mwenye haki mbele za Mungu. Kwa nini alisamehewa? Kwa nini alikwenda nyumbani kwake akiwa amesimama vyema mbele za Mungu na siyo mwanadini Mfarisayo? Ilikuwa ni kwa sababu Farisayo alijiinua mwenyewe, akisema "mimi ni bora kuliko watu wengine! Mimi si mtenda dhambi! Mimi si kama watu wengine," Wakati mtoza ushuru alijua kuwa hakuwa amesimama vyema mbele za Mungu, hakuna ambacho angeweza kumpa. Alikuwa ni mtu mwenye dhambi. Biblia inasema Yesu hakuja kuwaokoa wenye haki bali wenye dhambi, na wote tumetenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. Mtoza ushuru huyu alijinyenyekeza na akapata msamaha na huruma.

Tunaongea kuhusu wokovu kwa neema. Neema ni neno la ajabu, na nitakwenda kukupa tafsiri inayokubalika ya hakika neema ina maana gani, lakini neema ina maanisha zaidi sana. Katika lugha ya Kiyunani ambayo imetumika kuandikia Agano Jipya, neema ndiyo neon charis. Tafsiri ya neema inayokubalika ni: upendeleo wa bure wa Mungu kwa watu ambao hawaistahili. Mtoza ushuru huyu hakustahili chochote kutoka kwa Mungu, lakini alipata neema ya Mungu kwa kuwa alijinyenyekeza mwenyewe. Kuna neno jengine kwa Kiyunani, charisma, ambalo ni charis likiwa na neno lililoongezwa mwishoni ma. Ina maanisha udhihirisho mahususi au aina

ya neema ya Mungu, na mtoza ushuru huyu alihesabiwa haki, kusimama sawa sawa, mbele za Mungu kama zawadi.

Warumi 5:17 inasema, "… Wao wapokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo." Mungu anatupa wewe na mimi msimamo sahihi mbele Zake kama kipawa na, kufuatana na kifungu chetu, mtoza ushuru alipata kipawa hicho cha kujihesabia haki, kipawa hicho cha haki ambacho huja tu kupitia Yesu Kristo. Biblia inasema katika kitabu cha Yohana1:17, "Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa; neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo" Neema hii inatolewa tu kwa mtu wa aina moja – wale wanaojinyenyekeza wenyewe na wanojua ya kuwa hawawezi kusimama mbele za Mungu, ambao hulia kwa ajili ya neema ya Mungu. Watu hawa watapata rehema na msamaha wa Mungu.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Luka 18:9. Mfano ni nini? ________
______________________________________

2. Soma Luka 18:9. Ni kwa nani Yesu alielekeza mfano huu? _________________
______________________________________

3. Soma Luka 18:9 (sehemu ya mwisho ya mstari). Watu ambao hujihesabia haki mara zote huonyesha tabia fulani kwa kufuatana na Luka 18:9, tabia hiyo ni ipi?
   - A. Wanapendelea zaidi wengine.
   - B. Wanawadharau wengine au kuwashusha wengine.
   - C. Wanawapenda wengine.

4. Soma Luka 18:10. Watu wawili walikwenda kuomba; katika lugha ya kisasa, walikwenda kuomba wapi? _____________
______________________________________
______________________________________

5. Soma Luka 18:10. Watu hawa walikuwa ni nani? _______________________________
______________________________________

6. Soma Luka 18:11. Moambi ya Farisayo yalikuwaje? _________________________
______________________________________

7. Soma Luka 18:12. Kufunga kuna maana ga ni?__________________________________

8. Soma Luka 18:12. Ina maana gani kutoa fungu la kumi? ________________________
______________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Luka 18:9
"Akawaambia mfano huu watu walioyo weka imani yao ndani yao wenyewe ya kuwa wao ni wenye haki, wakiwadharau wengine wote."

### Luka 18:10
"Watu wawili walipanda kwenda hekaluni kusali, mmoja Farisayo, wa pili mtoza ushuru."

### Luka 18:11
"Yule Farisayo akasimama akiomba hivi moyoni mwake; Ee Mungu, nakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine, wanyang'anyi, wadhalimu, wazinzi, wala kama huyu mtoza ushuru.."

### Luka 18:12
"Mimi nafunga mara mbili kwa juma; hutoa zaka katika mapato yangu yote."

### Luka 18:13
"Lakini yule mtoza ushuru alisimama mbali, wala hakuthubutu hata kuinua macho yake mbinguni, bali alijipiga-piga kifua akisema, Ee Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhamb."

### Luka 18:14
"Nawaambia, huyu alishuka kwenda nyumbani kwake amehesabiwa haki kuliko yule; kwa maana kila ajikwezaye atashushwa, naye ajishushaye atakwezwa."

### Warumi 10:13
"Kwa kuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokoka."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

9. Soma Luka 18:13. Mtoza ushuru alikuwa amesimama wapi? ___________________ Kwa nii? _____________________________
_____________________________________

10. Soma Luka 18:13. Ni kwa nini mtoza ushuru aliinamisha kichwa chake na hakuangalia juu? _____________________
_____________________________________
_____________________________________

11. Soma Luka 18:13. Maombi ya mtoza ushuru huyu yalikuwaje? _______________
_____________________________________

12. Soma Luka 18:14. Yupi katika watu hawa alitangazwa kuwa mwenye haki mbele za Mungu alipokwenda nyumbani kwake?
_____________________________________
_____________________________________

13. Soma Luka 18:14. Ni kwa nini mtoza ushuru alitangazwa mwenye haki na si Farisayo? ____________________________
_____________________________________

14. Soma Luka 18:14. Je Mungu alimsamehe mtoza ushuru huyu?
___________________________ __________
_____________________________________

15. Soma Warumi 10:13. Ikiwa sasa hivi umepiga magoti na kumlilia Mungu kutoka moyoni mwako "Mungu unirehemu, mtenda dhambi," Je Mungu atakutendea jinsi ile ile kama alivyomtendea mtoza ushuru? __________
_____________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

1 Yohana 1:8-9

"Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu. Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."

# MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Luka 18:9. Mfano ni nini? **Mfano wa kibiblia ni simulizi inayoelezea ukweli wa Kiroho.**

2. Soma Luka 18:9. Yesu alielekeza mfano wake kwa nani? **Kwa wale waliyokuwa wanajianmini wao wenyewe ya kuwa ni wenye haki; yaani, walijihesabia haki wao wenyewe.**

3. Soma Luka 18:9 (sehemu yamwisho ya mstari). Watu ambao wanjihesabia haki mar azote huonyesha tabiafulanikwa wengine. Kufuatana na Luka 18:9, Tabia hiyo ni ipi?

   **B. Wanawadharau wengine au wanawashusha chini.**

4. Soma Luka 18:10. Watu wawili walikwenda kuomba; kwa lugha ya kisasa, walikwenda kuomba wapi? **Kanisani**.

5. Soma Luka 18:10. Watu hawa walikuwa ninani? **Farisayo na Mtoza ushuru.**

6. Soma Luka 18:11. Maombi ya Farisayo yalikuwa ni yapi? **Mungu, Ninakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine wowote (si mtenda dhambi). Si mwivi, dhalimu, mzinzi, au hata kama mtoza ushuru huyu**.

7. Soma Luka 18:12. Kufunga kuna maana gani? **Kukaa pasipo kula.**

8. Soma Luka 18:12. Ina maana gani kutoa fungu la kumi? **Kutoa sehemu ya kumi ya kipato cha mtu.**

9. Soma Luka 18:13. Mtoza ushuru alisimama wapi? **Alisimama mbali sana. Kwa nini? Alijisikia aibu kuingia kanisani (hekaluni) kwa kuwa alikuwa ni mtenda dhambi mno, hivyo akakaa nje.**

10. Soma Luka 18:13. Ni kwa nini mtoza ushuru aliinamisha kichwa chake chini na wala hakuangalia juu? **Alikuwa anajisikia aibu. Je umeshawahi kufanya kitu ambacho si sahihi na hukuweza kumtazama mtu usoni mwake?**

11. Soma Luka 18:13. Maombi ya mtoza ushuru huyu yalikuwaje? **Mungu unirehemu; Mimi ni mwenye dhambi!**

12. Soma Luka 18:14. Yupi katika watu hawa alitangazwa kuwa mwenye haki mbele za Mungu alipokwenda nyumbani kwake? **Mtoza ushuru**.

13. Soma Luka 18:14. Ni kwa nini mtoza ushuru alitangazwa kuwa mwenye haki na si Farisayo? **Kwa sababu alijinyenyekeza mbele za Mungu. Farisayo alikuwa amejawa na kiburi; hakufikiri ya kuwa alihitaji Mwokozi.**

14. Soma Luka 18:14. Je Mungu alimsamehe mtoza ushuru huyu? **Ndiyo.**
15. Soma Warumi 10:13. Ikiwa sasa hivi umepiga magoti na kumlilia Mungu kutoka ndani ya moyo wako "Mungu unirehemu, mwenye dhambi," Je Mungu atakutendea vile vile kama alivyomtendea mtoza ushuru? **Ndiyo, atafanya hivyo. Atanisamehe na kunitakasa kutoka kwenye udhalimu wote. Angalia 1 Yohana 1:8-9**.

DARAJA 1

# SOMO 3
# HAKI KWA NEEMA

*Na Don Krow*

Leo tunakwenda kuangalia somo la haki kwa neema. Warumi 3:21-23 inasema, "Lakini sasa, haki ya Mungu imedhihirika pasipo sheria; inashuhudiwa na torati na manabii;

; ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote na kwa waaminio. Maana hakuna tofauti [utofauti]: Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa [kushuka] na utukufu wa Mungu.

Angalia ya kuwa andiko hili linasema, "Lakini sasa, haki ya Mungu imedhihirika pasipo sheria." Wakati fulani nilimuuliza mtu, "Nini unachofikiri unatakiwa kukifanya ili uweze kufika mbinguni?" Alijibu ya kuwa anatakiwa kuzishika amri kumi, awe mwaminifu kwa mke wake, aishi maisha yenye maadili mema, pamoja na mambo mengine kadhaa. Nikasema "Je unajua nini unachotakiwa kukifanya ili uweze kufika Mbinguni, uwe katika uwepo wa Mungu au kwenye ufalme wake? Unatakiwa kuwa na haki ambayo ni sawa na ya Mungu" Akasema, "Samahani? Hakuna mtu ambaye anaweza kuwa na haki inayofanana na ya Mungu." Mtu moja tu alikuwa na haki kama hiyo, na huyo alikuwa ni Yesu Kristo!" Nikasema, "Hapo una kitu chenye maana! Hilo ni sahihi kabisa! Hakuna kati yetu katika nafsi zetu wenyewe ameshawahi kushika Sheria au amri kwa ukamilifu, kwa nje au kwa ndani, lakini tunahitaji haki ambayo ni sawa na ya Mungu ili tuweze kukubalika mbele zake."

Hilo ndiyo haswa linalosemwa kwenye mstari wa 21-22, "Lakini sasa, haki ya Mungu imedhihirika pasipo sheria …hata haki ya Munguambayo ni kwa imani katika Kristo Yesu kwa wote na juu ya wote…" Aina ya haki ambayo Mungu anaitoa kwako na kwangu ni haki ambayo ni "kupitia imani katika Yesu Kristo", na ni kwa wote na juu ya wote waaminiyo. Kuna aina mbili ya haki – haki ya mwanadamu na haki ya Mungu. Haki ya mwanadamu ni tabia ya mtu iliyo bora kabisa na matendo mema wanayoyafanya, lakinihayo hayawezi kukufanya ukubalike mbele za Mungu. Unahitaji haki ambayo inafanana nay a Mungu, Na Yeye anakupatia wewe – Haki ya Munu ambayo haina sheria.

Kwa Kiyunani, Hakuna neno mahususi, ambayo ina maanisha ya kuwa maandishi haya hakika yanasema Mungu anatoa haki yake mwenyewe pasipo Sheria. Haki ambayo iko kufuatana na sheria ni haki ya kutenda, kupata na kufikia jambo ili mtu aweze kukubalika mbele za Mungu. Ulimwengu wote wa kidini leo unafikiria ya kuwa unapaswa kufanya jambo, kupata, na kufikia ili Mungu aweze kukupokea. Neno "Injili" lina maanisha "habari njema", na habari njema za Injili ni kuwa Mungu anamtoa aliye haki yakw mwenyewe na kuwakubali wale wote ambao wataamini katika kile ambacho Yesu Kristo alikitoa – Kifo chake msalabani kwa ajili ya dhambi zetu, akiweka kwetu haki ambayo inafanana na sheria. Hii ndiyo haki ya Mungu ambayo iko mbali na sheria, Pasipo sisi kufanya chochote, kupata chochote, au kufikia chochote; na inakuja kupitia Imani katika Yesu Kristo.

Angali kwenye mstari wa 22 ya kuwa ni haki ya Mungu ambayo ni kupitia Imani katika Yesu Kristo kwa wote na juu ya wote. Kwa nini Mungu anatoa haki yake kwa kila moja? "Maana hakuna tofauti [Hakuna Utofauti]: Kwa kuwa wote walitenda dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (brackets mine). Umetenda dhambi, NImetenda dhambi, na wote tumepungukiwa na kiwango cha Mungu au ukamilifu. Kwa sababu ya dhambi zetu, kitu kikubwa kuliko vyote tunachokihitaji ni kukubalika, mahusiano sahihi, na msimamo sahihi na Mungu … Na Mungu ametoa hili si kupitia kazi za Sheria bali kupitia Imani katika Yesu Kristo. Haki ya Mungu haiji kwa kufanya kazi kwako, kwa kujaribu kwako, kwa kupata kwako, au kwa mara kadhaa unazojaribu kufikia yale unayotaka kuyafikia; huja kwakupitia Imani, kutegemea, na kwa kumtumaini Bwana Yesu Kristo.

Ibrahimu (Baba wa Kiyahudi) aliokolewaje? Biblia inasema alimuani Mungu – aliamini ahadi ambayo Mungu alimpa – na ndipo haki ikahesabiwa kwake. Ukweli kuwa Ibrahamu alitangazwa mwenye haki mbele za Mungu kupitia Imani yake haikuwa tu kwa ajili yake. Tunasoma katika kitabu cha Warumi 3:21-22 ya kuwa mtu hutangazwa kuwa mwenye haki kwa kupitia Imani yake katika Yesu Kristo. Biblia inasema ya kuwa kwa sababu ya malipo ambayo Yesu aliyafanya msalabani alipomwaga damu Yake kwa ajili ya dhambi zetu, haki (msimamo sahihi) itahesabiwa kwa mtu yeyote ambaye tu ataamini katika Kristo.

Warumi 5:17 inasema, "Kwa maana ikiwa kwa kukosa mtu mmoja mauti ilitawala kwa sababu ya yule mmoja; zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo.". Mungu anakupa wewe zawadi cha haki, zawadi cha msimamo sahihi mbele Zake. Zawadi ambayo haigharimu kitu bali kwa yule anayeipokea. Ikiwa kama ungenipa mimi zawadi na kuniambia niilipie, itakuwa ni zawadi, lakini ilikugharimu kitu filani. Mungu aliifanya haki ipatikane kwako na kwangu kama zawadi, na zawadi hii ya haki, iliyoachiliwa, na msimamo sahihi mbele za Mungu huja kupitia Imani katika Yesu Kristo.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Tito 3:5. Je haki tunayoihitaji ni haki tunayoweza kuizalisha sisi wenyewe? ____

2. Soma 2 Wakorintho 5:21. Ni aina gani ya haki tunayoihitaji? ____

3. Soma Warumi 3:22. Tunaipokeaje haki hii? ____

4. Soma Wafilipi 3:9. Haki ya Sheria ni ipi? ____

5. Soma Wagalatia 2:21. Tunawezaje kuifanya neema ya Mungu kuwa batili? ____

6. Soma Warumi 5:17. Haki ya Mungu inapokelewa kama nini? ____

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Tito 3:5
"Si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, alituokoa, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa na kufanywa upya na Roho Mtakatifu."

### 2 Wakorintho 5:21
"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye."

### Warumi 3:22
"ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio. Maana hakuna tofauti."

### Wafilipi 3:9
"tena nionekane katika yeye, nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani."

### Wagalatia 2:21
"Siibatili neema ya Mungu; maana, ikiwa haki hupatikana kwa njia ya sheria, basi Kristo alikufa bure."

### Warumi 5:17
"Kwa maana ikiwa kwa kukosa mtu mmoja mauti ilitawala kwa sababu ya yule mmoja, zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Tito 3:5. Je haki tunayoihitaji ni haki tunayoweza kuizalisha sisi wenyewe? Hapana.
2. Soma 2 Wakorintho 5:21. Ni aina gani ya haki tunayoihitaji? Haki ya Mungu (ambayo huja kupitia Kristo).
3. Soma Warumi 3:22. Tunaipokeaje haki hii? Kupitia Imani katika Yesu Kristo.
4. Soma Wafilipi 3:9. Haki ya Sheria ni ipi? Haki ninayoimiliki – matendo ya haki ninayo weza kuyazalisha.
5. Soma Wagalatia 2:21. Tunawezaje kuifanya neema ya Mungu kuwa batili? Tunaweza kuibatilisha neema kwa kujaribu kuokolewa kwa matendo yetu mema badala ya kumtumaini Kristo na Kifo chake kwa ajili yetu kwa ajili ya wokovu wetu.
6. Soma Warumi 5:17. Haki ya Mungu inapokelewa kama nini? Zawadi.

DARAJA 1

# SOMO 4
# MAHUSIANO NA MUNGU

*Na Andrew Wommack*

Moja ya mambo ya muhimu sana kuhusu mahusiano ni kumuelewa mtu ambaye unakwenda kuwa na mahusiano naye, na hilo pia linafanyika na mahusiano na Mungu. Unahitaji kuelewa asili ya msingi na tabia ya Mungu ili kuwa na mahusiano mazuri na Yeye. Kutokuelewa tabia yake na asili ni moja ya sababu watu wengi hawana uhusiano chanya na Yeye. Hili ndilo hasa lililotokea katika bustani ya Eden wakati Adamu na Hawa walipojaribiwa na Shetani. Waliingia majaribuni, hatimaye hawakumtii Mungu, na wakawaingiza wanadamu wote dhambini. Kukosa kwao kuelewa asili ya Mungu ilikuwa hasa ni sehemu ya jaribu.

Habari katika Mwanzo 3:1-5 inafahamika na watu wengi: "Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani? Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa. Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya."

Kuna kauli ngumu kutoka kwa Shetani hapa ya kuwa Mungu hakika si Mungu mwema… ya kuwa alikuwa anajaribu kushikilia kitu fulani kutoka kwa Adamu na Hawa … ya kuwa hakutaka wafikie uwezo wao mkamilifu … ya kuwa hakutaka wawe kama Yeye … na ya kuwa sababu aliweka kanuni kuhusu wao kutokula Mti wa ujuzi wa Mema na Mabaya ilikuwa ni kuwazuia au kuwaumiza. Katika maana ya kuwa, Shetani alikuja dhidi ya asili ile ile ya Mungu na tabia ya Mungu pale alipodanganya kwa kusema kuwa Mungu hakutaka wao wawe na kilicho bora.Ni jambo hilo hilo ambalo ndilo linalotokea kwa watu leo. Shetani anawaambia, "Ikiwa kama mtamfuata Mungu na hamtafanya mambo haya yote ambayo yako kinyume na Neno lake, basi kamwe hamtawahi kupata furaha ya kweli. Maisha yatakuwa ni ya kuchosha … kufa." Ukweli unaohuzunisha ni kuwa watu hujaribu mambo mbali mbali kama vile madawa, pombe, ngono, uasi, kujifurahisha wenyewe, mafanikio katika kazi mbali mbali, na mengine mengi,

na ifikapo wakati watakapotambua ya kwamba mambo hayo hayawapi yale wanayoyatamani katika maisha yao, tayari wameshayaharibu maisha yao, familia zao, na afya zao.

Ukweli ni kuwa Mungu ni Mungu Mwema, na mapenzi yake kwetu ni mema pekee. Lakini Shetani anatumia majaribu yale yale kwetu sisi leo kama alivyofanya kwa Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni, kimsingi akimaanisha ya kuwa Mungu si Mungu mwema. Wale ambao wana uelewa mdogo tu wa Biblia wanaweza kupata uelewa wa aina hiyo kwa kuwa kuna matukio katika Neno ambapo Aliwatendea watu kwa ukali. Katika Hesabu 15:32-36, mtu alinyanyua fimbo siku ya Sabato na akapigwa mawe hata kufa kwa kushindwa kuishika Sabato. Hilo linaonekana ni jambo lenye ukali, lakini kulikuwa na madhumuni nyuma ya adhabu kama hiyo, Ingawa si kawaida kwa watu wengi katika kuyasoma Maandiko kikawaida tu. Kujifunza kwa uangalifu kunafunua ya kuwa Sheria ya Agano la Kale ilitolewa ili kuzifanya dhambi ambazo tumezitenda kuwa ni kitu chenye dhambi zaidi, Kama Paulo anavyosema katika Warumi 7:13. Madhumuni yalikuwa ni watu hawakutambua makosa yao yalikuwa ni mabaya kiasi gani na ya kuwa yalikuwa ni kikwazo dhidi ya Mungu. Walifanya kosa la kujilinganisha kati yao na kupima matendo yao kwa kile ambacho watu wengine walikuwa wanakifanya.

Ikiwa kama kuna mtu alitenda dhambi na hakupigwa mpaka afe, walifikiri ya kuwa basi dhambi si kitu kibaya sana, na walishusha viwango vyao. Walipoteza mtazamo wa kweli kuhusu nini kilkuwa sahihi na nini hakikuwa sahihi. Mungu ilibidi amrudishe mwanadamu kwenye mstari, kiwango sahihi cha kuishi maisha sahihi kilikuwa ni nini, hivyo wangemkataa Shetani na majaribu yake na kutambua matokeo ya mwisho ya kufanya maamuzi mabaya yangekuwaje. Na halafu alipofanya hivyo, Ilibidi Asisitizie Sheria aliyoitoa.

Mungu hakuzitoa amri za Agano la Kale kwa ajili ya kusema, "mpaka mtakapofanya mambo haya yote, Siwezi kuwakubali au kuwapenda." Hiyo siyo asili yake au tabia. Badala yake, alizitoa ili kuufanya ufahamu wetu wa kilicho sahihi na kisicho sahihi uwe na umakini Zaidi na kuturejesha kwenye ukweli kuwa tunamhitaji Mwokozi. Tatizo limekuwa kwamba watu walifikiria ya kuwa Mungu alikuwa anadai ukamilifu kabla Hajawapenda, ambayo ilipelekea kwenye tabia ambayo wengi wanayo ya kuwa upendo Wake kwao unahusiana moja kwa moja na utendaji wao. Wanajisikia ya kuwa ni mpaka pale watakapokuwa wamejaribu kufanya kila kitu sawa kabisa, hawatakubalika na Mungu, na huo si ujumbe wa Biblia.

Moyo wa Mungu ni kuwapatanisha wanadamu kwake Yeye mwenyewe na si kuwahukumu… na si kuwa hesabia kuwa wenye dhambi… na wala si kuzihesabu dhambi zao dhidi yao. Huo ndiyo moyo wa Mungu kwa ajili ya watu kwenye Biblia na pia moyo Wake kwa ajili yako leo. Unahitaji kuuelewa moyo Wake halisi, ya kuwa"Mungu ni upendo" (1 Yohana 4:8 Anatafuta kuziondoa dhambi zako na kitu chochote ambacho kingekutenga wewe Naye, Tayari ameshafanya kupitia Yesu Kristo na anakupatia wewe uhusiano leo, na si katika msingi wa utendaji wako bali katika Imani yako na kumkubali kwako Yesu aliyebebea dhambi zako.

Unaweza kuwa na uhusiano na Mungu leo bila kujali kushindwa kwako katika maisha yako. Anachokihitaji tu ni kuwa uweke Imani yako katika Bwana Yesu Kristo.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Mwanzo 3:1. Ni swali gani ambali Shetani alimuuliza Hawa? ______________ ______________________________________ ______________________________________

2. Soma Mwanzo 2:17 na Mwanzo 3:3. Ni neno gani au maneno ambayo Hawa aliongeza kwa kile ambacho Mungu alimuambia Adamu? __________________ ______________________________________

3. Soma Mwanzo 3:6. Mara Shetani alipoweza kuingiza mashaka ndani ya nia ya Hawa kuhusu Neno la Mungu, alifanya nin i katikamstari huu? ________________ ______________________________________ _______________________

4. Soma Mwanzo 3:9-10. Baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi, Je Mungu bado aliwasiliana nao na kufuatilia uhusiano nao? _________________________________ ______________________________________

5. Soma Mwanzo 3:22-24. Ni kwa nini Mungu alimfukuza Adamu na Hawa bustanini? ___________________________ ______________________________________

6. Je unaweza kuona ya kuwa hiki kilikuwa ni kitendo cha rehema na si adhabu? ______ ______________________________________ _________________________________

7. Soma Warumi 5:17. Tunapataje neema tele ya Mungu na karama ya haki?

   A. Tunainunua

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Mwanzo 3:1

"Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?"

### Mwanzo 2:17

"Walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika."

### Mwanzo 3:3

"Lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa."

### Mwanzo 3:6

"Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala."

### Mwanzo 3:9-10

"[9] Bwana Mungu akamwita Adamu, akamwambia, Uko wapi? [10] Akasema, Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha."

### Mwanzo 3:22-24

"[22] Bwana Mungu akasema, Basi, huyu mtu amekuwa kama mmoja wetu, kwa kujua mema na mabaya; na sasa asije akanyosha mkono wake akatwaa matunda ya mti wa uzima, akala, akaishi milele; [23] kwa hiyo BWANA Mungu akamtoa katika bustani ya Edeni, ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa. [24] Basi

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

B. Tunaipata kwa kuifanyia kazi

C. Tunaipokea

8. Soma Warumi 6:23. Nini ambacho hakika tunakistahili kama tukitenda dhambi? ___
_______________________________
_______________________________

9. Kwa neema, Nini ambacho Mungu anatupa badala yake? ___________
_______________________________
_______________________________

10. Soma Warumi 10:3. Ikiwa kama tutajaribu kuunda haki yetu wenyewe mbele za Mungu, nini ambacho tunashindwa kukifanya? ______________
_______________________________

11. Soma 1 Yohana 1:9 na Warumi 4:3. Nini ambacho Mungu anaahidi kukifanya na dhambi zetu ZOTE na makosa yetu dhidi Yake ikiwa kama tu tutaamini?
_______________________________

12. Hili linakuambia nini kuhusu tabia ya Mungu? ______________
_______________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

akamfukuza huyo mtu, akaweka Makerubi, upande wa mashariki wa bustani ya Edeni, na upanga wa moto uliogeuka huko na huko, kuilinda njia ya mti wa uzima."

### Warumi 5:17

"Kwa maana ikiwa kwa kukosa mtu mmoja mauti ilitawala kwa sababu ya yule mmoja, zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo."

### Warumi 6:23

"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu."

### Warumi 10:3

"Kwa maana, wakiwa hawaijui haki ya Mungu, na wakitaka kuithibitisha haki yao wenyewe, hawakujitia chini ya haki ya Mungu."

### 1 Yohana 1:9

"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."

### Warumi 4:3

"Maana maandiko yasemaje? Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Mwanzo 3:1. Ni swali gani ambali Shetani alimuuliza Hawa? **"Je Mungu amesema, Hamtakula matunda ya kila mti wa bustani?"**
2. Soma Mwanzo 2:17 and Genesis 3:3. Ni neno gani au maneno ambayo Hawa aliongeza kwa kile ambacho Mungu alimuambia Adamu? **Ya kuwa wasiuguse.**
3. Soma Mwanzo 3:6. Mara Shetani alipoweza kuingiza mashaka ndani ya nia ya Hawa kuhusu Neno la Mungu, alifanya nini katika mstari huu? **Alichukua na kula tunda la Mti.**
4. Soma Mwanzo 3:9-10. Baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi, Je Mungu bado aliwasiliana nao na kufuatilia uhusiano nao? **Ndiyo.**
5. Soma Mwanzo 3:22-24. Ni kwa nini Mungu alimfukuza Adamu na Hawa bustanini? **Ili wasile kwenye mti wa uzima na wakaishi milele katika hali ya dhambi.**
6. Je unaweza kuona ya kuwa hiki kilikuwa ni kitendo cha rehema na si adhabu? **Ndiyo.**
7. Soma Warumi 5:17. Tunapataje neema tele ya Mungu na karama ya haki? **C. Tunaipokea**
8. Soma Warumi 6:23. Nini ambacho hakika tunakistahili kama tukitenda dhambi? **Mauti.**
9. Kwa neema, Nini ambacho Mungu anatupa badala yake? **Uzima wa milele katika Yesu.**
10. Soma Warumi 10:3. Ikiwa kama tutajaribu kuunda haki yetu wenyewe mbele za Mungu, nini ambacho tunashindwa kukifanya? **Kumtii Yesu kama haki yetu.**
11. Soma 1 Yohana 1:9 and Romans 4:3. Nini ambacho Mungu anaahidi kukifanya na dhambi zetu ZOTE na makosa yetu dhidi Yake ikiwa kama tu tutaamini? **Kuziondoa, kuzisahau, na kuzisamehe.**
12. Hili linakuambia nini kuhusu tabia ya Mungu? **Ya kuwa Yeye ni wa rehema na mwenye upendo.**

DARAJA 1

# SOMO 5
# ASILI YA MUNGU

*Na Andrew Wommack*

Kuwa na uhusiano mzuri na BWANA, ni lazima tuijue asili yake na tabia Yake halisi. Je anahasira kwa sababu ya dhambi zetu, au Yeye ni Mungu mwenye rehema ambaye anataka kutupa sisi uzima Wake na Baraka, bila kutegemea utendaji wetu? Maandiko katika uhalisi yanatupa mitazamo miwili tofauti ya Mungu, Si ya kuwa amebadilika au kufanya kitu chochote tofauti. Kulikuwa na kipindi cha muda ambapo katika neno lililotumika kwenye Biblia, Mungu "alizishikilia dhambi za wanadamu dhidi yao."

Hili linaweza kulinganishwa na kulea watoto. Wanapokuwa ni wadogo sana, haiwezekani kujadiliana nao, kuwaambia kwa nini wanapaswa kuenenda sawa sawa au kwa nini hawapaswi kuwa wabinafsi na kuchukua wanasesere mbali na kaka na dada zao. Wanapaswa kuambiwa kanuni na, ikiwa kama watazivunja, waadabishwe. Sheria inabidi zitiliwe mkazo ingawa hawajui kuhusu Mungu na Shetani, au ya kuwa wanampa Shetani nafasi wanapokuwa wabinafsi. Wanaweza wasielewe dhana, lakini wanaweza kuelewa ya kuwa ikiwa kama watarudia vitendo hivyo, wataadhibiwa.

Ikimaanisha, ndicho ambacho Bwana alikifanya na Agano la Kale. Kabla watu hawajaokoka, hawakuwa na mtazamo wa kiroho tulionao chini ya Agano Jipya, hivyo ilimbidi Atoe sheria na kuzitilia mkazo kwa adhabu, mara nyengine hata mauti, ili kuwakatisha tamaa ya kutenda dhambi. Kwa sababu Shetani alikuwa akiangamiza watu kupitia dhambi, ilibidi vizuizi viwekwe kwenye dhambi, na ilibidi vitiliwe mkazo. Ingawa hili liliacha hisia zisizo halisi ya kuwa Mungu hakika hakutupenda kwa sababu ya dhambi zetu, hicho sicho ambacho Neno la Mungu linakifundisha. Warumi 5:13 inasema, "maana kabla ya sheria dhambi ilikuwamo ulimwenguni, lakini dhambi haihesabiwi isipokuwapo sheria." "Isipokuwapo sheria" ina maanisha mpaka siku za Munsa wakati Mungu alipotoa amri Kumi na sheria nyengine mbali mbali ambazo zilitumika kwenye taifa la Wayahudi. Mpaka wakati huo, dhambi ilikuwako duniani lakini haikuhesabiwa. Neno "kuhesabiwa" ni neno la watunza vitabu vya mahesabu; m.f., unaenda dukani kununua kitu na unasema, "Weka kwenye mahesabu yangu." Inapowekwa kwenye mahesabu yako, inarekodiwa na kutozwa kwenye akaunti yako, na manunuzi hayo

yanahesabiwa kwako. Ikiwa kama wameshindwa kuihesabia, hiyo maana yake haikurekodiwa na kuwekwa dhidi yako.

Mstari huu unasema ya kuwa mpaka wakati amri kumi zilipokuja, dhambi haikuwa ikihesabiwa dhidi ya watu. Hii ni kauli ya kushangaza. Angalia kwenye mwanzo 3 na 4. Watu wengi wana dhana kuwa wakati Adamu na Hawa walipotenda dhambi dhidi ya Mungu, kwa kuwa alikuwa mtakatifu na mwanadamu sasa alikuwa ni mwenye dhambi, Asingekuwa na chochote cha kumhusu mwanadamu mwenye dhambi. Wanafikiri ya kuwa Mungu alimfukuza mwanadamu kutoka Bustanini ili kumwondoa kutoka kwenye uwepo Wake kwa kuwa Mungu mtakatifu asingeweza kuwa na chochote kuhusiana na mwanadamu asiye mtakatifu. zaidi wanafikiri ya kuwa ni mpaka utakaposafisha matendo yako kupitia matendo sahihi, Mungu mara nyengine tena hawezi kuwa na uhusiano na wewe. Hilo liko kinyume na ujumbe ambao Yesu aliuleta. Warumi 5:8 inasema Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi; hivyo Agano Jipya linafundisha ya kuwa Mungu aliuonyesha upendo Wake kwako wakati bado ulipokuwa unaishi dhambini, na si baada ya kuwa umesha safisha matendo yako. Moja ya kweli kuu ya Injili ambayo itayabadilisha maisha yako ni kuelewa kuwa Mungu anakupenda jinsi kama ulivyo. Anakupenda sana kiasi kwamba kama utapokea upendo Wake, hutataka kubaki kama ulivyo. Utabadilika, lakini utabadilika kama matokeo ya upendo wa Mungu na si ili upate upendo Wake.

Katika Mwanzo 4 unaweza kuona ya kuwa Mungu bado alikuwa akiwa na ushirika na mwanadamu, bado anazungumza na Adamu na Hawa hata baada ya wao kutenda dhambi. Alizungumza na Kaini na Habili, na walipokuja kutoa dhabihu Kwake, Alizungumza nao katika sauti iliyosikika. Kupitia mwitikio wao, tunaweza kuona ya kuwa walikuwa wamezoea kuisikia sauti yake, na wala haikuwaogopesha. Wakati Kaini alipomwua kaka yake Habili na akafanyika kuwa ni muwaji wa kwanza ulimwenguni, sauti ya Mungu iliyosikika ilitoka mbinguni: "Ndugu yako Habili yuko wapi?" Kaini alidanganya mbele za Mungu, ikionekana pasipo kuwa na hatia. Hilo linaweza kutokea tu ikiwa kama mtu amezoea sana kuisiskia sauti ya Mungu ambayo wanaichukulia kirahisi tu na wala hawana hofu juu yake. Haya yote inachokesema ni kuwa Mungu bado alikuwa akiwa na ushirika na mwanadamu na alikuwa hajavunja ushirika, kama ambavyo invyoaminika, Hakuwa akimhesabia dhambi mwanadamu, Je hiyo ina maanisha ya kuwa alizikubali dhambi zao au ya kuwa hawakuwa sahihi? Hapana, hivyo ndiyo sababu hatimaye alitoa Sheria ili kumrudisha mwanadamu kwenye kiwango sahihi. Mungu ilibidi amwonyeshe mwanadamu ya kuwa anahitaji mwokozi na ya kuwa anapaswa kujinyenyekesha mwenyewe na kupokea msamaha kama kipawa. La kuhuzunisha ni kuwa dini, imetawala mambo haya na kufundisha ya kuwa Sheria ilitolewa ili uweze kuifuata na ndipo utakapopata msamaha wa Mungu na kukubalika. Hapana! Madhumuni ya Sheria ya Agano la Kale ilikuwa ni kukuza dhambi yako kwenye kiwango ambacho utakata tamaa kujiokoa mwenyewe na

kusema, “Mungu, ikiwa kama hiki ndicho kiwango chako cha utakatifu, siwezi kufanya. Nisamehe, unirehemu.” Asili ya Mungu kwa ujumla mara zote imekuwa ni upendo.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Warumi 5:13. Neno "kuhesabiwa" lina maanisha nini? ______________________

2. Soma Warumi 7:7. Nini yalikuwa ni madhumuni ya Sheria? ________________________

3. Soma Wagalatia 3:24. Kufuatana na mstari huu, nii yalikuwa ni madhumuni ya Sheria? ______________________________ ____________________________________

4. Soma Yohana 8:1-11. Yesu alishughulika vipi na mwanamke aliyefumaniwa katika uzizinzi? _____________________________ ____________________________________ _____________________

5. Je maneno ya Yesu na matendo yalionyesha asili halisi ya Mungu? Angalia Yohana 3:34. ____________________________________ ____________________________________

6. Soma 1 Yohana 4:8. Kufuatana na mstari huu, asili halisi ya Mungu ni ipi? ________

7. Soma Warumi 5:6. Upendo wa Mungu ulielekezwa kwetu wakati tulipokuwa watu gani? ______________________________ ____________________________________

8. Soma Warumi 5:8. Mungu alitupenda tungali tukiwa watu wa aina gani? _________________________

9. Soma Warumi 5:10. Mungu alitupenda tungali tukiwa watu wa aina gani? ________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Warumi 5:13

"Maana kabla ya sheria dhambi ilikuwamo ulimwenguni, lakini dhambi haihesabiwi isipokuwapo sheria;"

### Warumi 7:7

"Tusemeje, basi? Torati ni dhambi? Hasha! Walakini singalitambua dhambi ila kwa sheria; kwa kuwa singalijua kutamani, kama torati isingalisema, Usitamani."

### Wagalatia 3:24

"Hivyo torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo, ili tuhesabiwe haki kwa imani.."

### Yohana 8:1-11

"[1] Naye Yesu akaenda mpaka mlima wa Mizeituni. [2] Hata asubuhi kulipokucha akaingia tena hekaluni, na watu wote wakamwendea; naye akaketi, akawa akiwafundisha. [3] Waandishi na Mafarisayo wakamletea mwanamke aliyefumaniwa katika uzinzi, wakamweka katikati, [4] Wakamwambia, Mwalimu, mwanamke huyu amefumaniwa alipokuwa akizini. [5] Basi katika torati, Musa alituamuru kuwapiga kwa mawe wanawake namna hii; nawe wasemaje? [6] Nao wakasema neno hilo wakimjaribu, ili wapate sababu ya kumshitaki. Lakini Yesu akainama, akaandika kwa kidole chake katika nchi [7] Nao walipozidi kumhoji, alijiinua, akawaambia, Yeye asiye na dhambi miongoni mwenu na awe wa kwanza wa kumtupia jiwe. [8] Akainama tena, akaandika kwa kidole chake katika nchi. [9] Nao waliposikia, wakashitakiwa na dhamiri zao, wakatoka mmoja mmoja, wakianzia tangu wazee hata wa mwisho wao; akabaki Yesu peke yake, na yule

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

10. Kama ungemuuliza Yesu Kristo akusamehe na awe mwokozi na Bwana wako, utumaini dhabihu yaYesu kama malipo ya dhambi zako, Je Mungu atakuonyesha asili yake halisi ya rehema na neema? ____________
____________________________________
____________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

mwanamke amesimama katikati. [10] Yesu akajiinua asimwone mtu ila yule mwanamke, akamwambia, Mwanamke, wako wapi wale washitaki wako? Je! Hakuna aliyekuhukumu kuwa na hatia? [11] Akamwambia, Hakuna, Bwana. Yesu akamwambia, Wala mimi sikuhukumu. Enenda zako; wala usitende dhambi tena"

Yohana 3:34

"Kwa kuwa yeye aliyetumwa na Mungu huyanena maneno ya Mungu; kwa sababu hamtoi Roho kwa kipimo."

1 Yohana 4:8

"Yeye asiyependa, hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni upendo."

Warumi 5:6

"Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, Kristo alikufa kwa ajili ya waovu."

Warumi 5:8

"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi."

Warumi 5:10

"Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima wake."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Warumi 5:13. Neno “kuhesabia” lina maana gani? **Toza kwenye akaunti ya mtu fulani.**
2. Soma Warumi 7:7. Nini yalikuwa madhumuni ya Sheria? **Kuifanya dhambi ijulikane.**
3. Soma Wagalatia 3:24. Kufuatana na mstari huu, Madhumuni ya Sheria yalikuwa ni yapi? **Kuwaonyesha wanadamu uhitaji wa kuwa na Mwokozi, Yesu Kristo.**
4. Soma Yohana 8:1-11. Yesu alishughulika vipi na mwanamke aliyefumaniwa katika tendo la uzinzi? **Katika rehema na Neema.**
5. Je maneno na matendo ya Yesu yanaonyesha asili halisi ya Mungu? **Tazama Yohana 3:34. Ndiyo.**
6. Soma 1 Yohana 4:8. Kufuatana na mstari huu, asili ya kweli ya Mungu ni ipi? **Upendo.**
7. Soma Warumi 5:6. Upendo wa Mungu ulielekezwa kwetu wakati tulipokuwa watu wa namna gani? **Hatukua na nguvu; yaani., hatuna msaada na hatukuwa wa kimungu.**
8. Soma Warumi 5:8. Mungu alitupenda wakati tukiwa watu wa namna gani? **Wenye dhambi.**
9. Soma Warumi 5:10. Mungu alitupenda wakati tukiwa watu wa aina gani? **Maadui.**
10. Kama ungemuuliza Yesu Kristo akusamehe na awe mwokozi na Bwana wako, utumaini dhabihu yaYesu kama malipo ya dhambi zako, Je Mungu atakuonyesha asili yake halisi ya rehema na neema? **Ndiyo.**

DARAJA 1

# SOMO 6
# TOBA

*Na Don Krow*

Baadhi ya watu wamekosa kuelewa nini maana ya toba. Toba si kufanya ukamilifu bali ni mabadiliko kwenye mwelekeo. Tunaenda kuzungumza kuhusu mfano wa mwana mpotevu, au mwana aliyepotea. Yesu anaelezea simulizi ambayo kwa ukamilifu kabisa inaelezea ina maana gani kwa mtu kutubu. Katika Luka 15:11-12 Yesu alisema, "Akasema, Mtu mmoja alikuwa na wana wawili: yule mdogo akamwambia babaye, Baba, nipe sehemu ya mali inayoniangukia. Akawagawia vitu vyake."

Yule mdogo alitaka urithi wake kabla ya baba yake kufa, ambacho si kitu cha kawaida, lakini baba yake alimpa sawa sawa na ombi lake na akawapa watoto wake urithi wao. Mstari 13 unasema, "Hata baada ya siku si nyingi, yule mdogo akakusanya vyote, akasafiri kwenda nchi ya mbali; akatapanya mali zake huko kwa maisha ya uasherati." Mtoto mdogo alichukua urithi wake wote, sehemu yake ya urithi, akaenda katika nchi ya mbali, na akautapanya kwa maisha ya uasherati. Tafsiri moja inasema, "akijihusisha na sherehe na kutumia fedha zake kwa makahaba."

Mistari ya 14-15 inasomeka, "Alipokuwa amekwisha tumia vyote, njaa kuu iliingia nchi ile, [Nchi ikawa na uhitaji na watu walikuwa na njaa]; yeye naye akaanza kuhitaji. Akaenda akashikamana na mwenyeji mmoja wa nchi ile; naye alimpeleka shambani kwake kulisha nguruwe". Alipata kazi kwa kufanya kazi kwa mwenyeji mmoja wa nchi ile na akapelekwa kulisha nguruwe. Mstari 16 unasema, "Akawa akitamani kujishibisha kwa maganda waliyokula nguruwe, wala hapana mtu aliyempa kitu." Alikuwa na njaa sana, hata kufikia kiwango cha kutaka kufa na njaa, na akasema "nipe tu chakula cha nguruwe – chochote," lakini hakuna yeyote aliyempa chochote. Aliutumia vibaya urithi wake wote. Mstari 17 unaendelea, "Alipozingatia moyoni mwake, alisema, Ni watumishi wangapi wa baba yangu wanaokula chakula na kusaza, na mimi hapa ninakufa kwa njaa!" Tafsiri moja inasema, "aliporudi kwenye ufahamu wake." Kwa maneno mengine, watumishi wa baba yake walikuwa na zaidi ya vya kutosha, na yeye alikuwa akifa kwa njaa.

Alifanya uamuzi; akatubu. Toba ni kubadili nia, mabadiliko ya moyo ambayo yana msababisha mtu kugeuka na kuelekea kwenye mwelekeo mpya. Katika mistari ya 18-19, alisema, "Nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena; nifanye kama mmoja wa watumishi wako." "Nifanye tu kuwa mtumwa, baba. Nimetenda dhambi dhidi yako, nimetapanya mali yako, na kumtenda dhambi Mungu. Nifanye tu kuwa mtumwa." Halafu akaamka na kwenda kwa baba yake. Toba ni zaidi ya mabadiliko ya tabia, mabadiliko ya nia, na mabadiliko ya moyo; ina mwongoza mtu atende kwenye kile anachokiamini, kugeuka (au kurudi) na kwenda kwenye mwelekeo mpya. Sisi sote tumeguka mbali na Mungu, Baba yetu, na mbali na mbinguni, nyumbani kwetu. Biblia inasema katika Isaya 53:6 hivi "Sisi sote kama kondoo tumepotea; Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe," Lakini Mungu katika rehema zake amezichukua dhambi zetu na kuziweka kwa Yesu

.Habari hii inaendelea katika mistari ya 20-24. "Akaondoka, akaenda kwa babaye." Usiku moja nilikuwa nikimuelezea mtu habari hii ambaye hakuwahi kuisikia kabla, na alijua tu ya kuwa mtoto aliporudi, baba yake angesema, "Mwanagu, angalia ulichokifanya. Umepoteza utajiri wangu wote, Vyote nilivyovikusanya katika maisha yangu. Uwe moja wa watumwa wangu." Wengi wa mababa wa dunia inawezekana wakawa na hasira sana na kuwa na tabia kama hiyo, lakini angalia tabia ya baba: "Alipokuwa angali mbali, baba yake alimwona, akamwonea huruma [Upendo ukatoka moyoni mwake kwa ajili ya mwanawe], akaenda mbio akamwangukia shingoni, akambusu sana. Yule mwana akamwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena. Lakini baba aliwaambia watumwa wake, Lileteni upesi vazi lililo bora, mkamvike; mtieni na pete kidoleni, na viatu miguuni; mleteni ndama yule aliyenona mkamchinje; nasi tule na kufurahi; kwa kuwa huyu mwanangu alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana. Wakaanza kushangilia". Wakaanza kuwa na sherehe.

Wakati fulani nilimwambia hili mtu ambaye alisema, "Ninaona kile ambacho Yesu anakisema. Ikiwa tu nitamgeukia Baba wa Mbinguni kwa ajili ya rehema na 'Baba, Nimetenda dhambi dhidi yako, na sistahili kuwa mwanao,' Atanikubali." Baba yetu wa Mbinguni atatuhurumia, na hatakufanya uwe mtumwa. Atakurejesha kuwa mwana kamili pamoja Naye, na wala Hatakufanya uwe mtumwa. Atakurejesha kuwa mwana kamili Naye. Mungu anasubiri. Je umegeuka mbali Naye? Kwa nini usimgeukie Mungu, Baba yako, na Mbinguni, nyumbani kwako, leo?

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Elezea maana ya Toba. ____________________
________________________________________
________________________

2. Soma Luka 13:1-5. Mtu anapaswa kufanya nini ili asiangamie?
________________________

3. Soma 2 Petro 3:9. Nini ni matamanio ya Mungu kwa watu wote?
________________________________

4. Soma Luka 16:19-31. Katika Luka 16:28, ni kwa nini yule tajiri alitaka mtu arudi kutoka wafu ili azungumze na ndugu zake?
________________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Luka 13:1-5

"[1] Na wakati uo huo walikuwapo watu waliompasha habari ya Wagalilaya wale ambao Pilato alichanganya damu yao na dhabihu zao. [ 2] Akawajibu akawaambia, Je! Mwadhani ya kwamba Wagalilaya hao walikuwa wenye dhambi kuliko Wagalilaya wote, hata wakapatwa na mambo hayo? [3] Nawaambia, Sivyo; lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo. [4]Au wale kumi na wanane, walioangukiwa na mnara huko Siloamu, ukawaua, mwadhani ya kwamba wao walikuwa wakosaji kuliko watu wote waliokaa Yerusalemu? [5] Nawaambia, Sivyo; lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo."

### 2 Petro 3:9

"Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba."

### Luka 16:19-31

"[19] Akasema, Palikuwa na mtu mmoja, tajiri, aliyevaa nguo za rangi ya zambarau na kitani safi, na kula sikuzote kwa anasa: [20] Na maskini mmoja, jina lake Lazaro, huwekwa mlangoni pake, ana vidonda vingi,, [21] naye alikuwa akitamani kushibishwa kwa makombo yaliyoanguka katika meza ya yule tajiri; hata mbwa wakaja wakamramba vidonda vyake. [22] Ikawa yule maskini alikufa, akachukuliwa na malaika mpaka kifuani kwa Ibrahimu. Yule tajiri naye akafa, akazikwa [23] Basi, kule kuzimu aliyainua macho yake, alipokuwa katika mateso, akamwona Ibrahimu kwa mbali, na Lazaro kifuani mwake.. [24] Akalia, akasema, Ee baba Ibrahimu,

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

5. Soma Luka 16:30. Nini ambacho ndugu hawa wanapaswa kukifanya ili kuepuka mahali hapa pa mateso (kuzimu)? ________ ______________________________________ __________________

6. Soma Matendo 26:18. Ingawa haisemi mahususi, mstari huu unazungumza kuhusu toba. Nini kitakachotokea kwa wale watakaotubu? ____________________ ______________________________________ __________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

nihurumie, umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake majini, auburudishe ulimi wangu; kwa sababu ninateswa katika moto huu. [25] Ibrahimu akasema, Mwanangu, kumbuka ya kwamba wewe uliyapokea mambo mema yako katika maisha yako, na Lazaro vivyo alipata mabaya; na sasa yeye yupo hapa anafarijiwa, na wewe unaumizwa. [26] Na zaidi ya hayo, kati yetu sisi na ninyi kumewekwa shimo kubwa, ili wale watakao kutoka huku kwenda kwenu wasiweze; wala watu wa kwenu wasivuke kuja kwetu. [27] Akasema, Basi, baba, nakuomba, umtume nyumbani kwa baba yangu: [28] kwa kuwa ninao ndugu watano, ili awashuhudie, wasije wao pia wakafika mahali hapa pa mateso. [29] Ibrahimu akasema, Wanao Musa na manabii; na wawasikilize wao. [30] Akasema, La, baba Ibrahimu, lakini kama akiwaendea mtu atokaye kwa wafu, watatubu.. [31] Akamwambia, Wasipowasikia Musa na manabii, hawatashawishwa hata mtu akifufuka katika wafu."

### Luka 16:30

"Akasema, La, baba Ibrahimu, lakini kama akiwaendea mtu atokaye kwa wafu, watatubu."

### Matendo 26:18

"uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi.."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

7. Soma Matendo 26:20. Katika sehemu ya mwisho ya mstari huu, mambo matatu yanatajwa ambayo wamataifa wanapaswa kuyafanya. Mambo haya matatu ni yapi? ______________________________

8. Soma Matayo 7:21-23. Yesu alisema kuwa watu hawa walikuwa wakifanya nini badala ya mapenzi ya Mungu? _______________ ___________________________________ ___________

9. Hili linakuonyesha nini kuhusu umuhimu wa toba ya kweli dhidi ya maneno matupu tunayoyasema mbele za Mungu? ________ ___________________________________ _________________

10. Soma Isaya 55:7. Je waovu wanapaswa kufanya nini? _______________________ _________

11. Ni mambo gani mawili wenye haki wanapaswakuyafanya? ________________ __________________

12. Je Mungu atamfanya nini mtu afanyaye mambo hayo yaliyotajwa hapo juu? ___________

13. Soma Luka 15:7. Mwitikio wa Mbingu kwa mwenye dhambimoja anayetubu ukoje? __________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Matendo 26:20

"Bali kwanza niliwahubiri wale wa Dameski na Yerusalemu, na katika nchi yote ya Uyahudi, na watu wa Mataifa, kwamba watubu na kumwelekea Mungu, wakiyatenda matendo yanayopatana na kutubu kwao."

### Mathayo 7:21-23

"[21] Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. [22] Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? [23] Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu."

### Isaya 55:7

"Mtu mbaya na aache njia yake, Na mtu asiye haki aache mawazo yake; Na amrudie Bwana, Naye atamrehemu; Na arejee kwa Mungu wetu, Naye atamsamehe kabisa."

### Luka 15:7

"Nawaambia, Vivyo hivyo kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye, kuliko kwa ajili ya wenye haki tisini na kenda ambao hawana haja ya kutubu."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

14. Soma Matendo 3:19. Ikiwa kama utatubu na ukabadilishwa, nini kitakachotokea kwenye dhambi zako? ________________ ____________________________________ ____________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

Matendo 3:19

"Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana."

# MWONGOZO WA MAJIBU

1. Elezea maana ya Toba.
   A. Ni "kukabiliana" na maamuzi mapya ya kujitoa.
   B. Nimabadiliko ya nia.
   C. Mabadiliko ya moyo ambayo yanamsababisha mtu kumgeukia Mungu, kutoka kwenye njia za zamani za mtu kwenda kwenye njia za Mungu.
   D. Mabadiliko ya mwelekeosi ukamilifu.
   E. Kufanya maamuzi ambayo yanabadilisha kabisa mwelekeo wa maisha ya mtu.
   F. Kugeuka kutoka katika njia za zamani na kwa ukamilifu kujitoa kwa Mungu na njia Zake.
   G. Mtu kumgeukia Mungu kwa kupitia Yesu Kristo.
2. Soma Luka 13:1-5. Mtu anapaswa kufanya nini ili asiangamie? Atubu.
3. Soma 2 Petro 3:9. Nini ni matamanio ya Mungu kwa watu wote? Ya kuwa wote waifikilie toba.
4. Soma Luka 16:19-31. In Luke 16:28, ni kwa nini yule tajiri alitaka mtu arudi kutoka wafu ili azungumze na ndugu zake? Ili kwamba waweze kuepuka kufika mahali hapa pa mateso.
5. Soma Luka 16:30. Nini ambacho ndugu hawa wanapaswa kukifanya ili kuepuka mahali hapa pa mateso (kuzimu)? Ni lazima watubu.
6. Read Acts 26:18. Ingawa hausemi mahususi, mstari huu unazungumza kuhusu toba. Nini kitakachotokea kwa wale watakaotubu?
   A. Macho yatafunguliwa.
   B. Watageuka kutoka gizani kwenda Nuruni.
   C. Watageuka kutoka kwenye nguvu za Shetani kwenda kwa Mungu.
   D. Watapokea msamaha wa dhambi.
   E. Watapokea urithi.
7. Soma Matendo 26:20. Katika sehemu ya mwisho ya mstari huu, mambo matatu yanatajwa ambayo wamataifa wanapaswa kuyafanya. Mambo haya matatu ni yapi?
   A. Kutubu.
   B. Kumgeukia Mungu.
   C. Kuthibitisha kutubu kwao kwa matendo yao.

8. Soma Mathayo 7:21-23. Yesu alisema kuwa watu hawa walikuwa wakifanya nini badala ya mapenzi ya Mungu? Uovu au hawakuwa na sheria.

9. Hili linakuonyesha nini kuhusu umuhimu wa toba ya kweli dhidi ya maneno matupu tunayoyasema mbele za Mungu. Wokovu unatoka moyoni, Na si maneno matupu.

10. Soma Isaya 55:7. Je waovu wanapaswa kufanya nini? Waache njia zao.

11. Ni mambo gani mawili wenye haki wanapaswa kuyafanya? Waache mawazo yao na kumrudia Bwana.

12. Je Mungu atamfanya nini mtu afanyaye mambo hayo yaliyotajwa hapo juu? Atamrehemu na Kumsamehe kabisa.

13. Soma Luka 15:7. Mwitikio wa Mbingu kwa mwenye dhambi mmoja anayetubu ukoje? Kuna furaha Mbinguni.

14. Soma Matendo 3:19. Ikiwa kama utatubu na ukabadilishwa, nini kitakachotokea kwenye dhambi zako? Dhambi zangu zitafutwa.

DARAJA 1

# SOMO 7
# KUJITOA

*Na Don Krow*

Luka 14:25-26 – Makutano wengi walipokuwa wakifuatana naye, aligeuka, akawaambia, Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, na mama yake, na mke wake, na wanawe, na ndugu zake waume na wake; naam, na hata nafsi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu.

"Makutano mengi walipokuwa wakifuatana naye, aligeuka, akawaambia…" (Luka 14:25). Kwa wakati huu katika huduma ya Yesu, kulikuwa na watu wengi ambao walimfuata Yesu. Lugha ya Kiingereza hailileti hili vizuri,lakini katika lugha ya Kiyunani, hii ni kitenzi kisicho kikamilifu. Hii ina maanisha ya kuwa kwa wakati huu, makutano wengi walianza kumfuata Yesu kwa mwendelezo na kwa kurudia. Pengine ilikuwa kwa sababu ya miujiza Yake au kwa sababu aliwalisha, haujui sababau halisi, lakini makutano wengi walikuwa Wakimfuata. Ilikuwa ni katika wakati huu ya kuwa Yesu aligeuka na kwa makusudi kabisa alisema jambo ambalo lilikuwa linaonekana kusababisha watu wengi kugeukia na kutomfuata tena.

"Kama mtu akija Kwangu [hii ina maana anayetaka kwenda na mimi, anataka kuwa name, anataka kunifuata, hili ndilo linalohitajika], naye hamchukii baba yake, na mama yake, na mke wake, na wanawe, na ndugu zake waume na wake; naam, na hata nafsi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu" (Luka 14:26). Ninapotazama hili andiko, niliwaza, Bwana, huwezi kumaanisha hilo. Neno hilo "kuchukia" lina maana gani? Inawezekana lina maana kupenda kidogo au kitu kama hicho. Nilipoanza kujifunza, hata hivyo, Niligundua yakuwa neon lina maanisha "chuki".

Yesu alitumia neon lenye nguvu sana liwezekanavyo ili kusisitiza alichokuwa akikisema. Alisema ni mpaka umchukie baba yako, mama yako, dada yako, kaka yako, hata maisha yako mwenyewe, hamuwezi kuwa wanafunzi Wake. Ninataka nikuulize kitu: Upi ni uhusiano wa karibu sana ambao unaweza kuwa nao hapa duniani? Ni mama yako na baba yako au mwenzi wako na watoto. Nini kinachotokea wakati mke wako anapokuja kinyume nawe na anakupa talaka, au mama yako na baba yako wakifa? Nani atakaa nawe basi? Itakuwa ni kaka zako na

dada zako. Yesu alisema, ni mpaka pale utakapowachukia, hamuwezi kuwa wanafunzi Wake. Anasema nini?

Yesu anazungumza kuhusu uhusiano wa karibu zaidi ambao tuna weza kuwa nao. Anahitaji kuwe na kujitoa kutoka kwako, Kujitoa ambako kutatawaliwa na Yeye. Anataka kuwa namba moja maishani mwako. Atalinganisha uhusiano alionao na wewe na uhusiano uliyo nao wa karibu sana hapa duniani. "Chuki" ni neno linalokaribiana na, neno la kufananisha, na Yesu anasema, "Uhusiano Wangu na wewe ni wa muhimu sana kiasi kwamba ninataka kuwa juu ya mambo yote ya kidunia." Kuna mtu moja unampenda zaidi ya mke wako, watoto wako, mama yako, baba yako, au dada zako na kaka zako. Je unamjua huyo mtu ni nani? Si Mungu... ni Wewe. Unajipenda zaidi kuliko uwapendavyo wale waliyo na uhusiano wa karibu zaidi na wewe.

Ni kwa nini ndoa zinavunjika? Ni kwa nini watu wanatalakiana? Kwa sababu wanajipenda wenyewe kuliko wanavyowapenda wenzi wao. "Hufanyi kama vile ambavyo ningetaka ufanye, hivyo ninakuondoa."

Yesu alisema kuna uhusiano wa ambao ninataka kuwa namba moja juu ya yote – ni maisha yako mwenyewe ya ubinafsi. Huu ni uanafunzi wa kweli. Hazungumzii kuhusus uhusiano usiyo gharimu chochote. Anatuambia tumfuate Yeye. Anataka kuwa namba moja kwenye maisha yetu.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Luka 9:57-62. Kifungu hiki kinafundisha nini kuhusus kiwango cha kujitoa katika kumfuata Yesu Kristo? ____ ______________________________ __________

2. Soma Luka 8:13-14. Ni kwa nini watu wengine wanaonekana kuanguka, au kugeuka mbali na Imani ya Kikristo? ____ ______________________________ ________________

3. Soma Ezekieli 16:8. Mungu anatumia kielelezo cha ndoa kuelezea uhusiano na watu wake. Je mtu anakuwa mali ya nani katika uhusiano huu? ______________ _________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Luka 9:57-62

"[57] Nao walipokuwa wakienda njiani, mtu mmoja alimwambia,Bwana, Nitakufuata ko kote utakakokwenda.. [58] Yesu akamwambia, Mbweha wana mapango, na ndege wa angani wana viota, lakini Mwana wa Adamu hana pa kujilaza kichwa chake. [59] Akamwambia mwingine, Nifuate. Akasema, Bwana, nipe ruhusa kwanza niende nikamzike baba yangu. [60] Yesu akamwambia Waache wafu wawazike wafu wao; bali wewe enenda ukautangaze ufalme wa Mungu. [61] Mtu mwingine pia akamwambia, Bwana, nitakufuata; lakini, nipe ruhusa kwanza nikawaage watu wa nyumbani mwangu. [62] Yesu akamwambia, Mtu aliyetia mkono wake kulima, kisha akaangalia nyuma, hafai kwa ufalme wa Mungu."

### Luka 8:13-14

"[13] Na wale penye mwamba ndio wale ambao wasikiapo hulipokea lile neno kwa furaha; nao hawana mizizi, huamini kitambo kidogo, na wakati wa kujaribiwa hujitenga.. [14] Na zilizoanguka penye miiba ni wale waliosikia, na katika kuenenda kwao husongwa na shughuli na mali, na anasa za maisha haya, wasiivishe lo lote."

### Ezekieli 16:8

"Basi,nilipopitakaribunawe,nikakutazama; tazama, wakati wako ulikuwa wakati wa upendo; nikatandika upindo wa vazi langu juu yako, nikakufunika uchi wako; naam, nalikuapia, nikafanya agano nawe, asema Bwana MUNGU, ukawa wangu."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

4. Soma 1 Wakorintho 6:19. Je wewe unamilikiw an nani?

 ______________________________

5. Soma 1 Wakorintho 6:20. Mwili wako na roho yako vinamilikiwa na nani? _______

 ___________________________________

 ____________________________

6. Soma Yakobo 4:4. Je unaweza kufanya uzinzi wa kiroho dhidi ya Mungu?

 ______________

7. Ni nini kunacho husisha uzinzi wa kiroho machoni pa Mungu? Angalia Warumi 1:25.

 ___________________________________

 ______________________________

8. Soma Yohana 2:23-25. Nini tunachoweza kujifunza kuhusu kujitoa na imani kutoka kwenye mistari hii? Ya kuwa Yesu anaitaka mioyo yetu wote (kujitoa kikamilifu).

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### 1 Wakorintho 6:19

"Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe?"

### 1 Wakorintho 6:20

"maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu, na katika roho zenu, ambavyo ni vya Mungu."

### Yakobo 4:4

"Enyi wazinzi, hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu? Basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu."

### Warumi 1:25

"Kwa maana waliibadili kweli ya Mungu kuwa uongo, wakakisujudia kiumbe na kukiabudu badala ya Muumba anayehimidiwa milele. Amina."

### Yohana 2:23-25

"[23] Hata alipokuwapo Yerusalemu kwenye sikukuu wakati wa Pasaka, watu wengi waliamini jina lake, walipoziona ishara zake alizozifanya. [24] Lakini Yesu hakujiaminisha kwao; kwa kuwa yeye aliwajua wote, [25] Na kwa sababu hakuwa na haja ya mtu kushuhudia habari za mwanadamu; kwa maana yeye mwenyewe alijua yaliyomo ndani ya mwanadamu."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

9. Soma Luka 14:28-30. Je umehesabu gharama ya kumfuata Yesu? Je unataka kumfuata? Ndiyo.

8. Soma Yohana 2:23-25. Nini tunachoweza kujifunza kuhusu kujitoa na Imani kutoka kwenye mistari hii? ____________________
______________________________________
__________________

9. Soma Luka 14:28-30. Je umehesabu gharama ya kumfuata Yesu? Je unataka kumfuata? ___________________________
______________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Luka 14:28-30

“[28] Maana ni nani katika ninyi, kama akitaka kujenga mnara, asiyeketi kwanza na kuhesabu gharama, kwamba anavyo vya kuumalizia? [29] Asije akashindwa kuumaliza baada ya kuupiga msingi, watu wote waonao wakaanza kumdhihaki, [30] Wakisema, Mtu huyu alianza kujenga, akawa hana nguvu za kumaliza”

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Luka 9:5 7-62. Kifungu hiki kinafundisha nini kuhusus kiwango cha kujitoa katika kumfuata Yesu Kristo? **Kujitoa kikamilifu.**
2. Soma Luka 8:13-14. Ni kwa nini watu wengine wanaonekana kuanguka, au kugeuka mbali na Imani ya Kikristo? **Kamwe hawajaweka mfumo wa mizizi ya Neno la Mungu. Shughuli, mali, na anasa za maisha haya huwaondoa.**
3. Soma Ezekieli 16:8. Mungu anatumia kielelezo cha ndoa kuelezea uhusiano na watu wake. Je mtu anakuwa mali ya nani katika uhusiano huu? **Ya Mungu.**
4. Soma 1 Wakorintho 6:19. Je wewe unamilikiw an nani? **Mungu.**
5. Soma 1 Wakorintho 6:20. Mwili wako na roho yako vinamilikiwa na nani? **Mungu.**
6. Soma Yakobo 4:4. Je unaweza kufanya uzinzi wa kiroho dhidi ya Mungu? **Ndiyo.**
7. Ni nini kunacho husisha uzinzi wa kiroho machoni pa Mungu? **Moyo ambao umegeuka mbali na Yeye na kuabudu sanamu (mambo ambayo umeyafanya kuwa ya muhimu zaidi kuliko Mungu). Angalia Warumi 1:25.**
8. Soma Yohana 2:23-25. Nini tunachoweza kujifunza kuhusu kujitoa na imani kutoka kwenye mistari hii? **Ya kuwa Yesu anaitaka mioyo yetu wote (kujitoa kikamilifu).**
9. Soma Luka 14:28-30. Je umehesabu gharama ya kumfuata Yesu? Je unataka kumfuata? **Ndiyo.**

# SOMO 8
# UBATIZO WA MAJI

*Na Don Krow*

**Swali:** "Ninahitaji kujua kama ili uende mbinguni ni lazima ubatizwe. Ninampenda Mungu na nilibatizwa nilipokuwa na umri wa miaka saba. Sasa nina umri wa miaka kumi na nane, na mtu kutoka kwenye kanisa lisilo la kidhehebu akaniambia ya kuwa hakuna anayeweza kuokolewa na kubatizwa katika umri mdogo kama huo. Pia walisema ya kuwa ni lazima ubatizwe ili uende mbinguni, lakini familia yangu ya Kibaptisti imesema ya kuwa hauhitaji kubatizwa. Mimi ninataka tu kwenda Mbinguni. Ninaishi kwa ajili ya Mungu kwa kila jinsi ambayo ninaweza kuishi, Lakini ninahitaji kujua kama ni lazima nibatizwe tena sasa ya kuwa niko katika umri wa kuweza kubatizwa. Tafadhali nisaidie kwa haraka iwezekanavyo. Mungu akubariki na ahsante."

**Jibu:** Wokovu na msamaha wa dhambi huja bure kama zawadi kwa kupitia imani katika Kristo Yesu. Matendo 10:43 inasema: *"Hao manabii wote Humshuhudia, ya kwamba kwa Jina Lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi." (Tafsiri ya New International Version)*. Wokovu huja kupitia imani; yaani, kuamini na kutumaini katika Yesu na damu yake iliyomwagika ili ikupe wewe msimamo sahihi mbele za Mungu. Katika Matendo 10:44-48, Waliyoamini walipewa Roho Mtakatifu (ikithibitisha wokovu wao) kabla hawajabatizwa.

Hata ingawa hili ni kweli, katika nyakati nyengine inaonekana kuwa msamaha wa dhambi ulitokea wakati wa ubatizo (Matendo 2:38). Hii ni kwa sababu ubatizo ni kielelezo, au kitendo, cha Imani ambacho kilifanyika wakati ambapo mtu alipomgeukia Yesu katika toba na imani (Marko 16:16 anasema, *"Yeye aaminiye na kubatizwa ataokoka; lakini yule asiyeamini atahukumiwa"*). Ilikuwa pia ni njia ya kumwita Bwana kwa ajili ya dhamira safi (Matendo 22:16 na 1 Pet. 3:21).

Ikiwa kweli kutoka moyoni mwako ulimgeukia Yesu katika umri wa miaka saba na ukabatizwa, Mungu anaikubali imani yako kama ya mtoto. Ubatizo unayo mahitaji yake. Hitaji moja ni toba. Je ulipata badiliko la moyo na badiliko la nia ambalo lilitokana na kugeuka kwako kutoka kwenye dhambi kumuelekea Yesu na msamaha Wake (Matendo 2:38, 20:21, na 17:30)? Je ulitumia Imani katika Yesu kama Bwana na Mwokozi wako (Marko 16:16, Yohana 3:16, na

Warumi. 10:9-10)? Ikiwa kama hapana, basi mgeukie Yesu sasa, tubu kutoka kwenye dhambi zako, Geukia kwenye neema yake ya kukusamehe, na wekea mhuri uamuzi huo wa kumfuata Yeye kwa kupitia ubatizo wa maji.

**Ubatizo ni kitendo kinachoonyesha Imani ya mtu katika Yesu.** Pasipo imani hiyo, kitendo hicho hakimaanishi kitu. Watu ambao wamemgeukia Yesu kama Bwana na Mwokozi walikuwa tayari kuionyesha imani hiyo na kwa uwazi kumkiri Yesu katika njia hii ya wazi mbele za watu. Watu wanaosema "hapana" Kwenye amri ya Yesu wanaonyesha kwa kiwango fulani imani iliyokufa. Imani imekufa pale watu wanapokuwa hawako tayari kuionyesha (Yakobo 2:18-19). **Imani pekee yake inaokoa, lakini Imani inayookoa haiko pekee yake.** Mara zote iko tayari kijionyesha yenyewe. **Ubatizo ilikuwa ni njia ya kuonyesha imani hiyo. Ubatizo sicho kinachookoa; ni Yesu. Maji hayasafishi dhambi; ni damu ya Yesu.** Lakini imani ndiyo inayoachilia damu Yake kwako, na mara nyengine imani hiyo iliyoonyeshwa wakati mtu alipokuwa akibatizwa (Matendo 22:16). Swali ni, je umetubu? Unamwamini Yeye (Yesu)? Ikiwa ni hivyo, ni kwa nini unakawia – amka na ubatizwe!

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Ni swali gani ambalo kijana huyu analiuliza? ______________________________
______________________________

2. Kufuatana na Matendo 10:43, wokovu unakujaje kwetu? ______________________
______________________________

3. Ubatizo ni kielelezo cha imani ambacho kwa kawaida hufanyika wakati wa wokovu. Je Matendo 2:38 inaelezeaje kweli hii? _____
______________________________

4. Marko 16:16 anaelezeaje kweli hii? ______
______________________________

5. Ubatizo ni jinsi ya kumuita Bwana. Matendo 22:16 inaelezeaje kweli hii? _____
______________________________
______________________________

6. Ubatizo ni njia ya kumuita Bwana kwa ajili ya dhamira safi. Je 1 Petro 3:21 anathibitisha kweli hii? ________________
______________________________

7. Mahitaji kwa ajili ya ubatizo ni yapi, kufuatana na Matendo 2:38? ____________
______________________________

8. Mahitaji kwa ajili ya ubatizo ni yapi, kufuatana na Marko 16:16? _____________
______________________________

9. Je mtoto mchanga anaweza kutubu? _____
______________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Matendo 10:43

"Huyo manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi"

### Matendo 2:38

"Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."

### Marko 16:16

"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa."

### Matendo 22:16

"Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake."

### 1 Petro 3:21

"Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo."

### Matendo 10:44-48

"[44] Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile neno. [45] Na wale waliotahiriwa, walioamini, wakashangaa, watu wote waliokuja pamoja na Petro, kwa sababu Mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu.. [46] Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha, na kumwadhimisha Mungu. Ndipo Petro akajibu, [47] Ni nani awezaye kuzuia maji, hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi? [48]

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

10. Je mtoto mchanga anaweza kuamni?

_________________________________

_______________________

11. Soma Matendo 10:43-48. Hatua inayofuata ni ipi, baada ya Imani katika Kristo, ambayo anayeamini anapaswa kuichukua?

_________________________________

________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

Akaamuru wabatizwe kwa Jina lake Yesu Kristo. Ndipo wakamsihi azidi kukaa siku kadha wa kadha."

# MWONGOZO WA MAJIBU

1. Ni swali gani ambalo kijana huyu analiuliza? **Ikiwa kama anahitaji kubatizwa ili aende mbinguni.**

2. Kufuatana na Matendo 10:43, wokovu unakujaje kwetu? **Bure, kama kipawa kupitia Imani through faith in Jesus Christ.**

3. Ubatizo ni kielelezo cha imani ambacho kwa kawaida hufanyika wakati wa wokovu. Je Matendo 2:38 inaelezeaje kweli hii? **Petro akawaambia "tubuni na mkabatizwe."**

4. Marko 16:16 anaelezeaje kweli hii? **Yesu alisema, "Yeye aaminiye na kubatizwa ataokoka," iki maanisha ya kuwa inaweza kutokea kwa wakati mmoja.**

5. Ubatizo ni jinsi ya kumuita Bwana. Matendo 22:16 inaelezeaje kweli hii? **Andiko hili linasema ya kuwa mtu anapoliitia jina la Bwana, dhambi zao zitasafishwa. Inaonekana ya kuwa kuliitia jina la Bwana kunaweza kuwa kwa sauti inayosikika (Luka 18:13) au kupitia tendo la kubatizwa, kama inavyoonekana kuwa katika andiko hili.**

6. Ubatizo ni njia ya kumuita Bwana kwa ajili ya dhamira safi. Je 1 Petro 3:21 anathibitisha kweli hii? **Ndiyo.**

7. Mahitaji kwa ajili ya ubatizo ni yapi, kufuatana na Matendo 2:38? **Toba.**

8. Mahitaji kwa ajili ya ubatizo ni yapi, kufuatana na Marko 16:16? **Mtu ni lazima aamini.**

9. Je mtoto mchanga anaweza kutubu? **Hapana.**

10. Je mtoto mchanga anaweza kuamni? **Hapana.**

11. Soma Matendo 10:43-48. Hatua inayofuata ni ipi, baada ya Imani katika Kristo, ambayo anayeamini anapaswa kuichukua? **Ubatizo wa maji.**

DARAJA 1

# SOMO 9

# UTAMBULISHO KATIKA KRISTO (Sehemu 1)

*Na Andrew Wommack*

Wakorintho 5:17 inasema, “Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya.” Usemi “katika Kristo” ni neon ambalo limetumika zaidi ya mara katika Agano Jipya, mar azote likimaanisha muungaiko muhimu wa kimahusiano pamoja na Mungu. Mara hilo linapokuwa limefanyika, unafanyika kiumbe kipya. Baadhi ya tafsiri zinasema “uumbaji mpya”.

Hili linapelekea kwenye swala nyeti ambalo ninaamini ya kuwa ni swala la muhimu sana kukuwezesha kuelewa utambulisho wako katika Kristo: Halikufanyika kwenye ulimwengu wa mwili, Wala haizungumzii kuhusu mwili wako, kwa kusema ya kuwa unabadilika kabisa, ya kuwa mwonekano wako unabadilika. Ikiwa kama mtu alikuwa ni mnene kabla hajaokoka, bado ataendelea kuwa mnene hata baadaye, mpaka pale watakapoanza utaratibu wa kupunguza unene. Pia haizungumzii sehemu yako ya akili au hisia – kile kitu ambacho watu wengi huchukulia kuwa ndiyo walivyo “kiuhalisi”. Ikiwa kama hukuwa mwerevu sana kabla hujaokoka, wala hautakuwa mwerevu zaidi baada ya kuokoka, lakini bado utakuwa na kumbu kumbu nyingi na mawazo.

Kuna sehemu ya tatu, na kufuatana na andiko hili, kwa mchakato wa kupunguza kwa kutoa, inapaswa kuwa ni sehemu yetu ambayo inabadilika – mtu wetu wa ndani. Andiko ambalo linathibitisha hili ni 1 Wathesalonike 5:23 Pale ambapo Paulo anawaombea Wathethalonike, “Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo.” Sehemu hii inaonyesha ya kuwa tuna roho, nafsi na mwili. Sehemu ya mwili ni jambo la kawaida. Ni sehemu yetu ambayo inaonekana, mtu wetu wa nje. Sisi sote tunatambua ya kuwa kuna sehemu nyengine zaidi ya hapo; hisia zetu, sehemu yetu ya ufahamu; ambayo Maandiko inaiita nafsi. Tunafahamu ya kuwa ingawa mtu anaweza asikuguse kimwili, wanaweza kukugusa kwa maneno yao kwa jinsi ya chanya au hasi. Watu wengi wanaufahamu kuhusu ile ya kimwili na sehemu ya nafsi, lakini kufuatana na maandiko, kuna sehemu nyengine, ambayo ni roho..

Roho ni sehemu yetu ambayo inabadilishwa na inakuwa mpya baada ya wokovu. Ukweli ni kuwa ndiyo sehemu inyoleta uzima. Hilo linaonyesha ya kuwa ni roho anayepumzia uzima kwenye miili yetu. Ndipo uzima wetu unakotokea. Katika Mwanzo 2 Mungu alipomuumba Adamu na Hawa, mwili wa Adamu ulikuwa umekamilika, lakini baadaye Mungu akampulizia pumzi ya uhai. Neno hili "pulizia pumzi" Katika Kiebrania cha Agano la Kale lilikuwa ni neno lile lile ambalo tunalitumika kwa ajili ya kupulizia pumzi, na linatafsiriwa: "roho" katika maeneo mengine. Mungu aliumba mwili na nafsi ya Adamu, lakini baadaye akampulizia pumzi ya uhai ndani yake na akawa nafsi iliyo hai. Roho ni ile sehemu yetu inayotupa uzima.

Kabla ya wokovu, kabla ya mtu hajafanya uamuzi wa kujitoa maisha yake kikamilifu na Bwana kuingia ndani mwake, roho ndani yake ilikuwa umekufa. Waefeso 2:1 inasema, "Nanyi mlihuishwa [mlifanywa kuwa hai] ambao mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi". Tunajua ya kuwa tulikuwa hai kabla ya kuzaliwa mara ya pili, lakini neno "wafu" inaongea kuhusu hali ya kiroho. Mauti katika Biblia haimaanishi kukoma kuendelea kuwepo, kama ambavyo baadhi ya watu leo wanavyolifikiria. Ina maanisha haswa "kutenganishwa". Wakati mtu anapokufa kimwili, hakomi kuendelea kuwepo. Biblia inafundisha ya kuwa wanakwenda mara tu kwenye uwepo wa Mungu au uwepo wa kuzimu. Nafsi na roho vinaendelea kuishi, lakini kuna kutenganishwa na mwili, ambao unakufa na kuoza.

Wakati Mwanzo 2:17 inasema "Siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika." Haikumaanisha wangekufa kimwili lakini kiroho, ya kuwa wangetenganishwa na Mungu. Roho, sehemu ambayo Mungu alipulizia pumzi ndani mwetu, ambayo kwa ukweli inatoa uzima na kutuhamasisha, tukatengwa kutoka kwenye uzima wa kimungu … Maisha yake matakatifu na makamilifu … kile ambacho Biblia imekiita "zoe" uzima au "uzima katika hali ya uhakika au katika utele". Mwanadamu akaanza kuporomoka. Aliendelea kutenda, lakini alikuwa akitenda kwa kujisimamia mwenyewe, akiwa ametengwa kutoka kwa Mungu. Hilo ndilo ambalo hakika linasababisha matatizo yote maishani mwetu… misongo yetu yote ya kihisia.

Mtu anapokuja kwa Bwana, anapokea roho mpya na ana zaliwa mara ya pili, ambalo ndilo neno Yesu alilolitumia katika Yohana 3:5. Kwa jinsi hiyo hiyo mwanadamu anazaliwa kimwili na roho, nafsi na mwili, anapookoka, anampokea Roho wa Kristo. Wagalatia 4:6 inasema, "Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba." Mungu kabisa huweka Roho wake ndani yetu, na sasa tunakuwa na ubora mpya wa maisha, utambulisho mpya, na tunakuwa watu wapya kabisa ndani ya roho zetu.

Maisha mengine yaliyobaki ya Ukristo ni kujifunza kutoka kwenye nafsi yako, ulimwengu wa kiakili ambao umechukua nafasi katika roho yako. Ukweli ni kuwa theluthi moja ya wokovu wako unakamilika unapompokea Yesu Kristo kama Bwana wako. Roho yako inabadilishwa kabisa. Ni roho ile ile utakayokuwa nayo katika umilele wote. Tayari ina upendo, furaha, amani, na imejawa na uwepo wa Mungu. Hakuna kukosa au kutokutosheka katika roho yako, lakini ni

lazima ulione hilo, ambayo ndiyo sababu kwa nini kujifunza Neno la Mungu ni muhimu sana katika maisha ya Ukristo. Wewe ni mtu mpya kabisa, lakini ni mpaka utakapopata maarifa, hutabadilika. Ushindi katika maisha ya Kikristo unakuja pale unapoweza kulitazama Neno, ambalo ni Roho na uzima, tazama wewe ni nani, tazama kile ambacho Mungu amekifanya, na uanze kukiamini.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma 2 Wakorintho 5:17. Ikiwa yeyote yumo ndani ya Kristo, wao ni nini? ______
________________________________________
__________________________________

2. Soma 2 Wakorintho 5:17. Nini kimetokea kwenye mambo ya kale? ______________
________________________________________
________________________

3. Soma 2 Wakorintho 5:17. Ni vitu gani vimefanyika kuwa vipya? ______________
________________________________________
________________________

4. Soma Waefeso 2:1. Hali yako ilikuwaje kabla hujaokoka, au kufanywa hai? ______
________________________________________
______________________

5. Soma Waefeso 2:2. Kama mtu usiyeamini, ulienendaje, au kuishi? ______________
________________________________________
______________________

6. Soma Waefeso 2:3-5. Mungu ni mwingi wa nini? ______________________________
________________________________________
______________________________

7. Soma Waefeso 2:4. Kwa nini Mungu ana rehema sana?
__________________________________

8. Soma Waefeso 2:5. Mungu alitufanyia nini wakati bado tulipokuwa na makosa na dhambi? ______________________________
________________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### 2 Wakorintho 5:17

"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya."

### Waefeso 2:1

"Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu;."

### Waefeso 2:2

"ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi"

### Waefeso 2:3-5

"[3] ambao zamani, sisi sote nasi tulienenda kati yao, katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili na ya nia, tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama na hao wengine [4] Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda, [5] Hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema;)."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

9. Soma Waefeso 2:5. Mungu alituokoaje? ____________________

10. Soma 1 Wakorintho 6:9-10. Unaweza kujifananisha na yoyote katika maelezo yaliyoko kwenye orodha hii? ____________________

11. Soma 1 Wakorintho 6:11. Je neno "walikuwa" liko katika wakati uliyopita, uliyopo, au hali ya mbeleni? ____________________

12. Soma 1 Wakorintho 6:11. "Ulipozaliwa mara ya pili," Ni mambo gani matatu yaliyokutokea? ____________________

13. Soma 1 Wakorintho 6:11. Je hali hii ni ya wakati uliyopita, uliyopo, au hali ya siku zijazo? ____________________

14. Soma 1 Wakorintho 6:17. "Yeye aliyeunganishwa na Bwana ni __________ pamoja Naye."

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### 1 Wakorintho 6:9-10

"[9] Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu? Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, [10] wala wevi, wala watamanio, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi."

### 1 Wakorintho 6:11

"Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu."

### 1 Wakorintho 6:17

"Lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja naye."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma 2 Waorintho 5:17. Ikiwa yeyote yumo ndani ya Kristo, yeye ni nini? **Kiumbe kipya.**
2. Soma 2 Waorintho 5:17. Nini kimetokea kwenye mambo ya kale? **Yameondoka.**
3. Soma 2 Waorintho 5:17. Ni vitu gani vimefanyika kuwa vipya? **Mambo yote.**
4. Soma Waefeso 2:1. Hali yako ilikuwaje kabla hujaokoka, au kufanywa hai? **Nilikuwa nimekufa katika makosa na dhambi.**
5. Soma Waefeso 2:2. Kama mtu usiyeamini, ulienendaje, au kuishi? **Nilifuata njia za dunia, Nilimtii Shetani (mfalme wa nguvu za anga), na niliishi katika roho ya kutokutii.**
6. Soma Waefeso 2:3-5. Mungu ni mwingi wa nini? **Rehema.**
7. Soma Waefeso 2:4. Kwa nini Mungu ana rehema sana? **Kwa sababu ya upendo Wake mkuu kwetu.**
8. Soma Waefeso 2:5. Mungu alitufanyia nini wakati bado tulipokuwa na makosa na dhambi? **Alitufanya hai pamoja na Kristo.**
9. Soma Waefeso 2:5. Mungu alituokoaje? **Kwa Neema Yake.**
10. Soma 1 Wakorintho 6:9-10. Unaweza kujifananisha na yoyote katika maelezo yaliyoko kwenye orodha hii? **Ndiyo.**
11. Soma 1 Wakorintho 6:11. Je neno "walikuwa" liko katika wakati uliyopita, uliyopo, au hali ya mbeleni? **Uliyopita.**
12. Soma 1 Wakorintho 6:11. "Ulipozaliwa mara ya pili," Ni mambo gani matatu yaliyokutokea? **Ulisafishwa, ulifanywa mtakatifu, na ukahesabiwa haki (ilifanywa kuwa mwenye haki) mbele za Mungu.**
13. Soma 1 Wakorintho 6:11. Je hali hii ni ya wakati uliyopita, uliyopo, au hali ya siku zijazo? **Wakati Uliyopo.**
14. Soma 1 Wakorintho 6:17. "Yeye aliyeunganishwa na Bwana ni **roho moja** pamoja Naye."

DARAJA 1

# SOMO 10
# UTAMBULISHO KATIKA KRISTO (Sehemu 2)

*Na Andrew Wommack*

Somo letu lililopita, tulijadili ili maanisha nini kuzaliwa mara ya pili, ya kuwa katika roho zetu, mioyo yetu inabadilishwa. Tulitumia 2 Wakorintho 5:17, ambayo inasema, "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya." Tulianza kuona ya kuwa tunapozaliwa mara ya pili, mabadiliko makamilifu yamefanyika katika roho zetu, na njia pekee ya kujua nini kimetokea katika roho zetu ni kwa kupitia Neno la Mungu. Hatuwezi kuliona hilo kupitia vitu vya nje, na hatuwezi kuliona kwa kupitia hisia zetu, kwa sababu hilo liko kwenye ulimwengu wa nafsi. Lakini katika sehemu yetu ya roho, kuna mabadiliko makamilifu.

Ngoja nitumie maandiko machache ambayo yanaonyesha mambo ambayo yamefanyika pale mtu alipompokea Yesu maishani mwake. Waefeso 4:24 inasema, "Mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli." Mtu anapozaliwa mara ya pili, roho zao zinafanyika kuwa zenye haki na takatifu kweli. Biblia inazungumza kuhusu aina mbili za haki.

Kuna haki ambayo inatokana na matendo yako mwenyewe, na unatakiwa kuidumisha aina hiyo ya haki katika mahusiano na watu wengine. Ikiwa kama hutaishi sawa na kufanya yaliyo sawa, bosi wako anaweza kukufukuza au mwenzi wako anaweza kukupa talaka; hivyo unahitaji kuwa na haki yako mwenyewe. Mungu, hata hivyo, hakupokei wewe katika msingi wa haki ya nje. Mungu kabisa alikupa wewe haki Yake.

Katika 2 Wakorintho 5:21 Inasema ya kuwa Mungu Baba alimfanya Mwana kufanyika dhambi kwa ajili yetu ili tufanyike haki ya Mungu ndani Yake. Hivyo kuna haki ambayo inakwenda mbali zaidi ya haki yetu ya nje na iko katika msingi wa kile ambacho Mungu alikifanya kwa ajili yetu. Tumepokea haki ya Mungu kwa imani katika Kristo. Tuliumbwa katika haki na utakatifu wa kweli. Hatukui katika haki hiyo; sisi tayari ni wenye haki. Maana rahisi ni kuwa tayari tuko katika msismamo sahihi pamoja na Mungu.

Mungu anapendezwa nasi katika msingi wa Kristo, na si katika kitu kingine chochote. Roho zetu ziko pale ambapo mabadiliko yalifanyika. Tayari tumeumbwa katika haki na utakatifu wa kweli na ni viumbe wapya kabisa. Waefeso 2:10 inasema, "Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema..." Katika roho zetu, sisi tu wakamilifu na watimilifu. Hakuna dhambi au kupungukiwa. Waefeso 1:13 inasema, "…Tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu."

Baadhi yenu mnaweza kufikiri, Vyema, wakati mara ya kwanza nilipomwamini Bwana, Niliamini ya kuwa nilisamehewa kabisa na kutakaswa, na kila kitu kilikuwa sawa. Lakini toka wakati huo, Nimetenda dhambi, Nimemkosea Mungu tena. Ikiwa kama ulifanya, ulishindwa katika matendo yako na kwenye akili yako na sehemu yako ya hisia, lakini roho yako haikutenda dhambi. Ilifungwa kama vile ambavyo mwanamke awekavyo tunda kwenye gudulia na halafu anaweka mafuta ya taa juu yake na kufunga kiasi kwamba hewa haitaingia na kuzuia uchafu wote usiingie. Mungu alikufunga, kiasi kuwa ulipozaliwa mara ya pili, ulipokea roho mpya, na dhambi haipenyezi kuingia kwenye roho yako. Una utambulisho mpya. Kwa wewe kuwa na uhusiano na Mungu, unatakiwa uwe na ushirika Naye na kumuabudu Yeye, Ikitegemeana na wewe ni nani katika roho yako na siyo mwilini mwako.

Haya hakika nimabadiliko makubwa katika maisha ya Kikristo, kuwa mtu inabidi kubadilisha utambulisho wake. Unapaswa kujihusisha na Mungu siyo katika kile ambacho unakifanya katika ulimwengu wa mwili, siyo kile unachokifikiria kwenye akili yako, bali ni kwa wewe ulivyo rohoni, katika kile ambacho Amekufanyia. Hiyo ni kazi iliyokamilika, kitu ambacho haki pandi na kushuka (kubadilika badilika). Uliumbwa katika haki na utakatifu wa kweli. Hiyo ndiyo sehemu yako ya roho, na kuwa na ushirika na Mungu, Unapaswa kumuabudu Yeye katika roho na kweli. Unapaswa kusimama katika utambulisho huu wa wewe ni nani katika Kristo.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma 1 Wakorintho 6:17. Njia pekee tunavyoweza kujua ya kuwa mabadiliko makamilifu yamefanyika rohoni mwetu ni kwa Neno la Mungu. Mstari huu unasema nini kimetutokea? ____________________
____________________________________

2. Soma Waefeso 3:17. Kristo sasa anakaa wapi? ______________________________
____________________________________
________

3. Soma Waefeso 3:17. Hili linatokeaje? ____
____________________________________
___________________________________

4. Soma 1 Yohana 5:12. Ni nani ni lazima tuwe naye ili tuwe na wokovu?
_____________________

5. Soma Wakolosai 1:26-27. Ipi ni siri ambayo ilifichwa kutoka zamani sana na vizazi vingi lakini sasa imejulikana? __________
______________________________

6. Soma Waefeso 4:23-24. Nini kiliumbwa katika haki na utakatifu wa kweli? _______
____________________________________
_______________________________

7. Soma 2 Wakorintho 5:21. Ni haki ya nani tunayoimiliki? ___________________

8. Soma Waefeso 1:4. Nini ni msimamo wa anayeamini mbele za Mungu?
_______________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### 1 Wakorintho 6:17

"Lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja naye."

### Waefeso 3:17

"Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo."

### 1 Yohana 5:12

"Yeye aliye naye Mwana, anao huo uzima; asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima."

### Wakolosai 1:26-27

"[26] Siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake; [27] Ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu."

### Waefeso 4:23-24

"[23] Na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu;; [24] mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli."

### 2 Wakorintho 5:21

"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye."

### Waefeso 1:4

"According as he hath chosen us in him before the foundation of the world, that we should be holy and without blame before him in love."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

9. Soma Waefeso 1:6. Tulikubaliwa kwa jinsi gani? ______________________________ ___________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Waefeso 1:6

"Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha katika huyo Mpendwa."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma 1 Wakorintho 6:17. Njia pekee tunavyoweza kujua ya kuwa mabadiliko makamilifu yamefanyika rohoni mwetu ni kwa Neno la Mungu. Mstari huu unasema nini kimetutokea? **Roho zetu zimeunganishwa kwa Bwana.**
2. Soma Waefeso 3:17. Kristo sasa anakaa wapi? **Mioyoni mwetu.**
3. Soma Waefeso 3:17. Hili linatokeaje? **Kwa imani.**
4. Soma 1 Yohana 5:12. Ni nani ni lazima tuwe naye ili tuwe na wokovu? **Mwana (Yesu Kristo).**
5. Soma Wakolosai 1:26-27. Ipi ni siri ambayo ilifichwa kutoka zamani sana na vizazi vingi lakini sasa imejulikana? **Kristo ndani yetu, tumaini la utukufu.**
6. Soma Waefeso 4:23-24. Nini kiliumbwa katika haki na utakatifu wa kweli? **Mtu wetu mpya (roho zetu – zilizo zaliwa mara ya pili).**
7. Soma 2 Wakorintho 5:21. Ni haki ya nani tunayoimiliki? **Haki ya Mungu katika Kristo Yesu.**
8. Soma Waefeso 1:4. Nini ni msimamo wa anayeamini mbele za Mungu? **Mtakatifu na pasipo lawama.**
9. Soma Waefeso 1:6. Tulikubaliwa kwa jinsi gani? **Katika Mpendwa (Yesu Kristo).**

# SOMO 11
# NINI KINACHOTOKEA PALE MKRISTO ANAPOTENDA DHAMBI?

*Na Don Krow*

Leo tunataka kuangalia somo la "Nini kinachotokea pale mkristo anapotenda dhambi?" Biblia inatuambia katika 1 Yohana 1:8-9, *"Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu.Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."* Kama Wakristo, hatimaye tutajikwaa na hatimaye tutatenda dhambi. Nini kinachotufanya kuwa tofauti na vile ambavyo tulivyokuwa kabla ya kubadilishwa ni kuwa sasa tuna asili mpya. Inatuhuzunisha kutenda dhambi, hatutaki kutenda dhambi; tunataka kuishi maisha ya haki lakini nini kinachotokea pale tunapotenda dhambi? Je tunahitaji kuokoka tena? Ndicho hicho Biblia inachokifundisha? Katika swala hili, hatuna usalama, na katika hali fulani tunakuwa katika hali mbaya kuliko ulimwengu. Angalau ulimwengu hauteswi na dhamira ya dhambi. Kama watu tunaoamini, dhambi haipaswi kuwa ndiyo mtazamo wetu. Waebrania 10:2 inasema kuwa kupitia dhabihu ya Yesu, aliyeamini hapaswi kuwa na dhamira ya dhambi tena. Kwa maneno mengine, dhambi haipaswi kuwa ndiyo mtazamo wa maisha yetu. Mungu anapaswa kuwa ndiyo mtazamo wa maisha yetu.

Warumi 4:2 inasema, *"Kwa maana ikiwa Ibrahimu alihesabiwa haki[alitangazwa mwenye haki] kwa ajili ya matendo yake, analo la kujisifia; lakini si mbele za Mungu"* Ikiwa kama wokovu ulikuwa katika msingi wa sifa zetu, mambo tunayoyafanya, basi tungeweza kujisifu. Tunaweza kusema,"Bwana, Hakika ninashukuru kwa kile ulichokifanya msalabani, lakini kumbuka mambo niliyoyafanya!" Hivyo katika umilele wote, tutakwenda kumpiga piga Yesu mgongoni na kujipiga piga wenyewe mgogoni kwa mambo ambayo tumeyafanya. Hapana! Mungu ameutengeneza wokovu kwa jinsi ambayo hakutakuwa na kujigamba au kujitukuza kwa upande wa mwanadamu. Utukufu pekee na kujisifu viatakuwa ni katika Bwana Yesu Kristo (Warumi. 3:27). Karama ya uzima wa milele hakika ni karama, na haiwezi kupatikana kwa kuifanyia kazi (Warumi. 6:23).

Warumi 4:2 inasema ya kiwa kama Ibrahamu alihesabiwa haki kwa matendo yake mwenyewe, angekuwa na sababu za kujigamba, lakini hilo silo lililotokea. Maandiko yanasemaje kuhusus mtu anaokokaje? Kwa matendo yake mwenyewe? Kwa matendo yake mwenyewe? Kwa vitu anavyovifanya? Ibrahimu alihesabiwaje kuwa mwenye haki, au kutangazwa mwenye haki? Je ilikuwa kupitia vitu alivyovifanya au ambavyo hakuvifanya, au ilikuwa ya kuwa aliamini tu, akatumaini na kumtegemea Mungu kwa kupitia imani? Biblia inasema katika Warumi 4:3, *"Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki."*

Nini kinachonishikilia kwenye nafasi na kinanizuia nisiangamie, hata ingawa kuna nyakati nilipo shindwa na kutenda dhambi? Ni kuwa Yesu alizibeba dhambi zangu zote msalabani, na kwa kupitia imani katika Yeye (si kwa kazi zangu mwenyewe) Ninahesabiwa haki (nimefanywa mwenye haki mbele za Mungu).

Warumi 4:6 inasema, *"Kama vile Daudi aunenavyo uheri wake mtu yule ambaye Mungu amhesabia kuwa na haki pasipo matendo."* Daudi wa Agano la Kale anasema kutakuwa na siku kwa kupitia Agano Jipya wakati Mungu atakapohesabu haki, msimamo sahihi, pasipo mwanadamu kufanyia kazi. Halafu akasema katika mstari wa 7, *"Heri waliosamehewa makosa yao, Na waliositiriwa dhambi zao"* Hii ndiyo inakamilisha: *"Heri mtu yule ambaye Bwana hamhesabii dhambi"* (Rum. 4:8). Haisemi kuwa anaweza asifanye, mara nyengine atafanya na mara nyengine hatafanya. Inasema,*"Heri mtu yule ambaye Bwana hamhesabii dhambi."* Katika Kiyunani hicho ndicho kinachoitwa mkazo hasi. Inamaanisha kamwe hataweka dhambi kwenye hesabu yetu. Hizi ndizo habari njema za Agano Jipya. Waebrania 10:16 inasema, *"Nitatia sheria zangu mioyoni mwao, [ndani ya mioyo yao] na katika nia zao [juu ya nia zao] nitaziandika"*, na sehemu ya makubaliano hayo ni kuwa Mungu anasema hivi katika mstari wa 17: *"Na dhambi zao na uasi wao sitaukumbuka tena kabisa."*

Nini kinachokushikilia kwenye nafasi, katika haki na katika msimamo sahihi, hata pale unapotenda dhambi na huna muda wa kukiri dhambi yako? Ni Imani yako katika Yesu Kristo. Jina lake ni Yesu, na Anaokoa watu kutoka kwenye dhambi zao (Math. 1:21).

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Warumi 4:5. Mungu huhesabia haki (anafanya mtu kuwa na haki) watu ambao _______________.

2. Soma Warumi 4:2-3. Mungu aliweka kitu kwenye akaunti ya Ibrahimu (alipoamini) ambacho hakuwa nacho kabla. Kilikuwa ni nini? ________________________________

3. Soma Warumi 4:22-24. Ikiwa kama tutaamin kama Ibrahimu alivyofanya, Nini ambacho Mungu ataweka kwenye accounti? ____________________________
_____________________________________

4. Soma Warumi 4:6. Mungu anaweka haki (au msimamo sahiahi) kwenye akaunti ya mtu:
   A. kufuatana na matendo yao.
   B. mbali na matendo yao.
   C. kufuatana na wao ni wazuri kiasi gani.

5. Soma Waebrania 10:14. Ni kwa muda gani waumini wanakamilishwa mbele za Mungu? _____________

6. Soma Warumi 5:17. Haki inapokelewa:
   A. kwa kuifanyia kazi.
   B. kama karama.
   C. kupitia kufanya kazi kwa ajili yake.

7. Neno “karama” lina maanisha nini? ______
_____________________________________

8. Kumwamini Yesu awe mwokozi wako binafsi, ni lazima Umwamini akuchukue safari yote kwenda
   A. kanisani
   B. mbinguni
   C. Urusi

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Warumi 4:5

“Lakini kwa mtu asiyefanya kazi, bali anamwamini yeye ambaye amhesabia haki asiyekuwa mtauwa, imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki.”

### Warumi 4:2-3

“[2] Kwa maana ikiwa Ibrahimu alihesabiwa haki kwa ajili ya matendo yake, analo la kujisifia; lakini si mbele za Mungu. [3] Maana maandiko yasemaje? Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki..”

### Warumi 4:22-24

“[22] Kwa hiyo ilihesabiwa kwake kuwa ni haki. [23] Walakini haikuandikwa kwa ajili yake tu kwamba ilihesabiwa kwake [24] bali na kwa ajili yetu sisi mtakaohesabiwa vivyo hivyo, sisi tunaomwamini yeye aliyemfufua Yesu Bwana wetu katika wafu.”

### Warumi 4:6

“Kama vile Daudi aunenavyo uheri wake mtu yule ambaye Mungu amhesabia kuwa na haki pasipo matendo.”

### Waebrania 10:14

“Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.”

### Warumi 5:17

“Kwa maana ikiwa kwa kukosa mtu mmoja mauti ilitawala kwa sababu ya yule mmoja, zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo.”

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Warumi 4:5. Mungu anahesabia watu haki (anawafanya kuwa wenye haki) watu ambao **si wa kimungu**.

2. Soma Warumi 4:2-3. Mungu aliweka kitu kwenye akaunti ya Ibrahimu (pale alipoamini) ambacho hakuwa nacho kabla. Kilikuwa ni nini? **Haki, au msimamo sahihi, na Mungu.**

3. Soma Warumi 4:22-24. Ikiwa kama Ibrahimu aliamini, Mungu ataweka nini kwenye akaunti zetu? **Haki, au msimamo sahihi, pamoja na Mungu.**

4. Soma Warumi 4:6. Mungu anaweka haki (au msimamo sahihi) kwenye akaunti ya mtu: **B. mbali na matendo yao.**

5. Soma Waebrania 10:14. Ni kwa muda gani wanaoamini wanakamilishwa mbele za Mungu? **Milele**.

6. Soma Warumi 5:17. Haki inapokelewa: **B. kama kipawa.**

7. Neno "karama" lina maanisha nini? **Kitu ambacho tumepewa bure, Pasipo gharama kwa mtu anayepokea.**

8. Kumuamini Yesu awe Mwokozi wako binafsi, ni lazima umuamini Yeye akupeleke safari yote mpaka: **B. mbinguni.**

# SOMO 12
# UAMINIFU WA NENO LA MUNGU

*Na Andrew Wommack*

Marko 4 ni sura ya ajabu sana kuhusu uaminifu ambao Neno la Mungu linao – nguvu, tabia, na Imani ndani yake. Kulikuwa na angalau mifano kumi iliyofundishwa katika kipindi cha siku hii moja. Unatakiwa kufananisha Marko 4 na Mathayo 13 na Luka 8 ili kuja na hilo. Kulikuwa na mifano kadhaa, moja ambao ulikuwa kuhusu mpanzi akipanda mbegu. Katika Marko 4:26 inasema, *"Akasema, Ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbegu juu ya nchi."* Kumbuka ya kuwa katika mstari wa 14 inasema mbegu hii ni Neno la Mungu. Mungu si kuwa anakufundisha jinsi ya kuwa mkulima, lakini anatumia kitu cha asili kuelezea kweli ya kiroho. Mstari wa 27 unasema, *"Akawa akilala na kuamka, usiku na mchana, nayo mbegu ikamea na kukua, asivyojua yeye."* Sasa, Ninaamini ya kuwa hilo ni la muhimu. Inasema mtu yule hakika haelewei. Hafahamu hili linatokeaje.

Baadhi ya watu wanasema, "Mimi sielewi nini unachokizungumzia. Inawezekanaje kusoma Neno la Mungu kunaweza kunibadilisha na kusababisha maisha ya Mungu kuwa hai ndani yangu? Sielewi kabisa, lakini ninajua inafanya kazi. Sielewi ni kwa jinsi gani unaweza kuweka mbegu ndogo ardhini na kuwa na suke zima la mahindi likitoka pamoja na majani ya mahindi na kuzaa mara mia moja. Hakuna anaye elewa hili kwa ukamilifu, lakini inafanya kazi, na ninakuambia ya kuwa hili linafanya kazi. Kusoma Neno la Mungu na ukaliruhusu likuloweshe kabisa inakubadilisha tabia yako, uzoefu wako na mitazamo yako.

Mstari wa 28 unasema, *"Maana nchi huzaa yenyewe."* Ardhi iliumbwa ili kuatamia mbegu, na kuotesha na kuachilia uzima huo. Moyo wako uliumbwa kwa ajili ya Neno la Mungu – hakika ilikuwa hivyo. Neno la Mungu liliumbwa kuwekwa moyoni mwako. Kwa kuchukua tu Biblia na kuishika kwa karibu, kuiweka kwenye meza yako ya kahawa, au kuibebea pamoja nawe haina msaada wowote. Haiachilii nguvu maishani mwako. Unapaswa kulichukua Neno, lifanye kuwa mbegu, na ulipande moyoni mwako. Utakapofanya hivyo, moyo wako umeumbwa kuzaa matunda wenyewe. Itabadilisha jinsi mambo yanavyofanya kazi maishani mwako. Mstari unaendelea, *"kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke."* Hii ina maanishaya kuwa kuna hatua katika kukua au kukomaa. Watu huja kwangu mar azote wakielezea ya kuwa wana

mwamini Mungu kwa ajili ya kitu fulani ambacho ni chema sana, kitu cha kimungu ambacho ninaweza kukubaliana nacho. Lakini ikiwa kama hawajawahi kufanya chochote, ikiwa kama hawajawahi hata kumwongoza mtu kwa Bwana, ninaweza kuwahakikishia ya kuwa hawatapata hata huduma ya televisheni au redio ndani ya wiki chache zijazo.

Unapaswa kufanya mambo kwa hatua. Kuna hatua za kupokea kutoka kwa Mungu, na hiki ndicho mfano huu inachokielezea. Kwanza kabisa, unatakiwa kuanza, na hapo ndipo huja tumaini, na baadaye imani, na halafu inaleta matokeo. Mara zote kuna hatua za kufikia ushindi. Hakuna mtu anayeweza kutoka kwenye sifuri mpaka maili alfu kwa saa, zote mara moja. Ingawa inaweza kuwa ni matamanio ya kimungu, haitafanya kazi kwa jinsi hiyo. Andiko hili linaonyesha ya kuwa ufalme wa Mungu ni kama mbegu. Neno linatakiwa kupandwa moyoni mwako, kukua kuna kuja katika hatua mbali mbali: kwanza jani, halafu suke, kisha ngano pevu katika suke. Mstari unofuata unasema, *"Hata matunda yakiiva, mara atapeleka mundu, kwa kuwa mavuno yamefika."* Kuna hatua mbali mbali, Lakini hatimaye utafika muda wa matunda na kukomaa.

Kuna kitu kinazungumzwa katika mstari wa 35, *"Siku ile kulipokuwa jioni, akawaambia, Na tuvuke mpaka ng'ambo"* Yesu amekuwa akiwafundisha siku nzima kuhusus nguvu ya Neno, ni kwa jinsi gani Neno ni kama mbegu, na jinis litakavyoachilia uzima wa Mungu katika uzima wako. Amekuwa akiwafundisha hili angalau kwenye mifano kumi, kwa hiyo hapa Anawapa jaribio. Anawaambia, "Sawa, hapa kuna Neno kutoka kwa Bwana – twendeni upande mwengine wa ziwa." Hakusema "Tuingie chomboni, twende kati kati ya ziwa, na tukazame" lakini "Twendeni upande mwengine." Halafu akapanda chomboni na akalala. Habari hii inaendelea ya kuwa kukawa na upepo mkali na maji yakajaza kile chombo. Ni lazima ukumbuke ya kuwa chombo hiki hakikuwa cha kisasa chenye vyumba eneo la chini ambapo Yesu alikuwa hajalowana na hakujua nini kilichokuwa kikiendelea. Ilikuwa ni chombo cha wazi na Yesu alikuwa amelala usingizi, kikisukwa sukwa huku na kule kwenye maji. Sababu kwa nini hili lilikuwa na maana ilikuwa ni, Alijua nini kilikuwa kikiendelea, lakini bado alikuwa akijaribu kulala. Wanafunzi wakakasirika, wakamwendea, na kusema, "Bwana, je Wewe hujali ya kuwa tunaangamia?" Kwa maneno mengine, walikuwa wakisema, "Fanya kitu! Chukua ndoo na uchote maji! Piga makasia, fanya kitu! Huvuti uzito wako!"

Mara nyingi watu hufanya kitu hicho hicho na Mungu leo na wanasema, "Mungu, kwa nini hujafanya kitu?" Mungu amefanya kitu. Ametoa kila kitu tunachokihitaji kupitia kumwagika kwa damu ya Bwana Yesu. Ametoa Neno Lake na ametupa sisi mbegu hizi zote. Ni kazi yetu kuzipanda katika mioyo yetu. Ametupa maandiko, na ni kazi yetu kuchukua mbegu, kuziweka katika mioyo yetu, na kutafakari juu yake mpaka zitakapoachilia uzima. Lakini wanafunzi walitaka kumuamsha Yesu na kusema, "Ni kwa nini hufanyi kitu?" Aliamka, akakemea upepo na mawimbi, kukawa na utulivu mkuu. Halafu akageuka na akawaambia wanafunzi Wake,

"Ni kwa nini mna hofu sana? Inakuwaje hamna imani?" Hakusema, "Jamani, samahani. Nilipaswa kuwa nimefanya kitu." Hapana, Sehemu yake ilikuwa ni kuwafundisha Neno na kuwapa ahadi, na ilikuwa ni sehemu yao kulichukua Neno na kuamini ahadi. Mungu ametoa kila kitu kupitia Yesu Kristo kuja hapa ulimwenguni. Amekupa wewe kila kitu kinachohitajika ili ufanikiwe katika kila eneo lamaisha yako katika mfumo wa mbegu hapa ulimwenguni. Unachotakiwa kukifanya ni kuchukua mbegu ya Neno la Mungu na kuzipanda kwenye mioyo yenu kwa kupitia kulisoma, kulitafakari, kulifikiria, na uliache liweke mizizi ndani mwako. Unapofanya hivyo, utaweza kusimama na kusimamisha upepo wa maisha yako.

Ninaamini kilichokuwa bora kwa wanafunzi hawa ilikuwa ni kuchukua mafunzo ya Yesu aliyowapa siku ile na waseme, "Hebu twendeni upande mwengine." Wangeweza kusema, "Kufuatana na kila kitu alichotufundisha leo, hii ndiyo ahadi. Huyu ni Muumbaji wa ulimwengu aliyesema twendeni upande mwengine, na siyo twendeni nusu safari au kuzama. Wangeweza kulichukua hilo neno, wakalichanganya na imani, na kuukemea upepo na mawimbi. Hilo ndilo haswa Yesu alilolisema: "Enyi wenye Imani haba, ni kwa nini mlitia mashaka?" Unajua nini? Tunahitaji kuliamini Neno la Mungu na kulitendea kazi.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Mathayo 13:19. Kama hatupandi Neno la Mungu mioyoni mwetu, nini kitakachotokea? ______________________ ____________________________________

2. Soma Yoshua 1:8. Wakati gani tunapaswa kulitafakari Neno la Mungu? ___________________

3. Soma Yohana 6:63. Kufuatana na mstari huu, Neno la Mungu ni ______________________.

4. Soma Mathayo 4:4. Mwanadamu hapaswi kuishi kwa chakula cha kimwili pekee bali kwa _______________________________ ____________________________________

5. Soma Waefeso 6:17. Neno la Mungu ni kama aina gani ya silaha? _________________

6. Je upanga unaweza kuleta madhara kwa adui yake? __________________________ ________________________

7. Soma Warumi 8:6. Tunapolipa Neno la Mungu mahali sahihi maishani mwetu, tutakuwa na _________________________ ____________________________________ ____________________________.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Mathayo 13:19

"Kila mtu alisikiapo neno la ufalme asielewe nalo, huja yule mwovu, akalinyakua lililopandwa moyoni mwake. Huyo ndiye aliyepandwa karibu na njia."

### Joshua 1:8

"Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawasawa na maneno yote yaliyoandikwa humo; maana ndipo utakapoifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana."

### Yohana 6:63

"Roho ndiyo itiayo uzima, mwili haufai kitu; maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima."

### Mathayo 4:4

"Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

### Waefeso 6:17

"Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu."

### Warumi 8:6

"Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

8. Soma 2 Wakorintho 3:18. Kile ambacho tunakitazama ndicho kinachotujaz. Tunatakiwa kuweka mtazamo wetu kwenye nini? ________________________________
________________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

2 Wakorintho 3:18

"Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa Roho wa Bwana."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Mathayo 13:19. Kama hatupandi Neno la Mungu mioyoni mwetu, nini kitakachotokea? **Mwovu atalinyakua ili lisiweze kuzaa maishani mwetu.**
2. Soma Joshua 1:8. Wakati gani tunapaswa kulitafakari Neno la Mungu? **Usiku na Mchana.**
3. Soma Yohana 6:63. Kufuatana na mstari huu, Neno la Mungu ni **roho na uzima.**
4. Soma Mathayo 4:4. Mwanadamu hapaswi kuishi kwa chakula cha kimwili pekee bali kwa **kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu.**
5. Soma Waefeso 6:17. Neno la Mungu ni kama aina gani ya silaha? **Upanga.**
6. Je upanga unaweza kuleta madhara kwa adui yake? **Ndiyo.**
7. Soma Warumi 8:6. Tunapolipa Neno la Mungu mahali sahihi maishani mwetu, tutakuwa na **uzima na amani.**
8. Soma 2 Wakorintho 3:18. Kile ambacho tunakitazama ndicho kinachotujaz. Tunatakiwa kuweka mtazamo wetu kwenye nini? **Bwana na utukufu Wake.**

SOMO 13

# MUNGU HANA HATIA

*Na Andrew Wommack*

Leo nataka kukushirikisha moja ya jambo la muhimu sana ambalo Mungu ameshawahi kulifanya maishani mwangu. Inaonekana watu wanaamini kila kitu ambacho kinawatokea kinatoka kwa Mungu, ya kuwa anadhibiti kila kitu. Sababu ya hili ni kuwa maana yake, Mungu ni mkuu na mwenye uwezo wote, na wao wanadhania tu ya kuwa anadhibiti kila kitu kinachotokea maishani mwao. Sababu ya hili ni kuwa. Hata wasioamnini huliamini. Kuna Wakristo wengi ambao wanafundisha mafundisho haya, na imewaingia kwenye maisha yao. Ninaamini kile ambacho maandiko inakifundisha ni kinyume na hili, na ni muhimu sana ya kuwa ujifunze somo hili. Yakobo 1:13-17 inasema, *"Mtu ajaribiwapo, asiseme, Ninajaribiwa na Mungu; maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hamjaribu mtu. Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa. Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti. Ndugu zangu wapenzi, msidanganyike. Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga; kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka."*

Mistari hii inaeleza wazi sana ya kuwa Mungu ndiye mwanzilishi wa mambo mema. Yesu alisema katika Yohana 10:10, *"Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele."* Ikiwa kama ni chema, ni Mungu; Ikiwa kama ni kibaya, ni Shetani. Hiyo ni theolojia rahisi. Sababu kwa nini hili ni la muhimu sana ni kwakuwa Yakobo 4:7 inasema, *"Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia."* HIli linasema ni lazima tutii, au tujisalimishe, kwa Mungu na tumpinge Shetani. Neno "Kumpinga" linamaanisha kupambana dhidi ya.

Wakati watu wanapoamini ya kuwa kila kitu kinachotokea katika maisha kinatoka kwa Mungu – kwa mfano, magonjwa, kushindwa katika biashara, kupoteza kazi, watoto kuasi, au talaka – hilo linawaweka katika nafasi ya kuchukulia mambo kama yalivyo. Ikiwa kama hakika wanaamini ya kuwa Mungu ndiye aliyesababisha hali hiyo na anaitumia kuwaadhibu au kuwabadilisha, watakuwa wakipigana dhidi Yake kama watapinga. Bado, Yakobo 4:7

inatuambia tumpinge Shetani naye atatukimbia. Ni lazima umtii Mungu wewe mwenyewe. Hili linaonyesha ya kuwa kuna baadhi ya mambo yanatoka kwa Mungu na baadhi ya mambo ni ya Shetani. Kuna nguvu za uovu katika ulimwengu huu, na si kila kitu kinachotokea maishani mwako kinatoka kwa Mungu. Ikiwa kama huelewi hilo, utaishia kumtii Shetani, na ukweli ni kuwa unamwezesha Shetani

Ninataka kuleta kifungu kutoka Warumi kwa kuwa mara nyingi kinatumika vibaya. Nimeshawahi kuhudhuria mazishi ambapo watu hawajui chochote kuhusu Mungu, hawaendi kanisani, na hata hawajui andiko lolote, lakini wanalijua hili. Warumi 8:28 inasema, *"Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake."* Hili limetafsiriwa kusema ya kuwa chochote kinachotokea maishani mwako, Mungu hukifanya na hufanya kazi pamoja kwa mema kwa jinsi fulani. Nilikuwa kwenye mazishi ya kijana mdogo na binti ambao wamekuwa wakichanganya pombe na madawa ya kulevya, wakaingia kwenye gari, na kuendesha kwa kasi sana kwenye bara bara inayoteleza, wakateleza kwenye kona, na kugonga mlingoti wa simu, na wote waliuwawa. Mhubiri akanukuu andiko hili, "Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema", na kusema Mungu ni lazima awe na madhumuni kwa kufanya hili. Mungu hakuwaua wale vijana. Nina uhakika Shetani aliwadanganya kuasi dhidi ya viwango ambavyo wazazi wao na wengine waliwafundisha, lakini mwishowe ilikuwa ni uchaguzi wao. Wao ndiyo waliokuwa wakitumia madawa na kunywa pombe; wao ndiyo waliougonga mlingoti wa umeme. Hilo lililkuwa ni jambo la asili, na Mungu hakuwa chanzo cha hilo.

Ina maana gani inaposema "twajua ya kuwa mambo yote hutenda kazi kwa pamoja kwa wema"? Kwanza kabisa, haikusema tunajua vitu vyote hutoka kwa Mungu na vinatenda kazi kwa pamoja kwa wema. Inasema mambao yote hutenda kazi kwa pamoja kwa wema lakini inaweka maelezo ya ziada juu yake: *"kwao wao wampendao Mungu."* Andiko hili halifanyi kazi kwa mtu ambaye hampendi Mungu. Hilo ni kawaida kabisa ya kuwa inapaswa kwenda pasipo kusema, lakini inashangaza jinsi watu wanavyolitumia kwenye matukio kama vijana hawa ambao walikuwa wakitumia madawa ya kulevya na kunywa pombe na walikuwa katika uasi kabisa dhidi ya Mungu na kanuni Zake. Hili linasema inafanya kazi tu kwa wema kwa wale wampendao Mungu, na kwa wale ambao wameitwa kufuatana na madhumuni Yake.

Katika 1 Yohana 3:8 it says, *"Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi."* Mungu alijidhihirisha Yeye Mwenyewe ili aziharibu kazi za Shetani. Hayo ndiyo madhumuni Yake, na itaweza tu kufanya kazi kwa wema kwa wale wampendao na waliyoitwa sawa sawa na madhumuni Yake; yaani, wale ambao wanatembea katika wito huu, wanampinga Shetani, na wako kuziangamiza kazi zake. Wale ambao wanampinga Shetani na wanaishi kwa

ajili ya Mungu wanaweza kusema hivyo bila kujali kile ambacho Shetani anakifanya maishani mwao, Mungu anaweza kuigeuza na kuitumia kwa wema.

Tunahitaji kutambua ya kuwa Mungu hadhibiti kila kitu maishani mwetu. Kuna adui ambaye huja kuua, kuiba na kuharibu, lakini Yesu amekuja kutupa sisi uzima. Tunapaswa kuchagua uzima na kwa utashi wetu tutambue ya kuwa Mungu hana hatia ya kila kitu kinachokuja maishani mwetu.

Ikiwa Mungu alikuwa ni mwanadamu wa kawaida ambaye alifanya vitu ambavyo anashatakiwa kwavyo, kama vile kuleta saratani, ulemavu, mfadhaiko, huzuni, na majonzi ndani ya watu, Ninakuhakikishia hakuna serikali hapa duniani ambayo isinge mkamata, kumfunga au kujaribu Kumzuia. Bado tunafikiri Mungu, ambaye ana rehema sana kuliko mtu mwengine yeyote ambaye tumeshawahi kukutana naye au kumuwaza maishani mwetu, anazunguuka huko na huko akiwapiga watu na kufanya hivi. Kuna baadhi ya mambo ambayo ni mashambulizi ya kimapepo na baadhi ambayo ni ya asili, na si majanga yote yanaruhusiwa na Mungu. Kampuni za bima huandika kwenye sera zao "matendo ya Mungu, kama vile matetemeko ya ardhi na majanga". Hapana, Mungu siye anayesababisha mambo haya yote.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Yakobo 1:13. Je Mungu husababisha watu kujaribiwa na maovu? ____________________

2. Soma Yakobo 1:17. Vitu vyema vyatoka wapi? ______________________________

3. Soma Yohana 10:10. Mwivi ni nani? _____ ______________________________________ _

4. Soma Yohana 10:10. Madhumuni yake ni yapi? _________________________________

5. Soma Yohana 10:10. Ipi ni sababu ya Yesu kuja? _______________________________

6. Soma Yakobo 4:7. Nini ni matokeo ya kumtii Mungu na kumpinga Shetani? _____ ______________________________________ ______________________________

7. Soma Warumi 8:28. Je Warumi 8:28 inasema mambo yote yanatoka kwa Mungu? __________

8. Soma Matendo 10:38. Je magonjwa yanatoka kwa Mungu? _________________ ______________________

9. Soma 1 Yohana 3:8. Yapi yalikuwa madhumuni ya kufunuliwa kwa Mwana wa Mungu? __________________________ ______________________________________ ____________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Yakobo 1:13

"Mtu ajaribiwapo, asiseme, Ninajaribiwa na Mungu; maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hamjaribu mtu."

### Yakobo 1:17

"Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga; kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka."

### Yohana 10:10

"Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele."

### Yakobo 4:7

"Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia.."

### Warumi 8:28

"Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake."

### Matendo 10:38

"habari za Yesu wa Nazareti, jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye."

### 1 Yohana 3:8b

"Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili aziharibu kazi za Ibilisi."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Yakobo 1:13. Je Mungu husababisha watu kujaribiwa na maovu? **Hapana.**
2. Soma Yakobo 1:17. Vitu vyema vyatoka wapi? **Kwa Baba wa mianga.**
3. Soma Yohana 10:10. Mwivi ni nani? **Shetani.**
4. Soma Yohana 10:10. Madhumuni yake ni yapi? **Kuiba, kuua, na kuharibu.**
5. Soma Yohana 10:10. Ipi ni sababu ya Yesu kuja? **Kutupa uzima tele.**
6. Soma Yakobo 4:7. Nini ni matokeo ya kumtii Mungu na kumpinga Shetani? **Atakimbia mbali nami.**
7. Soma Warumi 8:28. Je Warumi 8:28 inasema mambo yote yanatoka kwa Mungu? **Hapana.**
8. Soma Matendo 10:38. Je magonjwa yanatoka kwa Mungu? **Hapana.**
9. Soma 1 Yohana 3:8. Yapi yalikuwa madhumuni ya kufunuliwa kwa Mwana wa Mungu? **Kuziharibu kazi za Shetani.**

DARAJA 1

# SOMO 14

# NGUVU YA MAISHA YALIYOJAZWA NA ROHO

*Na Don Krow*

Marko 16:15-16 inajulikana kama Agizo Kuu. Yesu aliwaambia wanafunzi Wake, *"Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa."* Katika Matendo 8, mstari 5 na 12, tunaona jinsi agizo hili lilivyofanyiwa kazi kupitia mahubiri ya Filipo katika Samaria. *"Filipo akatelemka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo … Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume na wanawake."*

Swali ni, Je watu hawa wa Samaria walifanyika Wakristo kufuatana na Marko 16:15-16. Ndiyo, walifanyika. Philip alikwenda kwenye mji wa Samaria, akamhubiri Yesu Kristo, na kwa kupitia imani katika Kristo, wakabatizwa, wote wanaume na wanawake. Kufutana na Agizo Kuu, tunaweza kusema watu hawa waliokoka, lakini je walipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu?

Biblia inazungumza kuhusu Yohana akibatiza kwenye maji, Lakini ni Yesu Kristo pekee anayeweza kubatiza kwa Roho Mtakatifu. Kufutana na maandiko, watu waliamini, waliokolewa na kubatizwa kwa maji, Lakini kamwe walikuwa hawajapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Matendo 8:14-17 inasema, *"Na mitume waliokuwako Yerusalemu, waliposikia ya kwamba Samaria imelikubali neno la Mungu, wakawapelekea Petro na Yohana; ambao waliposhuka, wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu;: (kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa jina lake Bwana Yesu.) Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu"*

Tunaweza kuona kutoka kwenye maandikoya kuwa kwa sababu tu mtu ameamini, amebatizwa na kuokolewa haimaanishi wamepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ameingia maishani mwao – Katika Yohana 20:22 tunaona ya kuwa Roho Mtakatifu aliwafanya upya wanafunzi – lakini ilikuwa ni kwenye Siku ya Pentekoste ndipo ambapo walibatizwa na Roho Mtakatifu na kuwezeshwa na Mungu. Kuna tofauti kati ya kuhuishwa na Roho Mtakatifu katika wokovu na ubatizo wa Roho Mtakatifu anaposhuka juu ya mtu. Kuna

kuzamishwa ndani ya Roho Mtakatifu ambako huja juu ya watu na kuwawezesha. Ingawa mtu ameokolewa, haimaanishi ya kuwa wamebatizwa na Roho Mtakatifu.

Katika Matendo 19:1-2 inasema, *"Ikawa, Apolo alipokuwa Korintho, Paulo, akiisha kupita kati ya nchi za juu, akafika Efeso; akakutana na wanafunzi kadha wa kadha huko, akawauliza, Je! Mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini? Wakamjibu, La, hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia."* Paulo alisema, "Je mlimpokea Roho Mtakatifu mlipoamini?" Wakasema, "Hatujui chochote kuhusu Roho Mtakatifu." Paulo akasema, "Ikiwa kama hamkubatizwa katika Roho Mtakatifu mlipoamini, mlibatizwa ubatizo gani?" Wakasema, "Tulibatizwa kwa ubatizo wa Yohana Mbatizaji." Nina amini Paulo alielezea vizuri zaidi kuhusu Yesu kuwa Kristo, na halafu baadaye waumini hawa wakajitambulisha na Yesu kwa kupitia ubatizo wa maji. Katika mistari ya 6 -7 inasema, *"Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao; wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri. Na jumla yao walipata wanaume kumi na wawili."*

Ingawa watu hawa walikuwa ni wanafunzi ambao waliamini katika Mesihi ambaye alikuwa anakuja, walikuwa hawajabatizwa na Roho Mtakatifu. Mtu anaweza kuwa amezaliwa mara ya pili na amebatizwa kwa maji pasipo kubatizwa katika Roho Mtakatifu. Ubatizo katika Roho Mtakatifu ni uzoefu wa tofauti na wa kipekee ukilinganisha na kubadilishwa.

Ingawa ninaweza kumbatiza mtu kwenye maji, siwezi kuwabatiza katika Roho Mtakatifu; Yesu pekee ndiye awezaye kufanya hilo. Ikiwa kama hujawahi kumwomba Yesu akubatize kwa Roho Mtakatifu, kwa nini usimwombe sasa? Luka 11:13 inasema, *"Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?"* Kwa nini usimwombe Yeye leo?

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Marko 16:16. Sasa soma Matendo 8:5, 12. Je watu waliyoelezwa katika Matendo 8:12 walifanyika Wakristo? ____
_________________________________
_______________

2. Soma Matendo 8:14-16. Je watu hawa walipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu? ___
_________________________________
_______________________________

3. Soma Matendo 19:1-5. Je watu hawa ni waumini? _________________________
____________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Marko 16:16

"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa."

### Matendo 8:5, 12

"[5] Filipo akatelemka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo. [12] Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume na wanawake."

### Matendo 8:14-16

"[14] Na mitume waliokuwako Yerusalemu, waliposikia ya kwamba Samaria imelikubali neno la Mungu, wakawapelekea Petro na Yohana: [15] ambao waliposhuka, wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu: [16] (kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa jina lake Bwana Yesu.)"

### Matendo 19:1-5

"[1] Ikawa, Apolo alipokuwa Korintho, Paulo, akiisha kupita kati ya nchi za juu, akafika Efeso; akakutana na wanafunzi kadha wa kadha huko;, [2] akawauliza, Je! Mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini? Wakamjibu, La, hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia.. [3] Akawauliza, Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani? Wakasema, Kwa ubatizo wa Yohana. [4] Paulo akasema, Yohana alibatiza kwa ubatizo wa toba, akiwaambia watu wamwamini yeye atakayekuja nyuma yake, yaani, Yesu. [5] Waliposikia haya wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

4. Soma Matendo 19:6-7. Je wangepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu? ____________

5. Soma Luka 11:13. Luka 11:13 inasema nini ambacho tunahitaji kukifanya ili kumpokea Roho Mtakatifu? ____________
____________________________________
____________________

6. Soma 1 Wakorintho 14:2. Wakati mtu akinenea kwa lugha, anafanya nini? _____
____________________________________
____________________________

7. Soma 1 Wakorintho 14:14. Wakati mtu akinena kwa lugha, anafanya nini? ______
____________________________________
___________________________

8. Soma 1 Wakorintho 14:16-17. Wakati mtu anaponena kwa lugha, anafanya nini? ____
____________________________________
_______________________

9. Soma Matendo 2:4. Wakati mtu anaponena kwa lugha, je ni Roho Mtakatifu ananena au ni mtu yule ananena mwenyewe? _____
____________________________________

10. Soma Matendo 2:4. Ni nani anayempa mtu kutamka? ______________________
____________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Matendo 19:6-7

"[6] Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao; wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri. [7] Na jumla yao walipata wanaume kumi na wawili"

### Luka 11:13

"Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?"

### 1 Wakorintho 14:2

"Maana yeye anenaye kwa lugha, hasemi na watu, bali husema na Mungu; maana hakuna asikiaye; lakini anena mambo ya siri katika roho yake."

### 1 Wakorintho 14:14

"Maana nikiomba kwa lugha, roho yangu huomba, lakini akili zangu hazina matunda."

### 1 Wakorintho 14:16-17

"[16] Kwa maana wewe ukibariki kwa roho, yeye aketiye katika mahali pa mjinga ataitikaje, Amina, baada ya kushukuru kwako, akiwa hayajui usemayo? [17] Maana ni kweli, wewe washukuru vema, bali yule mwingine hajengwi."

### Matendo 2:4

"Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Marko 16:16. Sasa soma Matendo 8:5, 12. Je watu waliyoelezwa katika Matendo 8:12 walifanyika Wakristo? **Ndiyo.**
2. Soma Matendo 8:14-16. Je watu hawa walipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu? **Hapana.**
3. Soma Matendo 19:1-5. Je watu hawa ni waumini? **Ndiyo.**
4. Soma Matendo 19:6-7. Je wangepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu? **Hapana.** **ANGALIZO: Hili linaonyesha uzoefu huu kuwa ni tofauti na wokove.**
5. Soma Luka 11:13. Luka 11:13 inasema nini ambacho tunahitaji kukifanya ili kumpokea Roho Mtakatifu. **Tuombe**
6. Soma 1 Wakorintho 14:2. Wakati mtu akinenea kwa lugha, anafanya nini? **Anazungumza na Mungu na anazungumza siri.**
7. Soma 1 Wakorintho 14:14. Wakati mtu akinena kwa lugha, wanafanya nini? **Roho zao zinamwomba Mungu.**
8. Soma 1 Wakorintho 14:16-17. Wakati mtu anaponena kwa lugha, anafanya nini? **Anambariki Mungu kwa roho zao na kutoa shukurani**
9. Soma Matendo 2:4. Wakati mtu anaponena kwa lugha, je ni Roho Mtakatifu ananena au ni mtu yule ananena mwenyewe? **Mtu yule ananena.**
10. Soma Matendo 2:4. Ni nani anayempa mtu kutamka? **Roho Mtakatifu**

# SOMO 15

# JINSI YA KUMPOKEA ROHO MTAKATIFU

*Na Don Krow*

Leo tunakwenda kuzungumza kuhusu jinsi ya kumpokea Roho Mtakatifu. Matendo 10:1 inasema, *"Palikuwa na mtu Kaisaria, jina lake Kornelio, akida wa kikosi kilichoitwa Kiitalia."* Kulikuwa na cheo cha kijeshi, inawezekana kapteni aliyekuwa akiongoza kikosi. Mstari wa 2 unaendelea, *"Mtu mtauwa, mchaji wa Mungu, yeye na nyumba yake yote, naye alikuwa akiwapa watu sadaka nyingi, na kumwomba Mungu daima."* Alikuwa mwenye haki, alifanya mambo ya haki, alimcha Mungu, alitoa fedha nyingi kwa watu wenye uhitaji, na Biblia inasema alimwomba Mungu wakati wote. Lakini tutakwenda kuona, na itakuwa ya kushangaza, kuwa ingawa alifanya mambo sawa, ingawa alimcha Mungu na alikuwa na maisha ya maombi, hakuwa na mahusiano binafsi na Mungu kupitia Yesu Kristo.

Inasema katika mistari ya 3-6, *"Akaona katika maono waziwazi, [kama saa tisa ya mchana] malaika wa Mungu, akimjia na kumwambia, Kornelio! Akamtazama sana, akaogopa akasema, Kuna nini, Bwana? Akamwambia, Sala zako na sadaka zako [kutoa] zimefika juu na kuwa ukumbusho mbele za Mungu. Sasa basi, peleka watu Yafa, ukamwite Simoni, aitwaye Petro. Yeye ni mgeni wa mtu mmoja, jina lake Simoni, mtengenezaji wa ngozi, ambaye nyumba yake iko pwani, atakuambia yakupasayo kutenda".*

Mtu huyu, ingawa alikuwa akimcha Mungu, mwenye haki kwa kadri akifanya mambo ambayo yalikuwa ni sahihi, na alikuwa na maisha ya maombi mbele za Mungu, alitumiwa malaika ambaye alimwambia amwite Simoni Petro ambaye angemwambia nini yaliyompasa kufanya. Tunaona katika Matendo 10:43 hasa kile ambacho Petro alielekezwa kumuambia: *"Kumpa ushuhuda wote wa manabii, ya kuwa kupitia jina lake [kupitia jina la Bwana Yesu] kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi".*Hili si ni la kushangaza? Mtu huyu ambaye alikuwa na mambo haya yote kwenye sifa zake hakuwa na mahusiano binafsi na Mungu kupitia Yesu Kristo. Mungu alisema, "Mambo unayoyafanya ni makuu, ni ya ajabu, na yamekuwa ukumbusho mbele zangu, lakini ninakuambia kile ambacho nitakwenda kukifanya. Nimemtuma malaika kukuambia umwite mtu aitwa Petro, naye atakuambia yakupasayo kuyafanya." Katika Matendo

10:43, Petro alipokwenda nyumbani kwa Kornelio', alisema, *"Kila amwaminiye* [Bwana Yesu Kristo] *atapata ondoleo la dhambi"*.

Sasa tazama nini kilitokea hapa. *"Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile neno"* (Matendo 10:44). Kornelio alikuwa akipokea kama alivyokuwa na imani katika Kristo, na akaweka imani yake katika Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Mara alipofanya hivyo, Roho Mtakatifu alimshukia na wote waliyokuwapo nyumbani kwake. Inasema katika mstari wa 45, *"Na wale waliotahiriwa, walioamini, wakashangaa, watu wote waliokuja pamoja na Petro, kwa sababu Mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu."* Walijuaje hilo? *"Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha, na kumwadhimisha Mungu"* (mstari 46).

Kila mara Roho Mtakatifu anapomshukia mtu katika Agano Jipya, karama ya Roho Mtakatifu hujidhihirisha na kutoa uthibitisho ya kuwa wamepokea ujazo wa Roho. Katika Agano Jipya, kwa kawaida walinena kwa lugha au walitabiri.

Nilipiga magoti jioni moja kwenye shamba moja mjini Dallas, Texas, na nikasema, "Mungu, sijui kuhusu mambo haya yote ya kunena kwa lugha na ubatizo katika Roho Mtakatifu ambayo watu wanayazungumzia, lakini kama kuna njia ninaweza kukusifu Wewe, njia ambayo ninaweza kukuinua, njia ambayo ninaweza kwenda zaidi ya lugha yangu ya kibinadamu ya Kiingereza, basi ninahitaji. Nilianza kumuabudu Mungu, na nilipokuwa nikifanya hivyo, Roho Mtakatifu alinipa lugha, matamshi ambayo sikuyajua au kujifunza. Biblia inasema katika Matendo 2:4, "*Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka*" Nani aliye nena? Wao walinena. Nani aliye toa matamshi? Roho Mtakatifu.

Luka 11:13 inasema, *"Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?"* Unachopaswa kukifanya kwa sasa ni kuomba, amini ya kuwa umepokea, jikabidhi kwa Mungu, anza kumuabudu Bwana, naye atakupa matamshi ya kumuabudu na kumsifu Yeye katika lugha ambayo hujawahi kujifunza.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Elezea baadhi ya maneno ambayo Biblia inayatumia kwa ajili ya wokovu. ________
____________________________________
____________________________

2. Soma Matendo 11:15. Mstari huu unaelezeaje uzoefu wa ubatizo wa Roho Mtakatifu? __________________________
_________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

Yohana 3:3

"Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.."

Matendo 3:19

"Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana;."

Marko 16:16

"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa."

Wakolosai 2:13

"Na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu, aliwafanya hai pamoja naye, akiisha kutusamehe makosa yote;."

Warumi 8:9

"Lakini ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake."

Mathayo 25:46

"Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele."

Matendo 11:15

"Ikawa nilipoanza kunena, Roho Mtakatifu akawashukia kama alivyotushukia sisi mwanzo."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

3. Wanafunzi wa Yesu walimpokea Roho Mtakatifu (Yohana 20:22), lakini siku chache baadaye walibatizwa na Roho Mtakatifu (Matendo 2:1-4). Angalia na ufananishe kweli hizi (Yohana 20:22 na Acts 2:1-4). ____________________________ ________________________

4. Soma Matendo 1:8. Nini ni madhumuni ya ubatizo wa Roho Mtakatifu? ____________ ______________________________________ ___________________________

5. Soma Matendo 2:38-39 na 1 Wakorintho 1:7. Je ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kwa ajili yetu leo? __________________________ ______________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Yohana 20:22

"Naye akiisha kusema hayo, akawavuvia, akawaambia, Pokeeni Roho Mtakatifu."

### Matendo 2:1-4

"[1] Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. [2] Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. [3] Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. [4] Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka."

### Matendo 1:8

"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi."

### Matendo 2:38-39

"[38] Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. [39] Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.."

### 1 Wakorinthians 1:7

"hata hamkupungukiwa na karama yo yote, mkikutazamia sana kufunuliwa kwake Bwana wetu Yesu Kristo."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

6. Soma Luka 11:13 Ikiwa kama hujapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, Nini unachopaswa kukifanya sasa? ___________ ____________________________________

7. Soma Matendo 2:4. Je utaomba, utapokea, utanena, na kumuabudu Mungu katika lugha ya maombi ambayo Mungu anakupa? ____________________________ ____________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Luka 11:13

"Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao??"

### Matendo 2:4

"Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Elezea baadhi ya maneno ambayo Biblia inayatumia kwa ajili ya wokovu. **Kuzaliwa mara ya pili (Yohana 3:3), kubadilishwa (Matendo 3:19), kuamini na kubatizwa (Marko 16:16), baada ya kusamehewa (Kol. 2:13), baada ya kumpokea Roho wa Kristo (Rumi. 8:9), na uzima wa milele (Math. 25:46).**

2. Soma Matendo 11:15. Mstari huu unaelezeaje uzoefu wa ubatizo wa Roho Mtakatifu? **Pale Roho Mtakatifu anapomshukia mtu.**

3. Wanafunzi wa Yesu walimpokea Roho Mtakatifu (Yohana 20:22), lakini siku chache baadaye walibatizwa na Roho Mtakatifu (Matendo 2:1-4). Angalia na ufananishe kweli hizi (Yohana 20:22 na Matendo 2:1-4). **Katika Yohana 20:22, wanafunzi walimpokea Roho Mtakatifu. Katika Matendo 2:1-4, wanafunzi hao hao tena wakajazwa na Roho Mtakatifu (ambako ni kuzamishwa kwa ndani na kwa nje). Tazama Matendo 1:8.**

4. Soma Matendo 1:8. Nini ni madhumuni ya ubatizo wa Roho Mtakatifu? **Kuwezesha kwa ajili ya huduma (au kushuhudia).**

5. Soma Matendo 2:38-39 na 1 Wakorintho 1:7. Je ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kwa ajili yetu leo? **Ndiyo. Karama ya Roho Mtakatifu itakoma katika ujio wa mara ya pili wa Kristo, lakini si mpaka wakati huo.**

6. Soma Luka 11:13. Ikiwa kama hujapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, Nini unachopaswa kukifanya sasa? **Omba ili upokee.**

7. Soma Matendo 2:4. Je utaomba, utapokea, utanena, na kumuabudu Mungu katika lugha ya maombi ambayo Mungu anakupa? **Ndiyo, Nitanena, Lakini Roho Mtakatifu atanipa matamshi (lugha).**

# SOMO 16

# FAIDA ZA KUNENA KWA LUGHA

*Na Andrew Wommack*

Moja ya jambo lililotokea wakati ubatizo wa Roho Mtakatifu ulipokuja kwanza ilikuwa ni kuwa watu wote ambao walikuwapo pale walinena kwa lugha. Matendo 2:4 inasema kuwa katika Siku ya Pentekoste, walijazwa na Roho Mtakatifu na walinena kwa lugha nyengine kama Roho alivyowajalia kunena. Kwa muendelezo wakati wote kwenye kitabu chote cha Matendo, kulikuwa na udhihirisho wa uwepo wa Mungu wakati watu walipompokea Roho Mtakatifu.

Ndiyo, Kuna mambo ya zaidi kwa Roho Mtakatifu kuliko tu kunenea kwa lugha, lakini ni moja ya madhihirisho ya muhimu. Wakorintho wa Kwanza 14:13-14 inasema, *"Kwa sababu hiyo yeye anenaye kwa lugha na aombe apewe kufasiri. Maana nikiomba kwa lugha, roho yangu huomba, lakini akili zangu hazina matunda."* Unapoomba kwa lugha, roho yako inaomba. Mara unaponena kwa lugha, omba ya kuwa utatafsiri ili ufahamu wako uwe wenye matunda.

Ninaweza kutoa ushuhuda wangu binafsi kuwa nilipopokea ubatizo wa Roho Mtakatifu na kuanza kunena kwa lugha, ilibadilisha maisha yangu sana. Ninaamini nilipozaliwa mara ya pili, Kristo alikuja kuishi ndani yangu na akawekeza kila kitu humo ndani, Lakini wakati Roho Mtakatifu alipokuja juu yangu, vikaanza kujidhihirisha kwangu na kwa watu wengine. Kuna mambo kadhaa ambayo yalitokea. Mwaka wa kwanza nilipoomba kwa lugha, akili yangu iliniambia tendo hilo lilikuwa ni ukichaa, ya kuwa yote niliyokuwa ninayafanya ilikuwa ni kupoteza muda. Ilihitaji Imani kwangu mimi kuomba kwa lugha, na ndiyo sababu Yuda 20 inasema mjijenge juu ya imani yenu iliyo takatifu sana. Inakuondoa kutoka kwenye fikra na tafakari za asili na kukuweka wewe kwenye ulimwengu wa kiroho wa Imani.

Jambo jengine nililolipitia ilikuwa, nilipoomba katika lugha, watu ambao sikuwahi kuwawaza kwa miaka mingi walianza kuja kwenye kumbu kumbu yangu. Nikaanza kuwaombea, na ndani ya siku moja au mbili, wangewasiliana nami na ningekuta kuna jambo la kimiujiza limewatokea. Hili lilitokea mara nyingi sana kiasi kuwa hatimaye nikaanza kuyakusanya mambo haya kwa pamoja na kutambua ya kuwa nilipokuwa nikiomba katika lugha, nilikuwa nikiomba kwa hekima ambayo ilikwenda zaidi ya uwezo wa kiakili. Roho yangu ambayo ilijua

mambo yote na ilikuwa na nia ya Kristo ilikuwa ikiwaombea watu kwa njia ambazo nisingeweza kuzifanya kwa kupitia ufahamu wangu mwenyewe wa kimwili.

Siku moja nilikuwa nikiomba kwa lugha – kama nilivyosema, ilihitaji imani kwangu mimi kuomba katika lugha– na nilikuwa nikipambana na baadhi ya mawazo kama vile, *Ungeweza kuongea kwa Kiingereza na kufanya vyema badala ya kuomba kwa maneno yasiyo na maana.* Ilibidi nishughulike na mawazo haya na kuyashusha chini, na nikaendelea tu kuomba. Mtu ambaye sikuwahi kumuona kwa miaka mine akabisha hodi mlangoni kwangu. Akaingia, hakusalimia au kusema chochote, akaketi chini, na akaanza kulia na kuumimina moyo wake kwa sababu alikuwa na matatizo mengi sana. Nilikaa pale nikiwaza, *Nilipaswa kuwa ninaomba kwa Kiingereza.* Wazo langu lililofuata lilikuwa, *Ningewezaje kujua kumuombea wakati sijamwona kwa kipindi cha miaka minne?* Hatimaye, ikazama ndani mwangu ya kuwa nimekuwa nikimwombea, na Mungu amekuwa akiniandaa. Nimekuwa nikifanya maombezi kwa ajili yake katika jinsi ambayo nisingeweza kufanya kama nilikuwa ninaomba kwa ufahamu wangu mwenyewe. Ghafla, ufunuo ukaanza kuja kwangu na nikamwambia, "Ninaweza kusema tatizo lako ni nini." Nikamaliza kumueleza habari yake na kumpa jibu lake.

Ni lazima uelewe ya kuwa haya yalitokea zamani wakati nilipokuwa katika kanisa la kidini. Hakujua nini kilichonitokea na mimi sikuwa na uhakika. Ilituogopesha sisi wote. Lakini ilikuwa ni nguvu ya Mungu katika udhihirisho, na akaitumia katika uwezo wake wa Kimungu. Hiki ndicho tukui hili linachokimaanisha: Unapoomba kwa lugha, ni roho yako inaomba. Roho yako imeokolewa, ina nia ya Kristo, na inafahamu haswa nini cha kufanya. Ina upako kutoka kwa Mungu ili kwamba ujue mambo yote, na hakuna kizuizi katika roho yako. Ikiwa kama ungeweza kutembea katika nguvu na ufunuo wa roho yako, itabadilisha maisha yako ya kimwili. Njia moja ya kulifanya hilo, ingawa siyo ndiyo njia pekee yake, ni kuanza tu kunenea kwa lugha. Tambua na uamini ya kuwa unapofanya hivyo, unajijenga wewe mwenyewe katika imai iliyo takatifu sana, ya kuwa roho yako inaomba hekima iliyofichika ya Mungu, na ufunuo mkamilifu wa Mungu unakuja. Halafu, kufuatana na1 Wakorintho 14:13, omba ya kuwa utaweza kutafsiri. Hiyo haimaanishi unatakiwa kuacha kuomba kwa lugha na kuomba kwa Kiingereza/lugha yako ili utafsiri; ina maanisha tu ufahamu wako unazaa matunda.

Ikiwa kama utatoa ujumbe kwa lugha katika ibada ya kanisa, inabidi utulie na kutafsiri kwa Kiingereza au kwa lugha itakayoeleweka. Unapoomba wewe mwenyewe, Ninachokifanya ni kuomba kwa lugha na kuamini ya kuwa Mungu ananipa ufunuo. Mara nyengine tabia yangu hugeuka tu. Sina neno mahususi, lakini ghafla ninaona vitu kwa uwazi na kupata mtazamo wa tofauti. Inaweza kuchukua wiki kabla sijapata ufunuo wote kamili, lakini ninaamini muda uliyotumika kuomba kwa lugha na kuamini Ninatafsiri ni sehemu ya hilo.

Kunena kwa lugha ni muhimu kwa sababu nyingi, hakika zaidi ya kuthibitisha ya kuwa umempokea Roho Mtakatifu. Inapaswa kuwa ni sehemu ya maisha ya kila siku. Ni

jinsi ya kuwasiliana moja kwa moja kutoka kwenye moyo wako kwenda kwa Baba, kwa kuipita akili yako na mashaka yake na hofu zake. Inakujenga wewe katika imai yako iliyo takatifu sana na kuachilia hekima iliyofichika ya Mungu. Ninaomba tu ya kuwa ninyi nyote mtaweza kumiminika katika hili, mkaachilia imani yenu, na kupokea faida kamilifu ya kunena kwa lugha.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Yuda 20. Ni faida gani kubwa inayopatikana kwa kuomba katika Roho Mtakatifu? ____________________________________________

2. Soma Matendo 2:4. Ni watu wangapi walijazwa na Roho Mtakatifu? ____________________________________________

3. Soma Matendo 2:4. Walifanya nini kama matokeo ya kujazwa? ____________________________________________

4. Soma 1 Wakorintho 14:14. Ni sehemu gani ya kwako inayo omba wakati unapoomba katika lugha isiyofahamika? ____________________________________________

5. Soma 1 Wakorintho 14:2. Wakati mtu anaponena katika lugha isiyofahamika, huwa anazungumza na nani? ____________________________________________

6. Soma 1 Wakorintho 14:2. Wakati mtu anaponena katika lugha isiyofahamika, Je watu wanaelewa nini kinachosemwa? ____________________________________________

7. Soma 1 Wakorintho 14:2. Unapoomba katika lugha isiyofahamika, roho yako inazungumza nini? ____________________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Yuda 20

"Bali ninyi, wapenzi, mkijijenga juu ya imani yenu iliyo takatifu sana, na kuomba katika Roho Mtakatifu."

### Matendo 2:4

"Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka."

### 1 Wakorintho 14:14

"Maana nikiomba kwa lugha, roho yangu huomba, lakini akili zangu hazina matunda."

### 1 Wakorintho 14:2

"Maana yeye anenaye kwa lugha, hasemi na watu, bali husema na Mungu; maana hakuna asikiaye; lakini anena mambo ya siri katika roho yake."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

8. Soma 1 Wakorintho 14:4. Unapoomba katika lugha, unafanya nini? ________________

9. Soma 1 Wakorintho 14:16. Unapoomba katika lugha, unafanya nini? ____________ ______________________________________ ______________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### 1 Wakorintho 14:4

"Yeye anenaye kwa lugha hujijenga nafsi yake; bali ahutubuye hulijenga kanisa."

### 1 Wakorintho 14:16

"Kwa maana wewe ukibariki kwa roho, yeye aketiye katika mahali pa mjinga ataitikaje, Amina, baada ya kushukuru kwako, akiwa hayajui usemayo?"

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Yuda 20. Ni faida gani kubwa inayopatikana kwa kuomba katika Roho Mtakatifu? Ninapoomba katika Roho Mtakatifu, Ninajijenga mimi mwenyewe.
2. Soma Matendo 2:4. Ni watu wangapi walijazwa na Roho Mtakatifu? Watu wote.
3. Soma Matendo 2:4. Walifanya nini kama matokeo ya kujazwa? Walinena kwa lugha.
4. Soma 1 Wakorintho 14:14. Ni sehemu gani ya kwako inayo omba wakati unapoomba katika lugha isiyofahamika? Roho yangu inaomba.
5. Soma 1 Wakorintho 14:2. Wakati mtu anaponena katika lugha isiyofahamika, huwa anazungumza na nani? Mungu.
6. Soma 1 Wakorintho 14:2. Wakati mtu anaponena katika lugha isiyofahamika, Je watu wanaelewa nini kinachosemwa? Hapana.
7. Soma 1 Wakorintho 14:2. Unapoomba katika lugha isiyofahamika, roho yako inazungumza nini? Siri, mambo ya sirini (Toleo la New Century), Mambo ya ndani ya mahusiano kati yangu na Mungu tu (Ujumbe).
8. Soma 1 Wakorintho 14:4. Unapoomba katika lugha, unafanya nini? Ninajijenga mwenyewe.
9. Soma 1 Wakorintho 14:16. Unapoomba katika lugha, unafanya nini? Baraka na unatoa shukurani kwa Mungu.

# KOZI YA UINJILISTI YA UANAFUNZI WA YESU

# DARAJA 2

Ruhusa imetolewa kutoa nakala au kuchapisha kwa ajili ya madhumuni ya kufundisha wanafunzi wa Yesu katika sharti kuwa kitasambazwa bure bila gharama.

DARAJA 2

# SOMO 1
# UBINAFSI

*Na Andrew Wommack*

Ubinafsi ni chanzo cha mambo mengi sana tunayoyapitia. Kuna mstari katika Methali 13 ambao hakika unatakiwa uuangalie, kwa sababu hutauamini ikiwa kama hujausoma katika Biblia yako mwenyewe. Mstari wa 10 unasema, *"Kiburi huleta mashindano tu: bali hekima hukaa nao wanaoshauriana."* Watu wengi mwanzoni watachukua swala na huu mstari na kusema, "Subiri kidogo. Kiburi hakiwezi kuwa ndiyo kitu pekee kinachosababisha mashindano au ugomvi. Methali 17:14 inasema kuwa Mwanzo wa ugomvi ni chanzo cha mashindano, hivyo mashindano ni lazima yanasababishwa na zaidi ya kiburi tu. Ni kile ambacho fulani na fulani wamenifanyia." Wengine watasema, "Huelewi; hivi ndivyo nilivyo." Hapana, maandiko yanasema kuwa ni kwa kiburi pekee huja mashindano. Siyo moja ya sababu zinazoongoza; ndiyo sababu pekee. Baadhi ya watu tena watachukulia swala na kusema, "Nina aina ya matatizo yote, lakini kiburi si kimoja wapo ya hayo matatizo. Ikiwa kama kuna chochote basi nina kiwango changu cha kujiamini kiko chini, hivyo hakuna yeyote anayeweza kunishitaki kwa sababau ya kuwa na kiburi."

Inatubidi kuelezea upya kiburi ni nini. Si tu kufikiria ya kuwa wewe ni bora kuliko mtu mwengine, lakini katika maneno rahisi, ni kujiona wewe mwenyewe kama chanzo cha kila kitu. Ubinafsi hakika ndiyo mzizi wa kiburi chote. Katika Hesabu 12:2 Mariamu na Haruni, Dada na kaka yake Musa, waliinuka dhidi yake, wakimshutumu kwa sababu ya kuoa mtu ambaye hakuwa wa kabila lao, wakisema, *"Je! Ni kweli Bwana amenena na Musa tu? Hakunena na sisi pia?"* Maandiko baadaye yanasema katika mabano kwenye mstari wa 3 ya kuwa Musa alikuwa mpole sana zaidi ya wanadamu wote waliokuwa juu ya uso wa nchi. Badala ya kukwazika katika kile walichokisema, alianza kuwaombea.

Inaposema Musa alikuwa mpole sana zaidi ya wanadamu wote waliokuwa juu ya uso wa nchi, hebu subiri na ulitafakari hilo. Hatujui kulikuwa na watu wangapi ulimwenguni, lakini hakika walikuwako mamilioni, na Musa alikuwa ndiye mpole kwa watu wote hawa. Nini kinachofanya hii iwe ni kauli ya kushangaza ni kuwa Yeye alikuwa ndiye aliyeiandika. Watu wengi wanafikiri ya kuwa ikiwa kama wewe hakika ni mnyenyekevu au mpole, hata hutajua.

Hizo ni hisia za uongo kuhusus hasa ukorofi ni nini. Kiburi si tu kufikiria ya kuwa wewe ni bora kuliko kila mtu – bali ni ubinafsi. Ni kama vile kuwa na fimbo yenye kiburi upande moja na kuwa na kiwango cha chini cha ujasiri upande mwengine. Hizo ni hisia tofauti zilizo kinyume za kitu kile kile, lakini zote ziko kwenye fimbo hiyo hiyo. Ni ubinafsi. Haijalishi ikiwa kama unafikiri ya kuwa wewe ni bora kuliko mtu mwengine yeyote au wewe ni mbaya kuliko watu wengine wowote, wewe ni mbinafsi bila shaka. Kila kitu kinachujwa kupitia hilo. Mwoga, mtu mwenye aibu ana majivuno sana, hujifikiria tu kuhusu yeye.

Kitu ninachokiongea hapa ni kuwa ubinafsi hakika ndiyo mzizi wa kiburi chote, na kama utaichomeka hiyo kwenye Methali 13:10, *"Kiburi huleta mashindano tu"* inachokisema hapa ni kuwa ni ubinafsi wetu wenyewe ndiyo unaotufanya sisi kuwa na hasira, na siyo kile ambacho watu wanatufanyia. Ni ubinafsi wetu wenyewe ndiyo unaosababisha sisi kuitikia vile tunavyoitikia kwenye kile ambacho watu hukifanya. Kamwe hutaweza kuwazuia watu wasikutendee vibaya; haiwezi kutokea. Imani si kwa ajili ya kuwadhibiti watu wengine bali kukusaidia wewe kushughulika na nafsi yako na kushughulika na vitu ambavyo vimo ndani mwako. Hivyo haijalishi watu watakufanyia nini.

Wakati Yesu alipokuwa anasulubiwa, Aliweza kuwageukia watu wale wale ambao walikuwa Wakimsulubisha na kusema, "Baba, uwasamehe, kwa maana hawajui walitendalo." Hakuwadhibiti watu wale bali badala yake alijidhibiti mwenyewe. Alimfikiria mama Yake alipokuwa msalabani na akazungumza na mmoja wa wanafunzi Wake kuhusu kumtunza. Sababu Yesu aliweza kusamehe na kutenda katika upendo – kati kati ya maumivu makali, kuonewa, na kila kitu kilichokuja kwake – ilikuwa ni kwa sababu hakuwa mbinafsi.

Ni ubinafsi wako mwenyewe ndiyo unaokufanya uwe na hasira, bado Maandiko yanasema unapaswa kufa katika nafsi yako. Ikiwa kama ningekuwa na maiti mbele yangu, nisingeweza kuuiukana, kuipiga mateke, au kuitemea mate, au kuidharau, lakini kama kweli ni maiti, usingeweza kuitikia. Sababu unaitikia jinsi unavyoitikia kwenye vitu vinavyo kuzunguuka si kwa sababu ya mambo hayo ya nje bali ni kwa sababu ya kile kilichoko ndani yako. Kamwe hutakuwa na nguvu katika imani kiasi kwamba utaweza kuhamisha vikwazo vyote na kila kitu ambacho kinakugusa kwa jinsi isivyo sahihi, lakini unaweza kushughulika na nafsi yako. Unaweza kufika mahali ambapo utamfanya Yesu kuwa Bwana wa maisha yako na utampenda, Utaupenda Ufalme Wake na watu wengine zaidi ya unavyojipenda mwenyewe. Utaona ya kuwa utakapofanya hivyo na kushughulika na nafsi yako mashindano na ugomvi maishani mwako vitakoma.

Moja ya funguo kuu kwa ajili ya kutumia vitu hivi vyote ambavyo Mungu amevifanya katika maisha yako ni kutambua ya kuwa Hakukupa Ufalme kwa ajili ya madhumuni ya binafsi. Hakuyafanya haya yote ili kwamba upate kuwa na mahitaji yako yote. Unahitaji kujifunza ni katika kujikana wewe mwenyewe na kuyapoteza maisha yako ndipo hakika unaanza kugundua

maisha yana husu nini. Ni katika kuwapenda watu wengine na Mungu zaidi yako wewe mwenyewe ndipo utakapoanza kuimaliza hasira yako na maumivu, mambo yale yote ambayo yako ndani mwako.

Nina omba ya kuwa leo Mungu atachukua vitu hivi vichache nilivyo visema na kuvitumia kuufungua moyo wako ili kutambua ya kuwa ni hali yako wewe mwenyewe ya ubinafsi ndiyo inayo kusababishia huzuni. Badala ya kuweka lawama mahali pengine, unahitaji kukubali jukumu, kabiliana nalo, jinyenyekeze mbele za Mungu, na mwombe aingie na Ajifanye yeye Mwenyewe kuwa mkubwa maishani mwako. Hiyo ndiyo njia kwako wewe ya kutembea katika ushindi.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Marko 9:33-34. Wanafunzi walikuwa wakijadiliana kuhusu nini walipokuwa njiani kwenda Kapernaumu? ____________________________________________

2. Je hili linaonyesha ubinafsi ndani yetu sisi wote? ______________________________

3. Soma Marko 9:35. Kufuatana na andiko hili, ikiwa mtu anataka kuwa wa kwanza, ni lazima wafanyike kuwa nani? ____________________________________________

4. Elezea kwa undani mafundisho ya Yesu katika kitabu cha Luka 22:24-27. ____________________________________________

5. Soma Methali 13:10. Ni kitu gani pekee kinachosababisha mashindano? ____________

6. Soma Wagalatia 2:20. Tunapaswa kuishi vipi maisha yetu? ______________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Marko 9:33-34

"[33] Wakafika Kapernaumu; hata alipokuwamo nyumbani, akawauliza, Mlishindania nini njiani? [34] Wakanyamaza; kwa maana njiani walikuwa wakibishana wao kwa wao, ni nani aliye mkubwa

### Marko 9:35

"Akaketi chini, akawaita wale Thenashara akawaambia, Mtu atakaye kuwa wa kwanza atakuwa wa mwisho kuliko wote, na mtumishi wa wote.."

### Luka 22:24-27

"[24] Yakatokea mashindano kati yao, kwamba ni nani anayehesabiwa kuwa mkubwa. [25] Akawaambia, Wafalme wa Mataifa huwatawala, na wenye mamlaka juu yao huitwa Wenye fadhili;[26] lakini kwenu ninyi sivyo; bali aliye mkubwa kwenu na awe kama aliye mdogo; na mwenye kuongoza kama yule atumikaye.. [27] Maana aliye mkubwa ni yupi? Yeye aketiye chakulani, au yule atumikaye? Siye yule aketiye chakulani? Lakini mimi kati yenu ni kama atumikaye.."

### Methali 13:10

"Kiburi huleta mashindano tu; Bali hekima hukaa nao wanaoshauriana.."

### Wagalatia 2:20

"Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

7. Soma Mathayo 7:12. Nini ni dawa ya ubinafsi? ______________________________ ________________________________________ ___________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

Mathayo 7:12

"Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Marko 9:33-34. Wanafunzi walikuwa wakijadiliana kuhusu nini walipokuwa njiani kwenda Kapernaumu? **Walikuwa wakijadiliana kuhusu nani ni mkuu.**

2. Je hili linaonyesha ubinafsi ndani yetu sisi wote? **Ndiyo.**

3. Soma Marko 9:35. Kufuatana na andiko hili, ikiwa mtu anataka kuwa wa kwanza, ni lazima wafanyike kuwa nani? **Mtumishi wa wote.**

4. Elezea kwa undani mafundisho ya Yesu katika kitabu cha Luka 22:24-27. **"Na wakaanza kubishana kati yao kwamba nani atakuwa mkuu kwenye Ufalme ujao. Yesu akawaambia, 'Katika ulimwengu huu wafalme na wakuu hutawala watu wao, na bado wanaitwa "marafiki wa watu". Lakini kati yenu, wale waliyo wakuu zaidi wanapaswa kuchukua nafasi ya chini kabisa, na kiongozi anapaswa kuwa kama mtumishi. Kwa kawaida mkuu huketi mezani na kuhudumiwa na watumishi wake. Lakini siyo hapa! Kwa kuwa mimi ni mtumishi wenu" (Luka 22:24-27,** *Tafsiri ya New Living***).**

5. Soma Methali 13:10. Ni kitu gani pekee kinachosababisha mashindano? **Kiburi.**

6. Soma Wagalatia 2:20. Tunapaswa kuishi vipi maisha yetu? **Kwa imani ya Kristo (au imani katika Kristo), haiko katika nguvu zetu wenyewe au udhaifu.**

7. Soma Mathayo 7:12. Nini ni dawa ya ubinafsi? **Kumweka Mungu mbele na wengine. Wafanyie wengine kama ambavyo unavyotaka ufanyiwe.**

## SOMO 2

# JINSI YA KULITAFAKARI NENO LA MUNGU

*Na Don Krow*

Neno *tafakari* linamaanisha "Kufikiri juu ya, kuwaza, kupanga akilini, kunuia, au kukusudia". Neno la Kiyunani lina maanisha "Kuzunguusha kitu katika akili" na pia linatafsiriwa kuwa ni *kufikiria*.

Sababu mbili kwa ajili ya kutafakari kibiblia "kutafakari juu ya maarifa sahihi, pia inamaanishwa kuwa kama kufanya upya nia na kuwasiliana na Mungu nyuma ya Neno lake" kupitia maombi, sifa, na kutafakari; yaani, kufikiri juu ya, kuwaza, na kufikiria kuhusu Yeye.

*Kutafakari kunaweza kufanywa kupitia kujifunza mada.* Kuchagua mada ya kuitafakari. Mfano: Ubatizo. Elezea neno kutoka Kiyunani, Kiebrania, au kamusi nzuri. Tafuta neno la asili kutoka kule lilikotolewa. Zingatia na tafakari kwenye muktadha wa mistari ambayo itakupeleka kujifunza masomo mengine yanayofanana, kama vile ondoleo (Matendo 2:38), toba (Matendo 2:38), imani (Marko 16:16), dhamira (1 Petro. 3:21), kumuita Bwana (Matendo 22:16), n.k.

Unahitaji kutafakari juu ya maswali ambayo unayo au ambayo maandiko yanayaibua, kama vile: Je kuna sifa ambazo zinatakiwa kufikiwa kabla ya ubatizo? Nini ni madhumuniya Ubatizo? Ni wakati gani ulifanyika? Katika kipindi gani cha muda

*Kutafakari kunaweza kufanywa kutoka kwenye kujifunza kwa ufafanuzi; yaani., kujifunza mstari-kwa-mstari ya kitabu cha Biblia.* Ufunguo ni kutafakari na kufikiri kuhusus kitabu kwa muda mrefu kiasi kuwa unazoea muktadha wake (mistari na sura).

*Kutafakari kunaweza kufanyika kupitia kujifunza maneno.* Baadhi ya maneno yan maanisha nini? Ina maana gani kuamini? Neno Bwana lina maana gani? Neno Yesu lina maana gani? Neno Kristo linamaanisha nini? Neno hesabia haki lina maana gani, n.k.

*Unaweza kutafakari kutoka kwenye aya (vifungu vya maneno) katika Biblia. Aya (Kifungu cha maneno) ni mkusanyiko wa mawazo yaliyoko katika maandishi, kwa kawaida ina sentensi*

*kadhaa.* Wakati mwandishi anapobadilisha somo lake la msisitizo katika kuandika kwao, kwa kawaida huanza kifungu kipya cha maneno.

Unapotafakari kupitia maandiko, angalia alama kama alama za kuuliza. Ni kwa nini swali hili linaulizwa? Linahusiana vipi na muktadha, n.k..?

Kutafakari Kibiblia si tu kuangalia maneno, bali kwa ajili ya Mungu nyuma ya Neno.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Neno "kutafakari" lina maanisha nini? ____
_______________________________________
_____________________________________

2. Zipi ni sababu mbili za kutafakari kibiblia?
_______________________________________
__________________________________

3. Kujifunza kwa mada ni nini? ____________
_____________________________________

4. Kujifunza Maandiko kwa ufafanuzi kuna maana gani? __________________________
_______________________________________
______________

5. Soma Luka 6:46. Unafikiri neno "Bwana" lina maana gani? ______________________
_______________________________________
__________________

6. Soma Mathayo 1:21. Unfikiri neno "Yesu" kinamaana gani? ______________________
_______________________________________
__________________

7. Soma Luka 23:1-2. Unfikiri neno "Kristo" lina maana gani? ______________________
_______________________________________
__________________

8. Aya (kifungu cha maneno) ina maanisha nini? __________________________________
________________________

9. Kutafakari Kibiblia si tu kuangalia maneno, bali kwa ajili ya
__________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Luka 6:46

"Na kwa nini mnaniita, Bwana, Bwana, walakini hamyatendi nisemayo?"

### Mathayo 1:21

"Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake YESU, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao."

### Luka 23:1-2

"[1] Wakasimama mkutano wote, wakampeleka kwa Pilato.. [2] Wakaanza kumshitaki, wakisema, Tumemwona huyu akipotosha taifa letu, na kuwazuia watu wasimpe Kaisari kodi, akisema kwamba yeye mwenyewe ni Kristo, mfalme."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Neno "kutafakari" lina maanisha nini? **Kufikiri juu ya, kuwaza, au kuzunguusha kitu katika akili ya mtu.**
2. Zipi ni sababu mbili za kutafakari kibiblia? **Kutafakari kuhusu maarifa sahihi (kufanya upya nia yangu) Na kuwasiliana na Mungu kupitia Neno Lake (kwa kutafakari, kufikiri, na kumuwaza Yeye).**
3. Kujifunza kwa mada ni nini? **Ni kuchagua mada kutoka kwenye Biblia ili kujifunza na kutafakari.**
4. Kujifunza Maandiko kwa ufafanuzi kuna maana gani? **Kujifunza mstari kwa mstari wa kitabu cha Biblia.**
5. Soma Luka 6:46. Unafikiri neno "Bwana" lina maana gani? **Yule ambaye tunamtii (kama bosi).**
6. Soma Mathayo 1:21. Unfikiri neno "Yesu" kinamaana gani? **Mwokozi ambaye anawaokoa wengine na dhambi zao.**
7. Soma Luka 23:1-2. Unfikiri neno "Kristo" lina maana gani? **Yule aliyepakwa mafuta kuwa mfalme.**
8. Aya (kifungu cha maneno) ina maanisha nini? **Wazo lililowekwa katika maandishi.**
9. Kutafakari Kibiblia si tu kuangalia maneno, bali <u>**kwa ajili ya kuwasiliana na Mungu kupitia Neno Lake.**</u>

DARAJA 2

# SOMO 3
# KUFANYA UPYA NIA

*Na Don Krow*

Leo tunataka kuzungumza kuhusu kufanya upya nia. Ningependa kusoma vifungu viwili vya maandiko. Cha kwanza kinatoka Wafilipi 4:8. kinasema, *"Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo."* Mtume Paulo dhahiri kabisa anatuambia ya kuwa kuna mambo ambayo tunapaswa kuyatafakari. Kwa maneno mengine, tunaweza kuchagua mawazo yetu. Sasa ninajua ya kuwa wote tunayo mawazo ambayo mara nyengine yako kinyume na Neno la Mungu, kufuatana na Warumi, sura ya 7, mistari ya 22 na 23. Sheria ya dhambi ambayo inapambana ndani yetu inashambulia nia zetu. Lakini Biblia inatuambia katika Wafilipi kuwa hatutakiwi kukaa hapo na kuyaacha mawazo yetu yajenge kiota, kuwa tunaweza kuchagua kile ambacho tunakifikiria. Biblia pia inatuambia kuwa kama awazavyo mtu nafsini mwake, ndivyo alivyo (Methali. 23:7). Hivyo ni muhimu sana kile ambacho tunakifikiria.

Katika Warumi 12:1 na 2, Biblia inasema, *"Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana.. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu,..."* Biblia inasema tunaweza kubadilishwa kwa kufanywa upya nia zetu. Je ulijua ya kuwa chombo cha angani cha Apollo kilenda juu angani, ilibidi wafanye marekebisho ya njia kila baada ya dakika kumi? Walikwenda mwezini kwa mtindo wa kupinda pinda. Na hatimaye walipotua, walikuwa na eneo la maili 500 lililokuwepo kwa ajili ya kutulia, na kwa taabu sana walifika katika eneo hilo kwa futi chache tu. Bado safari nzima ya chombo hicho ilifanikiwa. Tunahitaji kuweka njia na kujitoa kikamilifu kwa Bwana Yesu Kristo kwa kuwa dhabihu iliyo hai. Tatizo na dhabihu iliyo hai ni kuwa mara nyengine inataka kutambaa na kutoka madhabahuni, hivyo tunatakiwa kufanya marekebisho ya njia katika mawazo yetu. Tunatakiwa kuwa na moyo ambao unasema, "Mungu, Ninakutaka Wewe na Ninaitaka njia Yako."

Si tu tunahitaji kujitoa kikamilifu, Lakini ili kuwa na maisha ya ushindi ya Kikristo kunahitajika kuchukua hatua zaidi na kubadilishwa kwa kufanywa upya nia zetu. Hatuwezi

kufikiri kama ulimwengu, ikiwa kama hatutaki matokeo ya ulimwengu. Kama tunavyosoma katika Wafilipi 4:8, tunaweza kuchagua katika kile tunachokifikiri. *"Mambo yo yote yenye kupendeza, ya haki, yo yote yenye sifa njema, yatafakarini hayo."* Kile ambacho wangekifanya katika Agano la Kale ni kuchukua Neno la Mungu na kuliweka kwenye miimo ya milango yao na kwenye mavazi yao. Ilikuwa mbele yao kwa mwendelezo. Mungu aliagiza ya kuwa walipaswa kuzungumza kuhusu Neno la Mungu usiku na mchana ili waweze kufuata na kufanya kile Neno linachokisema. Na pia walipaswa kuwaambia watoto wao mambo haya yote. Ni muhimu sana nini tunachokifikiria. Ni muhimu sana ya kuwa tutalishika Neno la Mungu mbele yetu wakati wote ili tuweze kuwa na maisha ya ushindi. Kinyume cha kutafakari kwenye kile ambacho ni kizuri, cha haki na chenye sifa njema ni kutafakari kwenye mambo ya Mungu na mambo ya roho. Warumi 8:6 inasema, *"Kuwa na nia ya mwili ni mauti,"* lakini sehemu inayofuata ya mstari inasema, *"bali nia ya roho ni uzima na amani."* Ni uzima na ni amani kufikiri kwenye mambo ya Roho wa Mungu. Lakini kama tutaanza kufikiri kuhusu uzinzi, mambo ya ulimwengu, fedha, kutamani, na kuendelea, unajua nini kitakachotokea maishani mwetu? Kama awazavyo mtu moyoni mwake, ndivyo alivyo. Anza kutendea kazi mambo hayo. Tutaanza kuyafanya mambo hayo maishani mwetu na, na yataangamiza maisha yetu. Unaona, vita halisi vya kiroho kwa anayeamini hakika si kupinga na kumkemea Shetani wakati wote, ingawa kuna nyakati ambapo tunahitaji kufanya hivyo. Lakini vita vya kiroho vinahusiana na kile ambacho tunakifikiria na kile ambacho tunatumia muda wetu mwingi katika hicho.

Unaona Biblia inasema katika Isaya 26:3 ya kuwa Mungu atamlinda katika amani kamilifu ambaye nia yake imemtegemea. Kuna wakati katika siku ambapo sisi wote tunahitaji kufanya marekebisho ya njia, kama ambavyo inasema katika Warumi 12. Tunahitaji kusema, "Mungu, hayo ni mawazo yasiyo sahihi. Ninahitaji kugeuka na kufanya upya nia yangu na kuanza kufikiri kuhusu mambo ambayo ni ya staha, ya haki, na yenye sifa njema."

Ikiwa kama una ngome imara, Ikiwa kama uko katika kifungo, ikiwa unajikuta unafikiria mambo ambayo hupaswi kuyafikiria, unahitaji kujirudi kwa haraka. Biblia inasema, *"Ikiwa kama mtamsogelea Mungu, Atattusogelea. Ikiwa tutampinga adui, atatukimbia."* Kuna nyakati maishani mwangu ambapo niliacha vitu kwenda vibaya na kuruhusu msongo kuchukua nafasi yake. Katika nyakati hizo, ni vigumu kuchukua Biblia na kuketi chini na kusoma kifungu cha maandiko na kusema, "Mungu, Hiki ndicho unachokisema kuhusu mimi. Hivi ndivyo Unavyosema mimi nilivyo. Wewe ni nguvu yangu." Je ulijua ya kuwa ushindi wako ni rahisi jinsi hiyo? Unahitaji kusema, "Sasa nitakwenda kupinga kile ambacho nina mruhusu adui kunifanyia. Nitakwenda kuketi chini na kufungua Biblia, na sita soma tu baadhi ya maneno kwenye kurasa hizi, lakini nitakwenda kujiunganisha na Mungu aliye nyuma ya maneno haya. Nitakwenda kuruhusu nia yangu ikae juu Yake. Na, Bwana, hiki ndicho unachokisema kuhusu mimi. Unasema kuwa mimi nimesamehewa. Inasema ya kuwa nimetakasika. Unasema ya kuwa hakuna kinachoweza kunitenganisha na upendo Wako." Unapoketi pale na kutafakari kuhusu

mambo yote mema ambayo Mungu ameyafanya kwako, katika dakika chache, utakwenda kusahau kuhusu mambo yale mengine.

Hebu nitumie kielelezo. Nimemsikia mtu wakati fulani akisema, "Sasa, Ninakuasa tu usifikirie kuhusu tembo wa pinki kwa dakika kumi zijazo. "Je unajua nini kimetokea? Kwa dakika kumi zijazo, tulichokifanya tu ilikuwa ni kufikiria kuhusu tembo wa pinki. Halafu akauliza, "Mnara wa Uhuru una rangi gani?" Mtu fulani akasema kijani. Na akasema, "Vyema, ni mkono upi mnara wa uhuru umenyooshwa kuelekea juu?" Na mtu moja akasema itakuwa ni mkono wa kuume. Halafu akauliza, "Mnara wa uhuru umeshika nini kwenye mkono wake." Na mtu moja akasema ilikuwa ni tochi. Halafu mtu yule akasema, "Nini kimetokea kwenye mawazo yako kuhusu tembo wa pinki?" yaliondoka. Unaona, si swala la kusema, "Sasa, haufikiri kuwa mawazo haya," kwa kuwa unajua utayafikiria hayo mawazo. Maandiko hakika yanatuambia ya kuwa tunahitaji kubadilisha mawazo hayo na mawazo ya Mungu, na wakati tunapoyaona haya yanapokuja kinyume nasi na tunawaza kitu ambacho hatupaswi kuwaza, tunahitaji kwa haraka kurudi kwenye nia zetu utambulisho mpya. Tunahitaji kumgeukia Mungu mara tu, kujiunganisha Naye, na si tu kwa maneno kwenye ukurasa, bali na Mungu ambaye ndiyo mwenye maneno hayo. Na Biblia inatuambia katika Warumi Warumi 8:6 ya kuwa tunapofanya, tutaona mabadiliko ambayo uzima na Amani ya Mungu inavyoutoa, Wakati nia zetu zinakaa katika Yeye na mambo ya Roho. Tafakari mambo haya, Ndugu zangu, na utembee siku hii katika uhuru ambao Kristo ameununua kwa ajili yako.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Warumi 12:1. Nini tunachopaswa kukifanya na miili yetu? ________________ ________________________________________ ________________________

2. Soma Warumi 12:2. Andiko hili linatuambia ya kuwa tunatakiwa kuwa tofauti kuliko __________________________ ________________________________________ _____________.

3. Soma Matendo 17:11. Ni lazima tufanye kufikiri kwetu kuendane na? ___________________

4. Soma Warumi 8:5-6. Kuwa na nia ya kiroho ni __________________________________.

5. Soma Warumi 12:1-2. Ni mambo gani mawili tunayohitaji kuyafanya, kufuatana na mistari hii? _______________________ ________________________________________ ________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Warumi 12:1

"Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana."

### Warumi 12:2

"Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.."

### Matendo 17:11

"Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo."

### Warumi 8:5-6

"[5] Kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili; bali wale waifuatao roho huyafikiri mambo ya roho.. [6] Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti; bali nia ya roho ni uzima na amani."

### Warumi 12:1-2

"[1] Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. [2] Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

6. Soma Isaya 26:3. Tunakaaje katika amani kamilifu? ______________________________________________

7. Soma Isaya 26:3. Zipi ni baadhi ya njia tunazoweza kutumia ili kuziweka nia zetu katika Bwana? ______________________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

Isaya 26:3

"Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea Katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini.."

Isaya 26:4

"Mtumainini Bwana siku zote Maana BWANA YEHOVA ni mwamba wa milele.."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Warumi 12:1. Nini tunachopaswa kukifanya na miili yetu? **Kuitoa, kwa Mungu.**
2. Soma Warumi 12:2. Andiko hili linatuambia ya kuwa tunatakiwa kuwa tofauti kuliko **ulimwengu, au wasioamini.**
3. Soma Matendo 17:11. Ni lazima tufanye kufikiri kwetu kuendane na? **Maandiko, Neno la Mungu**.
4. Soma Warumi 8:5-6. Kuwa na nia ya kiroho ni **uzima na amani.**
5. Soma Warumi 12:1-2. Ni mambo gani mawili tunayohitaji kuyafanya, kufuatana na mistari hii? **Kujitoa kwa Mungu kama dhabihu iliyo hai na kuanza kuzifanya upya nia zetu**.
6. Soma Isaya26:3. Tunakaaje katika amani kamilifu? **Kwa kuziweka nia zetu kwa Bwana.**
7. Soma Isaya 26:3-4. Zipi ni baadhi ya njia tunazoweza kutumia ili kuziweka nia zetu katika Bwana? **Maombi, sifa, kutafakari kwenye Neno, kutoa shukurani, n.k.**

DARAJA 2

# SOMO 4
# UMUHIMU WA KANISA LA KRISTO

*Na Don Krow*

Leo tunazungumza kuhusus umuhimu wa kanisa la Kristo. Ningependa kusoma andiko kutoka kwenye kitabu cha Waebrania 10:25. Inasema, *"Wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia."* Tunapoangalia umuhimu wa kanisa la Kristo, swali langu ni hili, "Kanisa ni nini?"

Niliichukua Programu ya Uanafunzi ya Uinjilisti kwenye kanisa la mahali hapa Colorado Springs. Tuliwafundisha watu kanisani kuhusu jinsi ya kuitumia, na tuliitumia kwenye maeneo ya kazi. Ndani yamiezi sita ya kufanya kazi na kanisa la mahali, tulianzisha vikundi ishirini vya kujifunza Biblia nje ya kusanyiko la mahali. Kwa miezi, tulikuwa tukifanya kazi na watu hawa katika kujifunza Biblia. Mchungaji hakika alinichanganya siku moja pale aliposema, "Unajua, Biblia inasema ya kuwa Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa. Ni kwa nini hatuwaoni watu hawa kutoka kwenye mafunzo ya Biblia wakija kanisani kwetu?"

Tulipokuwa nje kwenye uwanja, watu walikuwa wakiokolewa na walikuwa wakifanywa wanafunzi. Lakini kile ambacho mchungaji hakika alikimaanisha kilikuwa ni, "Kwa nini hawaji kukutana pamoja Jumaapili asubuhi katika jengo hili?" Dhana yangu ya kanisa kidogo haikuwa sahihi. Kile ambacho mchungaji alikisema hakika kilinisumbua, Na sikujua nini cha kufanya. Nikawaza, *Je Programu* ya Uanafunzi ya Uinjilisti *hakika inafanya kazi? Je hakika tunayafikia maisha ya watu?* Nilijua tulikuwa tunawafikia watu wengi, Lakini kile kilichonichanganya kilikuwa ni kwa nini walikuwa hawaji kwenye ibada ya Jumapili asubuhi.

Nikaamua kujifunza kwa kina neno "kanisa". Nini kinachofundishwa katika somo hili Nilichogundua. Katika Warumi 16:3, 1 Wakorintho 16:19, Wakolosai 4:15, Philemoni 2, Matendo 5:42, na Matendo 20:20, Biblia kimsingi inazungumza kuhusu kanisa la kwanza la Agano Jipya likikutana nyumbani kwa mtu fulani. Ninafahamu ya kuwa kuna aina zote za makanisa. Kuna makanisa ya nyumbani, makanisa yenye mikusanyiko midogo na mikubwa, na makanisa makubwa sana. Jambo moja ambalo hakika lilishika usikivu wangu katika maandiko

ilikuwa ni kwamba Kanisa la Agano jipya walionekana wakikutana pamoja katika mikusanyiko midogo kwenye nyumba za watu.

Kamusi ya ufafanuzi ya maneno ya Biblia na Lawrence O. Richards (uk.164) inasema, "Yeyote anaweza kusamehewa kwa kuchanganyikiwa kidogo kuhusu maana ya neno, 'kanisa; tunalitumia neno hili kwa jinsi nyingi sana. Ina maanisha jengo mahususi (m.f., kanisa lililoko kweye mtaa wa 4), dhehebu au Imani iliyojikusanya (Kanisa lililofanywa upya Marekani) [au kanisa la Kibaptisti], na hata mkutano wa Jumaapili (m.f., je ulikwenda kanisani leo). Hakuna katika matumizi haya ambayo haswa ni ya kibiblia." Na nika waza, *Hili hakika lina maanisha nini? Neno "kanisa" hasa lina maana gani?* Nitakwenda kunukuu zaidi. Inasema, "Kwa kuwa watu wengi hufikiria kanisa kuwa kama ni jengo kwa ajili ya ibada za kidini kuliko kuwa ni mikusanyiko ikijihusisha katika kuabudu, kanisa linalohusika inaweza kuwa inapotosha." Neno la Kiyunani kwa ajili ya "kanisa" ni *ecclesia* na kabisa ina maanisha mkusanyiko wa watu kwa pamoja kwa madhumuni ya kuabudu au maombi au sifa au kumuangalia tu Mungu. Nitakwenda kusoma baadhi ya mambo mengine hapa. Inasema, "Ecclesia katika Agano Jipya inaweza kuchukua idadi yoyote ile ya waumini. Inaweza kutumiwa na kundi dogo ambalo linakutana majumbani (Warumi 16:5). Imechukua waumini wote wanaoishi kwenye mji mkubwa (Matendo 11:22), au wilaya kubwa kijiografia, kama vile Asia au Galatia." Inaendelea kwa kusema, "Mkutano halisi wa kanisa ulikuwa kwenye nyumba. Wakati kusanyiko kama hilo lilipokutana 'kila mmoja alikuwa na wimbo[alikuwa], neno la maelkezo, ufunuo, ndimi au tafasiri'

(1 Wakorintho 14:26). Watu binafsi walishirikiana na wengine 'kwa uangalifu walipima nini kilikuwa kinatokea, nini kilisemwa'

(1 Wakorintho 14:29) … kushirikishana huko kunabaki kuwa ni muhimu kwenye uwepo wa kanisa kama jamii ya imani … Kila mtu alikuwa anatarajiwa kuchangia na kuwatumikia wengine na vipawa vyake vya kiroho."

Katika Waebrania 10:25 inasema, *"wala tusiache kukusanyika pamoja."* Kanisa ni kusanyiko la watu walikuja pamoja wakiwa na madhumuni ya kumuangalia Yesu, wakimsifu Bwana, ili kupokea mwelekeo kutoka kwa Bwana, kufuata mwelekeo huo. Madhumuni ya msingi ya kanisa la kwanza la Agano Jipya ilikuwa ni kujengana.Walikutana pamoja kwa madhumuni ya kujengana wao kwa wao katika Imani.

Kanisa la kwanza lilikuwa ni kanisa la kiinjilisti. Watu walikuwa wametawanyika kila mahali, wakishirisha wengine imani yao katika Yesu Kristo, na walipofanya hivyo, Bwana akazidisha kanisa – siyo kwenye jengo – bali aliongezea kwenye watu wa Mungu walipotubu na kuamini. Halafu wakakusanyika kwa pamoja ili kutiana moyo wao kwa wao, ili kuvitumia vipawa vyao vya kiroho, kutumikiana wao kwa wao na kuwa na muda wa ushirika wao kwa wao kwa

kushirikiana chakula kwa pamoja. Walipokuwa pamoja, walivitumia vipawa vyao kujengana wao kwa wao. Halafu walitoka nje na kulihubiri Neno, na mzunguuko wote ungeanza tena. Waliamini katika Bwana Yesu Kristo, na walijikusanya wao wenyewe kwa pamoja. Haikujalisha walikusanyikia wapi. Ingeweza kuwa kwenye jengo au nyumbani kwa mtu. Ingeweza kuwa ni idadi kubwa ya watu, au ingeweza kuwa ni idadi ndogo ya watu walikutana majumbani. Hakika haikujalisha, kwa kuwa walikutana pamoja katika jina la Bwana kwa madhumuni ya kuvitumia vipawa vyao, kutiana moyo wao kwa wao, na kuwa na ushirika kati yao na huku matokeo ya mwisho yakiwa kuinuana kila moja au kujengana.

Niligundua ya kuwa kile ambacho tulikuwa tukikifanya na programu ya Uanafunzi ya Uinjilisti kwa kupitia kanisa la mahali niliyoitaja hapo awali, kwa kukutana katika vikundi ishirini tofauti vya kujifunza Biblia katika mji mzima ni kuwa tulikuwa tukikutana katika makanisa ishirini tofauti. Hayakuwa makanisa kama tunavyoyajua leo, lakini tulikuwa tukikutana kama kanisa, mara ishirini kwa wiki, kwa sababu tulikuwa tukikutana pamoja katika jina la Bwana Yesu ili kutiana moyo, kumuangalia Bwana Yesu, kuelekezwa kutoka kwenye Neno la Mungu, na kuvitumia vipawa vyetu vya kiroho.

Haijalishi ni kanisa gani unalokwenda – haijalishi kama uko kwenye kanisa la kidhehebu au kanisa lisilo la kidhehebu, ikiwa kama mnakutana kwenye kanisa kubwa au kikundi kidogo cha nyumbani – Maandiko yanatuambia unapoiona siku ikiingia, na kwa kadri dhambi inapokuwepo, neema ya Mungu iko zaidi. Neema itakwenda kukaa ndani ya mikusa nyiko hii ya watu wa Mungu. Katika kanisa ambapo kila muumini ana sehemu ya huduma ya Yesu Kristo, mna weza kuhudumiana, kuinuana ninyi kwa ninyi, na kutiana moyo ninyi kwa ninyi wakati mkitumia vipawa vyenu vya kiroho kati ya ninyi na ninyi.

Wote tutafaidika kwa kukutana na kikundi cha waumini kwa jinsi hii. Hata kama itakuwa ni wawili au watatu wanokutana katika jina la Bwana Yesu, tunahitaji kukutana kwa pamoja kila mara. Ni vyema kukutana pamoja kutumia vipawa vyetu vya kiroho, kuinuana ninyi kwa ninyi, kutiana moyo ninyi kwa ninyi, kumuangalia Yesu kwa pamoja, na kuombeana ninyi kwa ninyi. Kuna mengi ambayo tungeweza kuyasema kuhusu kanisa. Tunaweza kuzu ngumza kuhusu wazee, waangalizi wachungaji na serikali ya kanisa lakini hayo si madhumuni ya mafundisho yetu leo. Madhumuni ya mafundisho yetu ni kujua madhumuni ya kanisa na kujua ya kuwa hatutakiwi kutengwa kama mtu moja kisiwani vyote vilikuwa kwa jili yake. Hatuwezi kuishi kwa jinsi hiyo. Tulipopokea wokovu, Mungu alituweka katika mwili wa Kristo – mwili wa waumini duniani. Tunahitajiana, na tunahitaji kukutana kwa pamoja kama kanisa la Mungu kutiana moyo sisi kwa sisi na kutumikiana sisi kwa sisi kwa vipawa vyetu vya kiroho ambavyo Mungu ametupa. Ninakutia moyo, kutana kwa pamoja leo na watu wa Mungu.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Waebrania 10:25. Nini ambacho hatutakiwi kukiacha? ____________________
____________________________________________
____________________

2. Soma Matendo 5:42. Kila siku hekaluni na kwenye kila nyumba,Yesu ali ______________ na ______________________
____________________________________________
______.

3. Soma Matendo 2:42. Ni mambo gani manne ambayo kanisa la kwanza liliendelea kuyafanya? __________________
____________________________________________
__________

4. Soma Matendo 2:44-45. Kanisa la kwanza liliendelea kutoa fedha kujenga eneo la kuegeshea magari la kanisa. Kweli au Si Kweli.

5. Soma 1 Wakorintho 12:28. Orodhesha aina nane tofauti za vipawa ambavuo Mungu ameviweka kwenye kanisa Lake. _________
____________________________________________
____________________

6. Soma 1 Wakorintho 14:26. Wakati watu wa Mungu walipokutana kwa pamoja kama kanisa, kulikuwa na uhuru wa kuonyesha vipawa vyao. Taja mambo matano ambayo yalitokea walipokutana. ________________
____________________________________________
____________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Waebrania 10:25

"Wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia."

### Matendo 5:42

"Na kila siku, ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo."

### Matendo 2:42

"Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali."

### Matendo 2:44-45

"[44] Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja, na kuwa na vitu vyote shirika,; [45] wakiuza mali zao, na vitu vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja.."

### 1 Wakorintho 12:28

"Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha."

### 1 Wakorintho 14:26

"Basi, ndugu, imekuwaje? Mkutanapo pamoja, kila mmoja ana zaburi, ana fundisho, ana ufunuo, ana lugha, ana tafsiri. Mambo yote na yatendeke kwa kusudi la kujenga."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

7. Soma Matendo 6:1. Kanisa la kwanza la Agano Jipya walishiriki chakula cha kila siku na _________.

8. Soma Yakobo 1:27. Aina pekee ya dini ambayo Mungu anaijali ni dini ambayo __ __________________________________ _________________________________.

9. Soma 1 Timotheo 5:9-11. Wajane ambao walikuwa wakisaidiwa na kanisa la kwanza la Agano Jipya ilibidi wafikie kigezo gani? __________________________________ __________________________________

10. Soma 1 Wakorintho 9:14. Pamoja na kanisa kuwasaidia wajane, yatima, na masikini, pia liliwasaidia _______________ __________________________________

11. Soma Mathayo 25:35-40. Ni kwa nini watu wanafikiri ya kua kutoa fedha kwenye sahani ya sadaka ndiyo njia pekee ya kumtolea Mungu? ___________________ ____________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Matendo 6:1

"Hata siku zile wanafunzi walipokuwa wakiongezeka hesabu yao, palikuwa na manung'uniko ya Wayahudi wa Kiyunani juu ya Waebrania kwa sababu wajane wao walisahauliwa katika huduma ya kila siku."

### Yakobo 1:27

"Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa."

### 1 Timotheo 5:9-11

"[9] Mjane asiandikwe isipokuwa umri wake amepata miaka sitini; naye amekuwa mke wa mume mmoja;, [10] Naye ameshuhudiwa kwa matendo mema; ikiwa amelea watoto, ikiwa amekaribisha wageni, ikiwa amewaosha watakatifu miguu, ikiwa amewasaidia wateswao, ikiwa amefuata kwa bidii kila tendo jema. [11] Bali wajane walio vijana ukatae kuwaandika hao, maana, wakizidiwa na tamaa kinyume cha Kristo, wataka kuolewa."

### 1 Wakorintho 9:14

"Na Bwana vivyo hivyo ameamuru kwamba wale waihubirio Injili wapate riziki kwa hiyo Injili."

### Mathayo 25:35-40

"[35] kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha: [36] nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia. [37] Ndipo wenye haki watakapomjibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona una njaa, tukakulisha,

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

12. Soma Matendo 4:32-35 na Methali 3:9-10. Wazee wa kanisa la kwanza na wachungaji walifanyia nini fedha zao? ______________
_____________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

au una kiu tukakunywesha? [38] Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha, au u uchi, tukakuvika? [39] Ni lini tena tulipokuona u mgonjwa, au kifungoni, tukakujia? [40] Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi"

### Matendo 4:32-35

"[32] Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja; wala hapana mmoja aliyesema ya kuwa kitu cho chote alicho nacho ni mali yake mwenyewe; bali walikuwa na vitu vyote shirika.. [33] Na mitume wakatoa ushuhuda wa kufufuka kwake Yesu kwa nguvu nyingi, na neema nyingi ikawa juu yao wote. [34] Wala hapakuwa na mtu mmoja miongoni mwao mwenye mahitaji; kwa sababu watu wote waliokuwa na viwanja au nyumba waliviuza, wakaileta thamani ya vitu vile vilivyouzwa [35] wakaiweka miguuni pa mitume; kila mtu akagawiwa kwa kadiri ya alivyohitaji."

### Methali 3:9-10

"[9] Mheshimu Bwana kwa mali yako, Na kwa malimbuko ya mazao yako yote: [10] Ndipo ghala zako zitakapojazwa kwa wingi, Na mashinikizo yako yatafurika divai mpya."

# MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Waebrania 10:25. Nini ambacho hatutakiwi kukiacha? **Sisi kukusanyika kama waumini.**

2. Soma Matendo 5:42. Kila siku hekaluni na kwenye kila nyumba,Yesu ali **fundisha** na **alihubiri.**

3. Soma Matendo 2:42. Ni mambo gani manne ambayo kanisa la kwanza liliendelea kuyafanya? **Waliendelea katika mafundisho ya mitume, ushirika, wakiumega mkate (wakila pamoja na kushirikiana meza ya Bwana), na maombi.**

4. Soma Matendo 2:44-45. Kanisa la kwanza liliendelea kutoa fedha kujenga eneo la kuegeshea magari la kanisa. **Si Kweli.**

5. Soma 1 Wakorintho 12:28. Orodhesha aina nane tofauti za vipawa ambavuo Mungu ameviweka kwenye kanisa Lake. **Mitume, manabii, waalimu, wale wafanyao miujiza, wale walio na karama ya uponyaji, kusaidia, wale wenye kipawa cha utawala, na wale wanaonena katika lugha isiyofahamika.**

6. Soma 1 Wakorintho 14:26. Wakati watu wa Mungu walipokutana kwa pamoja kama kanisa, kulikuwa na uhuru wa kuonyesha vipawa vyao. Taja mambo matano ambayo yalitokea walipokutana. **Mtu moja alikuwa na wimbo, mwengine mafundisho, mwengine angesema maono ambayo Mungu amempa, mwengine angenena katika lugha isiyofahammika, na mwengine angeelezea lugha ile isiyojulikana ina maanisha nini.**

7. Soma Matendo 6:1. Kanisa la kwanza la Agano Jipya walishiriki chakula cha kila siku na **wajane.**

8. Soma Yakobo 1:27. Aina pekee ya dini ambayo Mungu anaijali ni dini ambayo **inawajali yatima na wajane katika shida zao.**

9. Soma 1 Timotheo 5:9-11. Wajane ambao walikuwa wakisaidiwa na kanisa la kwanza la Agano Jipya ilibidi wafikie kigezo gani? **"Mjane anayewekwa kwenye orodha ya kusaidiwa ni lazima awe ni mwanamke mwenye angalau miaka sitini na alikuwa mwaminifu kwa mume wake. Lazima awe anaheshimika vyema na kila mmoja kwa sababu ya mema ambayo amefanya. Je amewalea watoto wake? Je amekuwa ni mkarimu kwa wageni? Je amewatumikia vyema Wakristo wengine kwa unyenyekevu? Je amewasaidia wale waliyoko shidani? Je amekuwa tayari mar azote kutenda mema? Wajane waliyo vijana hawapaswi kuwa kwenye orodha …" (1 Timotheo 5:9-11,** *Tafsiri ya New Living***).**

10. Soma 1 Wakorintho 9:14. Pamoja na kanisa kuwasaidia wajane, yatima, na masikini, pia liliwasaidia **wale waliyohudumu Neno.**

11. Soma Mathayo 25:35-40. Ni kwa nini watu wanafikiri ya kua kutoa fedha kwenye sahani ya sadaka ndiyo njia pekee ya kumtolea Mungu? **Kwa sababu hicho ndicho ambacho wamekuwa wakifundishwa.**

12. Soma Matendo 4:32-35 na Methali 3:9-10. Wazee wa kanisa la kwanza na wachungaji walifanyia nini fedha zao? **Waliwapa wale wenye uhitaji, wakimheshimu Bwana kwa utoaji wao.**

DARAJA 2

# SOMO 5
# UKOMBOZI

*Na Don Krow*

Leo tunakwenda kuzungumza kuhusu elimu ya mapepo. Yesu alitumia huduma Yake hapa duniani akifukuza mapepo, akiwaponya wagonjwa, akifufua wafu, na akifanya miujiza myengine. Takriban moja ya nne ya Huduma yake ilitumika kufukuza roho chafu kutoka kwa watu. Biblia inatuambia katika Matendo 10:38, *"Habari za Yesu wa Nazareti, jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja Naye."* Pia, 1 Yohana 3:8 inasema, *"Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi."* Nilikuwa nina mtazamo tofauti kuhusu elimu hii ya mapepo – ya kuwa mapepo, roho zenye uovu, roho chafu, maShetani chochote kile ambacho unataka kuwaita – walitokea tu nchini India au nchi za ulimwengu wa tatu ambapo watu hawamwabudu Mungu wa Kweli na aliye hai bali wanaabudu sanamu. Nilikuwa siko sahihi.

Ninataka nikuelezee kuhusu uzoefu nilioupata miaka michache iliyopita katika kanisa moja huko Dallas, Texas. Watu wote walikuwa wanaimba mara ghafla binti huyu akaanguka tu sakafuni. Ilionekana kana kwamba alikuwa na kifafa. Pale palitokea kuwepo na daktari (tabibu) ambaye jina lake alikuwa akiitwa Dk. Rice. Baadhi ya watu katika kanisa walikuwa wakiishi umbali mfupi tu kutoka kanisani, na akasema apelekwe nyumbani kwa watu hao ili aweze kumfanyia uchunguzi. Tulipomfikisha kwenye nyumba hiyo, binti huyo alikuwa kama paka wa mwituni! Macho yake yalikuwa yamekuwa makubwa, na kulikuwa na sauti yenye nguvu ya kiume ikizungumza kutoka ndani ya binti huyu mdogo kijana, ambaye pengine uzito wake ulikuwa chini ya kilo arubaini na tano, Ghafla, kitu hiki kikaanza kunishambulia kwa maneno, kikisema maneno kama, "UNAKWENDA KUZIMU!" Nikasema, "Hapana, Siendi." Nilikuwa naogopa kwa kuwa sijawahi kuona kitu chochote kama hiki kabla. Kikasema,"NDIYO, UNAKWENDA KUZIMU," na Nikasema, "Hapana, Siendi. Siendi kuzimu." Kilionekana kuwa na nguvu au mamlaka juu yangu, na sikujua nini cha kufanya au jinsi ya kushughulikia kitu hicho ambacho kilikuwa ndani ya binti huyu going to hell."

Moja wa marafiki zangu wa karibu alikuwa na hofu sana akaondoka mara moja, na hapo nilikuwapo. Nikawaza, *Sasa ninafanya nini?* Binti huyo alikuwa na nguvu zisizo za kawaida, na akaanza kusema maneno kama vile ya lugha ya Kijerumani ambacho hakuwahi kujifunza – aina zote za madhihirisho ya nguvu za Shetani zilitoka ndani yake. Alikuwa amepagawa na mapepo, na ingawa sikujua nini cha kufanya mara zote niliamini ya kuwa Biblia ina nguvu. Ni kama vile ambapo wakati ulikuwa mtoto na ukatazama filamu zile za kutisha za Dracula. Jitu lenye makucha linalonyonya damu lingekuja kwa mtu, na ghafla mtu huyo atatoa msalaba na jitu hilo litaondoka "ARRRGH!" Hivyo ndivyo niliwaza kuhusu Biblia. Nilijua ilikuwa na nguvu, lakini sikujua jinsi ya kuipata nguvu hiyo kutoka kwenye Biblia. Neema ya Mungu ilinisaidia, kwa sababu nilikuwa sijawahi kupitia kitu chochote kama hiki kabla. Nikafungua Biblia yangu kwenye Agano Jipya na ikatokea nimefungua kitabu cha Wafilipi. Nikaanza kusoma katika sura ya 2 mistari ya 8-11, *"Tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba. Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba."*

Pepo likasema, "Usiseme hiyo! Siwezi kuvumilia maneno hayo! Usisema hiyo!" Nikadhani, *Mwitikio wa aina gani!* Hivyo nikasema, "Vyema, katika Jina la Yesu, kila goti lazima lipigwe – vitu vilivyoko mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi." "Usiseme hivyo! Siwezi kuvumilia maneno haya! Usiseme hivyo, usiseme hivyo!" akapiga kelele. Nikawaza, *Huyu Shetani anachanganyikiwa ndani ya binti huyu, na ninchokifanya ni kusoma Neno la Mungu tu!* Hivyo Nikasoma tena, *"Tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba. Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe."* Tena, kukawa na mwitikio ule ule; "Usiseme hivyo! Siwezi kuvumilia maneno hayo!" Halafu pepo likamshika binti yule kwa masikio yake, na binti akasema, "Usiseme hivyo! Siwezi kuvumilia maneno hayo, usiseme hivyo!" Shetani akamtupa binti yule chini mbele yangu, na akaanza kutii katika Jina la Yesu. Na nikasema, "Katika Jina la Yesu kila goti litapigwa, iwe ni mbinguni au duniani au chini ya nchi."

Muda mfupi tu kabla, Shetani alikuwa na mamlaka na nguvu juu yangu. Nilifikiria angenichapa, angenipiga, na kunitupa nje ya pale – Sikujua! Nilichokijua tu ni kuwa Biblia ina nguvu, na nikaifungua na kuanza kuisoma. Biblia inasema katika Waefeso 6:17, *"Tena … na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu."* Unaona, kuna silaha ya kujikinga ambayo iko kama upanga ambayo itamkata na kumuumiza adui. Ni Upanga wa Roho, Neno la Mungu. Je unakumbuka wakati Yesu alipojaribiwa? Shetani alikuja Kwake na kusema, "Nitakupa falme zote za ulimwengu ikiwa kama utanisujudia na kuniabudu." Yesu akasema, *"Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake."*

(Matt. 4:10). Halafu Shetani akamjaribu, na akamjaribu tena, na Yesu akasema "Imeandikwa, Shetani … imeandikwa," na halafu akanukuu Neno la Mungu. Alitumia Upanga wa Roho, na Biblia inasema Shetani akaondoka na akamwacha kwa kipindi.

Silaha pekee tuliyo nayo tunayoweza kumshinda adui kwayo ni Upanga wa Roho, ambao ni Neno la Mungu. Je unajua ya kuwa nilijifunza kutoka kwenye hilo? Nilijifunza hili: Kila mara ninapotaka kujifunza Neno, Ninafikiria kuhusu nina njaa kiasi gani na inabidi niende kutafuta kitu cha kula, au Ninafikiria kuhusu vitu vyote ambavyo sikuvifanya siku ile. Ninafahamu ya kuwa wale waliyoko katika darasa hili la wanafunzi wa Yesu watakuwa na aina zote za sababu kwa nini hawawezi kuja. Hatimaye nilikuja kujua ni kwa nini. Kuna kitu kwenye Biblia ambacho Mungu anataka tukijue na Shetani hataki sisi tukijue. Hivyo kila mara unapokuja kujifunza Neno la Mungu, au kufanya darasa la uanafunzi wa Yesu, kuna kitu katika Neno la Mungu ambacho adui hataki wewe ukifahamu – hataki wewe umjue Mungu aliyeko nyuma ya maneno haya.

Kuna ufalme wa giza, na kuna ufalme wa Mwana wake mpendwa. Katika Wakolosai 1:13, Paulo anasema, *"Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake."* Uko katika ufalme gani? Ufalme ni mahali ambapo mtu ana utawala na anatawala. Yesu Kristo ni mfalme. Umeshawahi kumpa maisha Yako? Je unamfuata Yeye leo, au unaviruhusu vitu vyengine viwe na nafasi ya mbele katika maisha yako? Yesu alisema hivi katika Luka 6:46, *"Na kwa nini mnaniita, Bwana, Bwana, walakini hamyatendi nisemayo?"* Anataka kutawala katika maisha yako, awe nambari moja. Kuna ufalme wa giza ambao unajaribu kumzuia asipate nafasi hiyo ya kutawala, sehemu ile ya kutawala maishani mwako. Sababu ya hili ni kuwa adui anataka kuinuka katika mahali hapo pa kutawala. Mgeukie Yesu leo kwa moyo wako wote, na utambue ya kuwa kuna adui. Jina lake ni Shetani na ana nguvu za kimapepo, lakini Biblia inatuambia tunayo mamlaka juu yake.

Yesu alisema katika Mathayo 10:8, *"Ponyeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure."* Hubirini injili ya ufalme, na mnapokwenda mnayo mamlaka juu ya adui. Usimruhusu tena adui akuambie chochote nje ya kile ambacho Mungu anacho kwa ajili ya maisha yako. Mfanye Yesu Bwana na nambari moja katika maisha yako. Kamwe hutajuta.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Waefeso 6:12. Mstari huu unaelezeaje mgogoro wetu wa kiroho na ulimwengu wa kipepo? ______________________
______________________________________

2. Soma Marko 16:17. Mstari huu unatufundisha nini kuhusu mamlaka ya anayeamini? ______________________________
__________________________________________

3. Soma Yakobo 4:7. Mtu anayetafuta kukombolewa kutoka kwenye mapepo anapaswa kufanya nini? _____________________
_____________________________________________
___________________________

4. Soma Yakobo 1:14. Shetani anatudanganyaje katika kufanya kitu kiovu kionekane cha kutamanika? ________________
_____________________________________________
___________________________________

5. Soma Warumi 6:13. Ikiwa mtu atayajaza maisha yake na mambo ya Kristo, Mapepeo watakosa raha na kuondoka wao wenyewe. Mstari huu unatuambia tufanye nini? ________
_____________________________________________
______________________________

6. Soma Warumi 13:14. Mapepo hujilisha kwenye kazi za mwili, hivyo wafanye wawe na njaa kwa kutembea katika njia za Mungu za upendo na usafi. Hatupaswi kufanya ___________ kwa ajili ya mwili.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Waefeso 6:12

"Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho."

### Marko 16:17

"Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;."

### Yakobo 4:7

"Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia.."

### Yakobo 1:14

"Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa."

### Warumi 6:13

"Wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki."

### Warumi 13:14

"Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tamaa zake."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

7. Soma Luka 10:17-19. Yesu kamwe hatuambii tumuombe Yeye ili kufukuza mapepo. Ametupa mamlaka. Mstari huu unatuambia ya kuwa tunayo nguvu na mamlaka juu ya______
________________________________________
____________________________.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Luka 10:17-19

"[17] Ndipo wale sabini waliporudi kwa furaha, wakisema, Bwana, hata pepo wanatutii kwa jina lako. [18] Akawaambia, Nilimwona Shetani, akianguka kutoka mbinguni kama umeme. [19] Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru."

# MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Waefeso 6:12. Mstari huu unaelezeaje mgogoro wetu wa kiroho na ulimwengu wa kipepo? **Inaelezewa kama mashindano.**
2. Soma Marko 16:17. Mstari huu unatufundisha nini kuhusu mamlaka ya anayeamini? **Tunayo mamlaka katika Jina la Yesu kufukuza mapepo.**
3. Soma Yakobo 4:7. Mtu anayetafuta kukombolewa kutoka kwenye mapepo anapaswa kufanya nini? **Wamtii Mungu na kumpinga Shetani.**
4. Soma Yakobo 1:14. Shetani anatudanganyaje katika kufanya kitu kiovu kionekane cha kutamanika? **Anafanya kazi na tamaa zetu wenyewe (kukifanya kitu kiovu kiwe cha kutamanika).**
5. Soma Warumi 6:13. Ikiwa mtu atayajaza maisha yake na mambo ya Kristo, Mapepeo watakosa raha na kuondoka wao wenyewe. Mstari huu unatuambia tufanye nini? **Usikubaliane na dhambi bali umtii Mungu. Tutiishe viungo vyetu(viungo vya miili yetu) kama vyombo vya kufanya yaliyo sahihi.**
6. Soma Warumi 13:14. Mapepo hujilisha kwenye kazi za mwili, hivyo wafanye wawe na njaa kwa kutembea katika njia za Mungu za upendo na usafi. Hatupaswi kutoa **nafasi** kwa ajili ya mwili.
7. Soma Luka 10:17-19. Yesu kamwe hatuambii tumuombe Yeye ili kufukuza mapepo. Ametupa mamlaka. Mstari huu unatuambia ya kuwa tunayo nguvu na mamlaka juu ya **nguvu zote za adui.**

DARAJA 2

# SOMO 6
# MAMLAKA YA MUUMINI

*Na Andrew Wommack*

Katika kipindi cha leo, Ninataka kuzungumzia kuhusu mamlaka ambayo Mungu ametupa kama tunaoamini. Ili kulishughulikia hili, Itabidi tusishughulike tu na mamlaka tuliyo nayo lakini mamlaka ya Shetani. Amefumuliwa nje ya uwiano. Wakristo wameongozwa kuamini ya kuwa tunapigana na kiumbe ambaye nguvu yake ni kubwa kuliko ya kwetu, Na kwa ugumu sana tuna weza kupambana naye. Hivyo sivyo ambavyo maandiko yanafundisha kabisa. Inasema kaika Waefeso 6:12, *"Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho."* Hivyo Shetani ndiye swala hapa; yuko. Ana mfumo wa utawala wa falme na mamlaka ambayo tunashughulika nayo, lakini katika mstari kabla ya huo, inasema ya kuwa inabidi tusimame dhidi ya mbinu za Shetani. Nguvu pekee ambayo Shetani anayo dhidi yetu ni uongo. Hana nguvu ya kutushinda tu.

Katika Mwanzo 3 tunaona ya kuwa wakati jaribu la kwanza lilipokuja dhidi ya Adamu na Hawa, Shetani hakuja na nguvu kubwa. Kwa mfano, badala ya kuingia ndani ya mnyama mkubwa au tembo, kuweka mguu wake kwenye kichwa cha Adamu, akiwatisha, na kusema "Mnitumikie ama sivyo…" akaingia ndani ya nyoka, kiumbe mwerevu ambaye Mungu alimuumba. Neno "mwerevu" lina maanisha "hila, mdanganyifu, au mjanja". Sababu kwa nini Shetani alikuja kupitia nyoka ilikuwa ni kwa sababu hakika hakuwa na nguvu ya kumlazimisha Adamu na Hawa kufanya chochote. Aliweza tu kudanganya. Akaja kinyume na asili na tabia ya Mungu na akaanza kumshutumu, akisema, "Mungu hakika hawapendi – Anazuia vitu ili usivipate." Alitumia udanganyifu kumjaribu Adamu na Hawa watende dhambi dhidi ya Mungu. Walikuwa ndiyo wenye mamalaka yote, na sababu kwa nini Shetani ilibidi afanye kwa jinsi hii ni kwa sababu hakuwa na nguvu ya kuja kinyume na Mungu

Kuna mengi zaidi sina muda wa kwenda ndani zaidi, lakini moja ya jambo ninalotaka kulieleza ni kuhusu mamlaka ya muumini, unatakiwa kutambua ya kuwa Shetani hana nguvu yoyote na mamlaka juu yako. Yeye ni adui aliyeshindwa. Nguvu yake pekee dhidi yako ni kuja kinyume na wewe kwa uongo na ulaghai. Ikiwa kama maisha yako yana angamizwa, unaweza

kusema "Shetani ndiye anayenishambulia," lakini wewe ndiye unayempa silaha. Wewe ndiye unayepaswa kujibu dhidi ya uongo wake na ulaghai. Ikiwa kama hukumsikiliza na kumkubali Shetani, asingekuwa na njia za ndani au nguvu juu yako. Katika 2 Wakorintho 10:3-5 inasema, *"Maana ingawa tunaenenda katika mwili, hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili: (Maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome, tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo;."* Maandiko haya yanazungumzia kuhusu silaha zako za vita, na kila silaha iliyotajwa inarejea kwenye nia yako, ikishughulika na mawazo. Shetani hana nguvu ya kufanya chochote kwako isipokuwa kupitia uongo.

Ninataka kwa haraka kuweka muhtasari wa baadhi ya mambo. Japo mwanzo Mungu, bila shaka, alikuwa na mamlaka yote. Nguvu zote na mamlaka yanapaswa kutoka kwa Mungu kwa sababu yeye ndiye pekee mwenye nguvu. Kila kitu chengine kinatoka Kwake. Alipoumba mbingu na nchi, Alikuwa na nguvu zote na mamlaka. Halafu katika Mwanzo 1:26, Wakati Mungu alipomuumba Adamu na Hawa, Alisema, *"Na wakatawale … juu ya ulimwengu wote."* Weka hilo pamoja na Zaburi 115:16, ambayo inasema, *"Mbingu ni mbingu za BWANA, Bali nchi amewapa wanadamu.:."* Mungu alikuwa na umiliki wa kila kitu kwa haki ya kwa Muumbaji, lakini alitoa utawala, au mamlaka, ulimwenguni kwa wanadamu wa kawaida. Shetani hajawahi kuwa na haki na nguvu ya kutawala dunia. Aliipata kwa kupitia kumdanganya mwanadamu atende dhambi. Mungu alimpa mwanadamu nguvu hiyo, na wakati mwanadamu alipoanguka, alipoteza mamlaka yake aliyopewa na Mungu na nguvu zake kwa Shetani. Shetani kamwe hakuwahi kupewa nguvu na Mungu ili kumkandamiza mwanadamu au kutawala ulimwengu huu.

Maandiko yanasema ya kuwa Shetani ndiye mungu wa ulimwengu huu, lakini si kwa sababu Mungu alimuumba kuwa ni mungu wa ulimwengu huu. Mungu kamwe hakuwahi kumuweka Shetani katika nafasi iliyo juu ya mwanadamu. Alimpa mwanadamu utawala na mamlaka juu ya ulimwengu huu. Sababu pekee inayomfanya Shetani kuweza kutukandamiza, kutawala, au kusababisha matatizo anayoyafanya ni kwa sababu watu walimkabidhi mamlaka yao waliyopewa na Mungu. Hili liliteta tatizo haswa kwa Mungu, kwa sababu alikuwa ni roho, na alitoa mamlaka juu ya ulimwengu huu na juu ya wanadamu. Ni watu waliyokuwa na miili ya kibinadamu pekee walikuwa na mamlaka na nguvu ya kutawala na kutumia ushawishi katika ulimwengu huu. Shetani ilibidi aje kwetu na kutufanya sisi tuachie mamlaka yetu kwake. Na hiyo ndiyo sababu anapenda kukaa katika mwili. Katika maandiko, mapepo ilibidi wapate mwili ili kumvamia mtu kwa sababu Shetani hawezi kufanya chochote mpaka iwe anatumia mwili wa mwanadamu. Kwa kuwa Mungu alikuwa ni Roho na alishatoa mamalaka kwa wanadamu wenye mwili, sasa kwa kumaanisha mikono yake ilikuwa imefungwa. Haikuwa kwa sababu Mungu hakuwa na nguvu na mamlaka lakini kwa sababu ya uaminifu Wake. Aliwapa mamlaka wandamu, na kuwa mkweli katika Neno lake Mwenyewe, Hakuweza tu kulirejesha

na kusema, "Hivi sivyo ambavyo nilitaka; pumzika, acha, tunakwenda kuifanya tena." Hapana, Mungu alijifunga Yeye mwenyewe kwa Neno lake. Katika historia yote Alimtafuta mtu ambaye angeweza kuendana naye, lakini tatizo lilikuwa ni kuwa watu wote walikuwa ni mafisadi na walishajitoa wao wenyewe kwa Shetani. Hivyo nini alichopaswa kukifanya?

Hatimaye alichokifanya Mungu ilikuwa ni kuja ulimwenguni Yeye mwenyewe na kufanyika mwanadamu. Hili ni la ajabu sana utakapolielewa, kwa sababu sasa Shetani alikuwa matatizoni. Amekuwa akitumia nguvu ya mwanadamu, na Mungu asingeingilia kati moja kwa moja kuyatatua matatizo haya yote, kwa sababu mwanadamu kwa kutaka kwake, kisheria alikabidhi Shetani mamlaka yake aliyopewa na Mungu. Shetani alikosea katika kile alichokifanya, lakini mwanadamu akampa mamlaka na nguvu ambazo zilikuwa ni zao. Lakini sasa, hapa akaja Mungu, na Hakuwa tena Roho tu lakini alikuwa katika mfano wa mwili. Hili lina muweka Shetani katika hali mbaya, kwa sababu si tu kuwa Mungu alikuwa na mamlaka mbinguni, lakini kwa kufanyika wanadamu ilimpa mamlaka hapa duniani. Yesu alisema katika Yohana 5:26-27, *"Maana kama vile Baba alivyo na uzima nafsini mwake, vivyo hivyo alimpa na Mwana kuwa na uzima nafsini mwake. Naye akampa amri ya kufanya hukumu kwa sababu ni Mwana wa Adamu."* Alikuwa akimaanisha mwili wake.

Yesu alikuja na kuyatumia mamlaka aliyopewa na Mungu. Shetani alimjaribu, na kamwe Yesu hakumkubalia. Shetani alipoteza katika kila vita na Yeye. Halafu Yesu akazichukua dhambi zetu, akafa kwa ajili yao, akaenda kuzimu, akafufuka tena, na akasema katika Mathayo 28:18, "*Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na.*" Alirejesha tena mamalaka ambayo Mungu alimpa mwanadamu, ambayo mwanadamu aliyatumia mamlaka hayo vibaya, na kama Mungu katika mwili, Yesu sasa alikuwa na mamlaka yote mbinguni na duniani. Katika mstari unaofuata Alisema, "Sasa muende, na mfanye mambo haya." Alichokuwa akikisema ni, "Sasa ninayo mamlaka yote mbinguni na duniani, nami ninashirikiana nawe." Wakati huu, hata hivyo, kuna tofauti ya kipekee katika mamlaka Mungu ameturudishia kama waumini. Ni mamlaka ya pamoja kati yetu na Bwana Yesu Kristo. Hatupewi tena yote kama alivyopewa Adamu na Hawa. Wangeweza kuyatoa mamlaka yao, kumruhusu awakandamize,na kimsingi wawe bila tumaini, lakini leo mamlaka yetu ianashirikishwa na Bwana Yesu Kristo. Ni kama kuwa na akaunti ya Benki ya pamoja ambayo inahitaji sahihi zote ili kuweza kutoa fedha. Mamlaka yetu inashirikishwa na Bwana Yesu, na Mamlaka Yake inashirikishwa na Kanisa.

Ingawa tunaweza kushindwa, Mungu kamwe tena hatakwenda kuyaachia mamlaka haya kwa Shetani. Shetani kabisa hana nguvu. Hana uwezo wa kufanya chochote maishani mwako isipokuwa kile ambacho atakudanganya na kile ambacho utampa kwa hiari yako. Unaweza kumpa mamlaka maishani mwako, unaweza kuteseka wewe binafsi kwa ajili ya hilo, lakini mamalaka aliyopewa na Mungu kamwe haitakwenda tena kwa Shetani. Sasa inashirikishwa kati

yetu na Bwana Yesu, na Atabaki kuwa mwaminifu pasipo kujali chochote. Unahitaji kutambua ya kuwa wewe ndiye ambaye sasa unayo mamlaka na nguvu. Shetani anapambana nawe kwa kupitia mawazo, na silaha zako ziko ambavyo unaweza kuyapeleka mawazo haya utekani. Unaweza kutambua ya kuwa si sahihi kwa Shetani kukukandamiza wewe kimwili na tafuta maandiko yana nini cha kusema kuhusu uponyaji. Yohana 8:32 inasema, *"Tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru."* Ninyi ndiyo wenye nguvu na mamlaka. Mungu amekupa wewe na kitu pekee kinachokuzuia usifanyie mazoezi ni kuwa bado hujapelekwa utekani. Hujawahi kutumia silaha hizi za kiroho kufanya upya nia yako na kutambua kile ulicho nacho. Inatia moyo kujua ya kuwa wewe ni moja mwenye mamlaka na nguvu.

Ninaomba ya kuwa utayachukua haya, utatafakari juu yake, na Mungu atakupa mafunuo ya kuwa wewe ni mmoja ambaye Shetani atakutetemekea. Hupaswi kumtetemekea Shetani, Kwa kuwa wewe ndiwe mwenye nguvu na mamlaka uliyopewa na Mungu. Ikiwa kama utampinga Shetani, atakukimbia (Yakobo 4:7).

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Mwanzo 3:1. Shetani yuko, lakini nguvu yake halisi imo katika uwezo wake ili kutudanganya. Nini ambacho nyoka (Shetani) alijaribu kumfanya Hawa akitilie mashaka? ______________________________
_______________________________________
___________

2. Soma Mwanzo 3:1. Ni kwa nini unafikiri ya kuwa Shetani alitumia uongo? ________
_______________________________________
_________________________________

3. Soma Mwanzo 1:26, 28. Nani alimpa mwanadamu mamlaka yake?
_____________________________

4. Soma Zaburi 8:4-8. Mungu alimuumbaje mwanadamu? _________________________
___________

5. Soma 2 Wakorintho 4:4. Nini kilichotokea, ambacho andiko hili linakionyesha? ______
_______________________________________
___________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Mwanzo 3:1

"Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?"

### Mwanzo 1:26

"Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi." Mwanzo 1:28 "Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi."

### Zaburi 8:4-8

"[4] Mtu ni kitu gani hata umkumbuke, Na binadamu hata umwangalie? [5] Umemfanya mdogo punde kuliko Mungu; Umemvika taji ya utukufu na heshima; [6] Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; Umevitia vitu vyote chini ya miguu yake. [7] Kondoo, na ng'ombe wote pia; Naam, na wanyama wa kondeni; [8] Ndege wa angani, na samaki wa baharini; Na kila kipitacho njia za baharini."

### 2 Wakorintho 4:4

"Ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake Kristo aliye sura yake Mungu."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

6. Soma Mathayo 4:8-9. Je mistari hii inasisitiza kipengele hiki? ____________________

7. Soma Mathayo 28:18. Baada yakufa na kufufuka kwa Yesu, nani sasa mwenye mamlaka yote mbinguni na duniani? ____ ________________________________ _

8. Soma Mathayo 28:18-19. Ni nani aliyepewa mamlaka, kufuatana na msatri huu? ______________________________ ______________________________

9. Soma Waefeso 1:19. Na ubora wa ukuu wa uweza wa Mungu umeelekezwa kwa nani? ________________________________ ________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Mathayo 4:8-9

"[8] Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za ulimwengu, na fahari yake; [9] akamwambia, Haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia."

### Mathayo 28:18

"Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.."

### Mathayo 28:19

"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu."

### Waefeso 1:19

"Na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake."

# MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Mwanzo 3:1. Shetani yuko, lakini nguvu yake halisi imo katika uwezo wake ili kutudanganya. Nini ambacho nyoka (Shetani) alijaribu kumfanya Hawa akitilie mashaka? **Neno la Mungu (Je Mungu amesema?).**

2. Soma Mwanzo 3:1. Ni kwa nini unafikiri ya kuwa Shetani alitumia uongo? **Hakuweza kuwalazimisha kutokutii. Ilibidi awadanganye ili waachie mamlaka yao.**

3. Soma Mwanzo 1:26, 28. Nani alimpa mwanadamu mamlaka yake? **Mungu.**

4. Soma Zaburi 8:4-8. Mungu alimuumbaje mwanadamu? **Akiwa na utawala juu ya kazi ya Mikono Yake (Mungu).**

5. Soma 2 Wakorintho 4:4. Nini kilichotokea, ambacho andiko hili linakionyesha? **Ya kuwa Shetani alichukua mamlaka ya mwanadamu na akafanyika mungu wa ulimwengu huu (mfumo huu, au zama).**

6. Soma Mathayo 4:8-9. Je mistari hii inasisitiza kipengele hiki? **Ndiyo.**

7. Soma Mathayo 28:18. Baada yakufa na kufufuka kwa Yesu, nani sasa mwenye mamlaka yote mbinguni na duniani? **Yesu.**

8. Soma Mathayo 28:18-19. Ni nani aliyepewa mamlaka, kufuatana na msatri huu? **Muumini.**

9. Soma Waefeso 1:19. Na ubora wa ukuu wa uweza wa Mungu umeelekezwa kwa nani? **Kwetu sisi tunaoamini.**

DARAJA 2

# SOMO 7
# UPONYAJI KATIKA MSAMAHA

*Na Andrew Wommack*

Kipindi cha leo ni kuhusu uponyaji na ni kwa jinsi gani u sehemu ya kile ambacho Yesu tayari alisha kinunua kwa ajili yetu. Katika Marko 2 na Luka 5 Yesu alikuwa akifundisha kwenye nyumba iliyojaa watu wengi kiasi kwamba mtu aliyepooza aliteremshwa chini na rafiki zake pale Yesu alipokuwapo kupitia paa la nyumba, na Yesu kimuujiza akamponya. Katika Mathayo 8:14-16, baada ya Yesu akiwa amekwisha waponya watu, Biblia inasema, *"Hata Yesu alipofika nyumbani kwa Petro, akamwona mkwe wa Petro, mamaye mkewe, amelala kitandani hawezi homa. Akamgusa mkono, homa ikamwacha; naye akaondoka, akawatumikia. Hata kulipokuwa jioni, wakamletea wengi wenye pepo; akawatoa pepo kwa neno lake, akawaponya wote waliokuwa hawawezi."* Halafu mstari wa 17 unatoa sababu ya tukio hili: *"Ili litimie lile neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema, Mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, Na kuyachukua magonjwa yetu."* Katika tukio hili, Yesu alikuwa akiponya watu wengi, na mahususi inarejea nyuma kwenye na kunukuu kutoka kitabu cha Isaya 53:3-5: *"Alidharauliwa na kukataliwa na watu*[Huu ni unabii kuhusus Bwana Yesu Kristo]; *Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu. Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona*".

Hivi ni vifungu vyenye nguvu sana vya Maandiko. Baadhi ya watu huvichukua na kusema, "Subiri kidogo; huku ni kuongea katika ulimwengu wa roho." Kanisa nilikokuziwa halikuamini katika uponyaji wa mwili. Wangechukua andiko kama hili na kulifanya kuwa la kiroho – na kulitumia kwa kusema tulichubuliwa kihisia, na tunapo yatoa maisha yetu kwa Bwana, Hutuponya. Lakini kama tutaweka kifungu hiki pamoja na vifungu tulivyoanza navyo, milele inamalizia utumiaji wa maandiko haya. Ni kweli kuwa Yesu atakuponya kihisia na katika njia nyengine, lakini maandiko haya yanazungumza kuhusu uponyaji wa kimwili. Unaweza kuona ya kuwa kwa sababu katika 8:17, inasema ya kuwa uponyaji huu ambao ulifanyika ulikuwa ni utimilifu wa unabii uliyonenwa na Isaya ambao tumeusoma tu, *"Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona."* Inasema huu ulikuwa ni utimilifu kuwa Yeye Mwenyewe aliyachukua

madhaifu yetu na alibeba magonjwa yetu. Hii ni kuzungumzia kuhusu magonjwa ya mwilini, kuumizwa na maumivu. Yesu aliwaponya watu kimwili ili kutimiza maandikoyanayosema tumeponywa kwa kupigwa Kwake.

Biblia inaendelea kusema katika 1 Petro 2:24, *"Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa."* Hii iko katika wakati uliyopita. Yesu alikuja, na sehemu ya Alichokuja kukifanya ilikuwa ni kuiponya miili yenu. Siudharau ukweli kuwa alikuja pia kuzisamehe dhambi zako. Hilo ni la muhimu, na msamaha wa dhambi ni kama mlango, mlango wa kuingia kwenye kila kitu, lakini hakuja tu kusamehe dhambi zako. Pia alikuja kuuponya mwili wako. Katika Kiyunani, neno lililotumika kwa ajili ya wokovu katika Agano Jipya ni sozo, neno linalobeba yote ambalo linatumika kwenye mambo mengi tofauti. Lakini kama ukiliangalia, pia linatafsiriwa kama "aliyeponywa." Yakobo 5:14 inasema, *"Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana. Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule."* Neno "kuokoa" kuna neno la Kiyunani sozo, na linazungumza kuhusu mgonjwa akiponywa kimwili katika mwili wake. Neno hili hili ambalo lilitafsiriwa msamaha wa dhambi mara mia kadhaa kwenye Agano Jipya pia lilitafsiriwa kama aliyeponywa.

Wakati Yesu alipowatuma wanafunzi wake katika Mathayo 10, amri aliyowapa ilikuwa ni kuwaponya wagonjwa, kuwatakasa wakoma, kuwafufua wafu, kufukuza mapepo, na kuihubiri Injili, Aliwaambia wawaponye wagonjwa, wawatakase wakoma, na kufukuza mapepo. Uponyaji ni sehemu ya kile ambacho Yesu alikuja kukikamilisha maishani mwako kama msamaha wa dhambi ulivyo.

Kwa jinsi hiyo hiyo ambavyo kamwe huwezi kuwaza ya kuwa Bwana atataka wewe utende dhambi ili akufundishe ya kuwa unaweza kujifunza kitu kupitia dhambi yako, Kamwe hatataka wewe uishi katika magonjwa. Mungu siye anayeleta magonjwa maishani mwako. Mara nyengine watu husema vitu kama, "Vyema, ugonjwa huu hakika ni Baraka kutoka kwa Mungu kwa sababu umenielekeza Kwake." Ni kweli kuwa katika nyakati za matatizo watu humgeukia Mungu, lakini hayatumi magonjwa ili akufundishe. Hata fanya hivyo tena wala kuweka dhambi kwako. Unaweza kujifunza kitu ikiwa kama utaendelea kuishi dhambini? Ikiwa kama utaishi maisha ya uasherati au ushoga na ukapata magonjwa, je unaweza kujifunza ya kuwa mtindo huo wa maisha haukuwa sahihi? Hakika unaweza, lakini Mungu hakukusababisha uishi maisha ya aina hiyo. Hakuweka dhambi maishani mwako, bado unaweza kujifunza kutokana na kutenda dhambi. Unaweza kukipiga kichwa chako dhidi ya ukuta na kujifunza kuwa hicho sicho kitu cha kufanya, lakini pia unaweza kujifunza hilo pasipo kukipiga kichwa chako kwenye ukuta. Si lazima ujifunze kila kitu kwa kujipiga piga. Mungu haweki magonjwa maishani mwako ili akunyenyekeze na akufundishe jambo. Yesu alikufa ili akusamehe dhambi zako na pia

akuponye magonjwa yako. Alizibebea dhambi zako kwenye mwili Wake mwenyewe, na kwa kupigwa kwake uliponywa.

Uponyaji wa Mungu unapatikana kwetu sisi sote na ni sehemu ya msamaha ambao Yesu alikufa ili aulete. Ikiwa kama hupokei uponyaji wako, Mungu hakasirishwi na wewe. Si lazima uponywe ili umpende Mungu. Unaweza kumpenda Mungu kwa moyo wako wote, na si kuamini katika uponyaji, na bado ukaenda mbinguni. Ukweli ni kuwa, unaweza kufika huko kwa haraka kwa kuwa hujui jinsi ya kutembea katika afya. Lakini unajua nini – unapatikana kwako. Yesu alikufa ili aulete. Mungu anataka wewe uwe mzima.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Mathayo 8:16-17. Yesu aliwaponya watu wangapi

2. Soma Isaya 53:3-5. Mistari hii inazungumzia kuhusu uponyaji wa aina gani? ______________________________ ______________________________ _______

3. Soma Mathayo 8:17. Nini kilichotokea kwenye magonjwa yetu na udhaifu wetu? ______________________________ ______________________________

4. Soma 1Petro 2:24. Ni mambo gani mawili mstari huu unayasema kuwa Yesu alitufanyia? ______________________________ ______________________________ ______________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Mathayo 8:16-17

"[16] Hata kulipokuwa jioni, wakamletea wengi wenye pepo; akawatoa pepo kwa neno lake, akawaponya wote waliokuwa hawawezi, [17] Ili litimie lile neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema, Mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, Na kuyachukua magonjwa yetu."

### Isaya 53:3-5

"[3] Alidharauliwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu. [4] Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa. [5] Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona."

### Mathayo 8:17

"Ili litimie lile neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema, Mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, Na kuyachukua magonjwa yetu.."

### 1 Petro 2:24

"Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

5. Soma Yakobo 5:14-15. Neno "kutamwokoa" katika mstari wa 15 ni neno la Kiyunani sozo, ambalo linatafsiriwa kama "kukomboa, kulinda, kuponya, kuhifadhi, kuwa mzima." Ni neno lile lile ambalo Biblia inalizungumzia kama "wokovu." Kufuatana na mistari hii na maana ya Kiyunani kwa ajili ya wokovu, nini kilichomo kwenye wokovu? ________ ____________________________________ ____

6. Soma Mathayo 10:7. Wakati Yesu alipowatuma wanafunzi Wake, aliwaambia waseme nini? ________________________ ____________________________________

7. Soma Mathayo 10:8. Yesu aliwaambia wafanye nini? ________________________ ____________________________________ ______________

8. Soma Marko 16:15. Yesu aliwaambia wanafunzi wake wafanye nini? _________ ____________________________________ ______________________________

9. Soma Marko 16:16. Wale wanaoikubali Injili watafanya nini? _________________ ____________________________________ _____________________

10. Soma Marko 16:17. Ni ishara gani zitamfuata anaye amini? _______________ ____________________________________ ________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Yakobo 5:14-15

"[14] Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana. [15] Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa."

### Mathayo 10:7

"Na katika kuenenda kwenu, hubirini, mkisema, Ufalme wa mbinguni umekaribia.."

### Mathayo 10:8

"Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure."

### Marko 16:15

"Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.."

### Marko 16:16

"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa."

### Marko 16:17

"Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

11. Soma Marko 16:18. Ni ishara gani nyengine zitawafuata wanao amini? ______
______________________________________
____________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

Marko 16:18

"Watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Mathayo 8:16-17. Yesu aliwaponya watu wangapi? **Wote wale waliokuja Kwake.**
2. Soma Isaya 53:3-5. Mistari hii inazungumzia kuhusu uponyaji wa aina gani? **Ain azote za uponyaji (pamoja na uponyaji wa kimwili).**
3. Soma Mathayo 8:17. Nini kilichotokea kwenye magonjwa yetu na udhaifu wetu? **Yesu aliyabeba.**
4. Soma 1Petro 2:24. Ni mambo gani mawili mstari huu unayasema kuwa Yesu alitufanyia? **Alizibeba dhambi zetu mwilini mwake na alipigwa mijeledi kwa ajili ya uponyaji wetu.**
5. Soma Yakobo 5:14-15. Neno "kutamwokoa" katika mstari wa 15 ni neno la Kiyunani sozo, ambalo linatafsiriwa kama "kukomboa, kulinda, kuponya, kuhifadhi, kuwa mzima." Ni neno lile lile ambalo Biblia inalizungumzia kama "wokovu." Kufuatana na mistari hii na maana ya Kiyunani kwa ajili ya wokovu, nini kilichomo kwenye wokovu? **Uponyaji.**
6. Soma Mathayo 10:7. Wakati Yesu alipowatuma wanafunzi Wake, aliwaambia waseme nini? **Ufalme wa Mbinguni umekaribia.**
7. Soma Mathayo 10:8. Yesu aliwaambia wafanye nini? **Wawaponye wagonjwa, wafufue wafu, na kufukuza mapepo.**
8. Soma Marko 16:15. Yesu aliwaambia wanafunzi wake wafanye nini? **Kwenda kwenye mataifa yote na kuihubiri Injili kwa kila kiumbe.**
9. Soma Marko 16:16. Wale wanaoikubali Injili watafanya nini? **Wataamini na kubatizwa.**
10. Soma Marko 16:17. Ni ishara gani zitamfuata anaye amini? **Watatoa mapepo na kunena kwa lugha.**
11. Soma Marko 16:18. Ni ishara gani nyengine zitawafuata wanao amini? **Kuwa wekea mikono wagonjwa na kwaona wakipona.**

DARAJA 2

# SOMO 8
# VIZUIZI VYA UPONYAJI

*Na Andrew Wommack*

Katika somo langu lililopita, Nilizungumza kuhusu ukweli kuwa ni mapenzi ya Mungu kuponya, na ya kuwa uponyaji ni sehemu ya msamaha. Mengi yanaweza kusemwa, kwa sababu hata kama utakubali na kuliona kwenye maandiko, bado linaleta maswali mengi kama vile, “Ikiwa kama ni mapenzi ya Mungu kutuponya, ni kwa nini basi kila mtu hajapokea uponyaji?” Kuna sababu nyingi, Na ninazungumzia kidogo kuhusu mambo ninayoyajua. Kuna taarifa nyingi sana ambazo sitaweza kuzigusa, lakini kama ni mapenzi ya Mungu kuponya, ninataka nishughulike na sehemu ya kwa nini watu wahapokei uponyaji. Moja ya sababu ni kutokujua. Huwezi kutenda katika kitu ambacho hukijui au hukielewi, na katika maisha yangu mwenyewe, hilo lilikuwa kweli.

Nilifundishwa kuamini kuwa mapenzi ya Mungu yametimia moja kwa moja, ya kuwa sikuwa na mamlaka, uwezo, au kusema hivyo katika hilo. Hivyo kupitia kutokujua kwangu, mambo kadhaa yalitokea. Baba yangu alifariki nilipokuwa na miaka kumi na miwili tu na watu wawili au watatu walifariki mbele yangu ilipofika wakati nina umri wa miaka ishirini na moja. Nilikuwa niki waombea wote wapokee uponyaji, lakini sikuona uponyaji ukidhihirika, si kwa sababu haikuwa ni mapenzi ya Mungu, lakini kwa sababu ya kukosa kujua katika upande wangu. Kukosa kujua ndiyo sababu kwa nini mambo hutokea, lakini hiyo siyo sababu. Ni kama kanuni ya mvutano: mtu anaweza kusema, “Vyema, sikutambua ya kuwa kama nikiruka kwenye jengo la ghorofa kumi nina weza kufa.” Si lazima utambue hilo ili upate matokeo kamili ya kanuni ifanye kazi kinyume nawe. Watu hawafahamu kuhusu baadhi ya kanuni za Mungu. Hawajui jinsi mfumo wake wa uponyaji unavyofanya kazi, hivyo kutokujua kunaua watu wengi sana.

Jambo jengine ambalo linaweza kutuzuia tusipokee uponyaji ni dhambi. Hakika inawaudhi watu unaposema hivyo, kwa kuwa wanatafsiri kile unachokisema kuwa magonjwa yote ni matokeo ya dhambi kwa upande wetu, ambalo si kweli. Hilo silo nina lolisema. Katika Yohana 9, kulikuwa na tukio ambapo Yesu alikuwa akitoka hekaluni, na wanafunzi wake wakamwonyesha mtu ambaye alizaliwa kipofu. Wanafunzi wake walisema katika mstari wa

2, “Wanafunzi wake wakamwuliza wakisema, Rabi, ni yupi aliyetenda dhambi, mtu huyu au wazazi wake, hata azaliwe kipofu?” Kwa maneno mengine, walikuwa wakijaribu kufananisha ugonjwa wake moja kwa moja na dhambi, wakiuliza kama ilikuwa ni dhambi yake au dhambi ya wazazi wake iliyosababisha ugonjwa huu kumvamia. Jibu la Yesu lilikuwa hakuna yoyote kati yao aliyetenda dhambi. Hilo si kusema kuwa wazazi au mtoto wao hawajawahi kutenda dhambi bali ni kuwa haikuwa dhambi zao ndizo zilizo sababisha upofu. Siyo kweli kusema ya kuwa magonjwa yote yanahusiana na dhambi, lakini pia siyo kweli kusema ya kuwa dhambi si moja ya kigezo.

Katika Yohana 5 kuna tukio ambapo wakati Yesu alipokuwa kwenye birika la Bethzatha, na akamponya mtu kwa uwezo wake. Kulikuwa na watu wengi sana mahali pale, na lakini ni mtu mmoja pekee aliponywa. Baadaye sura inaonyesha ya kuwa mtu yule hakujua ni nani aliyemponya wakati wayahudi walipomuuliza katika mstari wa 12, “Basi wakamwuliza, Yule aliyekuambia, Jitwike, uende, ni nani?” Mistari ya 13-14 inaendelea, “Lakini yule mtu aliyeponywa hakumjua ni nani; maana Yesu alikuwa amejitenga, kwa sababu palikuwa na watu wengi mahali pale. Baada ya hayo Yesu akamkuta ndani ya hekalu, akamwambia, Angalia, umekuwa mzima; usitende dhambi tena, lisije likakupata jambo lililo baya zaidi.” Yesu akasema pale pale kuwa dhambi inaweza kusababisha jambo baya zaidi kumpata kuliko kupooza kwake. Aliunganisha matokeo ya ugonjwa na dhambi. Pia alisema katika Yohana 9 ya kuwa haikuwa kwa sababu ya dhambi ya mtu yeyote ya kuwa mtu huyo alizaliwa kipofu.

Baadhi ya mambo hutokea tu bila kupangwa, lakini kuna nyakati ambapo magonjwa, maradhi, au matatizo yanaweza kuwa ni matokeo ya moja kwa moja ya dhambi. Hata katika hali kama hizo, haimaanishi ya kuwa Mungu ndiye anayeyafanya mambo haya yatokee kwetu. Chukua, kwa mfano, mtu anayeishi maisha ya ushoga, ambayo ni maisha ya upotovu na ukaidi dhidi ya asili. Mwili wa mwanadamu haukumaanishwa kuishi kwa jinsi hiyo. Magonjwa yanayosababishwa na kujamiiana kimwili kwa jinsi hiyo huja kutoka kwenyemtindo huo wa maisha. Mungu siye anayeyaleta magonjwa haya – ni asili tu inaasi kwa kuwa haijaumbwa kuishi kwa jinsi hiyo. Kwa mfano, ikiwa kama utakwenda na kula chakula kisicho sahihi, mwili wako utaitikia, na siyo Mungu ndiye anayeyafanya hayo kwako. Kuna kanuni za asili, mambo ya asili hapa. Hivyo ni kweli kuwa dhambi inaweza kuwa ni moja ya sababu ya watu kutokuponywa.

Ikiwa kama kuna dhambi inayojulikana na unamwamini Mungu kwa ajili ya uponyaji, unahitaji kuiacha hiyo dhambi, kwa sababu kupiti hiyo, unampa Shetani njia ya moja kwa moja kukufikia ambayo inakuzuia wewe usipokee kile ambacho Mungu anakifanya maishani mwako. Warumi 6:16 says, “Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki.?” Hivyo si kusema ya

kuwa Shetani anakuwa ndiye mtawala kwa jinsi kwamba unapoteza wokovu wako na kwenda kuzimu, lakini ina manisha ya kuwa iwe wewe ni Mkristo au la– ikiwa kama unaishi dhambini – unampa Shetani njia ya kuingia maishani mwako. Yohana 10:10 inasema ya kuwa mwivi haji ila kuiba, kuua na kuharibu. Lakini Yesu alikuja kukupa uzima. Hivyo unaye Yesu anayejaribu kuleta Uzima wake na afya kwako, lakini pia unaye Shetani akijaribu kukufanya uugue. Ikiwa kama kupitia dhambi unajikabidhi kwa Shetani, unamwezesha na kumpa fursa maishani mwako. Unaweza kumuomba Mungu akuponye na yote, lakini matendo yako yanamruhusu Shetani aingie na kuleta magonjwa. Hivyo, ikiwa kama unaishi dhambini, unahitaji kuacha.

Ninahitaji kuongeza ya kuwa unaweza kuwa unachunguza sana mawazo yako kiasi kwamba utasema "Vyema, Mara zote mimi ni chini ya kile ambacho ninapaswa kuwa" na ufike mahali pale ambapo hata kama unaamini Mungu anaweza kuponya, unaamini kuwa hatafanya kwa sababu hustahili. Hilo bila shaka si sawa pia. Hakuna kati yetu atakayepata uponyaji kutoka kwa Mungu kwa sababu tunastahili. Mungu kamwe hajawahi kuwa na mtu yeyote aliyestahili kwa kuwa na sifa za kumfanyia kazi, hivyo hauhitaji kumhusisha Mungu atembee maishani mwako kwenye utendaji wako tu, utakatifu wako. Inahitaji kukaa katika msingi wa kile ambacho Yesu alichokifanya kwa ajili yako na imani yako katika Yeye. Wakati huo huo, huwezi kudharau matendo yako na kujikabidhi kwa Shetani pasipo yeye kukuzuia wewe. Utaona uponyaji unafanya kazi kwa urahisi zaidi, vizuri zaidi maishani mwako ikiwa kama utatubu na kuacha chochote kile unachokifanya ambacho kitampa Shetani njia ya kuingia maishani mwako.

Jambo jengine ambalo linahusiana na uponyaji ambalo baadhi ya watu hawalifikirii sana ni kuwa kinyume na kutokuamini watu wengine kuwa wanaweza kukugusa. Moja ya mifano ya hili ni katika kitabu cha Marko 6 pale ambapo Yesu alikuwa mjini kwakwe, na watu hawakumheshimu kwa sababu walimkumbuka kama kijana mdogo. Walimfahamu baba na mama Yake, kaka na dada zake, na wala hawakumheshimu jinsi ambavyo baadhi ya watu wengine walivyofanya. Walikuja kinyume naye na kumshutumu. Marko 6:4-6 inasema, "Yesu akawaambia, Nabii hakosi heshima, isipokuwa katika nchi yake mwenyewe, na kwa jamaa zake, na nyumbani mwake. Wala hakuweza kufanya mwujiza wo wote huko, isipokuwa aliweka mikono yake juu ya wagonjwa wachache, akawaponya. Akastaajabu kwa sababu ya kutokuamini kwao." Hili halisemi ya kuwa Yesu asingefanya kazi zozote kuu, lakini kuwa hakuweza. Hapa yuko Yesu, Mwana wa Mungu, ambaye alikuja ulimwenguni kama mwanadamu, ambaye hakuwa na mapungufu kwenye imani Yake. Na bila shaka hakukuwa na njia yoyote ya dhambi ndani ya maisha Yake. Bado alikuwa na ukomo katika yale aliyoweza kuyafanya kwa watu wengine kwa sababu ya kutokuamini kwao. Weka hili pamoja na Mathayo 13:58 pale inaposema, "Wala hakufanya miujiza mingi huko, kwa sababu ya kutokuamini kwao," na tunaona ya kuwa Yesu, ambaye hakuwa na mipaka ndani Yake na bila shaka hakuwa na dhambi maishani mwake hata

ampe Shetani njia ya kuingia, alikuwa na ukomo katika kile ambacho aliweza kukifanya kwa sababu ya watu waliyo mzunguuka.

Hili ni la muhimu sana kulielewa ya kuwa nina sema ni mapenzi ya Mungu kumponya kila mtu wakati wote. Ikiwa kama unaamini hilo, inawezekana ukafanya kosa la kwenda hospitalini na kujaribu kuondoa kila mtu aliye mgonjwa kwa kuwa unaamini ni mapenzi ya Mungu kwao kuponywa wote. Ni mapenzi ya Mungu kwao wao kuponywa, lakini hatafanya kinyume na mapenzi yao. Mungu atailinda haki yao ya kuugua, haki yao ya kutokuponywa. Hakuna atakayeweza kuwalazimisha waponywe – na hawawezi kuponywa kwa imani ya mtu mwengine. Imani ya mtu mwengine inaweza kuwasaidia ikiwa kama wanapambana, lakini hakuna atakayeweza kuwafanyia. Unaweza kusukuma gari likiwa katika gia huru, lakini huwezi kusukuma gari likiwa kwenye gia ya kuegesha gari au gia ya kurudi nyuma. Ikiwa kama mtu yuko kinyume na uponyaji, huwezi kulishinda hilo. Kwa sababu ya hili, huwezi kuondoa watu wote hospitalini au kwenda kwenye ibada ya kanisa na kuona kila mtu akiponywa pasipo kutoa ushirikiano wake.

Kuna mambo mengi sana ambayo yangeweza kusemwa kuhusu hili. Wakati Yesu alipowaponya watu, hata kufufua wafu, Angemwendea mtu na kusema, "Usilie." Angemwambia mama asilie na baadaye akamfufua mwanawe toka wafu. Imani ya mtu mwengine inabidi itumike mahali pengine. Kuna hitajika kuwa na imani upande wetu, na kuna mambo mengi mengi sana yanayohusika katika uponyaji. Nimejadili mambo machache tu hapa leo, na natumaini yatakusaidia, lakini moja ya mambo ya msingi unayohitaji kupata kutoka kwenye hili ni kuwa Mungu ni mwaminifu. Ni mapenzi Yake kwako wewe kuponywa, lakini unatakiwa kujifunza jinsi ya kushirikiana Naye. Hawezi kukufanyia; Inabidi Afanye kupitia kwako. Itatoka ndani yako.

Ninaomba ya kuwa mambo haya yatakusaidia kuanza kujitoa wewe mwenyewe, kuiruhusu nguvu ya Mungu kutiririka kupitia wewe, na utembee katika afya yake ya Kiungu.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Mathayo 8:17. Yesu alifanya nini ili kupata uponyaji kwa ajili yetu? __________ ____________________________________ ____________________________

2. Soma Hosea 4:6. Baadhi ya watu hawaponywi kwa sababu ya:

   A. kutokujua (kukosa maarifa).

   B. hawaendi kanisani.

   C. si wema wa kutosha.

3. Soma Yohana 9:1-3. Wanafunzi walifikiri nini kilisababisha upofu wa mtu huyu?

   ______________________

   Kufikiri kwao kulikuwa sahihi?

   _________________________

4. Soma Yohana 5:14. Dhambi hufungua mlango kwa magonjwa, lakini si mara zote. Mbali na magonjwa, nini kingine dhambi inaweza kusababisha ndani ya mtu? _____ ____________________________________ _________________________________

5. Soma Warumi 5:12-14 (katika tafsiri ya The Living Bible kama inawezekana). Ikiwa kama dhambi mar azote si sababu ya magonjwa, ipi inaweza kuwa sababu nyengine inayowezekana?

   ______________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Mathayo 8:17

"Ili litimie lile neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema, Mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, Na kuyachukua magonjwa yetu."

### Hosea 4:6

"Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa; kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa, mimi nami nitakukataa wewe, usiwe kuhani kwangu mimi; kwa kuwa umeisahau sheria ya Mungu wako, mimi nami nitawasahau watoto wako."

### Yohana 9:1-3

"Hata alipokuwa akipita alimwona mtu, kipofu tangu kuzaliwa. Wanafunzi wake wakamwuliza wakisema, Rabi, ni yupi aliyetenda dhambi, mtu huyu au wazazi wake, hata azaliwe kipofu?Yesu akajibu, Huyu hakutenda dhambi, wala wazazi wake; bali kazi za Mungu zidhihirishwe ndani yake."

### Yohana 5:14

"Baada ya hayo Yesu akamkuta ndani ya hekalu, akamwambia, Angalia, umekuwa mzima; usitende dhambi tena, lisije likakupata jambo lililo baya zaidi."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

6. Soma Matendo 10:38. Kufuatana na Matendo 10:38, magonjwa yanaweza kusababishwa na? ____________________ ____________________________________ __________________

7. Soma Mathayo 13:58. Uponyaji unaweza kuzuiwa na? _________________________ _____________________________

8. Soma Yakobo 5:15. Nini kitakacho mwokoa mgonjwa? ___________________ _________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Warumi 5:12-14 (Tafsiri ya The Living Bible)

"[12] Adamu alipotenda dhambi, dhambi iliingia ulimwenguni mote. Dhambi yake ikasambaza mauti katika ulimwengu wote, hivyo kila kitu kikaanza kuzeeka na kufa, kwa kua wote walitenda dhambi. [13] Twajua ya kuwa ilikuwa ni dhambi ya Adamu iliyosababisha haya kwa sababu ingawa, ndiyo, watu walikuwa wakitenda dhambi kutoka wakati wa Adamu mpaka wa Mus, Mungu katika siku zile hakuhukumu kwa hatia ya mauti kwa kuvunja sharia zake – kwa kuwa bado alikuwa hajatoa sheria zake kwao wala kuwaambia kile alichokitaka wakifanye. [14] Hivyo miili yao ilipokufa haikuwa kwa ajili ya dhambi zao wenyewe kwa kuwa wao wenyewe hawakuwahi kuacha kuzitii sharia maalumu za Mungu dhidi ya kula tunda lililokatazwa, Kama ambavyo Adamu alifanya. Tofauti iliyoje kati ya Adamu na Kristo ambaye alikuwa bado hajaja!"

### Matendo 10:38

"Habari za Yesu wa Nazareti, jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye."

### Mathayo 13:58

"Wala hakufanya miujiza mingi huko, kwa sababu ya kutokuamini kwao."

### Yakobo 5:15

"Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Mathayo 8:17. Yesu alifanya nini ili kupata uponyaji kwa ajili yetu? **Aliyachukua maovu yetu na kubeba magonjwa yetu.**

2. Soma Hosea 4:6. Baadhi ya watu hawaponywi kwa sababu ya: **A. kutokujua (kukosa maarifa).**

3. Soma Yohana 9:1-3. Wanafunzi walifikiri nini kilisababisha upofu wa mtu huyu? **Dhambi. Kufikiri kwao kulikuwa sahihi? Hapana.**

4. Soma Yohana 5:14. Dhambi hufungua mlango kwa magonjwa, lakini si mara zote. Mbali na magonjwa, nini kingine dhambi inaweza kusababisha ndani ya mtu? **Mambo mengi mabaya kuliko magonjwa, hata mauti (Warumi. 6:23).**

5. Soma Warumi 5:12-14 (katika tafsiri ya The Living Bible kama inawezekana). Ikiwa kama dhambi mar azote si sababu ya magonjwa, ipi inaweza kuwa sababu nyengine inayowezekana? **Anguko (Mwnanzo. 3). Adamu kupitia makosa yake alitambulisha dhambi na magonjwa ulimwenguni.**

6. Soma Matendo 10:38. Kufuatana na Matendo 10:38, magonjwa yanaweza kusababishwa na? **Kukandamizwa na ibilisi.**

7. Soma Mathayo 13:58. Uponyaji unaweza kuzuiwa na? **Kutokuamini.**

8. Soma Yakobo 5:15. Nini kitakacho mwokoa mgonjwa? **Maombi ya imani.**

# SOMO 9
# KUSAMEHE WENGINE

*Na Don Krow*

Leo tunakwenda kuangalia somo la msamaha kutoka Mathayo 18:21-22, *"Kisha Petro akamwendea [Yesu], akamwambia, Bwana, ndugu yangu anikose mara ngapi nami nimsamehe? Hata mara saba? Yesu akamwambia, Sikuambii hata mara saba, bali hata saba mara sabini"*. Nafikiri Petro aliwaza kuwa alikuwa mkarimu sana kwa kuuliza ni mara ngapi anapaswa kumsamehe mtu aliyemkosea, " Hiyo ni mara 490. Lakini haimaanishi ya kuwa baada ya mara 490 hutakiwi kusamehe. Kile Yesu alichokisema ilikuwa ni namba isiyowezekana ya makosa ambayo yangetokea kwa mtu mmoja katika siku. Alikuwa akisema ya kuwa msamaha unapaswa kuwa ni kitu endelevu, yaani inapaswa kuendelea bila kukoma. Kusamehe kunapaswa kuwa ndiyo tabia halisi ya Mkristo. Yesu alisema katika Luka 23:34, *"Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo."* Na pia Stephano aliyeuawa kwa sababu ya Imani yake, katika Matendo 7:60 ilisema, *"usiwahesabie dhambi hii."* Si watu wote watapokea msamaha, bali tabia ndani ya moyo wa Mkristo inatakiwa mara zote iwe ni kuutoa msamaha huo.

Yesu anatoa mfano kuhusu msamaha anapoendelea kwenye mstari wa 23 wa kitabu cha Mathayo 18, *"Kwa sababu hii ufalme wa mbinguni umefanana na mfalme mmoja aliyetaka kufanya hesabu na watumwa wake, Alipoanza kuifanya, aliletewa mtu mmoja awiwaye talanta elfu kumi. [tafsiri ya Living Bible* inasema hiyo ilikuwa kama dola millioni kumi.] *Naye alipokosa cha kulipa, bwana wake akaamuru auzwe, yeye na mkewe na watoto wake, na vitu vyote alivyo navyo, ikalipwe ile deni. Basi yule mtumwa akaanguka, akamsujudia akisema, Bwana, nivumilie, nami nitakulipa yote pia"*. Sasa, hapa ndipo penye hali ilivyo: Kuna mtu ambaye kwa ukweli anadaiwa dola millioni kumi na bwana wake. Hakuna jinsi atakavyoweza kuilipa – anajua hawezi na bwana wake anajua hawezi. Katika siku zile, hukuweza kutangaza kuwa umefilisika kama unavyoweza kufanya nchini Marekani– wange kuuza wewe, mke wako, watoto wako, na kila kitu ulichokuwa nacho, na ungeenda kuwa mtumwa. Ungepelekwa gerezani mpaka kila kitu kiwe kimelipwa, na kama hakijalipwa, ungebaki gerezani maisha yako yote. Mtu huyu alifanya kitu pekee alichojua kukifanya: Akapiga magoti na kulia ili apewe rehema, "O bwana, tafadhali univumilie! Tafadhali, Ninakuomba. Nitakulipa kila kitu. Univumilie tu!" Angalia

nini kilitokea kwenye mstari wa 27. Inasema bwana wa mtumwa yule akamhurumia, na akamsamehe deni lake.

Tulikuwa na deni ambalo hatukuweza kulilipa. Biblia inasema ya kuwa mshahara wa dhambi ni mauti (Warumi. 6:23) – tulitengwa na Mungu milele – dhahabu yote na fedha ya ulimwengu haikuweza kutukomboa. Halafu Mungu katika huruma yake na neema Yake alimtuma Mwanawe Yesu Kristo hapa ulimwenguni alipe deni ambalo hatukuweza kulilipa. Mungu alituangalia katika Huruma Yake na rehema na akasema, "Nina wasamehe hilo deni."

Mtu huyu ambaye ndiyo kwanza amesamehewa dola milioni kumi alikuwa anadaiwa kitu kama dola ishirini na mtumishi mwenzake. Alimpata na kusema, "Nime samehewa tu dola millioni kumi, na dola ishirini kwangu ni nini? Ninataka wewe uwe huru kama nilivyo huru. Ni sawa, kwa kuwa nimesamehewa dola millioni kumi!" Hilo ndilo lililopaswa kutokea, lakini halikutokea. Hebu tusome nini hasa kilitokea katika Mathayo:28-31, *"Mtumwa yule akatoka, akamwona mmoja wa wajoli wake, aliyemwia dinari mia akamkamata,akamshika koo,akisema Nilipe uwiwacho. Basi mjoli wake akaanguka miguuni pake, akamsihi, akisema, Nivumilie, nami nitakulipa yote pia. Lakini hakutaka, akaenda, akamtupa kifungoni, hata atakapoilipa ile deni. Basi wajoli wake walipoyaona yaliyotendeka, walisikitika sana, wakaenda wakamweleza bwana wao yote yaliyotendeka."* Akamtupa mtu yule gerezani kwa ajili ya dola ishirini baada tu ya kuwa amesamehewa dola millioni kumi! Unaweza kufikiri hilo?

Mistari ya 32-34 inasema, *"Ndipo bwana wake akamwita, akamwambia, Ewe mtumwa mwovu, nalikusamehe wewe deni ile yote, uliponisihi. nawe, je! Haikukupasa kumrehemu mjoli wako, kama mimi nilivyokurehemu wewe? Bwana wake akaghadhibika, akampeleka kwa watesaji, hata atakapoilipa deni ile yote."* Mtu huyu tena alitupwa gerezani kwa sababu ya jinsi alivyomtendea mtumishi mwenzake, na hivyo akaupoteza msamaha wake wa kwanza. Yesu alisema katika mstari wa 35, *"Ndivyo na Baba yangu wa mbinguni atakavyowatenda ninyi, msiposamehe kwa mioyo yenu kila mtu ndugu yake."* Je si ni upumbavu, baada ya kuwa tumesamehewa dhambi zetu zote – mishahara ambayo ni mauti na kutengwa na Mungu milele – kukataa kusamehe? Tunamsihi Mungu, tukisema "Nisamehe na unirehemu kupitia Yesu Kristo," pokea msamaha, na halafu ugeuke na kukataa kusamehe mtu mwengine kwa kitu kidogo ambacho tunafikiri ni kikubwa sana – baada ya kupokea msamaha kwa mambo yote tuliyoyafanya. Mungu anasema huo ni uovu.

Nilichunga kanisa kipindi fulani kilichopita, na kulikuwa na mwanamke kijana katika kusanyiko ambaye aliweza kuona mambo yaliyo mbeleni. Alikuja kwangu siku moja na kusema, "Roho Mtakatifu ananiambia mambo yajayo na ananionyesha mambo yaliyoko mbele? Ninajua watu wanapokwenda kufa na wakati mtu atakapokwenda kupata ajali ya gari, na mambo kama hayo." Nikasema, "Hutapenda jibu langu, lakini mimi siamini ya kuwa huyo ni Roho Mtakatifu. Ninafikiri ni roho wa utambuzi, roho ile ile ambayo alimfuata Mtume Paulo katika

Matendo ya Mitume 16. Hatimaye aliikemea na kuiamuru itoke nje ya yule binti na akapoteza uwezo wake wa kutabiri." Nikaendelea kwa kumuambia ya kuwa mimi si Mungu, na nikasema, "Ninataka umwendee Yesu na kumuuliza, 'Bwana, nini kinachoniambia na kunipa taarifa, hata kabla sijaokolewa? Je ni Roho Mtakatifu wako, au ni kitu kingine?'" Alirudi kwangu siku moja na akasema, "Nimezungumza na Bwana kuhusu hilo, na ninafikiri ya kuwa ni sawa." Nilisema, "Chochote Bwana atakachosema ni sawa– Mimi si Mchungaji Mkuu."

Hii ilikuwa mwanzoni mwaka 1986, na unajua nini kilitokea mwaka 1986? Tulikuwa na chombo cha angani kiitwacho " Challenger", na watu nane walipanda katika chombo hicho. Mmoja wao alikuwa ni mwanamke mwalimu wa shule. Wakati binti huyu kijana alipokuwa akiangalia televisheni, alimwona mwanamke akisema, "Kesho nina kwenda kupanda kwenye chombo kinacho kwenda mwezini (Challenger)," na akawa anakizungumzia. Roho ikaongea naye na kusema, "Anakwenda kufa, anakwenda kufa." Siku iliyofuata Chombo hicho cha angani kilipoachiliwa kupaa, kililipuka wakati ulimwengu wote ulipokuwa ukitazama, na wanaanga wote wakaangamia. Binti yule kijana alirudi kwangu na kusema, "Ndugu Don, Ninafikiri kinachozungumza nami na kunipa taarifa inaweza kuwa si Roho Mtakatifu. Je utaniombea?" Ibaada iliyofuata usiku ule, baada ya kila moja kuondoka, Nilimchukua kwa mkono wake na kusema, "Wewe roho mchafu wa utambuzi, toka ndani yake!" Hakuna kilichotokea. Wanafunzi wa Yesu walijaribu kufukuza roho chafu kutoka kwa kijana mmoja na hawakufanikiwa. Yesu alisema, "Mleteni kijana huyo kwangu." Hivyo nikasema, "Bwana, Nilifikiri ninajua nini kinachoendelea hapa, lakini ninamleta binti huyu kwako. Tuonyeshe nini kinachoendelea." Mke wangu alikuwa akiomba pamoja nasi na Mungu akampa neno la maarifa. Akasema, "Inahusiana na mama yake." Nikamwambia yule mwanamke, "Je utamsamehe mama wako?" Mara niliposema hivyo, sauti ikapiga kelele kutoka ndani yake, "HAPANA! Alinipa njia!" Halafu nikasema "Ninakufunga, wewe roho mchafu" na nikamuuliza tena yule mwanamke kama atamsamehe mama yake. Halafu akasamehe na kumuachilia mama yake na kumuachia aende kwa neema na msaada wa Mungu. Aliweza kuachilia kwa kufanya uamuzi wa kusamehe, na halafu akapokea ukombozi wake na uhuru.

Kama ambavyo Yesu alivyosema kwenye mfano katika Mathayo 18, Ninasema ya kuwa ikiwa kama hatuta samehe kutoka mioyoni mwetu baada ya sisi kuwa tumesamehewa deni kubwa kama hilo na Baba yetu wa mbinguni, tutakabidhiwa mikononi mwa watesaji. Watesaji ni nani? Wanaweza kuwa ni aina ya vitu vyote – ngome za kipepo, kukandamizwa, maradhi, mfadhaiko, magonjwa, na mambo mengine mengi. Chanzo ni kutokusamehe. Kutokusamehe baada ya kuwa tumesamehewa kuna mruhusu Shetani kuwa na nafasi katika maisha yetu Biblia inasema ni lazima tufanye uamuzi wa kusamehe. Katika sala ya Baba yetu (Matt. 6:9-11), Yesu alisema tusamehe kama ambavyo tumesamehewa.

Marko 11:25-26 inasema ya kuwa tunapoomba, ikiwa kama tuna chochote dhidi ya mtu yeyote, tunatakiwa kusamehe, hilo lina maanisha nini? Kutoku samehe kunapaswa kubaki ndani yetu kwa muda gani? Mpaka pale tu inapotuchukua sisi kwenda kwa Bwana kuomba. Na ikiwa kama hata tuna punje ndogo ya kutokusamehe dhidi ya kila mmoja, tunapaswa kuwaachia na kusema, "Mungu, nina waachilia waende leo. Nina wasamehe. Ninafanya uchaguzi leo kwa sababu Ulinisamehe deni kubwa kiasi hicho."

Bwana, Nina mwombea yeyote anayesoma somo hili ambaye ana hali ya kutokusamehe maishani mwake, ya kuwa watafanya maamuzi sasa katika muda huu wamwachilie mtu huyo awe huru, wawa samehe iwe wako hai au wamekufa. Ninaomba ya kuwa wataachilia na kuruhusu maumivu hayo kupokea uponyaji kwa nguvu yako na neema yako leo, Bwana. Ninakushukuru, Katika Jina la Yesu. Amina.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Mathayo 18:21. Ni mara ngapi Petro alitoa fursa ya kusamehe? ______________________________________________

2. Soma Mathayo 18:22. Ni mara ngapi Yesu alisema tulitakiwa kusamehe? ______________________________________________

3. Soma Mathayo 18:23-24. Ni fedha kiasi gani mtumishi huyu alikuwa anadaiwa na Bwana wake? ______________________________________________

4. Soma Mathayo 18:25. Kwa kuwa mtumishi huyu hakuweza kutangaza kuwa amefilisika, nini kingetokea? ______________________________________________

5. Soma Mathayo 18:26. Nini lilikuwa ni ombi la mtumishi?

   ____________________

   Je angeweza kulilipa deni lake?

   ____________________

6. Soma Mathayo 18:27. Ni tabia gani yule bwana alioonyesha kwa mtumishi wake?

   ____________________

   Ni tabia gani Mungu alituonyesha na kwenye deni letu (dhambi)?

   ____________________

7. Soma Mathayo 18:28. Mtumishi ambaye alisamehewa alikuwa na mtumishi mwenzake aliyemdai kiasi gani? ______________________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

Mathayo 18:21

"Kisha Petro akamwendea akamwambia, Bwana, ndugu yangu anikose mara ngapi nami nimsamehe? Hata mara saba?"

Mathayo 18:22

"Yesu akamwambia, Sikuambii hata mara saba, bali hata saba mara sabini."

Mathayo 18:23-24

"[23] Kwa sababu hii ufalme wa mbinguni umefanana na mfalme mmoja aliyetaka kufanya hesabu na watumwa wake. [24] Alipoanza kuifanya, aliletewa mtu mmoja awiwaye talanta elfu kumi."

Mathayo 18:25

"Naye alipokosa cha kulipa, bwana wake akaamuru auzwe, yeye na mkewe na watoto wake, na vitu vyote alivyo navyo, ikalipwe ile deni.."

Mathayo 18:26

"Basi yule mtumwa akaanguka, akamsujudia akisema, Bwana, nivumilie, nami nitakulipa yote pia."

Mathayo 18:27

"Bwana wa mtumwa yule akamhurumia, akamfungua, akamsamehe ile deni."

Mathayo 18:28

"Mtumwa yule akatoka, akamwona mmoja wa wajoli wake, aliyemwia dinari mia akamkamata,akamshika koo,akisema Nilipe uwiwacho.."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

8. Soma Mathayo 18:28. Tabia ya mtumishi huyu ilikuwaje kwa mtumishi mwenzake? ____________________________________ ____________________________________

9. Soma Mathayo 18:29-30. Mtumishi huyu alifanya nini kwa mtumishi mwenzake? __ ____________________________________ ___________________________________

10. Soma Mathayo 18:31-33. Yule bwana alimwitaje mtumishi yule ambaye hakumsamehe mwenzake? _____________ ____________________________________ ________________________

11. Soma Mathayo 18:33. Yule bwana alimwambia mtumishi wake alipaswa kufanya nini? ________________________ ____________________________________ _____________

12. Soma Mathayo 18:34. Yule bwana alipojua kilichotokea, iliathiri vipi hisia zake? ____ ____________________________________ ________________

13. Soma Mathayo 18:34. Je mtumishi huyu aliyeshindwa kusamehe kwa matendo yake (au maamuzi) aliacha msamaha ambao ulishatolewa kwake hapo awali? __________________

14. Soma Mathayo 18:35. Mfano huu unamanisha nini? ____________________ ____________________________________ _________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Mathayo 18:29-30

"[29] Basi mjoli wake akaanguka miguuni pake, akamsihi, akisema, Nivumilie, nami nitakulipa yote pia. [30] Lakini hakutaka, akaenda, akamtupa kifungoni, hata atakapoilipa ile deni.."

### Mathayo 18:31-33

"[31] Basi wajoli wake walipoyaona yaliyotendeka, walisikitika sana, wakaenda wakamweleza bwana wao yote yaliyotendeka.. [32] Ndipo bwana wake akamwita, akamwambia, Ewe mtumwa mwovu, nalikusamehe wewe deni ile yote, uliponisihi: [33] Nawe, je! Haikukupasa kumrehemu mjoli wako, kama mimi nilivyokurehemu wewe?"

### Mathayo 18:33

"Nawe, je! Haikukupasa kumrehemu mjoli wako, kama mimi nilivyokurehemu wewe??"

### Mathayo 18:34

"Bwana wake akaghadhibika, akampeleka kwa watesaji, hata atakapoilipa deni ile yote."

### Mathayo 18:35 (The Message Bible)

"Ndivyo na Baba yangu wa mbinguni atakavyowatenda ninyi, msiposamehe kwa mioyo yenu kila mtu ndugu yake."

# MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Mathayo 18:21. Ni mara ngapi Petro alitoa fursa ya kusamehe? **Mara saba.**

2. Soma Mathayo 18:22. Ni mara ngapi Yesu alisema tulitakiwa kusamehe? **Mia nne na tisini (au bila mwisho, inayoendelea).**

3. Soma Mathayo 18:23-24. Ni fedha kiasi gani mtumishi huyu alikuwa anadaiwa na Bwana wake? **Talanta elfu kumi, au dolla millioni kumi (kiwango ambacho inawezekana kamwe kisiweze kulipwa).**

4. Soma Mathayo 18:25. Kwa kuwa mtumishi huyu hakuweza kutangaza kuwa amefilisika, nini kingetokea? **Yeye, mke wake, watoto wake, na vyote alivyovimiliki vilipaswa kuuzwa kwenye soko la watumwa ili kulipa deni lake.**

5. Soma Mathayo 18:26. Nini lilikuwa ni ombi la mtumishi? Kwa bwana wake kumvumilia na angemlipa kila kitu. ______________________ Je angeweza kulilipa deni lake? **Inawezekana hapana.**

6. Soma Mathayo 18:27. Ni tabia gani yule bwana alioonyesha kwa mtumishi wake? Ile ya huruma na msamaha. Ni tabia gani Mungu alituonyesha na kwenye deni letu (dhambi)? **Ile ya huruma na msamaha.**

7. Soma Mathayo 18:28. Mtumishi ambaye alisamehewa alikuwa na mtumishi mwenzake aliyemdai kiasi gani? **Dinari mia (mshahara wa siku).**

8. Soma Mathayo 18:28. Tabia ya mtumishi huyu ilikuwaje kwa mtumishi mwenzake? **Ile ya kukosa uvumilivu, vurugu, na kutokusamehe.**

9. Soma Mathayo 18:29-30. Mtumishi huyu alifanya nini kwa mtumishi mwenzake? Alimtupa kifungoni mpaka atakapolipa deni lake dogo.

10. Soma Mathayo 18:31-33. Yule bwana alimwitaje mtumishi yule ambaye hakumsamehe mwenzake? **"Ewe mtumishi mwovu."**

11. Soma Mathayo 18:33. Yule bwana alimwambia mtumishi wake alipaswa kufanya nini? **Alipaswa kuwa na huruma kwa mtumishi mwenzake kama ambavyo bwana wake alivyomhurumia. Alipaswa kumwachilia na kumsamehe.**

12. Soma Mathayo 18:34. Yule bwana alipojua kilichotokea, iliathiri vipi hisia zake? **Alikasirika.**

13. Soma Mathayo 18:34 Je mtumishi huyu aliyeshindwa kusamehe kwa matendo yake (au maamuzi) aliacha msamaha ambao ulishatolewa kwake hapo awali? **Ndiyo.**

14. Soma Mathayo 18:35. Mfano huu unamanisha nini? **"Ndivyo na Baba yangu wa mbinguni atakavyowatenda ninyi, msiposamehe bila masharti yeyote atakayeomba rehema" (Matt. 18:35, Ujumbe).**

DARAJA 2

# SOMO 10

# NDOA (Sehemu 1)

*Na Don Krow*

Leo tunakwenda kuzungumza kuhusu ndoa. Awali ya yote, ninataka nikupe baadhi ya takwimu: asilimia 75 ya familia zitahitaji kupewa aina fulani ya ushauri nasaha kuhusu ndoa. Moja kati ya ndoa mbili zitaishia kwenye talaka. Katika asilimia 50 ya ndoa, mwana ndoa mmoja atakosa uaminifu ndani ya miaka mitano ya kwanza ya ndoa,. Hata katika ulimwengu wa Wakristo, wanasema ya kuwa kwa kadri ilivyo juu katika kiwango cha asilimia 30 ya watumishi wata jihusisha katika mahusiano yasiyo sahihi na mtu fulani ndani ya kanisa. Inaonekana kwangu ya kuwa hatuja elewa kabisa kanuni za Biblia ikiwa kama takwimu hizo zitakuwa hivyo. Tunakwenda kuliangalia somo la ndoa na kuona baadhi ya vitu ambavyo Mungu ana vizungumzia – Jinsi ambavyo unaweza kuimarisha mahusiano yako ya ndoa.

Awali ya yote, Ninataka kusema hili: Ndoa ilikuwa ni wazo la Mungu; Yeye ndiye aliye itengeneza. Mwanzo 2:18 inasema, *"Bwana Mungu akasema, Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye."* Na pia Mwanzo 1:31 inasema, *"Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya sita.."* Ni lazima ukumbuke ya kuwa huu ulikuwa ni uumbaji mkamilifu. Mungu alikuja na akawa na ushirika na mwanadamu. Alikuwa na uhusiano mzuri sana naye. Kila siku angekuja kwenye utulivu wa siku na kuwa na ushirika na Adamu. Mara nyengine tunafikiria ya kuwa ikiwa kama tutakuwa na uhusiano mkamilifu na Mungu, hakika hatuta hitaji kitu kingine chochote, lakini siyo kweli. Mungu alisema katika Mwanzo 1:31, kuhusiana na uumbaji aliyo uumba, *"Na tazama ni chema sana."* Kitu cha kwanza ambacho Mungu alikisema ilikuwa ni "si vyema" inapatikana katika Mwanzo 2:18, *"Si vyema kwa mtu kuwa pekee yake."* Hivyo ndoa ilikuwa ni wazo la Mungu kukutana na hitaji ambalo mwanadamu alikuwa nalo, ili ampe msadizi ili ashughulike na matatizo ya upweke ambayo angeweza kuyapitia maishani mwake. Ndoa, ikiwa kama tutafuata melekezo yaliyomo kwenye mwongozo na kuweka ndani kile ambacho Mungu anakitaka, Ikimaanishwa kuleta furaha na siyo huzuni.

Mwanzo 2:24 ni mara ya kwanza Biblia hakika inazungumzia sana kuhusu ndoa. inasema, *"Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na*

*mkewe, nao watakuwa mwili mmoja."* Ndoa ni kuacha mahusiano mengine yote na kuweka mtazamo wa maisha yako kwa mtu mwengine, na Mungu aliitengeneza kwa jinsi hiyo. Ni kama uhusiano wenye watu watatu waliyounganishwa. Sielewi kama unelewa nina chomaanisha, lakini katika mahusiano ya ndoa wakati Mungu alipomwita Adamu na Hawa pamoja, haikuwa Adamu tu akihusiana na Mungu au Hawa akihusiana na Mungu. Sasa ilikuwa Adamu na Hawa kama kitu kimoja, katika umoja wa madhumuni wakihusiana na Mungu. Biblia inasema katika 1 Peter 3:7, *"Kadhalika ninyi waume, kaeni na [wake zenu] kwa akili; na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu; na kama warithi pamoja wa neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe."*. Mwanzo 5:1-2, hakika andiko kuu, inasema, *"Hiki ndicho kitabu cha vizazi vya Adamu. Siku ile Mungu alipoumba mtu, kwa sura ya Mungu alimfanya;mwanamume na mwanamke aliwaumba, akawabariki akawaita jina lao Adamu, siku ile walipoumbwa."* Angalia ya kuwa Adamu alimwita mke wake, Hawa, lakini Mungu aliwaita Adamu na Hawa, pamoja kama kitu kimoja, Adamu. Hivyo katika mahusiano ya ndoa, Si tena Mungu na mimi au Mungu na mwanamke yule – ni mimi na mke wangu katika umoja, warithi sawa sawa na neema ya uzima ambao tumeitwa kumtumika Mungu katika madhumuni, kutembea katika umoja.

Mwanzo 2:24, ambayo tumeisoma tu, inasema mtu atamwacha baba na mama yake na ataambatana na mke wake, nao watakuwa mwili mmoja. Neno "kuambatana" lina maanisha: kugandana au kufuatana na, kufanyika kitu kimoja, kuwa wamoja katika madhumuni. Ikiwa kama una matatizo katika mahusiano yako ya ndoa leo, acha nikuulize maswali machache: Je mambo unayoyafanya, Jinsi unavyomfanyia mwenzi wako, mambo unayo mwambia, je yana wasababisha muwe karibu kama kitu kimoja? Au, yanasababisha mpasuko, au utengano? Amri ya maandiko kwa ajili ya ndoa ni kuambatana, kugandana pamoja. Hivyo, mambo unayo yafanya yanajenga mahusiano yenu au yana yasambaratisha? Unahitaji kuangalia katika baadhi ya mambo haya.

Watu wanafikiri ya kuwa upendo ni jambo tu la kihisia: "Nilikuwa nina kupenda, lakini sina upendo – Sikupendi tena." Kwa mfano umetokea kwenye familia isiyojiendesha vizuri. Unaenda mbele ya mtumishi au hakimu kufunga ndoa; unajitoa kuyatoa maisha yako kwa huyo mtu; hakika unataka ndoa hiyo idumu mpaka kifo kitakapo watenganisha. Lakini kwa sababu ya familia yako ambayo haikuwa na amani, hujawahi kuuona upendo, wala hujawahi kuuona ukionyeshwa kwenye familia yako, na wala hujawahi kuwaona wazazi wako wakionyeshana upendo. Mwenzi wako inawezekana anatokea kwenye familia ambayo ilikuwa ikionyesha upendo sana, lakini wewe hujui ni kwa jinsi gani. Ingawa unataka kumpenda mtu huyu ambaye unajitoa kwake, kwa kwa wewe mwenyewe hauendi vyema kabisa, ukiwa hujawahi kuuona upendo ukionyeshwa hapo awali, inawezekana ukashindwa. Uwezekano ni kuwa ndani ya miaka michache utakwenda kwa ajili ya ushauri nasaha na kusema, "Hatuendani tu, simpendi tena" Vyema, Nina habari njema kwa ajili yako leo: Ikiwa kama una matatizo katika ndoa yako, kuna kitu ambacho kinaweza kurekebisha.

Unaponunua friji mpya na ukapata tatizo nalo, unajua kuenda kwenye mwongozo wake. Mwongozo utakuambia nini hakiko sawa, au unaweza kulipeleka kwa fundi. Kuna mwongozo wa kuifanyia kazi ndoa yako, kuitengeneza. Unaitwa Neno la Mungu, na Biblia inatuambi katika Tito 2:4 ya kuwa upendo ni kitu ambacho kinaweza kufundishwa, kitu ambacho mtu anaweza kujifunza. Ikiwa kama untoka kwenye familia ambayo haiendi vyema na hakika hufahamu jinsi ya kumpenda mwenzi wako – ndoa yako inasambaratika – kun ahabari njema. Katika 1 Yohana 5:3 inasema, *"Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito."* Kupitia amri za Yesu Kristo, ambaye anatuonyesha jinsi ya kupenda, jinsi ya kuonyesha wema na ukarimu, na jinsi ya kutafuta ustawi wa mtu mwengine katika mahusiano yako ya ndoa, Mungu anaweza kuigeuza hiyo hali kwa ajili yako.

Huu ni utangulizi tu wa somo la ndoa. Tutakwenda kuendeleza somo jengine kuhusus ndoa na Ninataka tu kusema, "Mungu awabariki leo mnapoendelea katika masomo yenu." Tunaamini Mungu anataka kuwekeza hekima na maarifa zaidi mnapoangalia somo hili.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Waefeso 5:31-32. Waefeso 5:31 ni nukuu kutoka Mwanzo 2:24. Kwa kuangalia Waefeso 5:32, nini ambacho unfikiri Mungu anakizungumzia kwenye kifungu hiki? ________________________________________

2. Soma Yakobo 4:4-5. Mistari hii inafundisha nini? ________________________________________

3. Soma 1 Petro 3:7. Ni kwa nini unapaswa kutembea katika umoja na upendo kwa mke wako na mume wako? ________________________________________

4. Soma Yohana 15:5. Je ndoa yako inaweza kufanikiwa pasipo Kristo kama Bwana wa maisha yako? ________________________________________

5. Soma Tito 2:4. Upendo si tu hisia. Kufuatana na maandiko, upendo unaweza ________________________________________

6. Soma 1 Yohana 5:3. Tunapotembea katika amri za Mungu, tunatembea katika ________________.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Waefeso 5:31-32

“[31] Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja. [32] Siri hiyo ni kubwa; ila mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa.”

### Yakobo 4:4-5

“[4] Enyi wazinzi, hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu? Basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu. [5] Au mwadhani ya kwamba maandiko yasema bure? Huyo Roho akaaye ndani yetu hututamani kiasi cha kuona wivu?”

### 1 Petro 3:7

“Kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu; na kama warithi pamoja wa neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe.”

### Yohana 15:5

“Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote.”

### Tito 2:4

“ili wawatie wanawake vijana akili, wawapende waume zao, na kuwapenda watoto wao.”

### 1 Yohana 5:3

“Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito..”

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

7. Soma Mathayo 7:12. Ikiwa kama tuna matatizo katika ndoa yetu, ni kwa sababu mtu fulani hatembei katika ____________ ____________________________________

8. Soma 1 Wakorintho 13:4. Upendo ni:

   A. hisia.

   B. hisia nzuri.

   C. hufadhili.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Mathayo 7:12

"Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii."

### 1 Wakorintho 13:4

"Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Waefeso 5:31-32. Waefeso 5:31 ni nukuu kutoka Mwanzo 2:24. Kwa kuangalia Waefeso 5:32, nini ambacho unfikiri Mungu anakizungumzia kwenye kifungu hiki? **Uhusiano kati ya Kristo na Kanisa lake (limefananishw ana ndoa).**

2. Soma Yakobo 4:4-5. Mistari hii inafundisha nini? **Mungu ana wivu juu yetu na anataka tuwe wa kweli Kwake.**

3. Soma 1 Petro 3:7. Ni kwa nini unapaswa kutembea katika umoja na upendo kwa mke wako na mume wako? **Ili maombi yetu yasizuiwe.**

4. Soma Yohana 15:5. Je ndoa yako inaweza kufanikiwa pasipo Kristo kama Bwana wa maisha yako? **Hapana.**

5. Soma Tito 2:4. Upendo si tu hisia. Kufuatana na maandiko, upendo unaweza **kufundishwa**.

6. Soma 1 Yohana 5:3. Tunapotembea katika amri za Mungu, tunatembea katika upendo.

7. Soma Mathayo 7:12. Ikiwa kama tuna matatizo katika ndoa yetu, ni kwa sababu mtu fulani hatembei katika **upendo**.

8. Soma 1 Wakorintho 13:4. Upendo ni: **C. hufadhil**i.

DARAJA 2

# SOMO 11

# NDOA (Sehemu 2)

*Na Don Krow*

Leo tunakwenda kuangalia tena kwenye somo la ndoa, na swali ni, "Ndoa ni nini?" Je umeshawahi kufikiria kuhusu hilo? Kufuatana na Biblia, ilikuwa ni wazo la Mungu kuunda ndoa. Ndoa ni kuunganishwa pamoja, kuwa wamoja, kuungana. Mwanzo 2:24 inasema, *"Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe,* [wataunganishwa, na mwanamume ataambatana na mke wake] *nao watakuwa mwili mmoja*" (Tafsiri ya *New International Version*). Je ulifahamu kuwa ndoa ni zaidi ya kuunganishwa, zaidi ya kuwa kitu kimoja? Kwa mfano, 1 Wakorintho 6:15-6 inasema nikienda nje, kama Mkristo, na kujiunganisha na kahaba, Ninafanyika mwili mmoja naye. Halafu zingatia nukuu kutoka Mwanzo 2:24 kuhusu ndoa. Mimi kujiunganisha na kahaba si tu kuwa moja kwa moja kutanifanya mimi kuwa nimepata talaka kutoka kwa mke wangu au kunifanya kuwa nimemwoa kahaba kwa sababu nilifanya tendo la ndoa naye. Hivyo ndoa ni nini? Ikiwa ndoa ni kuwa kitu kimoja, ikiwa kama ni kuunganishwa kwa pamoja, ikiwa kama ni kufanyika mwili mmoja, nini ni tofauti kati ya hilo na kwenda kwa kahaba? Ni dhahiri, ikiwa kama ulikwenda kwa kahaba, utafanyika mwili mmoja naye.

Biblia inasema kuwa ndoa ni kule kuwa kitu kimoja, kuunganishwa pamoja, kufanywa kuwa pamoja, lakini ni zaidi ya hayo. Ni kuunganishwa pamoja kupitia agano. Neno "agano" kwa Kiebrania ni berith, na ina dhana ya kufunga pamoja. Ni kujitoa kwa mwisho kwa mtu, hata kujitoa mpaka kifo kitakapo watenganisha. Sasa, ikiwa kama ningeenda kwa kahaba, ikiwa kama nimetenda dhambi mbaya kama hiyo, hakuta kuwa na kujitoa kwa upande wangu kwake. Chanzo cha ndoa ni kwanza kuacha wengine wote. Biblia inasema utamwacha baba na mama yako nawe utaambatana na mke wako. Ezekieli anasema, *"Umefanyika kuwa wangu."* Ni kuwaacha wengine wote kwa ajili ya huyu – kujitoa wewe mwenyewe kwa huyu. Kawaida ikiwa kama wewe, katika jinsi ya kawaida, ukienda kwa mtu mwengine wakati umeoa, hilo lita kwenda kinyume na kanuni ya ndoa, kule kuwa kitu kimoja na umoja ambao unakuja kutokana na agano, au kujitoa. Ezekieli 16:8 analiita agano la ndoa. Katika Waefeso 5, tunajifunza kuwa katika ndoa, mume anapaswa kumpenda mke wake, kama ambavyo Kristo alivyolipenda kanisa, hivyo ni agano la upendo. Sababu kuwa ni agano la upendo ni kwa kuwa upendo

ndiyo kanuni inayotawala katika ndoa. zaidi ya vitu vyote, upendo ni lazima uwe ni kanuni inayotawala ya ndoa.

Ndoa ni agano la kuwa kitu kimoja. Inasema katika 1 Petro 3:7 kuwa kama sita mheshimu na kumpenda mke wangu kuwa kama chombo dhaifu na kutambua ya kuwa sisi tu warithi pamoja wa neema ya uzima, maombi yetu yatazuiwa. Fikiria kuhus hilo – maisha yetu ya kiroho yanaweza kuzuiliwa ikiwa kama hatutatembea katika umoja na upendo ambao Mungu ameutengeneza kwa ajili ya mahusiano ya ndoa. Methali 2:16-17 inazungumzia kuhusu mwanamke mkaidi ambaye anaacha agano la ndoa yake, mwongozo wa ujana wake, na mahusiano hayo ya ndoa yanaitwa agano la Mungu wake. Hili ni jambo la kumaanisha sana. Ni agano tunalolifanya kwa mtu mwengine, lakini pia ni agano tunalolifanya mbele za Mungu. Kwa kadiri nina vyopenda kuwa hudumia watu, Mungu ana kipa umbele, na hilo ni kuweka mtazamo wetu kwenye ndoa yetu. Ndoa hakika ni kuweka mtazamo wa maisha yangu kwa mtu mwengine, na kama nilivyosema, kanuni inayotawala ni upendo.

Mathayo 7:12 inasema basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabi. Hii ndiyo haswa kanuni ambayo inapaswa kutawala katika ndoa. Si kitu cha ubinafsi, siyo kwa ajili ya mtu binafsi, siyo kuhusu nini ambacho mtu huyu anaweza kukupa. Biblia inasema katika 1 Wakorintho 13:4 upendo hufadhili. Hiyo ina maanisha kutafuta ustawi wa mwengine, kuwa mkarimu na mwema, na mara zote kutafuta kilicho bora kwa ajili ya wengine. Sababu kwa nini ndoa imetengenezwa jinsi hiyo ni kwa sababu ni mfano, muundo, wa kile ambacho uhusiano wa kweli na Mungu unavyopaswa kuwa. Ametupa kielelezo katika hali ya asili. Ametuonyesha jinsi ya kuwa na ndoa nzuri, ndoa kuu, kwa sababu Anataka sisi tuwe na muundo wa haswa nini ni mahusiano ya umeilele pamoja Naye. Ndoa ni mpaka pale kifo kitakapotutenganisha, kitu cha muda mfupi. Biblia inasema ya kuwa katika ufufuo, wala hawaoi au kuoana. Mungu anatutaka tuelewe kuwa na ndoa nzuri – kanuni za upendo – kanuni ya kutoa bila ubinafsi kwa mwengine. Anasema, "Ninachotaka hakika ukielewe ni kuwa Nimekuita kwenye mahusiano ya ndoa pamoja Nami – siyo mahusiano ya muda mfupi, siyo yale ambayo yatadumu tu kwa miaka michache na halafu yanakwisha, bali mahusiano ya milele ambapo upendo Wangu wote utadhihirishwa kwako milele na milele."

Ngoja nikupe kanuni chache za ndoa. Ndoa ni kuunganishwa na si tu kuwa katika kushirikiana. Biblia inalizungumzia katika Mwanzo 4 kama kujua na katika 1 Petro 3:7 kama kuwa warithi pamoja wa neema ya uzima. Ndoa ni agano, ambayo maana yake ni kitu kinachofunga; Kuna kujitoa kunakohusika. Dhambi haikuingia katika kanisa la kwanza; iliingia kwenye ndoa ya kwanza, hivyo tunahitaji kupata kitabu cha mwongozo, pata maelekezo kuhusu ndoa, na tekeleza kanuni za upendo maishani mwetu. Pia tunauliza, "Upendo ni nini?" Maelezo ya maana ya upendo hakika yako katika, hali ya kutokuwa na ubinafsi. Isaya 53:6

inasema sisi kama kondoo,tumepotea na kil ammoja ameigeukia njia yake, bali katika ndoa, tunamtazama mwengine na kutafuta ustawi wao na faida.

Biblia inatuambia katika Waefeso kuwa kumpenda mke wako ni kama kuupenda mwili wako mwenyewe. Sisi waume tunapaswa kumfurahia na kumheshimu mke ambaye Mungu ametupa, ambayo maana yake ni kumfurahia na kumshukuru. Kuupenda mwili wako mwenyewe haimaanishi kuwa unakaa na kujishika mikono wewe mwenyewe, unajipongeza mwenyewe kwa kujipiga piga, na kusema, "Oo, nina kupenda." Si hivyo kabisa. Kujipenda mwenyewe ni kujilinda mwenyewe, kujilisha, na kujitunza wewe mwenyewe. Kamwe hatupaswi kuwachukulia wake zetu kirahisi tu, kamwe usichukue moja ya udhaifu wake na kuuweka wazi kwa watu wengine, kamwe usimtanie, au kufanya mambo ambayo yata muumiza. Tunapaswa kuwapenda kama tunavyojipenda wenyewe.

Ningependa ujiinue wewe mwenyewe kwa Mungu na awali ya yote umshukuru Yeye kwa kukupenda wewe. Jambo la pili nina lotaka ulifanye ni kumshukuru Yeye kwa ajili ya mwenzi wako, yule Aliyekupa. Hiyo ni sehemu ya tatizo. Hujawahi kumuonyesha mwenzi wako ya kuwa unamfurahia; unamdharau, na Biblia inasema kuwa kimsingi huo ni ubinafsi na ni dhambi. Inasema katika Waefeso 5 kuwa Yesu alilitakasa kanisa kwa kuliosha kwa maji na kwa Neno, kwa Maneno yake alinena kwa kanisa. Unapotamka maneno juu ya mwenzi wako, yata inuka kwenye kiwango cha maneno unayoyatamka. Ikiwa kama utasema "Wewe hufai,"Sura yako mbaya, Umenenepa sana," utaikandamiza ndoa yako na wala hutaleta umoja bali utengano na mafarakano. Lakini kama utatamka maneno ya ukarimu kama vile "Mpenzi, Ninashukuru kwa kile unachokifanya. Ninakufurahia wewe. Nina kupenda," na uyasindikize maneno hayo na matendo yako, mwenzi wako atainuka kwenye kiwango cha maneno hayo.

Je huwezi kuona leo ya kuwa mengi ya matatizo yako katika mahusiano yako ya ndoa ni maneno uliyoyanena? Umemwangusha mwenzi wako chini badala ya kumuinua juu. Ninakutia moyo utamke maneno mazuri kwa mwenzi wako leo. Upendo si hisia; upendo ni kutafuta ustawi na faida za mtu mwengine bila kujali jinsi unavyojisikia. Anza leo na matendo ya ukarimu, ni kama vile kupaka matabaka kadhaa ya vanishi kwenye kipande cha mbao. Ndivyo ambavyo upendo unavyojengwa – kwa matendo madogo ya ukarimu. Anza kuenzi, kuheshimu, kuthamini, na kutamka maneno ya upendo kwa mwenzi wako, na utaona tofauti. Mungu akubariki unavyozitekeleza kanuni hizi.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Methali 18:22. Ndoa ni:

   A. kitu chema

   B. kibaya

   C. kinachopendeza mbele za Bwana

2. Soma Waebrania 13:4. Tendo la ndoa katika ndoa (au kitanda cha ndoa) ni:

   A. Dhambi

   B. chafu na lenye uovu

   C. lisilo najisi

3. Soma Mhubiri 9:9 (Tafsiri ya Toleo la New American Standard). Ndoa ya kimungu ni zawadi na thawabu kwako katika maisha haya kutoka kwa Bwana. Kweli au Si Kweli.

4. Soma 1 Yohana 3:18 (Tafsiri ya New Century Version). "Hakimu Phillip Gilliam alisema kuwa kati ya kesi za mahakama za watoto 28,000 ambazo alizihukumu, kukosa upendo kati ya baba na mama ilikuwa ndiyo sababu kubwa aliyoijua ya kesi hizo kutokea " (Kwa pamoja Milele, uk. 152). Tunapaswa kuonyeshaje upendo?

   ______________________________________

   ________

5. Soma Waefeso 5:28. Sitakiwi kutokumjali mke wangu tena kuliko ninavyoacha kuujali mwili wangu. Kweli au Si Kweli.

6. Soma 1 Yohana 3:16. Maneno "Ninakupenda" yanaweza kuwa mazuri ikiwa kama yatasindikizwa na matendo. Yesu aliyasindikiza maneno yake kwa kuyatoa maisha Yake kwa ajili yetu. Tunapaswa kuyatoa maisha yetu kwa

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Methali 18:22

"Apataye mke apata kitu chema; Naye ajipatia kibali kwa BWANA."

### Waebrania 13:4

"Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia."

### Mhubiri 9:9 (Toleo la Tafsiri ya New American Standard)

"Furaha maisha pamoja na mke umpendaye, siku zote za maisha yako ya ubatili, Alizokupa chini ya jua; kwa maana hii ndiyo thawabu yako katika maisha; na katika taabu zako ulizozitaabika chini ya jua."

### 1 Yohana 3:18 (Tafsiri ya New Century)

"Watoto wangu, tuwapende watu sit u kwa maneno pekee na kwa kuzungumza, bali kwa matendo yetu na kuwajali kweli kweli."

### Waefeso 5:28

"Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Ampendaye mkewe hujipenda mwenyewe."

### 1 Yohana 3:16

"Katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

ajili ya wenzi wetu katika njia nyingi za kimatendo iwezekanavyo kwa kadri tutakavyoweza. Kweli au Si Kweli. Shirikisha baadhi ya njia za kimatendo ambazo kwazo ungependa upendwe. ____ ________________________________ ____________________

7. Soma Waefeso 5:25-26. Mke wangu atakwenda kuishi kwenye kiwango kutokana na kile ambacho nitakwenda kumtamkia. Nina mleta kwenye uwezo wa kile ambacho nina kitamka juu yake. Kweli au Si Kweli.

8. Soma Warumi 8:38-39 na 1 Yohana 4:19. Tunavutwa (au kupendwa) kwa maneno ya mapenzi yanayo nenwa kwetu yaki fuatiwa na matendo. Mungu alituvuta kwa kuzungumza nasi maneno yenye upendo kutoka kwenye barua Yake ya upendo, iliyoandikwa kwenye Maandiko. Kweli au Si Kweli.

9. Soma 1 Yohana 5:3 and 2 Yohana 6. Zile jinsi ya kufanya za upendo zinaelezewa na kujulikana na amri za Yesu. Tunaweza kujifunza kanuni hizi za upendo kutoka kwenye neno la Mungu. Kweli au Si kweli.

10. Soma Yohana 14:15. Upendo si swala la hisia zako bali utashi wako. Kila amri katika maandiko imepewa kwenye utashi wa mwanadamu, kamwe si kwenye hisia zake. Mungu kamwe hakuambii jinsi ya kujisikia, bali anakuambia jinsi ya kutenda. Kweli au Si Kweli.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Waefeso 5:25-26

“[25] Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; [26] Ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno.”

### Warumi 8:38-39

“[38] Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala wenye uwezo, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, [39] wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.”

### 1 Yohana 4:19

“Tunampenda, kwa maana Yeye alitupenda sisi kwanza.”

### 1 Yohana 5:3

“Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito.”

### 2 Yohana 6

“Na huu ndiyo upendo, ya kuwa twzishika amri zake. Na hii ndiyo amri, ya kuwa, kama mlivyosikia toka mwanzo, mnapaswa kutembea katika hizo.”

### Yohana 14:15

“Mkinipenda, mtazishika amri zangu.”

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

11. Soma Wagalatia 5:22-23. Upendo hauji kiasili. Ni lazima mtu ajifunze na uzaliwe ndani ya mwanadamu na Roho Mtakatifu. Upendo ni tunda la:

    A. kufikiri kwa mwanadamu

    B. asili ya mwanadamu

    C. Roho wa Mungu.

12. Soma Waefeso 5:31-32. Ndoa nzuri ni mfano wa kuigwa wa kipimo kidogo cha nini? ______________________________ ______________________________ ______________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Wagalatia 5:22-23

"[22] Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, [23] upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria."

### Waefeso 5:31-32

"[31] Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja. [32] Siri hiyo ni kubwa; ila mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa."

# MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Methali 18:22. Ndoa ni: **A. kitu chema na C. kinachopendeza mbele za Bwana.**
2. Soma Waebrania 13:4. Tendo la ndoa katika ndoa (au kitanda cha ndoa) ni: **C. lisilo najisi.**
3. Soma Mhubiri 9:9 *(Tafsiri ya Toleo la New American Standard)*. Ndoa ya kimungu ni zawadi na thawabu kwako katika maisha haya kutoka kwa Bwana. **Kweli.**
4. Soma 1 Yohana 3:18 *(Tafsiri ya New Century Version)*. "Hakimu Phillip Gilliam alisema kuwa kati ya kesi za mahakama za watoto 28,000 ambazo alizihukumu, kukosa upendo kati ya baba na mama ilikuwa ndiyo sababu kubwa aliyoijua ya kesi hizo kutokea " (Kwa pamoja Milele, uk. 152). Tunapaswa kuonyeshaje upendo? **Kwa matendo na kujali katika kweli.**
5. Soma Waefeso 5:28. Sitakiwi kutokumjali mke wangu tena kuliko ninavyoacha kuujali mwili wangu. **Kweli.**
6. Soma 1 Yohana 3:16. Maneno "Ninakupenda" yanaweza kuwa mazuri ikiwa kama yatasindikizwa na matendo. Yesu aliyasindikiza maneno yake kwa kuyatoa maisha Yake kwa ajili yetu. Tunapaswa kuyatoa maisha yetu kwa ajili ya wenzi wetu katika njia nyingi za kimatendo iwezekanavyo kwa kadri tutakavyoweza. **Kweli.** Shirikisha baadhi ya njia za kimatendo ambazo kwazo ungependa upendwe.
7. Soma Waefeso 5:25-26. Mke wangu atakwenda kuishi kwenye kiwango kutokana na kile ambacho nitakwenda kumtamkia. Nina mleta kwenye uwezo wa kile ambacho nina kitamka juu yake. Kweli. **Neno la Kiyunani katika Waefeso 5:26 ni** *rhema***, likimaanisha "maneno yaliyotamkwa".**
8. Soma Warumi 8:38-39 and 1 John 4:19. Tunavutwa (au kupendwa) kwa maneno ya mapenzi yanayo nenwa kwetu yaki fuatiwa na matendo. Mungu alituvuta kwa kuzungumza nasi maneno yenye upendo kutoka kwenye barua Yake ya upendo, iliyoandikwa kwenye Maandiko. **Kweli. Neno la Mungu limejawa na maneno ya upendo kwetu.**
9. Soma 1 Yohana 5:3 and 2 John 6. Zile jinsi ya kufanya za upendo zinaelezewa na kujulikana na amri za Yesu. Tunaweza kujifunza kanuni hizi za upendo kutoka kwenye neno la Mungu. **Kweli.**
10. Soma Yohana 14:15. Upendo si swala la hisia zako bali utashi wako. Kila amri katika maandiko imepewa kwenye utashi wa mwanadamu, kamwe si kwenye hisia zake. Mungu kamwe hakuambii jinsi ya kujisikia, bali anakuambia jinsi ya kutenda. **Kweli.**

11. Soma Wagalatia 5:22-23. Upendo hauji kiasili. Ni lazima mtu ajifunze na uzaliwe ndani ya mwanadamu na Roho Mtakatifu. Upendo ni tunda la : **C. Roho wa Mungu.**

12. Soma Waefeso 5:31-32. Ndoa nzuri ni mfano wa kuigwa wa kipimo kidogo cha nini? **Kristo na kanisa Lake.**

# SOMO 12
# AINA YA UPENDO WA MUNGU (Sehemu 1)

*Na Don Krow*

Leo tutaongelea kuhusu aina ya upendo wa Mungu. katika 1Wakorintho 13:13 inasema, *"Basi, sasa inadumu imani, tumaini, upendo, haya matatu; na katika hayo lililo kuu ni upendo"* (Upendo). Halafu 1 Wakorintho 14:1 inasema, *"Ufuateni upendo, na kutaka sana karama za rohoni, lakini zaidi kwamba mpate kuhutubu."* Bibilia inasema kufuata upendo, uufuatilie,na uufanaye kuwa lengo lako kuu. Tafsiri nyingine zinasema uufanye mpango wako mkuu. Ndicho kitu pekee tutakachoenda nacho toka kwenye maisha haya kwenda kwenye umilele. Hatuta chukua magari yetu,nyumba zetu,au fedha zetu, lakini tutachukua upendo ambao Yesu Kristo ameiongiza kwenye maisha yetu kupitia Roho Mtakatifu.Upendo ndiyo kitu pekee chenye thamani na maana ya milele.

Upendo una maanisha nini hasa? Nina sema ninampenda mke wangu, nina penda malai, nina penda chakula kilicho tengenezwa kwa matunda. Kuna neno moja tu katika kiingereza la kuueleza upendo, hiyo ninaposema nina mpenda mke wangu na halafu nikasema ninampenda paka, je mke wangu anafurahia? Hafurahii kabisa. Unaona ninacho sema? Tunapotumia neno upendo, watu wengine wanadhani ina maanisha tendo la ndoa, wengine wanafikiria ni hisisa kali sana za ndani – watu wana maana nyingi za maana ya upendo. Katika lugha ya Kiyunani kuna maneno manne makuu. Moja ni *eros*, ambalo hakika halitumiki katika Bibilia, na linaelezwa kuwa kama ni mvuto wa kimapenzi mapenzi ya kukutana kimwili. Mungu aliruhusu aina hiyo ya upendo pale Aliposema mwanaume atamwacha baba na mama yake, na ataambatana na mke wake, na watakuwa mwili mmoja. Kitabu katika Biblia kiitwacho Wimbo Uliyo Bora kinaongelea vitendo vya mapezi ambavyo Mungu aliagiza vifanyike katika mahusiano ya ndoa tu.

Aina nyigine ya upendo, inaitwa *storge* na ni muunganiko wa kiasili au upendo katika mahusiano ya familia. Halafu kuna *phileo*, ambao unatokana na neon la msingi *philia* Neno hili limetumika kama mara sabini na mbili kwenye Agano Jipya na lina maanisha hisia nzuri ya upendo huja na kuondoka katika kina. Watu wengi wanozungumzia kuhusus upendo hufikiria

kuwa hivyo ndivyo hakika upendo ulivyo, hivyo basi "Ninapenda na ninaacha kupenda." Ikiwa kama ndoa yako imejengwa juu ya aina hiyo ya upendo, basi kutakuwa na nyakati ambapo utakuwa na kiwango cha juu na kuna wakati utakuwa na kiwango cha chini. Unaweza kupenda na kutokupenda ukiwa kwenye msingi huo.

Biblia inasema tunatakiwa kupendana mithili ya aina ya upendo wa Mungu, ambao ni upendo wa *agape*. Upendo wa "*agape*" ni nini? Kuna sura nyingi, na 1 Wakorintho sura ya 13 inatupa maana pana kuhusiana na upendo unahusisha nini. Katika 1Yohana 5:3 inasema, *"Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito."* Amri za Yesu zinatuonyesha upendo, lakini kama ningekwenda kufupisha. NIngetumia Mathayo 7:12, *"Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii."* Siyo swala la watu wale wote kule kanisani kuwa hawanipendi, wala hawajali kuhusu mimi, na hili na lile. Hapana, Biblia inasema chochote ambacho ungetaka mtu akufanyie, wewe wafanyie kwanza. Huo ndiyo upendo. Inakwenda kinyume na miili yetu, kinyume na asili yetu ya kutafuta ustawi na faida ya watu wengine zaidi yetu sisi wenyewe. Inahitaji Mungu. Usifikiri ya kuwa ninasema hili linaweza kudhihirishwa bila Mungu. Biblia inasema tunda la Roho ni upendo, na Mungu ni upendo. Yeye ndiye chanzo cha upendo na ambaye ndiye atakayetuonyesha jinsi ya kupenda kwa kupitia amri zake. Yeye ndiye atakayetupa nguvu, katika katika miili yetu, ili kufanya uchaguzi sahihi na maamuzi na kutenda katika kanuni sahihi.

Nina fanya kazi kwenye huduma ya Andrew Wommack, na siku moja mika michache nyuma nilitaka kwenda kuomba kama ambavyo kwa kawaida hufanya baada ya kazi. NIlikuwa kwenye bustani ya kupumzikia, na nikasema, "Mungu, Hakika ninataka nihudumu kwa mtu fulani." Ilikuwa ni siku yenye joto, na nikamwona kijana mdogo wa kiume na wa kike wameketi kwenye mabembea. Kulikuwa na bembea wazi, hivyo nikaenda na kuketi kwenye bembea hiyo. Nikamgeukia binti yule mdogo na kusema, "Ni siku nzuri, si ndiyo?" Akasema "Mimi sizungumzi Kiingereza," Na nikauliza, "Unatokea wapi?" Akasema alikuwa anatokea nchini Romania. Nilijua kuliwa na watu kutoka Romania katika eneo lile, na nikawaona watu hawa wakiniangalia, pengine wakishangaa kwa nini nilikuwa nikizungumza na watoto wao. Nikawafuata na kusema, "NInataka kuwasaidia." Wakasema, "Ungetaka kutusaidia? Kwa nini ungetaka kufanya hivyo? Wala hutujui!" Nikasema, "Kwa sababu Mungu anataka kuwa saidia." NImekuwa nikitafakari kanuni za upendo kwenye kitabu cha 1 Yohana 3:18 ambapo inasema, *"Watoto wadogo, tusipende kwa neno, wala kwa ulimi, bali kwa tendo na kweli"* Hatutakiwi kupenda kwa maneno ya vinywa vyetu pekee, lakini pia kwa matendo yetu. Ingawa kwa kawaida sibebi fedha pamoja name, siku ile nilikuwa nzo kidogo mfukoni mwangu. Nikazichukua na kusema "Hizi ni kwa ajili yako," na kuwapa fedha hizo. Kwa kuwa nilikuwa nimefunga siku ile, Nilikuwa na chakula kidogo pamoja nami, hivyo nikasema, "Na hapa kuna chakula kwa ajili ya

familia yenu." Waliguswa na kusema, "Wewe ni nani? Nika waambia, "Mungu ametengeneza miadi ya kimungu kwetu sisi kukutana leo, na nitakwenda kuwaona tena."

Nilikwenda nyumbani na kumwambia mke wangu kuhusu kukutana na wale Warumania. Nikamtoa jogoo kwenye jokofu letu na kumpika. Siku iliyofuata nika nunua boksi limejaa vyombo kwenye mauzo ya gereji na nikarudi pale kwenye eneo la kupumzikia na mke wangu. Wale Warumania na watoto wao walikuwapo pale, na nikasema, "Ninawaletea zawadi. Ni nzito, Hivyo nitazibeba na gari yangu, na kama utanionyesha mahali mnapoishi, Nitazipeleka zawadi hizo nyumbani kwenu." Tulipofika kwenye nyumba yao ya chumba kimoja kidogo, Nikatoa vyombo – kila kitu kiliendana– nje ya boksi na nikaanza kuwapa vitu, kimoja baada ya kingine. Nilipokuwa nikiwakabidhi, machozi yalianza kutiririka nyusoni mwao, na yule mama akasema, "Mimi nitalia! Mimi nitalia!" Nikasema, "Jumatatu usiku tunakuwa na kipindi cha kujifunza Biblia nyumbani kwetu, na ningependa kukukaribisha." Wakasema "Tunataka kuja, " lakini nikasema, "Sitaki mje kwa sababu niliwapa zawadi." Wakasema, "Hapana, tunataka kuja na kukutana na marafiki zako."

Kwa kuwa hawakuwa na usafiri, Nikawachukua, nikawapeleka nyumbani kwangu, na kabla ya muda kupita, Mungu akaanza kuwagusa. Hawakuweza kuzungumza Kiingereza vizuri sana, lakini Aliwagusa pale tulipowaombea. Upendo wa Mungu ulikuwa ukidhihirika ndani mwao. Kabla ya muda kupita, tulikutana na wana ndoa wengine wa Kirumania, na nikasema kwa wale wana ndoa wa kwanza, "Je mtaenda na mimi kunisaidia kukutana na wana ndoa wengine kutoka Rumania?" Walikubali na siku moja nilipata simu kutoka kwao, "Ndugu Don, tumesikia kuhusu wewe. Tuna *'hali ya upweke',* na tunataka kukutana na wewe," Hivyo nikawachukua marafiki zangu wa Kirumania na tukaenda kukutana nao. Nilichukua zawadi, chakula, na aina zote za vitu ili kuwapelekea. Nilipofanya hivyo na kuanza kuwatembelea, kila kitu kilikuwa kizuri sana mpaka pale moja ya wana ndoa wa kwanza wa Kirumania aliposema, "Unahitaji kwenda kwenye kipindi cha kujifunza Biblia. Wanaongea kuhusu Yesu, na ni ya ajabu sana!" Walisema, "Subiri kidogo! Tumekuja kutoka kwenye nchi ya Kikomonisti na hatujui kama kuna Mungu. Hatutaki haya mambo kuhusu Yesu."

Nilisema "Acha niwe rafiki," na nikaanza kuwatoa nje siku za mwisho wa wiki na kuwanunulia nguo, makoti, na vitu walivyovihitaji. Walijisikia kuwa na aibu sana na kusita mno. "Vyema, hauhitaji koti?" "Vyema, ndiyo ninahitaji, lakini …" "Basi acha tuchukue koti hili kwa ajili yako." Nilianza kuwapenda kwa matendo, lakini walikuwa bado hawaji kwenye kipindi chetu cha kujifunza Biblia mpaka pale niliposema, "Inawezekana pale kuna baadhi ya Wamarekani ambao wanaweza kuwasaidia kupata kazi." Hapo ndipo walipokuja mara tu. Katika kipindi cha kujifunza Biblia usiku ule, Nilisema kitu cha kijinga sana kwa Bwana, "Bwana, itabidi unipe zawadi ya kweli ya lugha jioni ya leo kwa kuwa hatuwezi hata kuwasiliana sisi kwa sisi vizuri." Kulikuwa na baadhi ya Wamarekani kwenye kipindi cha kujifunza Biblia usiku

ule ambao walitoa shuhuda zao. Nilipoanza kuongea, mama kutoka kwenye wale wana ndoa wa pili wa Kirumania akaanza kufungunka, na nikajua kuna kitu kilikuwa kikitokea. Baada ya kipindi nikasema "Ngoja niwaombee," na tulipokuwa tukiomba, Ghafla Mungu akawagusa na kujaza eneo lote tulipokuwapo na upendo Wake. Halafu yule mama akasema, "Unajua, Wakati Wamarekani walipokuwa wakizungumza, Sikuweza kuelewa chochote walichokuwa wakikisema, lakini ulipoamka na kuanza kuzungumz akuhusu Yesu, Upendo Wake kwetu, na kile alichokifanya ili tuweze kuwa na uhusiano na Yeye, Nilielewa kila neno ulilosema! Nilielewa vizuri kabisa! Ni lazima itakuwa ni Mungu! Itakuwa ni Mungu!" Matokeo yake, maisha yakabadilishwa, sit u kwa wale Warumania.

Ngoja nikuambie nini kilichotokea baada ya hapo. Nyumba yangu ikaanza kujaa siku za Jumatatu usiku na watu wa kimataifa – Warumania, Wabulgaria, na watu kutoka Urusi. Mungu alikuwa akiyabadilisha maisha, na walijua ya kuwa tunawapenda. Hata tulikuwa na watu kutoka Afrika. Ingawa tuliongea sisi kwa sisi kwa taabu, jambo moja walilolijua: Tulipoomba, Mungu angejidhihirish aYeye mwenyewe kwao. Wao pia walijua ya kuwa ningefanya chochote kwa ajili yao nay a kuwa niliwapenda. Mungu aliyabadilisha maisha yao na maisha ya watu wengine wengi, na ninataka kukuambia jinsi ilivyotokea. Ilitokea kwa sababu siku moja kwenye eneo la kupumzikia, Niliwaona baadhi ya watu wa rangi nyengine, Taifa jengine. Sikuwa na hisia zozote za upendo, lakini nilijua ya kuwa huu ndiyo upendo: Chochote ambacho ungependa mtu akufanyie, wewe wafanyie kwanza. Nilitafuta ustawi wao na faida zao biia kujali jinsi nilivyokuwa ninajisikai, na unajua nini kilichotokea? Walishukuru sana kiasi kwamba kile kilichoibuka ndani yao kwa ajili yangu ilikuwa ni upendo wa philia, upendo ambao una hisia, na wakaanza kuniambia "Nina kupenda" na kunikumbatia na kunibusu. Ilichokifanya ndani yangu ilikuwa ni kujenga aina hiyo ya hisia kwa ajili yao. Ikiwa kama unataka kuwa na upendo ambao una hisia maishani mwako, basi weka katika matendo upendo wa agape. Tafuta ustawi na faida za wengine bila kujali jinsi unavyojisikia, Na hili litajenga upendo ambao unahisia.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma 1 Yohana 5:3. Upendo wa Mungu unaonyeshwa kupitia ____________________________.

2. Soma Warumi 13:9-10. Elezea ni kwa jinsi gani amri katika mistari hii inavyo onyesha upendo. ____________________________ ____________________________________ ______________________

3. Soma Warumi 12:19-21. Tunawezaje kuwapenda maadui zetu, hata kama hatujisikii kuwapenda? ________________ ____________________________________ ____________________

4. Soma Tito 2:4. Nini ambacho kifungu hiki cha maneno kina tuonyesha kuhusu upendo? ____________________________ ____________________________________ _____________________

5. Soma 1 Wakorintho 13:4-8 (*Toleo la Contemporary English*). Elezea kanuni za upendo kwa undani. __________________ ____________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### 1 Yohana 5:3

"Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito."

### Warumi 13:9-10

"[9] Maana kule kusema, Usizini, Usiue, Usiibe, Usitamani; na ikiwapo amri nyingine yo yote, inajumlishwa katika neno hili, ya kwamba, Mpende jirani yako kama nafsi yako.[10] Pendo halimfanyii jirani neno baya; basi pendo ndilo utimilifu wa sheria."

### Warumi 12:19-21

"[19] Wapenzi, msijilipize kisasi, bali ipisheni ghadhabu ya Mungu; maana imeandikwa, Kisasi ni juu yangu mimi; mimi nitalipa, anena Bwana.[20] Lakini, Adui yako akiwa na njaa, mlishe; akiwa na kiu, mnyweshe; maana ufanyapo hivyo, utampalia makaa ya moto kichwani pake. [21] Usishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema.."

### Tito 2:4

"Ili wawatie wanawake vijana akili, wawapende waume zao, na kuwapenda watoto wao."

### 1 Wakorintho 13:4-8

(Contemporary English Version) – "[4] Upendo huvumilia na hufadhili, kamwe hauna wivu, haujivuni, hauna kiburi, au kukosa adabu. [5] Upendo hauna ubinafsi au haushikwi na hasira kwa haraka. Hautunzi kumbu kumbu ya mabaya ambayo wengine wanayafanya. [6] Upendo hufurahia katika kweli, lakini si katika maovu. [7] Upendo mar azote husaidia,

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

6. Soma 1 Yohana 3:18. Tunawezaje kujizoeza upendo kimatendo? ____________________
_______________________________________
____________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

una ukweli, una tumaini, na kuamini. [8] Upendo haukomi!"

1 Yohana 3:18 – "Watoto wadogo, tusipende kwa neno, wala kwa ulimi, bali kwa tendo na kweli"

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma 1 Yohana 5:3. Upendo wa Mungu unaonyeshwa kupitia **amri zake**.

2. Soma Warumi 13:9-10. Elezea ni kwa jinsi gani amri katika mistari hii inavyo onyesha upendo.. **Upendo haumtendei mabaya jirani yake. Kila mari inonyesaha upendo kwa kuonyesha tunatakiwa kuitiki vipi kwa majirani zetu.**

3. Soma Warumi 12:19-21. Tunawezaje kuwapenda maadui zetu, hata kama hatujisikii kuwapenda? **Ikiwa kama adui yetu ana njaa, tunawez akuwalisha; ikiwa kama wana kiu, tunaweza kuwapa kitu cha kunywa. Tunaweza kutafuta ustawi na faida za wengine, bila kujali tunavyojisikia.**

4. Soma Tito 2:4. Nini ambacho kifungu hiki cha maneno kina tuonyesha kuhusu upendo? **Upendo unaweza kufundishika. Si hisia tu.**

5. Soma 1 Wakorintho 13:4-8 (*Toleo la Contemporary English*). Elezea kanuni za upendo kwa undani. **"Upendo huvumilia na hufadhili, kamwe hauna wivu, haujivuni, hauna kiburi, au kukosa adabu. Upendo hauna ubinafsi au haushikwi na hasira kwa haraka. Hautunzi kumbu kumbu ya mabaya ambayo wengine wanayafanya. Upendo hufurahia katika kweli, lakini si katika maovu. Upendo mar azote husaidia, una ukweli, una tumaini, na kuamini. Upendo haukomi !"**

6. Soma 1 Yohana 3:18. Tunawezaje kujizoeza upendo kimatendo? **Tusipende tu kwa maneno yetu, lakini pia katika matendo yetu.**

DARAJA 2

# SOMO 13
# AINA YA UPENDO WA MUNGU (Sehemu 2)

*Na Don Krow*

Katika somo la "Aina ya upendo wa Mungu," sehemu ya 1, niliwaambia kuhusu wanandoa wa Kiromania niliokutana nao katika sehemu ya kupumzikia. Nataka nikwambia maelezo zaidi kuhusu nini kilitokea, bali kabla ya kufanya hivyo, nataka turejee baadhi ya vitu tulivyovisema kuhusu upendo wa Mungu. Yesu Kristo alikuwa kielelezo cha juu sana cha upendo kilicho wahi kuonyeshwa duniani, lakini kutegemeana na yale yalioandikwa katika Biblia, Hakuwahi kusema neno "Nakupenda." Je hili halishangazi? Kielelezo kikubwa cha upendo hakikuwahi kusema "Nakupenda." Unajua kwanini? Ni kwa sababu upendo ni zaidi ya maneno; ni matendo. Kwa mfano nimwambie mke wangu "Nakupenda" halafu natoka na kufanya uzinzi kinyume naye? Je angeamini maneno yangu, au angeamini matendo yangu? Angaliniamini kutegemeana na matendo, kwa sababu asilimia 95 ya upendo si maneno. Si katika maneno unayosema; ni yale tunayoyafanya.

Katika 1Yohana 3:18 tunasoma, *"Watoto wadogo, tusipende kwa neno, wala kwa ulimi,* [tusipende kwa maneno tu ]*; bali kwa tendo na kweli"*. Upendo ni neno la matendo. Katika Mathayo 25:35-36, Yesu anaelezea upendo kwa matendo yatokanayo, akisema, "Nilikuwa njaa, mkanilisha, nilikuwa na kiu, mkaninywesha, nilikuwa uchi, pasipo na nguo, na mkanivika, nilikuwa naumwa, na mkaja kuniangalia." Halafu katika mstari wa 40 Anasema, "Kwa kufanya haya kwa moja wapo wa ndugu zangu waliowadogo, mmenifanyia mimimi." Unaona upendo ni matendo; ni kitu unachokifanya. Waebrania 6:10 inasema, *"Maana Mungu si dhalimu hata aisahau kazi yenu, na pendo lile mlilolidhihirisha kwa jina lake, kwa kuwa mmewahudumia watakatifu, na hata hivi sasa mngali mkiwahudumia"*. Katika Mathayo 22 wakati Yesu alipoulizwa amri iliyo kuu ni ipi, Akasema ni kumpenda Mungu na kuwapenda wengine. Amri hizi mbili ni moja kiuhalisi, kama umeelewa kwa usahihi. Wakati unapoonyesha upendo kwa hawa ndugu zangu walio wadogo, Yesu akasema ni kwamba mtakuwa mnaonyesha upendo kwangu. Biblia inafundisha kwamba tuna fursa nzuri ya kumpenda Yesu Kristo katika njia za utendaji, kwa kuwapenda wengine.

Katika somo letu lililopita, Niliwaambia kuhusu wanandoa wa Kiromania niliokutana nao kwenye eneo la kupumzikia. Maisha yao yalibadilika kwa sababu nilitafuta ustawi na faida yao pasipo kujali nilikuwa najisikia vipi. Walikuwa watu wa ngozi tofauti nan chi tofauti, bali nilijua upendo wa Mungu unajionyesha wenyewe hasa pale tunapowafikia wengine kwa kujali ustawi na faida yao kama Kristo alivyofanya. Hakujisikia kwenda msalabani. Alisema, "Baba, kama kuna njia nyingine, na iwe hivyo, Bali isiwe mapenzi yangu bali ya kwako yatimie." Yesu alitafuta ustawi na faida yetu pasipo kujali yeye alijisikiaje.

Siku moja nilipata simu toka kwa Waromania hawa. Walikuwa wanalia kwa hisia. walikuwa wamekaa Marekani kwa miaka saba na nusu. Sasa hivi wanaishi Kansas na wanafanya kazi, Wakasema, "Mwishowe tumepata nafasi ya kusikilizwa kuhusu makaratasi yetu ya kimbilio la hifathi ya kisiasa. Wanatupa siku thelathini ili kukata rufaa, na halafu tutafukuzwa nchini." Watu kikawaida huwa wana nafasi ya asilimia 2-5 kwa kupata haki ya hifathi ya kisiasa katika nchi hii. Walimuendea mwanasheria akawaambia haiwezekani. Niliwaambia tutaomba na kujaribu kuwasaidia. Kwa vipi, sikujua. Nilifikiri ingalikuwa si haki kwa wao kurudishwa kwao – haswa wakati watoto wao hawakuweza hata kuongea Kiromania.

Rafiki yangu ambaye ni mbunge wa jimbo la Colorado aliyesema tuwasiliane na Mbunge anayeitwa Sam Brownback wa huko Kansas, kwa sababu wakati huo wale waromania walikuwa wanaishi huko Kansas. Hilo lilikuwa jema maana nilikuw ana rafiki anayeitwa Kim ambaye alikuwa anamfanya kazi ofisisni kwa mbunge huyo Brownback. Niliwasiliana na Kim na akapata watu wane huko Washington D.C. ambao walianza kufanyia kazi kesi hii. Jamii ya eneo linaloitwa Sublette, huko Kansas, walisimama nyuma ya wale waromania kwa kutuma maombi kwamba wanaomba waromania hawa wabaki katika jamii yao na kuweka sahihi zao kwenye barua ya maombi. "Hawa waromania ni watu wazuri, wanalipa kodi kwa uaminifu, na wanafanya kazi kwa bidiii. Walisema wanawataka wakae katika jamii yao." Kukawa na habari kwenye magazeti kuhusu swala hili. Hakika ilikuwa muugiza, na kwasababu kulikuwa na maafisi wa ngazi za juu katika serikali walioelewa kilichokuwa kinaendelea, wale Waromania wakapata barua ikiwataarifu kwamba maamuzi yamebadilishwa na wanaweza kuendelea kuishi Marekani.

Nilienda Sublette, huko Kansas. Marafiki zangu hawakujua kama nilikuw anaenda, na nilipofika huko, walikuwa wanaongea na mbunge Brownback kwenye simu kumshukuru kwa kuwasaidia kupata hifathi ya kisiasa. Hakuweza kuwepo yeye mwenyewe maana ilikuwa ni siku ya mwisho ya kusikilizwa kwa kesi ya Rais Clinton, bali mashirika ya habari ya ABC na NBC walikuwepo pale na kamera zao. Walipomaliza kuongea na simu, walikimbia na kunikumbatia, na kamera zile zikanimulika moja kwa moja. Wakasema, "Wewe ni nani, na unawafahamuje hawa watu?" Nikawaambia hadithi nzima ilivyokuwa, jinsi nilivyokutana nao na kutafuta ustawi na faida yao kwa sababu ya Mungu na kile Yesu alichosema katika Mathayo 7:12.

Halafu tukaend akwenye jumba la michezo ambapo kulikuwa na Maputo mekundu, meupe nay a kibluukila mahali na nyimbo za kizalendozilikuwa zinaimbwa. Wakati marafiki walipoingia, kila mtu akaanza kupiga kelele, na kulia kwa hisia. Meya wa mji akasema, "Leo tarehe, 12 Februari, itakuwa siku ya familia ya Jucan, kwa ajili ya kuwaheshimu hawa wa Romania." Wakachukua bendera ya Marekani ambayo mbungu alipeperusha juu ya jengo kule Washington, D.C., kwa ajili ya kuwaheshimu na kuwakabithi. Pia aliwakabithi makaratasi yalioandikwa kwamba wao ni raia halali na wanaishai kihalali – kimsingi katika maisha yao yote. Walitoa ushuhuda wao halafu wakaniomba niombe. Nikasema, "Kuna mtu mmoja hatujamshukuru vya kutosha leo na huyo ni Mungu mwenye enzi. Katika sehemu ya kupumzikia kule eneo la Colorado Springs, CO, miaka saba na nusu iliopita, nilikuwa namtafuta Mungu, nikimwambia natamani kuwafikia wengine na upendo wake. Na nikaongozwa kwa hawa waromania." Nikarudia simulizi na kusema, "Mungu anataka kukusaidia – karibuni U.S.A."

Njia ambayo haya yote yalitokea ni muugiza. Niliwajua watu sahihi kwa wakati sahihi katika sehemu sahihi. Rafiki yangu Kim alifanya mpango wa mbunge Brownback aje akutane na mimi kwenye huduma ya Andrew Wommack mwaka mmoja kabla ya haya yote kutokea. Akasema, "Unahitaji kukutana tu na Don Krow." Sikujua ni kwanini na sikuwa na amani na hili. Sikufahamu kwamba Mungu alikuwa anaweka mipango ya kuisaidia familia ambayo alijifunua mwenyewe tangu na upendo wake, kirahisi kwa sababu ya amri ya Yesu ya kwamba yale tungependa kutendewa na wengine, tuwatendee wengine. Ni muugiza ambao hawatakaa wakasahau, na watakwambia leo, "Ni kwa sababu ya Mungu." Anka, mama wa kiromania, alisema, "Imani yangu ilisita ila Mungu ni mwaminifu sana, na ameturusuhusu kuwepo Marekani."

Kuna watu wengi sasa hivi ambao wanalilia kupata upendo. Njia pekee wanayoweza kupata upendo ni pale mimi na wewe tunapofanya maamuzi kuelewa kanuni za upendo toka kwenye neno la Mungu. Upendo ni mkarimu, Upendo hutafuta ustawi wa wengine – Kama jinsi Yesu alivyotafuta ustawi wetu kwa kwenda msalabani. Mungu Akubariki leo unapoangalia zaidi kanuni za nini maana halisi ya kupenda kwa upendo wa Mungu.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Mathayo 7:12. Kwa maneno yako mwenyewe, tuelezee kanuni ya msingi. ____
______________________________________
______________________________________

2. Soma Mathayo 7:12. Katika kujaribu kujua kuhusu upendo, watu wengi hutafuta mtu sahihi. Je unatakiwa kujaribu kupata mtu sahihi au kufanyika mtu sahihi? _________
______________________________________
______________________________

3. Soma 1 Yohana 5:3. Je upendo ni hisia, au upendo ni kitu unafanya? ______________
______________________________________
_________________________

4. Soma 1 Yohana 3:18. Ukimwambia mke wako au mume wako "nakupenda !" bali ukatoka nje ya ndoa na kufanya uzinzi, je atakuamini kwa ajili ya matendo au maneno yako? ________________________
______________________________________

5. Soma Warumi 5:6-8. Je unafikiri Yesu alijisikia wepesi wa kufa msalabani? ______
______________________________________
_________________________________

6. Soma Wagalatia 5:22. Je tunaweza kupenda wengine pasipo Mungu kuwa kiini cha maisha yetu? ________________________
______________________________________

7. Soma Wagalatia 5:22. Je tunaweza kupenda wengine pasipo Mungu kuwa kiini cha maisha yetu __________________________
__________________.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Mathayo 7:12
"Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii.."

### 1 Yohana 5:3
"Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito."

### 1 Yohana 3:18
"Watoto wadogo, tusipende kwa neno, wala kwa ulimi, bali kwa tendo na kweli.."

### Warumi 5:6-8
Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, Kristo alikufa kwa ajili ya waovu. 7 Kwa kuwa ni shida mtu kufa kwa ajili ya mtu mwenye haki; lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema. 8 Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.."

### Wagalatia 5:22
"Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu,."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

8. Soma 1 Wakorintho 13: 5. Chagua toka katika maneno yafuatayo kuhusu maelezo ya chochote ambacho si upendo : Jeuri, ubinafsi, kutosamehe, ________________ ________________________________ ____________________

9. Soma 1 Wakorintho 13:8. Ni kitu gani ambacho ndicho pekee utachukua toka katika dunia hii kwenda nacho dunia ijayo, au upande wa pili wa kaburi? __________ ________________________________ __________________________

10. Soma 1 Wakorintho 10:12. 1 Wakorintho 13:5 inasema, "Upendo hauhes==abu mabaya." upendo hufunika wingi wa dhambi? ___________________________ ________________________________ ________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### 1 Yohana 4:8

"Yeye asiyependa, hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni upendo.."

### 1 Wakorintho 13:5

"haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya."

### 1 Wakorintho 13:8

"Upendo haupungui neno wakati wo wote; bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika.."

### Methali 10:12

"Kuchukiana huondokesha fitina; Bali kupendana husitiri makosa yote.."

# MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Mathayo 7:12. Kwa maneno yako mwenyewe, tuelezee kanuni ya msingi. **Wafanyie wengine kama unavyotaka wengine wakufanyie.**

2. Soma Mathayo 7:12. Katika kujaribu kujua kuhusu upendo, watu wengi hutafuta mtu sahihi. Je unatakiwa kujaribu kupata mtu sahihi au kufanyika mtu sahihi? **Uwe mtu sahihi.**

3. Soma 1 Yohana 5:3. Je upendo ni hisia, au upendo ni kitu unafanya? **Ni kitu tunachokifanya kwa kutembea katika kanuni za Mungu (amri).**

4. Soma 1 Yohana 3:18. Ukimwambia mke wako au mume wako "nakupenda !" bali ukatoka nje ya ndoa na kufanya uzinzi, je atakuamini kwa ajili ya matendo au maneno yako? **Matendo yako. Matendo hunena zaidi ya maneno.**

5. Soma Warumi 5:6-8. Je unafikiri Yesu alijisikia wepesi wa kufa msalabani? **hapana, bali alitafuta faida na ustawi wa sisi wote.**

6. Soma Wagalatia 5:22. Je tunaweza kupenda wengine pasipo Mungu kuwa kiini cha maisha yetu? **hapana.**

7. Soma Wagalatia 5:22. Je tunaweza kupenda wengine pasipo Mungu kuwa kiini cha maisha yetu? **Upendo.**

8. Soma 1 Wakorintho 13: 5. Chagua toka katika maneno yafuatayo kuhusu maelezo ya chochote ambacho si upendo : Jeuri, ubinafsi, kutosamehe. **maneno haya yote (jeuri, ubinafsi, na kutosamehe) vyote havielezi kuhusu upendo.**

9. Soma 1 Wakorintho 13:8. Ni kitu gani ambacho ndicho pekee utachukua toka katika dunia hii kwenda nacho dunia ijayo, au upande wa pili wa kaburi? **Upendo. ni wa milele.**

10. Soma 1 Wakorintho 10:12. 1 Wakorintho 13:5 inasema, "Upendo hauhesabu mabaya." upendo hufunika wingi wa dhambi? **Dhambi zote.**

DARAJA 2

# SOMO 14

# FEDHA (Sehemu 1)

*Na Andrew Wommack*

Leo nataka tushirikishane kuhusu jinsi Yesu anavyotaka tufanikiwe kifedha. Hiki ni kitu ambacho ni muhimu kwa kila mtu. Tunahitaji fedha ili tuishi, ili kupata mahitaji yetu, na kuwa Baraka kwa wengine. Mungu hajatuacha katika hili eneo na kusema,"Mimi nahusika na maisha yenu tu ya Kiroho, bali sijali kuhusu maisha yenu ya kifedha … hapo mnajijua wenyewe." Hapana, Anakupenda katika kila eneo – Roho, Nafsi, na mwili – na ameandaa majibu ya mahitaji yako. Watu wengi hugundua kwamba kiwango fulani cha mafanikio ya Kiroho ni muhimu, bali dini inamsimamao wa kuwa kinyume na hali ya kuw ana utelee.

Neno la Mungu linafundisha kinyume na tamaa ya fedha katika njia mbalimbali lakini pia liko wazi kwamba fedha ni Baraka. Katika 3 Yohana 2, Mtume Yohana anasema, *"Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo."* Hili ni tamko la nguvu sana. Yohana anasema, "Zaidi ya mambo yote!" inaongea kuhusu uponyaji, hisia, mahusiano, na fedha. Bwana anataka wewe ufanikiwe na kuwa katika afya njema zaidi ya mambo yote. Anataka ufanikiwe kiroho, katika nafsi, na mwili. Haya ndio mapenzi yake kwako.

Watu wengi wa Kidini wanaseam kwamba Mungu anataka uwe maskini, kwamba kuwa maskini ni jambo la kimungu, na kwa jinsi unavyokuwa maskini, ndivyo jinsi unavyokuwa wa kimungu. Nilikuzwa katika fikra za namna hiyo, kwamba wahubiri hawapaswi kuwa na mali nyingi, kwamba mkristo ni mtu ambaye anapaswa kupungukiwa. Hili halina tija katika maandiko. Abraham alikuwa mtu tajiri wakati wake, kwa kiasi ambacho wafalme walimuomba aondoke kwenye mipaka yao kwa ajili ya mali aliokuwa nayo kwa kuwa mali yake ilikuwa inaathiri utajiri wan chi zao. Ndivyo ilivyokuwa na Isaka na Yakobo. Yusufu alikuwa mtu aliye fanikiwa na alikuwa na utele. Daudi alimtolea Mungu sadaka toka kwenye hazina yake binafsi zaidi ya Dola za Marekani Bilioni 2.5 thamani ya dhahabu na fedha ili kujenga hekalu. Solomoni, mwanawe Daudi, alikuwa ndiyo mtu tajiri kati ya watu wote waliowahi kuishi duniani. Wakati unapoangalia maandiko, watu waliokuwa wakimtumikia Mungu, Mungu aliwabariki kifedha.

Kuna wengine walipambana bali walipungukiwa. Paulo alisema katika Filipi 4:13 Kwamba anayaweza mambo ypote katika Kristo amtia nguvu na alijifunza kurithika katika kila hali aliokuwa nayo. Alisema alijua jinsi ya kutosheka na jinsi kuwa katika kifungo. wakati watumishi wa Mungu walipitia umaskini na ugumu, bali huwezi kupata katika maandiko kwamba kwa kadri ulivyo maskini, ndivyo ulivyo wa Kiroho zaidi. Hili si kweli, unaweza kwenda mitaani na kukosa uthibitisho huo. Ni kweli kuna ukweli kwamba tamaa ni dhambi. Katika 1 Timotheo 6:10 inasema, *"Kupenda pesa ndio chanzo cha uovu …"* Watu wengine huchukua hilo na kusema fedha ndiyo chanzo cha uovu, bali inasema kupenda pesa ndiyo chanzo cha uovu. Kuna watu wanaopenda pesa na hawana hata senti; wengine wana mali nyingi bali hawapendi pesa. Wanaitumia tu.

Kumb 8:18 inaonyesha kwamba madhumuni halisi ya mafanikio ya kifedha. Bwana alikuwa anaongea na wana wa Israel, ambao walitakiwa kuingia katika nchi ya ahadi na walikuwa wapate utajiri na mafanikio kwa kiasi ambacho hawajawahi kufanikiwa. Aliwaambia, *"Bali utamkumbuka Bwana, Mungu wako, maana ndiye akupaye nguvu za kupata utajiri; ili alifanye imara agano lake alilowapa baba zako, kama hivi leo."* Kutegemeana na maandiko haya, madhumuni ya mafanikio si kuwa na utele wa vitu kwa ajili ya matumizi binafsi ya kichoyo, bali ili uweze kuimarisha agalo na Mungu hapa Duniani. Kwa maneno mengine, Mungu atakubariki ili na wewe uweze kuwabariki wengine. katika Mwanzo 12:2 Bwana alimwambia Abraham, *"Bwana akamwambia Abramu, Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha."* Kabla haujawa Baraka kwa mtu yeyote, wewe mwenyewe unatakiwa upoke Baraka.

Unahitaji baadhi ya vitu na kuwa na mahitaji ambayo Mungu anahitaji kututimizia, bali ni zaidi ya hali ya ubinafsi. anataka kukubariki ili aweze kupata fedha kupitia wewe na ili uwe Baraka. Katika 2 Wakorintho 9:8 inasema, *"Na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili ninyi, mkiwa na riziki za kila namna siku zote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema."* Hili linaeleza kwanini mungu atakwenda kukufanikisha – ili uweze kuendeleza kufanya mambo mema. Ni kama maelezo ya Kimaandiko kuhusu mafanikio. Mafanikio ni nini? Je ni kuwa na nyumba nzuri, gari zuri, nguo nzuri, na chakula mezani kwako? Kutegemeana na maandiko haya, Ni kuwa na kiwango cha kutosha kutimiza mahitaji yako yote na kuendeleza matendo mema. Kama unashindwa kutoa vitu ambavyo unahisi Mungu anagusa moyo wako kufanya hivyo, Kama unataka kuwa baraka kwa mwingine na unashindwa, basi wewe haujafanikiwa kifedha kutegemeana na maandiko yanavyosema. Mungu anasema atakubariki kwa kiwango ambacho mahitaji yako yote yatatimizwa, na utaweza kuendeleza kufanya mambo mema.

Mafanikio ya kweli ya kibibkia si tu kutimiza mahitaji yako, bali bali ili uwe Baraka kwa wengine. Mtu ambaye anajifikiria yeye mwenyewe inamaana yeye ni mbinafsi. Kama mtu akisema "Namwamini Mungu kwa ajili ya zaidi," wengine wanaweza kuwaona wabinafsi au

waroho, bali inategemeana na msukumo. Kama ukimwomba Mungu akupe mali zaidi ili uwe na nyumba bora au gari bora, huo si mtazamo wa kimaandiko. Bali kama unamwamini Mungu kwa ziada kwa sababu unaona zaidi ya mahitaji yako na unataka kuwa Baraka kwa wengine, huu ni mtazamo ambao Mungu anataka tuwe nao. Anataka ufanikiwe. Ni nia yake kwa wewe kufanikiwa.

Mathayo 6 inaongelea kuhusu mambo tunayohitaji na halafu inasema kama tukitafuta ufalme wa Mungu na haki yake, mambo mengine yote mtazidishiwa. Wakati unapoanza kumuweka Mungu kwanza, atatimiza haya mengine yote. Mahitaji yako yote,na wewe utakuwa Baraka kwa watu wengine. Mungu anataka ufanikiwe, bali inategemeana na msukumo na matendo yako katika hili eneo.

Ni maombi yangu kwamba haya yamewatia chngamoto na kwamba leo utaanza kumuamini Mungu kwa ajili ya ubora zaidi, ambao ni wa kufanikiwa.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma 2 Wakorintho 8:7-8 Wakati unapowapa wengine walio katika uhitaji, hii ndiyo njia moja ambayo unaweza kuthibitisha? ________________________

2. Soma 2 Wakorintho 8:13-14 Wakati wote tumeunganika na kuwa watoaji, Mungu anataka kuwe na aina ya nini? ________________________

3. Soma 2 Wakorintho 8:13-14. mahitaji ya kila mtu yatatimizwaje? ________________________

4. Soma Waefeso 4:28. Mtu ambaye amekuwa mwizi asiibe tena, bali aanze kufanya kazi na waendeshe maisha yao wenyewe. Waefeso 4:28 inasemaje, pia anasema wafanye nini? ________________________

5. Soma Mwanzo 13:2 na 12:2. Mungu alimwamini Abraham na utajiri kwa sababu Abraham alikuwa hajifikirii mwenyewe bali alikuwa ________________________ kwa wengine.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### 2 Wakorintho 8:7-8 (Tafsiri ya New Living)

"[7] Lakini kama mlivyo na wingi wa mambo yote; imani, na usemi, na elimu, na bidii yote, na upendo wenu kwetu sisi; basi vivyo hivyo mpate wingi wa neema hii pia. [8] Sisemi kuwa ni lazim amfanye, Ingawa makanisa mengin eyana shauku ya kufanya. Hii ni moja wapo ya njia ya kuthibitisha ya kuwa upendo wenu ni halisi."

### 2 Wakorintho 8:13-14 (Tafsiri ya New Living)

"[13] Sisemi kuwa mtoe sana kiasi kuwa ninyi mtateseka kwa kuwa na kidogo sana,. Nina maanisha tu kuwa kunatakiwa kuwa na usawa. [14] Kwa sasa mna vya kutosha na mnaweza kuwasaidia. Na kwa wakati mwengine wanaweza kuhirikiana nanyi pale mtakapokuwa na uhitaji. Kwa jinsi hii, mahitaji ya kila moja yatapatikana."

### Waefeso 4:28

"Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji.."

### Mwanzo 13:2

"Naye Abramu alikuwa ni tajiri sana kwa mifugo, kwa fedha, na kwa dhahab."

### Mwanzo 12:2

"Nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka; 3 nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

6. Soma 1 Timotheo 6:17-18 Mambo gani matatu matajiri hufanya na hela zao? ____ ________________________________ ____________

7. Je Mungu anaweza akakuamini na fedha

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

1 Timotheo 6:17-18 (Tafsiri ya New Living) –

"[17] Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune, wala wasiutumainie utajiri usio yakini, bali wamtumaini Mungu atupaye vitu vyote kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha [18] Watende mema, wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo

# MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma 2 Wakorintho 8:7-8 *(Tafsiri ya New Living)*. Unapowapa wengine waliyo katika uhitaji, hii ndiyo moja ya njia ambayo kwayo unaweza kuthibitisha? **Ya kuwa upendo wako ni wa kweli.**

2. Soma 2 Wakorintho 8:13-14 *(Tafsiri ya New Living)*. Wakati sisi wote tukiungana pamoja kutoa, Mungu anataka kuwe na nini? **Usawa, kila mtu na atoe kile awezacho.**

3. Soma 2 Wakorintho 8:13-14 *(Tafsiri ya New Living)*. Mahitaji ya kila mtu yatapatikanaje? **Kwa kutoa kile unachoweza, pale unapoweza.**

4. Soma Waefeso 4:28. Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji. Waefeso 4:28 pia inasema wanapaswa kufanya nini? **Wawape masikini, wale waliyo na uhitaji.**

5. Soma Mwanzo 13:2 na 12:2. Mungu angeweza kumwamini Abrahamu kwa kumpa utajiri kwa sababu Abrahamu hakuwa tu akijifikiria mwenyewe bali alikuwa ni **baraka** kwa wengine.

6. Soma 1 Timotheo 6:17-18 (Tafsiri ya New Living). Ni mambo gani matatu tajiri anapaswa kuyafanya na fedha? **Atende Mema, atoe kwa ukarimu kwa wale wenye uhitaji, Ashirikishe na wengine kile ambacho Munguamewapa.**

7. Je Mungu anaweza kukuamini wewe na fedha?

DARAJA 2

# SOMO 15
# FEDHA (Sehemu 2)

*Na Andrew Wommack*

Leo niantaka kukushirikisha zaidi kuhusu fedha. Katika kipindi kilichopita, Nilielezea kuwa ni mapenzi ya Mungu kwako wewe kufanikiwa. Sasa nina taka kukupa baadhi ya funguo kuhusu jinsi hilo linavyo fanya kazi.

Luka 6:38 inasema, "*Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa.*" Kuna kanuni nyingi zinazohusika, lakini huwezi kuzungumza kuhusu mafanikio pasipo kuzungumza kuhusu kutoa.

Unapozungumza kuhusu mafanikio ya kifedha, watu wengi sana husema, "Sawa, Hivyo Mungu anataka kunifanikisha, lakini sina ili niweze kutoa." Unaweza kuona kwenye Biblia pale ambapo Yesu alizungumza kuhusu mjane aliyeweka sarafu zake mbili za mwisho kwenye sadaka. Alikuwa aki waangalia matajiri wanaweka kiwango kikubwa cha fedha, nab ado akawaida wanafunzi wake pamoja na kusema mwanamke huyu ametoa fedha nyingi kuliko wale wote. Alisema hivi kwa kuwa walitoa kutokana na utele waliyokuwa nao. Lakini mwanmke yule alitoa kutoka kwenye umasikini wake. Mungu hapimi ukubwa wa zawadi yako kwa thamani yake ya kifedha bali kwa asilimia ya kile ambacho ulitakiwa kukitoa. Mtu anaposema "SIna kitu chochote cha kutoa," Si kweli. Ikiwa kama hakuna kingine, unaweza kuchukua kipande cha nguo ulichonaycho na ukitoe. Kila mtu ana kitu cha kutoa, hivyo achana na malumbano haya ya kuwa huna chochote cha kutoa. Ukweli ni kuwa, wakati unapoonekana kuwa na kidogo katika kila kitu ndipo pale ambapo utoaji wako unaweza kuwa asilimia kubwa kuliko wakati mwengine wowote ule. Mtu ambaye ana dola kumi na anatoa tano ametoa zawadi kubwa sana kuliko yule anayetoa dola millioni moja wakati wakiwa na mabilioni na mabilioni yamebaki. Mungu huiweka kiasi kuwa kila mtu anaweza kutoa.

Ni kwa nini Mungu alituambia tutoe? Kuna mambo memngi yanayohusika, lakini moja ya madhumuni yamsingi ni kuwa Mungu anakutaka wewe umtumaini Yeye katika kila eneo la maisha yako. Ikiwa kama hakuna Mungu, na ikiwa kama Neno Lake si kweli pale anaposema "Toeni, nanyi mtapewa," chukua sehemu ya kile ulicho nacho na kukitoa ni kitu cha kijinga sana

ambacho unaweza kukifanya. Badala ya kuelekea kwenye lengo la mahitaji yako yote kijibiwa, ukweli ni kuwa unakwenda mbali na hilo ikiwa kama Mungu hajakuahidi kukubariki. Inahitaji Imani kuweza kutoa jinsi ambavyo Mungu anasema, na hiyo ndiyo sababu Alikuambia ufanye.

Katika Luka 16 kuna mfano kuhusu wakili aliyemdanganya bwana wake, na hatimaye inaishia hapa: Anasema kama hujawa mwaminifu katika mali ya udhalimu (akiongea kuhusu fedha), ni nani atakayewapa amana mali ya kweli? Ikiwa kama hujamwamini Mungu katika mambo madogo, kuhusu fedha, unawezaje kuyafikia mambo yaliyo ya muhimu zaidi, kama vile maadili ya kiroho? Andiko kama hili linaifanya fedha kuwa ni moja ya daraja la chini sana la uwakili. Ikiwa kama hutaweza kumtumaini Mungu na fedha zako, unawezaje kumtumaini Yeye na mustakabali wako wa milele? Unawezaje kwa uhakika ukamwamini Yesu kuwa amekusamehe dhambi zako nay a kuwa unakwenda kuishi milele mbinguni? Katika kufananisha, mambo ya kiroho yalikuwa kuwa tunaweka Imani yetu katika Bwana kwa kuwa hilo linaonekana na kuwa na maana zaidi kuliko fedha. Fedha ni jambo dogo, Lakini ndiyo mstari wa chini wa kuanza kumtumaini Mungu.

Methali 11:24 inasema kuna baadhi ambao wanatoa zaidi ya vile ambavyo inaonekana ni lazima, na bado wanafanikiwa, na kuna wengine ambao huzuia kile walicho nacho, na inasababisha tu umasikini ndani mwao.

Ikiwa kama utautafuta ufalme wa kwanza Mungu na Haki yake, Basi atakuongezea vitu hivi. Ikiwa kama unasema kuwa unataka Mungu akusaidie kwenye fedha zako, na unaomba ili upate msaada Wake – lakini huutafuti kwanza ufalme wa Mungu, na wala huchukui hatua ya Imani, ukimtumaini Yeye na fedha zako, na kutoa – basi hakika wewe humtumainii Yeye.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Yohana 3:16. Nini kili msukuma Mungu kutoa?
___________________________

2. Soma 1 Wakorintho 13:3. Nini linapaswa kuwa lengo la kutoa kwetu? ___________
______________________________
____________________

3. Soma Yakobo 2:15-16. Elezea maana ya mstari huu. _____________________
______________________________
__________

4. Soma Luka 6:38 *(Tafsiri ya New Living)*. Mstari huu unasema nini kwako? _______
______________________________
________________________

5. Soma Waefeso 1:7. Je Mungu alitoa kutoka kwenye utajiri Wake au alitoa kufuatana na utajiri Wake? Elezea tofauti iliyopo. _____
______________________________
__________

6. Soma Methali 19:17. Unapowapa masikini, ni nini unachokifanya?
_______________________
e Mungu atakulipa?
___________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Yohana 3:16

"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.."

### 1 Wakorintho 13:3

"Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo, hainifaidii kitu.."

### Yakobo 2:15-16

"[15] Ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki,[ 16 ]na mtu wa kwenu akawaambia, Enendeni zenu kwa amani, mkaote moto na kushiba, lakini asiwape mahitaji ya mwili, yafaa nini?

### Luka 6:38
### (Tafsiri ya New Living Translation)

"Ukitoa, utapokea. zawadi yako itarudi kwako katika kipimo kilicho jaa, na kushindiliwa, kusukwa sukwa ili kutengeneza nafasi kwa ajili ya zaidi, na kufurika. Kipimo chochote utakachotumia katika kutoa – kikubwa au kidogo – kitatumika kupima kile ambacho utarudishiwa."

### Waefeso 1:7

"Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake"

### Methali 19:17

"Amhurumiaye maskini humkopesha Bwana; Naye atamlipa kwa tendo lake jema."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

7. Soma Zaburi 41:1-3 *(Tafsiri ya New Living)*. Taja vitu vitano ambavyo Mungu huvifanya kwa wale wanaowapa masikini.

______________________________________
______________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

Zaburi 41:1-3
(Tafsiri ya New Living)

"[1] Eh, furaha ya wale waliyo wakarimu kwa masikini. Bwana atawaokoa siku za taabu. [2] Bwana atawalinda na kuwahifadhi hai. Anawapa mafanikio na kuwakomboa na maadui zao. [3] Bwana atawategemezawanapokuwa wagonjwa na kuyaondoa maumivu yao na kukosa utulivu kwao."

# MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Yohana 3:16. Nini kili msukuma Mungu kutoa? **Upendo Wake.**
2. Soma 1 Wakorintho 13:3. Nini linapaswa kuwa lengo la kutoa kwetu? **Upendo; yaani., kutafuta ustawi na faida ya wengine bila kujali tunavyojisikia (Mathew. 7:12).**
3. Soma Yakobo 2:15-16. Elezea maana ya mstari huu. **Asilimia tisini na tano ya upendo wote hauko katika maneno. Hauko katika kile tunachokisema bali katika vitu tunavyovifanya.**
4. Soma Luka 6:38 *(Tafsiri ya New Living)*. Mstari huu unasema nini kwako? **Kipimo chochote utakachotumia katika kutoa (kikubwa au kidogo), kitatumika kupima kile ambacho utarejeshewa.**
5. Soma Waefeso 1:7. Je Mungu alitoa kutoka kwenye utajiri Wake au alitoa kufuatana na utajiri Wake? **Elezea tofauti iliyopo. Kufuatana na utajiri Wake. Alitoa kila kitu kutukomboa sisi, Mwana wake wa pekee.**
6. Soma Methali 19:17. Unapowapa masikini, ni nini unachokifanya? Unamkopesha Bwana. Je Mungu atakulipa? **Ndiyo.**
7. Soma Zaburi 41:1-3 *(Tafsiri ya New Living).* Taja vitu vitano ambavyo Mungu huvifanya kwa wale wanaowapa masikini. **Huwakomboa wakati wa shida. Huwalinda. Huwapa mafanikio. Huwakomboa na maadui. Huwaponya; yaani; huwarejeshea afya zao.**

DARAJA 2

# SOMO 16

# NINI CHA KUFANYA INAPOONEKANA MAOMBI YAKO HAYA JAJIBIWA

*Na Andrew Wommack*

Leo nataka nishirikiane nawe kuhusus nini cha kufanya pale inapoonekana maombi yako hayajajibiwa, nitaka kuweka msisitizo kwenye ukweli kuwa maombi yako "yanaonekana" kwamba hayajajibiwa. Ukweli ni kwamba Mungu mara zote, mara zote huwa anajibu maombi yoyote ambayo watu huomba sawa sawa na Neno Lake katika imani. Katika 1 Yohana 5:14-15 inasema, *"Na huu ndio ujasiri tulonao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na na mapenzi Yake atatusikia: na kama tukijua kwamba atatusikia, tuombacho chochote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba."* Huu ni ujasiri mkubwa sana. Mungu mara zote hujibu maombi, lakini huwa haionekani kana kwamba yamejibiwa. Mathayo 7:7-8 inasema, *"Ombeni nanyi mtapewa, tafuteni nanyi mtaona, bisheni nanyi mtafunguliwa, kwa maana kila aombaye hupokea naye atafutaye huona naye abishaye hufunguliwa."* Mistari hii inasema kwamba Mungu huwa anajibu maombi. Bado kila mmoja wetu anaweza kufikiria wakati katika maisha yetu tulipoomba kwa ajili ya kitu ambacho tuliamini kuwa kilikuwa ni kitu sahihi, kitu chema, na wala hakikuwa cha kibinafsi kabisa au nje ya mapenzi ya Mungu, lakini bado hatukuona majibu.

Neno la Mungu linatuambia tuombe na tutapewa; lakiniuzoefu wetu unasema tumeomba na wala hatukupewa. Kipi ni kweli? Jibu linaweza kukushangaza, lakini ukweli ni kuwa yote ni sahihi. *Watu wengi hufikiri, Sasa, subiri kidogo, Neno la Mungu linasema Mungu atatujibu, na sijaona hili likitokea.* Yohana 4:24 inaema, *"Mungu ni Roho: na wale wamuabuduo wamuabudu katika roho na kweli"* Mungu hufanya kazi katika ulimwengu wa kiroho katika kutujibu maombi yetu, lakini inahitaji imani kwa upande wetu ili iweze kudhihirika. Imani ndio inayochukua vitu kutoka katika ulimwengu wa roho na kuvileta katika ulimwengu wa kimwili. Hiki ndicho kimsingi Waebrania 11:1 inasema, "Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyo onekana." Haikusema kuwa imani ni bayana ya vitu ambavyo havipo. Vipo, lakini haviko katika ulimwengu unoonekana kimwili lakini

katika ule ulimwengu war oho usioonekana. Imani hufikia kwenye ulimwengu war oho na kuvivuta vitu hivyo kwenye ulimwengu wa mwili.

Ni kama mawimbi ya radio. Radio na vituo vya televisheni, vinatangaza wakati wote, unaweza kuwa kwenye chumba ambapo huwezi kuona au kusikia mawimbi ya sauti, lakini hilo halimaanishi ya kuwa hayapo. Unatakiwa kuiwasha radio na kutafuta masafa unayo taka kuyasikia. Na halafu radio itavuta mawimbi hayo kutoka kwenye sehemu usioijua na kuyatangaza kwenye ulimwengu ambapo unaweza kuyasikia kwa masikio yako ya kibinadamu. Mungu hujibu maombi yetu katika mfumo huo huo: Hutoa vitu katika ulimwengu wa kiroho, na kwa imani, unatakiwa kufikia na kuyaleta kwenye ulimwengu wa kimwili. Ulimwengu wa kimwili na kiroho hutembea sambamba pembeni ya kila mmoja. Mungu hutembea na hujibu maombi yako, lakini unawezakamwe usione iki jihidhihirisha katika ulimwengu wa mwili ni mpaka pale utakaporuhusu Imani iwe daraja la kuzibia mwanya kati ya ulimwengu wa Kiroho usioonekana na ulimwengu wa kimwili tunaouishi..

Kwa Mfano, Danieli, mtu wa Mungu, alikua akimwomba Mungu ampatie ufunuo.Kwa sababu ya muda nitaweka muhtasari wa habari hii. Bwana akamtuma malaika, Gabrieli, amtokee Danieli na kumjibu maombi yake, Danieli, 9:22-23 inasema, *"Akaniagiza, akaongea nami, akasema, Ee Danieli, nimetokea sasa, ili nikupe akili upate kufahamu.Mwanzo wa maombi yako ilitolewa amri, nami nimekuja kukupasha habari; maana wewe unapendwa sana; basi itafakari habari hii, na kuyafahamu maono haya."* Hapa ndipo penye kitu cha kuangalia:Gabrieli alisema kuwa mwanzoni mwa maombi ya Danieli, amri kutoka kwa Mungu ilikuja kwake ili kuleta majibu. Kama ukisoma ni muda gani ailichukua kuleta majibu, ilikua ni kama dakika tatu, dakika tatu za kusubiri kati ya amri ya Mungu na udhihirisho wa kimwili.

Mara nyingi sana tunakuwa na hali ya kusema inakuwaje kama Mungu kama kweli ni Mungu na kitu ni mapenzi Yake, hutokea tu kama kukutanisha vidole; lakini hilo si kweli. Kwa tukio hili, Mungu alitoa amri, na ilimchukua kwa kukadiria angalau dakika tatu kwa Gabrieli kuumaliza umbali. Sina sababu zote kwa hili, na hakikasi muhimu. Jambo ninalojaribu kulileta ni kuwa kutoka wakati Mungu alipotoa amri, kulikuwa na wakati wa kusubiri wa takriban dakika tatu kabla jibu halijadhihirishwa. Sasa kama huo ulikua ni muda mrefu mno tulitakiwa kuamini kwa ajili ya kupata jibu la maombi, wengi wetu inawezekana tungeweza kusubiri, Llakini si hivyo mara zote..

Katika Danieli 10 tunamkuta mtu huyo huyo akiomba maombi mengine, na wakati huu, ilimchukua wiki tatu kuweza kujibiwa maombi yake. Watu wengi wanaosoma hili wangesema, "Kwa nini Mungu alijibu moja ya maombi ya Danieli kwa dakika tatu na mombi mengine kwa wiki tatu?" Danieli 10:11-12 inasema, *"Akaniambia, Ee Danieli, mtu upendwaye sana, yafahamu maneno nikuambiayo, ukasimame kiwima-wima; maana kwako nimetumwa sasa. Na aliponiambia neno hili, nalisimama nikitetemeka.Ndipo akaniambia, Usiogope, Danieli;*

*kwa maana tangu siku ile ya kwanza ulipotia moyo wako ufahamu, na kujinyenyekeza mbele za Mungu wako, maneno yako yalisikiwa; nami nimekuja kwa ajili ya maneno yako..."* Hii ina onyesha kuwa Mungu alimwamuru mjumbe tangu siku ya kwanza kabisa ya maombi ya Danieli. Na ilichukua wiki tatu kwa jibu lile kudhihirika, lakini Mungu ni mwaminifu, Maandiko yanayosema Ni Yeye Yule jana, leo na hata milele (Waebrania.13:8).

Ukiweka mstari wa 9 na 10 kwa pamoja, naamini Mungu alijibu maombi yote papo hapo, moja lilichukua dakika tatu na jengine lilicukua wiki tatu. Lakini Mungu hakuwa ndiye anayewajibika kuchelewesha. Swala ni hili: Mungu hujibu maombi yetu. Hufanya mambo, lakini kuna mambo mengine mengi sana ambayo yanaweza kutokea kati ya muda atakaojibu maombi na wakati utakapoona majibu yamedhihirika,Unatakiwa kuamini; imani lazima ifike katika ulimwengu wa kiroho, na kuleta majibu katika ulimengu wa kimwili. Hivyo imani ndiyo kiungo kikuu.

Pia, unaweza kuona katika mstari wa 13 katika Danieli, sura ya 10, *"Lakini mkuu wa ufalme wa Uajemi alinipinga siku ishirini na moja; bali, tazama, huyo Mikaeli, mmoja wa hao wakuu wa mbele, akaja kunisaidia; nami nikamwacha huko pamoja na wafalme wa Uajemi..."* Hii haizungumzii mwanadamu wa kawaida bali kizuizi cha kipepo. Shetani ni kitu chengine kinachoweza kuzuia katika mchakato huo. Mara nyengine Mungu huyajibu maombi yetu, lakini Shetani huyazuia kwa kupitia watu wengine, Kwa mfano, kama unaamini kwa ajili ya kupata fedha. Mungu hatakwenda kukupa fedha, wala Hataghushi fedha za kimarekani au fedha yoyote ile ya ulimwengu huu. Hatakwenda kutengeneza fedha, na kuinyeesha kama mvua hapa chini kutoka mbinguni, na kuiweka ndani ya mfuko wako Luka 6:38 inasema, *"Wapeni watu vitu nanyi mtapewa kipimo cha kujaa na kushindiliwa na kusukwa sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani wenu, kwa kuwa kipimo kile kile umpimiacho ndicho utakachopimiwa."* Mungu atatembea na kuyajibu maombi yako, lakini jibu litakuja kwa kupitia watu. Baadhi ya watu wamefungwa na ulafi na wakiwa na hasira na wewe au unafanya vitu vya kuwakwaza, Shetani anaweza kuzuia udhihirisho wa maombi yako kwa kupitia wao. Unapoomba hasa kwa ajili ya fedha, unahitaji kutambua kuwa watu wengine wanaweza kuwa ni sehemu ya muujiza wako wa kifedha, na unatakiwa kuwaombea.

Mungu ni mwaminifu. Hajawahi kushindwa kujibu maombi yoyote ambayo yalikuwa kwenye msingi wa Neno lake na maombi ya imani. Mara zote hutofanya ujue kuwa Mungu mar azote hujibu maombi yako.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Mathayo 7:7-8. Tutegemee nini kutoka kwa Mungu tukiomba? ____________________

2. Soma Mathayo 7:7-8. Tukitafuta, tutarajie nini?____________________

3. Soma Mathayo 7:7-8. Nini tutarajie kitokee kama tutabisha? ____________________

4. Soma Yohana 10:35. Je Mungu atatoa kitu cha tofauti zaidi ya kile ambacho Neno lake limeahidi? ____________________

5. Soma Yakobo 4:1-3. Ni kwa nini watu hawa walizuiwa wasipokee kutoka kwa Mungu? ____________________

6. Soma 1 Petro 3:7. Ikiwa kama unamtendea vibaya mwenzako, nini yatakuwa matokeo katika maisha yako ya maombi? ____________________

7. Soma 1 Yohana 5:14-15. Ufungo wa maombi yako kujibiwa ni upi? ____________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Mathayo 7:7-8

"[7] Ombeni nanyi mtapewa, tafuteni nanyi mtaona, bisheni nanyi mtafunuliwa, [8] Kwa maana kila ambaye hupokea naye atafutaye huona na abishaye hufunguliwa."

### Yohana 10:35

"Ikiwa aliwaita miunu wale waliojiliwa na neno la Mungu na maandiko hayawezi kutanguka."

### Yakobo 4:1-3

"[1] Vita vyatoka wapi? Mapigano yaliyoko kati yenu yatoka wapi? Si humu katika tamaa zenu zifanyazo vita katika viungo vyenu. [2] Mwatamani, wala hamna kitu, mwaua na kuona wivu, wala hamwezi kupata mwafanya vita na kupigana, wala hamna kitu kwa kuwa hamwombi. [3] Hata mwaomba, wala hampati kwasababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tama zenu."

### Petro wa 1 3:7

"Kadhalika ninyi wanaume, kaeni na wake zetu kwa akili na kumpa mke heshima, kama chombo kischo na nguvu, na kama warithi pamoja na neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe."

### Yohana 1 5:14-15

"[14] Na huu ndio ujasiri tulionao kwake, ya kuwa tukiomba kitu sawa sawa na mmapenzi yake atatusikia. [15] Na kama tukijua kama atasikia tuombacho chochote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwoba."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

8. Soma Marko 11:24. Unapoomba, unapaswa kufanya nini? ________________
______________________________________
_________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

Marko 11:24 –

"Kwa sababu hiyo nawaambia, yo yote muombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakua yenu."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Mathayo 7:7-8. Tutegemee nini kutoka kwa Mungu tukiomba? **Tutarajie kupewa**

2. Soma Mathayo 7:7-8. Tukitafuta, tutarajie nini? **Kupata.**

3. Soma Mathayo 7:7-8. Nini tutarajie kitokee kama tutabisha? **Ya kuwa utafunguliwa**

4. Soma Yohana 10:35. Je Mungu atatoa kitu cha tofauti zaidi ya kile ambacho Neno lake limeahidi? **Hapana.**

5. Soma Yakobo 4:1-3. Ni kwa nini watu hawa walizuiwa wasipokee kutoka kwa Mungu? **Nia na mioyo yao haikuwa sahihi. KIla kitu kilikuwa kuhusu wao na kwa ajili yao. Ubinafsi ndiyo ulikuwa lengo lao.**

6. Soma 1 Petro 3:7. Ikiwa kama unamtendea vibaya mwenzako, nini yatakuwa matokeo katika maisha yako ya maombi? **Maombi yako yatazuiliwa.**

7. Soma 1 John 5:14-15. Ufungo wa maombi yako kujibiwa ni upi? **Kuomba sawa sawa na mapenzi Yake.**

8. Soma Mark 11:24. Unapoomba, unapaswa kufanya nini? **Amini ya kuwa unapokea, na itakuwa yako.**

# KOZI YA UINJILISTI YA UANAFUNZI WA YESU

# DARAJA 3

Ruhusa imetolewa kutoa nakala au kuchapisha kwa ajili ya madhumuni ya kufundisha wanafunzi wa Yesu katika sharti kuwa kitasambazwa bure bila gharama.

DARAJA 3

# SOMO 1
# MTIRIRIKO WA KIUNGU

*Na Andrew Wommack*

Nataka nikushirikishe baadhi ya vitu kuhusu jinsi unavyoweza kumruhusu Mungu atiririke kupitia wewe ili kuwahudumia watu wengine, unayo nguvu na upako wa Mungu ndani yako, lakini unawezaje kuvitoa ndani mwako kwenda kwa watu wengine? Kuna maandiko kadhaa tunayoweza kuanza nayo. Katika Filemoni 6 Paulo anaomba *"Ili kwamba ushirika wa imani yako ufanye kazi yake, katika ujuzi wa kila kitu chema kilicho kwetu, katika Kristo."* Hatua ya kwanza katika kuwa na nguvu za Mungu kutiririka ndani yako kwenda kwa wengine ni kuwa kwanza tambua mambo mazuri yaliyomo ndani yako. Huwezi kutoa kitu usicho nacho, lakini mara unapofahamu ni nini ulichonacho ndani yako, vitu vitaanza kutokea venyewe, utaanza kushirikisha wengine msisimko uliyo nao ndani yako, utaanza kutoa ushuhuda wa mambo ambayo Mungu ameyafanya katika maisha yako, na watu wengine wataweza kusaidika kwa urahisi zaidi.

Katika 1 Yohana 4:7-8 inasema, *"Wapenzi, na mpendane; kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu, na kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu... kwa maana Mungu ni upendo."* Kila wakati unaposikia upendo unamiminika ndani yako kwa ajili ya mtu mwingine, huyo ni Mungu anamiminika ndani yako kupitia wewe kwenda kwa wengine, kuna maneno manne makuu kwa ajili ya "upendo" kwa lugha ya Kiyunani, Ule wa juu zaidi ni upendo wa, agape, ni upendo wa kiungu. Unahitaji kutambua utofauti kati ya kuvutiwa na kutamani, kwenda kwa mtu mwingine na uweza huu wa kiungu, aina ya juu sana ya upendo wa Mungu, wakati wowote utakapogundua upendo wa Mungu ukitiririka kutoka ndani yako kwenda kwa mwengine, siyo kwa ajili yako. Unaweza kuthibitisha hili kwa kuangalia kwenye 1 Wakorintho 13:4 -8, ambayo inatoa sifa za aina ya upendo wa Mungu. Huvumilia, hufadhili, upendo uhusudu, upendo hautakabari, haujivuni,n.k. Unahitaji kutathmini kile unachokiita upendo na uhakikishe hakika ni upendo wa Mungu – ambao hautaki mambo yake wenyewe au kujitumikia wenyewe – Ya kuwa humpendi mtu kwa sababu ya kile anachoweza kukufanyia. Unapoendelea kukua katika huu na kuanza kutambua aina Yake ya upendo, na unaposikia unamiminika ndani yako kwa ajili ya mtu mwingine huyo ni Mungu anatembea ndani yako,

na unaposikia hivyo unachotakiwa kukifanya ni kuufuata kwa neno la kutia moyo au kitendo - fanya kitu.

Kuna muda ambao nimekuwa nikiomba kwamba mtu atakuja kwenye akili yangu, na niwe na upendo wa kiungu na huruma juu yao. Hakukua na sababu yoyote kwa hili kutokea, ilikuwa ni ya uwezo wa kiungu, nimejifunza kumpigia simu mtu, kuwaandikia barua au kuwasiliana wakati mwingine, na kila wakati mtu yule atasema, huyo ni Mungu alikuwa anazungumza na mimi kupitia wewe, na ameyagusa maisha yangu kupitia hili." Unajua hilo limetokeaje? Limetokea kwa sababu nilihisi upendo huu, huruma hii ya Kimungu ndani yangu, upendo huu wa kiungu unaotoka ndani yangu kwa ajili ya yule mtu. Ninaposikia hivyo sasa nina tambua kuwa si mimi - ni Mungu. Mungu ni upendo, na ninapo wapenda watu wengine ni Yeye anawapenda watu, ana wapenda watu wengine kupitia mimi. Hivi ndivyo Yesu alivyohudumu Mathayo 14:14 inasema *"Yesu akatoka, akaona mkutano mkuu, akawahurumia, akawaponya wagonjwa wao."* Jinsi ambavyo nguvu ya Mungu ilijidhihirisha kupitia Yesu ilikuwa ni kupitia huruma na upendo aliyousikia kwa watu aliyowahudumia. Katika Mathayo. 8:2-3 mtu mwenye ukoma ambaye alikuwa ni najisi na hakuweza kushikwa sawa sawa na sheria za Kiyahudi (hakuna aliyeweza kuwasiliana naye, au nao wangeambukizwa na wangenajisika) alipaza sauti yake na kumuita Yesu tokea mbali, *"Na tazama, akaja mtu mwenye ukoma akamsujudia, akisema, Bwana, ukitaka, waweza kunitakasa. Yesu akanyosha mkono, akamgusa, akisema Nataka; takasika. Na mara ukoma wake ukatakasika."* Alijawa na huruma kwa ajili ya mtu yule mwenye ukoma na kumshika, ukiwa unajifunza maandiko utaiona huruma, upendo huu wa kimungu katika maeneo mengi, si hisia tu, lakini huruma inyomiminika ndani yetu.

Yesu alipokua pale msalabani, Aliwapenda watu waliomzunguka sana kiasi kwamba alisema, *"Baba, wasamehe kwa maana hawajui walitendalo"* (Luka 23:34). Hawa watu waliokuwa ndiyo watu wale wale walio kuwa wakimsulubisha lakini bado Aliwahurumia na kumuomba Mungu aweze kuwasamehe. Tunajua hakuwa na msisimko wa mwili - haikuwa tu ni hisia - ilikuwa ni maamuzi. Hata hivyo, aliusikia ndani yake na akaachilia juu ya watu wengine. Kila mmoja wenu ambaye amezaliwa mara ya pili anaye Mungu anayeishi ndani yake. Kufuatana na mstari tuliyoanza nao 1Yohana 4:8, Mungu ni upendo, na anataka amiminike kwa kupitia kwako kuwafikia watu wengine. Ili afanye hivyo, ataachilia huruma hii, na utaisikia ikimiminika kutoka ndani yako kwenda kwa watu wengine, na utakavyofanya hivyo unahitaji kuitikia.

Si lazima mara zote ufanye jambo ambalo ni la kipekee. Si lazima iwe, "Asema Bwana" Mara nyengine, ikiwa kama una hisia za huruma kwa mtu fulani wakati mwingine unapowahurumia wengine nenda pale walipo wakumbatie na kuwaambia Mungu anawapenda na mimi pia, Ninajua wakati fulani hili lili fanya kazi nilipokuwa na uhitaji wa namna hiyo, katika hali ambapo karibu ilikuwa nifukuzwe kanisani, watu walisema uongo kuhusu mimi,

na hata mtu mmoja alitishia kuniua. Nilijisikia kukatishwa tamaa sana kama vile "Mungu, ina maana gani sasa? Hakuna hata anayefurahia kile ambacho nina jaribu kukifanya." Nilikuwa niki pambana na Shetani katika hili, na rafiki akanipigia simu kutoka mbali sana. Akaongea kwa dakika chache, na nikasema, "Vyema, umenipigia simu kwa sababu gani?" Akasema, "Nilitaka tu kupiga simu ili nikujulishe kuwa nina kupenda. Nilikuwa nina omba na nikahisi upendo wa Mungu kwako. Ninakufurahia." Ndiyo yote aliyoyasema. Hakujua chochote kuhusus hali iliyokuwa ikiendelea maishanimwangu, lakini Mungu alilitumia hilo. Nilijua ilikuwa ni Yeye akinipenda kupitia mtu yule, na hilo lika niweka katika huduma na ikabadilisha maisha yangu.

Si lazima liwe ni neno kubwa sana. Mungu ni upendo, na wakati wowote unapohisi upendo huo ukitiririka ndani yako, ni miminiko wa kiungu, maisha ya kiungu… uzima mtakatifu wa Mungu. Unapohisi hivyo, unahitaji kulifuatilia. Nenda kafanye kitu, sema kitu, uwe baraka kwa mtu fulani, Mungu ataweka maneno ndani ya kinywa chako. Atakutumia, na Atawaweka watu huru, unapoguswa na huruma na kuwahudumia wale wanaokuzunguuka.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

Angalizo: Katika Somo hili, tutaangalia kwa undani jinsi ya kukiruhusu kile ambacho Mungu amekiweka ndani yetu kitiririke kwenda kwa wengine.

1. Soma Filemoni 6. Ipi ni hatua ya kwanza katika kumruhusu Mungu atiririke nje yetu kwenda kwa wengine? ____________________________________________

2. Soma 1 Yohana 4:7-8. Nini ni chanzo halisi cha kuwapenda wengine? ____________________________________________

3. Andrea anasema, “Wakati wowote unapohisi upendo unamiminika kutoka kwako, huyo ni Mungu anajidhihirishia upendo wake ndani yako.” Ni kauli gani katika Yohana 1 4:7 inathibitisha ukweli hu? ____________________________________________

4. Soma 1 Wakorintho 13:4-8. Zipi ni baadhi ya tabia za upendo wa Mungu? ____________________________________________

5. Soma Mathayo 14:14. Yesu aliguswaje kwa kuwatumikia wengine? ____________________________________________

### Philemon 6

“ili kwamba ushirika wa imani yako ufanye kazi yake, katika ujuzi wa kila kitu chema kilicho kwetu, katika Kristo Yesu.”

### 1 Yohana 4:7-8

“[7] Wapenzi, na mpendane; kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu, na kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu. [8] Yeye asiyependa, hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni upendo”

### 1 Yohana 4:7

“Wapenzi, na mpendane; kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu, na kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu.”

### 1 Wakorintho 13:4-8

“[4] Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni;[5] haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya;[6] haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli;[7] huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote; hustahimili yote. [8] Upendo haupungui neno wakati wo wote; bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika..”

### Mathayo 14:14

“Yesu akatoka, akaona mkutano mkuu, akawahurumia, akawaponya wagonjwa wao..”

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

6. Soma Mathayo 25:37-40. Tunapowafikia wengine katika upendo na huruma, katika uhalisia ni ni nani tunayempenda na kumjali? ______________________________ _________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Mathayo 25:37-40

"[37] Ndipo wenye haki watakapomjibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona una njaa, tukakulisha, au una kiu tukakunywesha? [38] Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha, au u uchi, tukakuvika?[39] Ni lini tena tulipokuona u mgonjwa, au kifungoni, tukakujia?[40] Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi"

### Waebrania 6:10

### (Tafsiri ya New International Version)

"Maana Mungu si dhalimu hata aisahau kazi yenu, na pendo lile mlilolidhihirisha kwa jina lake, kwa kuwa mmewahudumia watakatifu, na hata hivi sasa mngali mkiwahudumia."

# MWONGOZO WA MAJIBU

Angalizo: Katika Somo hili, tutaangalia kwa undani jinsi ya kukiruhusu kile ambacho Mungu amekiweka ndani yetu kitiririke kwenda kwa wengine.

1. Soma Filemoni 6. Ipi ni hatua ya kwanza katika kumruhusu Mungu atiririke nje yetu kwenda kwa wengine? Kutambua kila kitu chema alichokiweka ndani yetu katika Kristo Yesu.

2. Soma yohana 1 4:7-8. Nini ni chanzo halisi cha kuwapenda wengine? Mungu, kwa kuwa Mungu ni Upendo (Yohana 1 4:8).

3. Andrea anasema "Wakati wowote unapohisi upendo unamiminika kutoka kwako, huyo ni Mungu anajidhihirishia upendo wake ndani yako." Ni kauli gani katika Yohana 1 4:7 inathibitisha ukweli huu? "Upendo ni wa Mungu" (Yeye ndiye chanzo).

4. Soma 1 Wakorintho 13:4-8. Zipi ni baadhi ya tabia za upendo wa Mungu?

   Upendo huvumilia na huvumilia,Iko katika tungo ya wakati uliyopo, ikimaanisha ya kuwa upendo haukomi kufanya hivyo
   Upendo hufadhili, unajionyesha wenyewe katika matendo yenye kufadhili. Iko katika tungo ya wakati uliyopo, ikimaanisha ya kuwa upendo haukomi kufanya hivyo
   Hauhusudu. Haukatai baahati nzuri au mafanikio ya wengine.
   Upendo hautakabari, haujisifii, au kujipigia kelele, kuhusus mtu, hauna majivuno
   Haujivuni. Haujajawa na ubinafsi, hauna kiburi, au jeuri
   Haukosi kuwa na adabu. Hauendi kinyume na kile kilicho sahihi. Hauna kiburi
   Hautafuti mambo yake kuwa na Adabu, hautafuti mambo yake, hauoni uchungu,hauhesabu mabaya, Hauangalii mambo yake wenye
   Hauoni Uchungu. Haukasirishwi kwa haraka, au wenye kukasirika haraka
   Hauhesabu mabaya. Mara zote haufikirii vibaya kuhusus wengine
   Haufurahii udhalimu. Haufurahii pasipo na haki, au kile ambacho si sahihi
   Upendo hufurahia pamoja na kweli.
   Huvumilia mambo yote. Mara zote husaidia, kamwe haukati tamaa
   Huamini yote. Upendo mar azote hutumaini
   Upendo haupungui neno wakati wote. Mara zote huhifadhi, huendelea kwenda mpaka mwisho na hudumu milele.

5. Soma Matahayo 14:14. Yesu aliguswaje kwa kuwatumikia wengine? Aliguswa na huruma kwa ajili ya wengine. Kamusi inaelezea "huruma" kama "hisia ya huruma; kuonea huruma, rehema".

6. Soma Mathayo 25:37-40. Tunapowafikia wengine katika upendo na huruma, katika uhalisia ni ni nani tunayempenda na kumjali?.Yesu Mwenyewe. Angalia Waebrania 6:10.

DARAJA 3

# SOMO 2
# KUTUMIA KARAMA KUHUDUMU

*Na Andrew Wommack*

Leo tunataka kuzungumzia kuhusus ni jinsi gani unavyoweza kutumia upendo wa Mungu ulionao na ukawashirikisha na wengine upendo huo – jinsi gani unavyoweza kuwa mtumishi mzuri kwa wengine katika 1 Petro 4:11 inasema, *"Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu; mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu."* Neno "mausia ya Mungu" linatoka kwenye Agano la Kale walipokuwa na patakatifu pa patakatifu na kuliweka Neno la Mungu kwenye Sanduku la Agano. Ndicho kilichokuwa kikiitwa "mausia", hivyo inaposema "sema kama mausia ya Mungu," ina maanisha sema kama unayemwakilisha Mungu. Hivyo sema kama vile uasema kutoka kwa Mungu. Inaendelea kusema kwamba, *"Mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu: ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo. Utukufu na uweza una yeye hata milele na milele."* Inachokisema ni kuwa unahitaji kuhududmu kwa wengine, si kutokana na uwezo wako mwenyewe, bali kutoka katika uwezo akupao Mungu.

Moja kati ya vitu vizuri kuhusu Maisha ya Ukristo ni kuwa si tu mimi au wewe kuzungumza na mtu mwengine na kuwashirikisha mambo kutoka kwenye uwezo wetu wenyewe, bali Mungu mwenyewe hushuka na kuishi ndani yetu. Na Anaanza kuzungumza kupitia sisi na kujidhihirisha kupitia sisi. Tunaweza kuwa tunatawaliwa na Mungu na kuwa na Roho wa Mungu akiwa anajidhihirisha ndani yetu. Tunapoanza kukizungumza na watu wengine, tunahitaji kukumbuka ya kuwa hiki ndicho kiitwacho karama ya Roho Mtakatifu na ndiyo kazi yake. Mungu humchukua kila mtu katika mwili wa Kristo na huwapa karama mahususi. Katika 1 Wakorintho, 12 inasema kwamba kila mmoja wetu amepewa karama tofauti sawa sawa na mapenzi ya Mungu, katika mistari ya 4 – 6 inasema *"Basi pana utofauti wa karama, bali roho ni yeye yule, tena pana tofauti za huduma, bali bwana ni yeye yule kasha kuna utofauti wa kutenda kazi bali Mungu ni yeye yule azitendae kazi katika wote, hii inamanisha kwamba Mungu hufanya kazi pamoja nasi katika kila tulifanyalo*". Hii ina maanisha Mungu huyafanya mambo haya yote kwetu sisi sote, kama mstari wa 7 unavyosema "*Lakini kila mmoja kupewa ufunuo wa roho kwa kufaidiana*". Au kumfaidisha kila moja.

Mistari hii inasema Mungu ameweka nguvu na uweza wake ndani ya kila mmoja wetu. Unaweza usiuhisi, unaweza usijue, lakini hii ni ahadi ya Neno la Mungu. Ikiwa kama umefika umbali huu katika masomo haya ya Uinjilisti wa Kiuanafunzi, ikiwa kama hakika umemfanya Yesu kuwa Bwana na mwokozi wa maisha yako, Ikiwa kama umejifunza jinsi ya kupokea kutoka kwa Mungu na kuyatenda hayo katika maisha yako, basi ninaweza kukuhakikishia kwamba nguvu ya Roho Mtakatifu ipo inafanya kazi ndani yako. Unayo miujiza ya watu wengine ndani yako. Mungu ameweka aina ya mbegu ya muujiza ndani yako kwa ajili ya mtu mwengine. Ni juu yako wewe kuweza kuuachilia muujiza huo na kuufikisha maishani mwao. Maandiko yanasema kila mmoja wetu amepewa hili na Roho. Hakuna hata mtu mmoja ambaye ameachwa nje, karama tisa tofauti za Roho zimeorodheshwa katika kitabu cha 1Wakorintho 12, kama vile neno la hekima, neno la maarifa, kupambanua roho, matendo ya miujiza, karama ya uponyaji n.k. Kuna karama nyingine zimeorozeshwa katika Warumi 12, ambazo sina muda wa kushughulika nazo. Unahitaji kujifunza wewe mwenyewe na kufahamu kwamba kila mmoja amewekewa na Roho Mtakatifu ndani yake upako maalumu – uwezo maalum - kuweza kuhudumia watu wengine. Si kila mtu ataweza kuhubiri kama vile mimi nifanyavyo, kwa mfano, Unaweza usiwe na karama ya ualimu, lakini kila mtu katika mwili wa Kristo anaweza kufundisha kwa kushirikisha wengine imani yake. Kuna watu ambao wameitwa kwa ajili ya kufundisha tu, watu ambao wameitwa kuhubiri na kuchunga makanisa. Karama nyingine iliyo orodheshwa katika kitabu cha Warumi 12 inasema kuna wale ambao karama yao ni ukarimu. Wengi wenu mnaweza kuwa na uwezo au karama, pasipo kujua mnazo. Una kuwa tu na matamanio ya kuweza kumbariki mtu mwengine. Unaweza kuwa ni aina ya mtu ambaye, unapoingia kwenye chumba, unaweza kujua watu ambao ni wagonjwa kwa urahisi sana. Na unaumia pamoja nao, unajua ni nini wanachokipitia, na una nia ya kuwafanya wajisikie vizuri na kuwahudumia. Je ulijua ya kuwa hali hiyo ni karama ya Mungu?

Warumi 12 inasema kuna baadhi ya watu wameitwa kwenye karama ya utoaji, uwezo wa kupata fedha na kutoa kwa ajili ya kutegemeza Injili, Hiyo ndiyo karama yao, wito wao katika maisha na baadhi yenu mnaweza kuitwa kwenye karama hiyo hiyo. Baadhi yenu mna karama ya kufariji wengine, Na wengine mna karama ya utawala ambayo inaitwa na kanisa karama ya usaidizi. Kuna aina ya vitu vingi ambavyo vinaweza kufanyika, si tu katika mazingira ya kanisani, lakini hata siku kwa siku katika kushughulika na mahitaji ya watu. Kuna baadhi yenu ambao wana uwezo wa kuwatia moyo wale waliyo vunjika moyo, kitu ambacho nisingeweza kukifanya kupitia mafundisho ya Neno la Mungu. Unakuwa tu na uwezo wa kiMungu wa kwenda, weka mkono wako kumzunguuka mtu fulani, wabariki na uwawezeshe. Kitu nina chokisema hapa ni kuwa huhitaji kuliona hili kama kuwa tu ni jambo la kawaida, na pia kuwa kama "Vyema, hivi ndivyo nilivyo" Unaweza kuwa umejiweka katika daraja la kuwa kama aina ya mtu huyo, lakini unajua nini, ilikuwa ni uwezo wa kiMungu ambao Mungu ameuweka ndani yako ndiyo ambao umekupa karama hizo, vipawa, na mtazamo ambao unakufanya wewe kuwa na nia ya kufanya baadhi ya vitu.

Unapokua unawahudumia watu wengine, Maandiko yanasema unahitaji kuhudumu vitu ambavyo Mungu ameviweka ndani mwako. Sisi wote tunahitaji kuwa watumishi, iwe ni watumishi wa kudumu tuliyojitoa moja kwa moja, tukiwa tunafanya kazi zetu, au popote pale tulipo. Ikiwa kama unaifanya na jirani zako au watu waliyoko dukani, unahitaji kuifanya kutokana na uwezo ambao Mungu anakupa, na siyo kutokana na uwezo wako mwenyewe. Hivyo nina kutia moyo umtafute Mungu, na ugundue karama ambazo Mungu ameweka ndani mwako, na wala usizidharau ikiwa kama hukuitiwa kwenye moja ya karama hizo za kihuduma ambazo ni za kudumu. Ukitambua ya kuwa Roho Mtakatifu ameweka ndani ya kila mmoja wenu uwezo wa kiMungu, na halafu uwahudumie watu wengine kupitia karama ambazo Mungu ameweka ndani yako.

Itachukua muda na mazoezi. Hutafanya kwa ukamilifu mara ya kwanza, lakini usiogope kufanyia mazoezi. Ikiwa kama utafanya makossa, Mungu hataondoka kwenye kiti chake cha enzi, na watu wengine wataona ukweli wa moyo wako. Upendo wako utawahudumia hata kama hutafanya kitu ambacho ni kikamilifu. Anza kuwahudumia wengine. Tambua ya kuwa umepewa karama na Mungu, na anza kushirikisha wengine uwezo wako wa kiMungu ambao Amekupa wewe.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma 1Petro 4:11. Tunatakiwa kuhududmu kwa kutumia uwezo wa nani? ____________________________________________

2. Soma 1 Wakorintho 12:4. Kuna aina mbali mbali na tofauti za karama za Roho, lakini nani ndiye chanzo cha hizo zote?. ______________________

3. Soma 1 Wakorintho 12:6. Chagua kauli sahihi.
   - A. Mungu anafanya kazi katika njia moja tu.
   - B. Kuna njia tofauti ambazo Mungu hufanya kazi kupitia watu.
   - C. Mungu hufanya kazi kupitia mhubiri tu.

4. Soma 1 Wakorintho 12:7. Uwepo wa Roho Mtakatifu na karama za kiroho amepewa kila moja wetu kwa ajili ya wema wa wote. Kweli au Si kweli.

5. Soma 1Wakorintho 12:8-10. Orodhesha na elezea baadhi ya karama za kiroho ambazo Mungu huwapa watu. ______________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### 1 Petro 4:11

"Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu; mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu; ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo. Utukufu na uweza una yeye hata milele na milele. Amina.

### 1 Wakorintho 12:4

"Basi pana tofauti za karama; bali Roho ni yeye yule."

### 1 Wakorintho 12:6

"Na kuna tofauti za kutenda kazi, bali Mungu ni yeye yule azitendaye kazi zote katika wote".

### 1 Wakorintho 12:7

"Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana."

### 1 Wakorintho 12:8-10

[8] "Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima, na mwingine neno la maarifa, apendavyo Roho yeye yule; [9] Mwingine imani katika Roho yeye yule, na mwingine karama za kuponya katika Roho yule mmoja; [10] Na mwingine matendo ya muujiza, na mwingine unabii, na mwengine kupambanua roho, mwingine aina za lugha, na mwingine tafsiri za lugha."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

6. Soma Warumi 12:6-8. Eleza maana ya karama za kiroho zilizo orodheshwa hapa ambazo Mungu amewapa watu. ________
____________________________________
____________________________________
____________________________________
____________________________________
____________________________________
____________________________________

7. Je umegundua karama yoyote katika hizi ambayo inafanya kazi kupitia wewe? Ikiwa ndiyo hivyo, ni karama gani? ____________
____________________________________
____________________________

8. Soma 1 Wakorintho 12:7. Nani ambaye anatakiwa kufaidika kutoka kwenye karama hizi? ________________________
____________________________________
_______________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Matendo 27:21-25

"[21] Na walipokua wamekaa wakati mwingi bila kula chakula, Paulo akasimama katikati yao, akasema, wanaume iliwapasa kunisikiliza mimi na kutokung'oa nanga huko krete,na kupata madhara haya na hasara hii. [22] Sasa nawapeni shauri, iweni na moyo mkuu, kwa maana hapana hata nafsi mmoja miongoni mwenu akayepotea, ila merikebu tu. [23] Kwa maana huu usiku wa leo malaika wa Mungu yule ambaye mimi ni wake, naye ndiye nimwabuduye, alisimama karibu nami. [24] Akaniambia, usiogope, Paulo, huna budi kusimama mbele ya kaisari, tena tazama, Mungu amekupa watu wote wanaosafiri pamoja nawe. [25] Basi, wanaume, changamkeni, kwa sababu namwamini Mungu, ya kwamba yatakua vile vile kama nilivyoambiwa."

### Matendo 9:11-12

"[11] Bwana akamwambia, Simama, enenda zako katika njia iitwayo Nyofu, ukaulize katika nyumba ya Yuda mtu aitwaye Sauli, wa Tarso; maana, angalia, anaomba;, [12] naye amemwona mtu, jina lake Anania, akiingia, na kumwekea mikono juu yake, apate kuona tena.,

### 1 Wakorintho 13:2

"Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, si kitu mimi."

### Marko 16:18

"Watashika nyoka, hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa wataweka mikono yao juu ya wagojwa nao watapata afya."

# MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

## Waebrania 2:3 - 4

"[3] Sisi je? Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ambao kwanza ulinenwa na bwana, kasha ukathibitishwa kwetu na wale waliousikia. [4] Mungu naye akishuhudia pamoja nao kwa ishara na maajabu na nguvu za namna nyingi na kwa magawanyo ya Roho Mtakatifu, kama alivyopenda mwenyewe.

## Matendo 11:27-28

"[27] Siku zizo hizo manabii walitelemka kutoka Yerusalemu hata Antiokia [28] Na tulipokusanyika akasimama mmoja wao, jina lake Agabo, akaonyesha kwa uweza wa Roho Mtakatifu kwamba njaa kubwa itakuja karibu katika dunia nzima, nayo ikatukia katika siku za Klaudio."

## 1 Wakorintho 14:3

"Bali yeye atubuye, anasema na watu maneno ya kuwajenga, na kuwafariji na kuwatia moyo."

## Matendo 16:16-18

"[16] Ikawa tulipokua tukienda mahali pale pa kusali kijakazi mmoja aliyekua na pepo wa uaguzi akatukuta, aliyewapatia bwana zake faida nyingi kwa kuagua, [17] Akamfuata Paulo na sisi akapiga kelele akisema, watu hawa ni watumishi wa Mungu aliye juu wenye kuwahubiria njia ya wokovu. [18] Akafanya hayo siku nyingi. Lakini Paulo akasikitika, akageuka akamwambia yule pepo, nakuamuru kwa jina la yesu kristo, mtoke huyu akamtoka saa ile ile."

## Matendo 2:4-11

"[4] Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine kama Roho alivyowajalia kutamka. [5] Na walikuwako yerusalemu wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila Taifa chini ya Mbingu. [6] Sauti hii iliposikiwa kwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe. [7] Wakashangaa wote, wakastaajabu, wakastaajabu wakakimbiana, tazama hawa wote wasemao si wagalilaya? [8] Imekuaje basi sisi kusikia kila mtu luhga yetu tuliyozaliwa nayo? [9] Warparthi na wamedi na waelami, nao wakaao mesopotania, uyahudi na kapadokia, ponto na asia. [10] Frigia na Pamfilia, Misri na pande za Libya karibu na kirene, na wageni watokao Rumi, wayahudi na waongofu. [11] Wakrete na Waarabu; tunawasikia hawa wakisema kwa lugha zetu matendo makuu ya Mungu."

## 1 Wakorintho 14:13-14

"[13] Kwa sababu hiyo yeye anenanye kwa lugha na aombe apewe kufasiri. [14] Maana nikiomba kwa lugha, roho yangu huomba, lakini akili zangu hazina matunda."

# MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

## Warumi 12:6-8

“[6] Basi kwa kuwa tunakarama zilizo mbali mbali, kwa kadiri ya neema mliyopewa; ikiwa unabii, tutoe unabii kwa kadiri ya imani.[7] Ikiwa huduma, tuwemo katika huduma yetu, mwenye kufundisha katika kufundisha kwake.[8] Mwenye kuonya, katika kuonya kwake, mwenye kukirimu kwa moyo mweupe, mwenye kusimamia kwa bii mwenye kurehemu, kwa furaha.”

## Timotheo 2 4:11

“Luka peke yake yupo hapa pamoja nami, umtwae marko umlete pamoja nawe, maana anifaa kwa utumishi.”

## Matendo 13:1

“Na huko antiokia katika kanisa lililokuwako palikuwa na manabii na walimu, nao ni barnaba na simon aitwaye ningeri, na Lukio Mkirene na manaeni aliyekuwa ndugu wa kunyonya wa mfalme herode, na sauli.”

## Matendo 13:15

“Kasha, baada ya kusomwa torati na chuo cha manabii wakuu wasinagogi wakatuma mtu kwao, na kuwaambia, ndugu, kama mkiwa na neno la kuwafaa watu hawa, lisemeni..”

## Methali 22:9

“Mwenye jicho la ukarimu atabarikiwa, maana uwapa masikini chakula chake.”

## Matendo 20:28

“Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake MUNGU, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe.”

## Mathayo 5:7

“Heri wenye rehema, maana hao watapata rehema.”

## 1Wakorintho 12:7

“Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana.”

# MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Petro 4:11. Tunatakiwa kuhududmu kwa kutumia uwezo wa nani? **Uweza wa Mungu.**

2. Soma 1 Wakorintho 12:4. Kuna aina mbali mbali na tofauti za karama za Roho, lakini nani ndiye chanzo cha hizo zote? **Mungu/Roho Mtakatifu.**

3. Soma 1 Wakorintho 12:6. Chagua kauli sahihi. **B. kuna njia tofauti ambazo Mungu hufanya kupitia watu.**

4. Soma Wakorintho 112:7. Uwepo wa Roho Mtakatifu na karama za kiroho amepewa kila moja wetu kwa ajili ya wema wa wote. **kweli.**

5. Soma 1 Wakorintho 12:8-10. Orodhesha na elezea baadhi ya karama za kiroho ambazo Mungu huwapa watu.

   **Neno la hekima = Ufunuo wa kiungu toka kwa Mungu wa nia yake na madhumuni. Angalia Matendo 27:21-25.**
   **Neno la Maarifa = Ufunuo wa kiungu kutoka toka kwa Mungu, wa kweli yoyote ile au tukio. Angalia Matendo 9:11-12.**
   **Karama ya imani = Uwezo wa kiungu katika kumuamini Mungu bila kuwa na shaka. Angalia 1 Wakorintho 13:2.**
   **Karama ya uponyaji = Uwezo wa kiungu wa kuponya magonjwa pasipo msaada wa mwanadamu au dawa. Angalia Marko 16:18.**
   **Karama ya kufanya miujiza = Uwezo wa kiungu wa kuingilia kati jambo ambao unaleta miujiza kinyume na kanuni za asili. Angalia Waebrania. 2:3-4.**
   **Unabii = Matamko ya kiungu yaliyotiwa nguvu na Mungu yenye kutamkwa katika lugha inayojulikana na anayenena. Matendo 11:27-28 na Wakorintho wa 1 14:3.**
   **Karama ya Utambuzi = Mafunuo ya kiungu toka kwa Mungu kujua uwepo wa shughuli za roho mbali mbali. Angalia Matendo 16:16-18.**
   **Lugha Mbali mbali = Uwezo wa kiungu wa kutamka, kuhuishwa na Mungu, katika lugha isiyojulikana. Angalia Matendo 2:4-11.**
   **Tafsiri za lugha = Uwezo wa kiungu wa kutamka, uliyohuishwa na Mungu, kuweza kutafsiri lugha isiyojulikana. Angalia 1 Wakorintho 14:13-14.**

6. Soma Warumi 12:6-8. Eleza maana ya karama za kiroho zilizo orodheshwa hapa ambazo Mungu amewapa watu.

   **Unabii = Uwezo wa kiungu wa kutamka, uliyohuishwa na Mungu, unaotamkwa kwenye lugha isiyofahamika na mnenaji.**
   **Huduma = Kuwahudumia wengine, huduma ya kimatendo. Angalia 2 Timotheo 4:11.**
   **Mafundisho = Kuelezea, elezea kwa undani zaidi. Angalia Matendo 13:1.**

   **Kuinuana = Kusihi, kushauri,kutia moyo,kuonya, Angalia Matendo 13:15.**
   **Utoaji = Kutoa zawadi kwa Mungu au kwa wengine. Angalia Methali. 22:9.**
   **Kutawala = kuongoza au uongozi. Angalia Matendo 20:28.**

**Huruma = Huruma inayoonyeshwa kwa mkosaji. Angalia Mathayo. 5:7.**

7. Je umegundua karama yoyote katika hizi ambayo inafanya kazi kupitia wewe? **Ikiwa ndiyo hivyo, ni karama gani?**

8. Soma 1 Wakorintho 12:7. Nani ambaye anatakiwa kufaidika kutoka kwenye karama hizi? **Kila mtu, Kwa kutumia karama kuweza kusaidia wengine, unamruhusu Mungu kufanya kazi kupitia wewe.**

DARAJA 3

# SOMO 3
# MIUJIZA HUMTUKUZA MUNGU

*Na, Andrew Wommack*

Tumezungumzia kuhusu kutembea katika nguvu za Mungu na kuwahudumia wengine kupitia karama ambazo Mungu ametupa. Ningependa kushirikisha baadhi ya mambo kuhusu haswa hili linavyo mtukuza Mungu na jinsi anavyotutarajia kutumia Uwezo wake wa kiungu. Kuna maandiko mengi sana kwenye hili ambayo ninaweza tu kugusia machache. Katika Mathayo 9 kuna tukio ambalo Yesu alimponya mtu aliye pooza, na ninashughulika na hilo kwa undani zaidi katika Marko 2. Mathayo 9:8 inasema. *"Makutano walipomuona, walishikwa na hofu, wakamtukuza Mungu aliyewapa watu nguvu ya namna hii."* Je ulijua ya kuwa karama za Roho - miujiza - inamtukuza Mungu, na hiyo ndiyo sababu Alitupa uwezo huo wa Kimiujiza sisi.

Unapoanza kushirikisha watu wengine, kuna tabia ya kiasili kwa wao kuwa na mashaka na kuanza kuwa na maswali, "Nina wezaje kujua kuwa kile unachokisema ni kweli?" Nimeshawahi kumsikia T. L. Osborne, mwinjilisti maarufu aliyewaongoza mamia kwa maelfu ya watu kwa Kristo, akielezea uzoefu wake kwa mara ya kwanza alipokuwa amekwenda kwenye safari ya kwanza ya umisheni. Alijaribu kuwashuhudia watu, na hawakuamini kile alichokisema. Hatimaye, siku moja alikua akizungumza na mtu mmoja, akasema "Lakini Biblia inasema," na yule mtu akasema, "Nini kinachofanya kitabu chako cheusi kuonekana kuwa ni tofauti na kitabu kingine chochote cheusi" Halafu T. L. Osborne akawaza, *Watu hawa wanajuaje kuwa Biblia ni kweli? Nina Imani ya kuwa Biblia ni Neno la Mungu, lakini ninawezaje kuwashawishi?*

Aliondoka kutoka kwenye umisheni akiwa ameshindwa na amekataa tamaa, akarudi nyumbani, na kuanza kumtafuta Mungu. Bwana alimwambia kwamba alipaswa kutumia uwezo wake wa Kiungu. Ishara na maajabu madhumuni yake ni kuthibitisha Neno la Mungu, ambalo ndilo litakalo badilisha maisha ya watu. Katika 1 Petro 1:23, inasema *"Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili, si kwa mbegu iaribikayo, bali kwa ile isiyo haribika kwa neno la Mungu lenye uzima lidumulo hata milele."* Neno la Mungu ndilo linalobadilisha maisha ya watu, lakini unawezaje kuwafanya waamini kwamba ni Mungu anayezungumza? Vyema, hayo ndiyo madhumuni ya miujiza. Tunapohubiri na kusema kuwa nu mapenzi ya Mungu

kwa mtu kuponywa, Tunalionyesha hilo kwa kunena juu yao katika jina la Yesu. Macho yao yaliyopofuka na masikio yasiyo sikia ambayo yanafunguliwa huthibitisha ya kuwa ni Mungu. Miujiza haiwezi kubadilisha watu, lakini itasababisha watu waamini kwamba neno ulilolinena ni Neno la Mungu.

Mfano wa maandiko kuhusu hilo ni Marko 2:1-9, ambapo kuna maelezo zaidi kuhusiana na habari ya kuponywa kwa aliyepooza. *"Akaingia [Yesu] kapernaumu tena, baada ya siku kadha wa kadha ikasikiwa ya kwamba yupo nyumbani wakakusanyika watu wengi isibaki nafasi hata mlangoni, akawa akisema nao neno lake. Wakaja watu wakimletea mtu mwenye kupooza, anachukuliwa na watu wanne na walipokua hawawezi kumkaribia kwa sababu ya makutano, waliitoboa dari pale alipokuwapo, na wakiisha kuivunja wakalitelemsha alilolalia yule mwenye kupooza. Naye yesu alipoiona imani yao akamwambia yule mwenye kupooza, mwanangu, umesamehewa dhambi zako. Na baadhi ya waandishi walikuwako huko, wameketi wakifikiri mioyoni mwao, mbona huyu ansema hivi? Anakufuru ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokua mmoja, ndiye Mungu Mara yesu akafahamu rohon mwake kwamba wanafikiri hivyo nafsini mwao, akawaambia mbona mnafikiri hivyo mioyoni mwenu? Vyepesi ni vip, kumwambia mwenye kupooza umesamehewa dhambi, au kusema ondoka ujitwike godoro lako, uende?"* Ukweli ni kwamba vitu hivyo yote kiutendaji haviwezekani. Haiwezekani kwa binadamu kusamehe dhambi, na pia haiwezekani binadamu wa kumponya binadamu mwingine aliye pooza. Hivyo kama Mungu anaweza kufanya moja, BIla shaka anaweza kufanya jengine.

Yesu alisema katika mistari ya 10-12, *"Lakini mpate kujua kwamba mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi hapo amwamia yule mwenye kupooza, nakuambia ondoka, ujitwike godoro lako uende nyumbani kwako. Mara akaondoka, akajitwika godoro lake, akatoka mbele yao wote hata wakastaajabu wote, wakamtukuza Mungu, wakisema, namna hii hatujapata kuiona kamwe."* Yesu aliweka wazi Aliposema, "Lakini mpate kujua ya kwamba mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi, (akamwambia yule mwenye kupooza)." Alileta uponyaji ili watu wajue ya kuwa kama Angeweza kufanya mambo katika ulimwengu wa mwili ambayo wangeweza kuyaona yakitikea kwa Neno Lake, basi vitu vya kiroho kama vile kusamehewa kwa dhambi vinaweza pia kufanyika.

Jambo linalofanana na hili limesemwa katika Waebrania 2:2-3: *"Kwa maana ikiwa lile neno lililonenwa na malaika lilikua imara na kila kosa na uasi ulipata ujira wa haki sisi je tutapataje kupona tusipojali wokovu mkuu namna hii ambao kwanza ulinenwa na bwana kasha ukadhibitika kwetu na wale waliosikia."* Inasema kwamba Mungu amedhihirisha Neno lake kwa nguvu ya Roho Mtakatifu. Unganisha hili pamoja na Marko 16:20, *"Nao wale wakatoka, wakihubiri kote kote, bwana akitenda kazi pamoja nao, na kudhibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo."* Ninachokisema ni hiki kuwa Mungu anakutaka wewe uweze kutumia uwezo wake wa Kiungu na nguvu kuwahudumia wengine. Anatumia miujiza inayofanyika

kupitia karama za Roho Mtakatifu kuthibitisha kwa watu kwamba kiu halisi Anazungumza nao. Hatima ya yote, anataka watu wawekwe huru mioyoni mwao, lakini mara nyengine njia ya kuufikia moyo wa mtu ni kwa kupitia miili yao na hisia. Kama utaweza kushughulikia maeneo hayo na kuona mtu akiwekwa huru, basi watafunguka na kuruhusu Bwana aguse maeneo mengine ya maisha yao na wajikabithi kikamilifu Kwake.

Katika 1 Wakorintho 2:1 Paulo alikuwa akiwaandikia Wakorintho, akiwaambia ni kwa jinsi gani kwanza alivyowafikia "Basi ndugu zangu mimi nilipokuja kwenu, sikujua niwahubiri siri ya Mungu kwa ufasaha wa maneno, wala kwa hekima." Maana naliazimu nisijue neno lolote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulubiwa. Nami nalikuwako kwenu katika hali ya udhaifu na hofu na matetemeko mengi. Na neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa adili za Roho na za Nguvu, ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu." Ameeleza wazi kabisa ya kuwa sababu kwa nini hakuja akisisitiza na kutumia maneno tu bali alikuja katika kudhihirisha nguvu ya Roho, ilikuwa ili imani yao ipate kusimama katika nguvu ya Mungu na si katika hekima ya mwanadamu.

Ukristo una mantiki ya ajabu katika hilo. Mara unapoiona kweli, unashangaa ni kwa jinsi gani uliikosa na kwa nini kila mtu haikubali. Lakini Ukristo si tu katika kuwa na mantiki… ni uzoefu halisi na Mungu aliye halisi. Na anataka ajidhihirishe katika nguvu kwa jinsi ile ile Alivyofanya kwenye Neno. Waebrania 13:8 amesema, *"Yesu kristo ni yeye yule jana leo na hata milele."* Yesu alikuja na alikiwa mtu aliyethibitishwa na Mungu kati yetu kwa ishara na maajabu na miujiza. Matendo 10:38 inasema, *"Habari za Yesu wa nazareti, jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu, naye akazunguka huko na huko akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na ibilisi, kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye."* Neno lake lilithibitishwa, na ile miujiza ilipiga kelele kama kengele ili kuwavuta watu kwenye ujumbe Wake. Walimtukuza Mungu Maandiko mengi yanasema kuwa miujiza hii ilimtukuza Mungu, na kama Yesu ilibidi atumie nguvu za Roho Mtakatifu kuhudumu na kubadilisha maisha ya watu, tunawezaje kufikiria ya kuwa tunaweza kufanya bora zaidi kuliko kile alichokifanya? Kama Yesu alitenda miujiza ili kuwavuta watu kuja kwake ili waupokee ujumbe Wake, Tunawezaje kufikiria ya kuwa tunaweza kuushawishi ulimwengu leo pasipo kutenda katika nguvu ya kiungu ya Mungu Ukweli ni kuwaa miujiza inamtukuza Mungu. Ni kengele inayowavuta watu. Ni kama kupiga kengele ya kuwaita watu kwa ajili ya chakula cha jioni – ni chakula ndicho kitakacho kujaza, bali ni kengele ndiyo itakayovuta usikivu wako. Pasipo kengele, baadhi ya watu watakosa chakula. Bila nguvu ya muujiza ya Mungu, watu wengi watakosa katika ukweli kuwa Mungu ni halisi na anaweza kuibadilisha mioyo yao na kuzisamehe dhambi zao.

Nakutia moyo utambue kuwa Mungu anataka kujidhihirisha kupitia kila moja wetu na kuifanya miujiza hii kupitia sisi kwenye maisha ya watu wengine. Baadhi yenu mnaweza

kusema "Lakini hilo linaniogopesha. Nini kinatokea kama nitamwombea mtu na asipone? Ninawezaje kujua hili litakwenda kutokea?" Unahitaji kutambua ya kuwa si wewe ndiye unayefanya miujiza, Huwajibiki ikiwa kama muujiza utafanikiwa na mtu akawekwa huru. Na huchukui lawama kama haitatokea. Wewe fanya nafasi yako ya kuomba tu; Mungu ndiye anayeponya, lakini ni lazima atende kazi kupitia wewe. Mungu anataka kukutumia wewe katika njia za miujiza. Unahitaji kuingia kwenye Neno la Mungu, na uone jinsi lilivyofanya kazi kwa wengine, uvifanye vitu hivyo maishani mwako, na uiache nguvy ya kimiujiza, ya kiungu ya Mungu ianze kufanya kazi ndani yake leo.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Muujiza ni nini? ____________________
____________________________________

2. Soma Marko 2:10-12. Miujiza aliyoifanya Yesu ilionyesha nguvu gani aliyo kuwa nayo? ____________________________
____________________________________
_______

3. Soma Marko 16:15-18. Kama waumini ni nini ambacho tunapaswa kufanya? ______
____________________________________
______________________________

4. Soma Matendo 8:5-8, 12. Watu waliona nini na waliitikiaje? __________________
____________________________________
__________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Marko 2:10-12

"[10] lakini mpate kujua kwamba mwana wa Adamu ana amri duniani ya kusamehe dhambi (hapo anamwambia yule mtu mwenye kupooza) [11] nakuambia ondoka ujitwike godoro lako uende nyumbani kwako [12] mara akajitwika godoro lake akatoka mbele yao wote hata wakastaajabu wote wakamtukuza Mungu wakisema naam hii hatujapata kuiona kamwe."

### Marko 16:15-18

"[15] Akawaambia endeni ulimwenguni mwote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. [16] Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini, atahukumiwa [17] Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, kwa jina langu watatoa pepo watasema kwa lugha mpya [18] Watashika nyoka, hata wakinywa kitu chenye kufisha hakita wazuru kabisa, wataweka mikono yao juu ya wagonjwa nao watapata afya."

### Matendo 8:5-8, 12

"[5] Filipo akateremka akaingiakatika mki wa samaria, akawahubiri kristo. [6] Na makutano kwa nia moja wakasikiliza maneno yale yaliyosemwa na filipo walipoyasikia na kuziona ishara alizokuwa akizifanya. [7] Kwa maana pepo wachafu wakatoka wengi waliopagawa nao, wakilia kwa sauti kuu, na watu wengi walipooza na viwete wakaponywa. [8] Ikawa furaha kubwa katika mji ule [12] lakini walipo mwamini filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu na jina lake Yesu kristo wakabatizwa wanaume na wanawake."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

5. Soma Matendo 3:12. Ni kitu gani Mtume Petro alikisema kuhusu utakatifu wake mwenyewe ukifanya miujiza? ____________________________________________

6. Soma Matendo 3:16. Miujiza inatokeaje? ____________________________________________

7. Je kuna matukio yoyote ya miujiza yanayotokea kwenye Agano Jipya ambayo haikufanywa na Mitume? ____________________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Matendo 3:12

"Hata Petro alipoyaona haya akawajibu wale watu, enyi waisrael, mbona mnastaajabia haya au mbona mnatukazia macho sisi, kama kwamba tumemfanya huyu aende kwa nguvu zetu sisi au kwa utauwa wetu sisi?"

### Matendo 3:16

"Na kwa imani katika jina lake jina lake limemtia nguvu mtu huyu mnayemuona na kumjua, na imani ile iliyo kwake yeye imempatia huyu uzima huu mkamilifu mbele yenu ninyi wote."

### Marko 9:38-39

"[38] Yohana akamjibu, akamwambia, mwalimu, tulimuona mtu akitoa pepo kwa jina lako, ambaye hafuatani nasi, tukamkataza kwa sababu hafuatani nasi, [39] Yesu akasema, msimkataze, kwa kuwa hakuna mtu atakaye fanya muujiza kwa jina langu akaweza mara kuninenea mabaya."

### Matendo 8:5-7

"[5] "Filipo akateremka akaingiakatika mki wa samaria, akawahubiri kristo. [6] Na makutano kwa nia moja wakasikiliza maneno yale yaliyosemwa na filipo walipoyasikia na kuziona ishara alizokuwa akizifanya. [7] Kwa maana pepo wachafu wakatoka wengi waliopagawa nao, wakilia kwa sauti kuu, na watu wengi walipooza na viwete wakaponywa.

### Matendo 9:10-18

"[10] Basi palikuwapo dameski mwanafunzi jina lake anania, bwana akamwambia katika maono, anania akasema mimi hapa Bwana [11] Bwana akamwambia,

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

8. Soma 1 Wakorinthrho 1:7. Ni lini karama ya miujiza itakoma? ______________________________________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

simama, enenda zako katika njia iitwayo nyoofu ukaulize katika nyumba ya yuda mtu aitwaye sauli wa tarso, maana angalia anaomba, [12] Naye amemuona mtu jina lake anania akiingia na kumweka mikono juu yake apate kuona tena. [13] Lakini anania akajibu bwana, nimesikia habari za mtu huyu kwa watu wengi mabaya mwengi aliyowatenda watakatifu wako yerusalemu, [14] Hata hapa ana amri itokayo kwa wakuu wa makuhani awafunge wote wakuitiao jina lako. [15] Lakini bwana akamwambia, nenda tu, kwa maana huyu ni combo kiteule, kwangu, alichukue jina langu mbele ya mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli. [16] Maana nitamuonyesha yalivyo mengi yatakayo mpasa kutswa kwa ajili ya jina langu. [17] Anania akaenda zake, akaingia mle nyumbani, akamwekea mikono akisema, ndugu sauli, bwana amenituma, yesu, yeye aliyekutokea katika njia uliyoijia, upate kuona tena ukajazwe Roho Mtakatifu. [18] Mara vikaanguka machoni pake vitu kama magamba, akapata kuona akasimama akabatizwa."

### Wakorintho 1 1:7

"Hata hamkupungukiwa na karama yoyote mkikutazamia sana kufunuliwa kwake bwana wetu yesu kristo,"

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Muujiza ni nini? **Tukio la kipekee au lisilo la kawaida ambalo linachukuliwa kuwa ni udhihirisho wa nguvu za Kimungu.Pia ni kuingilia kati kwa nguvu za Mungu juu ya sheria za asili.**

2. Soma marko 2:10-12. Muujiza wa yesu kristo ulikua unonyesha nini katika maisha ya binadamu? **Kusamehe dhambi.**

3. Soma Marko 16:15-18. Kama waumini ni nini ambacho tunapaswa kufanya? **Kuhubiri injili, kubatiza walio okoka, kutoa pepo wachafu, kunena kwa lugha, na kuponya wagonjwa.**

4. Soma Matendo 8:5-8, 12. Watu waliona nini na waliitikiaje? **Waliona miujiza (mstari wa 7), na waliamini katika Yesu, na walibatizwa kwa maji (mstari wa 12).**

5. Soma Matendo 3:12. Ni kitu gani Mtume Petro alikisema kuhusu utakatifu wake mwenyewe ukifanya miujiza? **Haikuwa utakatifu wake mwenyewe au nguvu iliyomponya mtu yule; Ilikuwa ni ya Mungu.**

6. Soma Matendo 3:16. Miujiza inatokeaje? **Kupitia Jina la Yesu na Imani katika Yeye.**

7. Je kuna matukio yoyote ya miujiza yanayotokea kwenye Agano Jipya ambayo haikufanywa na Mitume? **Ndiyo. Mfuasi wa Kristo ambaye hakutajwa jina (Marko 9:38-39). Filipo (Matendo 8:5-7), Anania (Matendo 9:10-18).**

8. Soma 1 Wakorintho wa 1:7. Ni lini karama ya miujiza itakoma? **Atakapo kuja Bwana Yesu; yaani atakaporudi.**

DARAJA 3

# SOMO 4
# NGUVU YA MAHUSIANO YA KIMUNGU

*Na, Don Krow*

Leo tunazungumza kuhusu nguvu ya mahusiano ya Kimungu. Unapolitafakari, Biblia yote inazungumza kuhusu mada hii. Kwa mfano, neno "kanisa" ni neno la Kiyunani ekklesia, na lina maanisha "kundi lililoitwa". Unapoangalia kwenye Neno la Mungu, utaona ya kuwa kanisa, au watu wa Mungu, wanatiwa moyo kukutana pamoja. Wanatiwa moyo kuomba kwa pamoja na kutiana moyo wao kwa wao kila siku. Wanatiwa moyo na nguvu ya mahusiano ya kimungu wanapotembea pamoja. Kama pia utazingatia neno "mzee", linatumika mara nyingi katika Maandiko, na linatumika kuelezea mtu ambaye ana umri mkubwa, mtu ambaye amekomaa, mtu ambaye ametembea maisha katika Kristo, na ambaye amefanikiwa katika familia yake na ndoa yake. Ingekuwa kama nilikuwa na tatizo na ndoa yangu, Ningependa kwenda kwa mtu ambaye alikuwa ni wa Kimungu, ambaye amepata hekima ya kimungu katika kipindi cha miaka kadhaa.

Pia tunatakiwa kutambua kuwa Maandiko yanaelezea mwili wa Kristo kama mwili wa kibinadamu. Una mikono, macho, masikio, na sehemu nyengine mbali mbali. Sisi sote tu sehemu ya kila mmoja wetu. Na kama Sehemu ya kila mmoja wetu, tunachukua nguvu kutoka kwa kila mmoja wetu. Kila kiungo, kila sehemu ya mwili kina karama yake, kipawa chake, jinsi yake chenyewe ya kutoa nguvu na maarifa.

Biblia inasema katika Yakobo 5:16, "Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidi." Huu ni mfano mmoja katika maandiko wa nguvu ya mahusiano ya kimungu. Unajua, Kuna kitu katika mwili wa Kristo ambacho kinakosekana. Ninafikiria ya kuwa kwa sababu tumeweka msisitizo kwenye ukuhani wa muumini, kwenda moja kwa moja kwa Mungu na si kwetu sisi kwa sisi, tumepoteza baadhi ya vitu. Biblia inazungumza kuhusu kuyaungama makosa yetu sisi kwa sisi. Ninaye rafiki anayeitwa Dr. Loren Lewis. Yeye ni mtu mwenye umri mkubwa kuliko sisi, na tumeshatumia muda mwingi pamoja. Ni msomi wa lugha ya Kigiriki na anasoma moja kwa moja kutoka lugha ya Kiyunani. Wakati kuna kitu kutoka kwenye maandiko ambacho siwezi kukielewa, nitakwenda kwake na kumuuliza nini Kiyunani kinasema kuhusu hilo. Pia

nita muuliza kuhusu tungo za Kigiriki, na hunisaidia sana katika kujifunza kwangu Biblia. Nimetumia masaa na masaa na mtu huyu. Yeye ni mtu wa hekima. Ni mtu wa kimungu. Ana ndoa yenye mafanikio. Ana familia iliyofanikiwa. Na kuna nyakati ambapo sisi wote tunahitaji kukiri makosa yetu. Sasa, Ninajua ya kuwa Biblia inasema kuwa tunapaswa kukiri dhambi zetu kwa Mungu, na sisemi kuwa uzikiri dhambi zako kwa mtu mwengine kana kwamba wanaweza kuzisamehe, Kwa sababu tunahitaji kwenda moja kwa moja kwa Mungu. Lakini tunahitaji kuwa na uwajibikaji katika maisha yetu.

Nguvu ya kuwa na mahusiano ya kimungu ndiyo nguvu tunayoihitaji kwa ajili ya uwajibikaji na kwa ajili ya mtu kututia moyo kumtafuta Bwana. Katika Waebrania, Biblia inatuambia tuinuane sisi kwa sisi kila siku, na wala tusiache kukutana pamoja, kutiana moyo sisi kwa sisi, na kuonyana sisi kwa sisi ili asije hata moja wetu akafanywa moyo wake kuwa mgumu kupitia uongo wa dhambi. Haya yote yana zungumza kuhusu umuhimu wa mahusiano ya kimungu. Kwenye upande hasi, Biblia inatuonya mara nyingi kuhusu mahuasiano yasiyo ya kimungu na ni kwa jinsi gani mahusiano hayo yasiyo ya kimungu yanavyoweza kuathiri nia zetu na kufikiri kwetu. Kabla hatujajua, tunaweza kwenda kwenye vitu ambavyo hatukutakiwa kuwa humo, ni kwa sababu hatujajilinda sisi wenyewe na kujizunguushia na mashauri ya Mungu (Methali. 11:14, 13:20, na 1 Wakor. 15:33). Biblia inasema, *"kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi?"* (2 Wakor. 6:14).

Unavyotembea katika maisha haya ya ukristo, ujipe moyo katika kujiunganisha na marafiki wa kiungu na wakimbie wale ambao watakusababishia kuingia katika dhambi. Ni muhimu sana kuwaweka watu wanao mwamin MUNGU karibu yetu, ambao watatusaidia na sisi katika kudumu katika imani ndani ya kristo (mith 27:17) MUNGU kubariki kadri unavyoendelea kutafakari na kumruhusu MUNGU zaidi katika maisha yako.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma 1 Wakorintho wa15:33. Mstari huu unatufundisha nini kuhusu mahusiano? ____________________ ____________________

2. Soma 1 Wakorintho wa12:12. Mstari huu unatuonyesha nini kuhusu maisha yetu ya kikristo? ____________________ ____________________ ________

3. Soma Waebrania 10:24. Tuna weza kujifunza nini kuhusu mahusiano ya kimungu kutoka kwa Waebrania 10:24? __ ____________________ ____________________

4. Soma Waebrania 10:25. Nini tunachoweza kujifunza kutoka mstari huu kuhusu mahusiano? ____________________ ____________________ ________

5. Soma Methali 5:22-23. Kwa nini ni lazima tuilinde miyo yetu dhidi ya mahusiano yasiyo ya kiungu? ____________________ ____________________ _____

6. Soma 2 Timotheo 2:22. Tunapaswa kutafuta haki, imani, upendo na amani na nani? ____________________ ____________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### 1 Wakorintho 15:33

"Msidanganyike, mazungumzo mabaya huaribu tabia njema."

### 1 Wakorintho 12:12

"Maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo."

### Waebrania 10:24

"Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri,"

Waebrania 10:25

"Wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengie, bali tuonyane na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri muonavyo siku ile kuwa inakaribia."

### Methali 5:22-23

"[22] Maovu yake yeye yatampata mdhalimu, naye atashikwa kwa kamba za dhambi zake. [23] Atakufa huyo kwa kukosa maonyo, naye atapotea kwa wingi wa ujinga wake.

### 2 Timotheo wa 2:22

"Lakini zikimbie tama z ujanani, ukafuate haki, na imani na upendo na amani pamoja na wale wamwitao bwana kwa moyo safi."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

7. Soma Waebrania 13:7. Ni nani tunayepaswa kumkumbuka na kumfuata katika maisha yetu? ____________________
____________________________________
____________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

Waebrania 13:7

"Wakumbukeni wale waliokuwa wakiongoza, waliowaambia neno la MUNGU, tena kwa kuchunguza sana mwisho wa mwenendo wao, iingieni imani yao."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma 1 Wakorintho 15:33. Mstari huu unatufundisha nini kuhusu mahusiano? **Marafiki wabaya huharibu tabia nzuri.**
2. Soma 1 Wakorintho 12:12. Mstari huu unatuonyesha nini kuhusu maisha yetu ya kikristo? **Kama mwili wa damu na nyama, sisi sote tunahitaji viungo vyengine vya mwili wa Kristo.**
3. Soma Waebrania 10:24. Tuna weza kujifunza nini kuhusu mahusiano ya kimungu kutoka kwa Waebrania 10:24? **Wale waliyo katika mahusiano ya kiungu huwah amasisha wengine kupenda na kutenda mema.**
4. Soma Waebrania 10:25. Nini tunachoweza kujifunza kutoka mstari huu kuhusu mahusiano? **Tunapaswa kukutana pamoja, na kuwa na ushirika pamoja, na kutiana moyo sisi kwa sisi.**
5. Soma Methali 5:22-23. Kwa nini ni lazima tuilinde miyo yetu dhidi ya mahusiano yasiyo ya kiungu? **Tusije tukapotezwa kwa ujinga (mstari wa 23).**
6. Soma 2 Timotheo 2:22. Tunapaswa kutafuta haki, imani, upendo na amani na nani? **Na wale wanaoita jina la Bwana wakiwa na moyo safi.**
7. Soma Waebrania 13:7. Ni nani tunayepaswa kumkumbuka na kumfuata katika maisha yetu? **Viongozi wako ambao wamezunguza Neno la Mungu kwako.**

DARAJA 3

# SOMO 5
# **MATESO**

*Na Don Krow*

Leo tunaenda kuangalia kwenye somo la mateso na maneno ya Yesu katika Mathayo 10:16-23. Alitaka kuwaanda wanafunzi wake dhidi ya upinzani, alitaka wajue kuwa upinzani utakwenda kutokea. Wale wote walioishi maisha ya kimungu, maisha yaliyo katika Kristo watapitia mateso (2 Timotheo wa 3:12). Si kitu ambacho unaweza kukikemea. Adui anawezakuwa nyuma yake, lakini mateso ni sehemu ya kusimama kwa ajili ya haki. Biblia inasema wale wanaoishi maisha ya utauwa katika Kristo watapitia mateso. Yesu anawaandaa wanafunzi wake kwa kusema *"Angalieni mimi nawatuma kama kondoo kati ya mbwa mwitu,* (Mathayo 10:16) Neno "tazama" ni kuusema, Nisikiilizeni Mimi. Ninataka mlipate hili. Nanakwenda kuwatuma kama kondoo katikati ya mbwa mwitu" Kondoo ndiyo wanyama ambao hawawezi kujitetea, Nina mfahamu kondoo ambaye hana meno makali, hana sumu kama nyoka - Hana ulinzi wowote, ulinzi pekee ambao hakika anoa ni kuwa na wchungaji. .

Jukumu la mchungaji, ni kuwaweka mbali mbwa mwitu na kundi la kondoo wake, lakini Yesu anasema kwa namna ya tofauti kabisa "Nawatuma kama kondoo kati kati ya mbwa mwitu." Je hili siyo la kushangaza? Sababu anasema hivi ni kuwa anawandaa kwa ajili ya upinzani. Waefeso 6:12 inasema, *"Kwa maana kushindana kwetu sisi kwa juu ya damu na nyama, bali ni juu ya ufalme wa mamlaka, juu yaw a kuu wa giza hili, juu ya majeshi ya mapepo wabaya katika ulimwengu wa Roho."* Kutakuwa na upinzani. Sehemu ya maisha ya Kikristo ni upinzani, na Yesu anataka ulijue hilo. Anataka kukuandaa wewe kwa ajili ya hilo kwa kusema *"Basi iweni na busara kama nyoka"* (Mathayo 10:16). Neno hilo "busara" lina maanisha katika kila hali, huta chochoea matatizo bila uhitaji wa kufanya hivyo lakini utakua na hekima uliyoibeba ndani yako. Kuwa na busara kama nyoka na wapole kama hua.

Halafu anasema, *"Lakini jihadharini na wanadamu"* (Mathayo 10:17). Kwa maana adui atatumia mwanadamu. Waefeso 2:2 inasema *"mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi."* Shetani atakwenda kutumia binadamu kutupinga, kupinga madhumuni la Yesu Kristo kulipinga Neno la Mungu. *"Jihadharini na wanadamu: kwa maana watawapeleka mabarazani, na katika masinagogi yao watawapiga* (Mathayo 10:17). Paulo

alisema, *"Mara tano nilipigwa mijeledi, mara tano nalipata mapigo arobaini kasoro moja. Kwa sababu ya Yesu Kristo, na ujumbe wa Yesu Kristo, na ujumbe wa injili"* (2 Wakorintho 11:23-24). Yesu alisema mtaletwa mbele ya wakuu - hata serikali wakati nyengine itatumika kuzuia madhumuni la Yesu Kristo, Mtapelekwa mbele ya wakuu na wafalme kwa ajili ya Yesu Kristo, kwa ajili ya kushuhudia upande wao au dhidi yao.

Mimi ni mwalimu wa chuo cha Biblia cha Chris. Nilikua nafundisha kozi kuhusu uinjilisti, na nilikuwa nawaonyesha wanafunzi ni jinsi gani wanaweza kutumia barua ya uinjilisti na ushuhuda binafsi kuwafikia waliyopotea. Na mimi pia nilishawahi kufanya ushuhuda mmoja na kuutuma kwa watu hamsini na kwa watu mia moja. Siku chache tu baada ya hapo, nilipigiwa simu kutoka kwa mwanamke mmoja aliyeitwa Mary Anne. Akasema, "Hautaweza kuliepuka hili; huwezi kuniambia kuhusus Yesu Kristo; huwezi kuliepuka hili, Umepata wapi jina langu? Nimesema "nimelipata kutoka katika kitabu cha majina." Alinijibu, "wewe ni muongo, hata hivyo?" Nilisema, "Vyema, Nililipata kutoka kwenye kitabu cha orodha ya namba za simu." akasema, "Wewe ni mwongo! JIna langu na anuani yangu havimo kwenye kitabu cha orodha ya namba za simu, "Hata hivyo huko ndiko nilikopata" Alisema, "Kesho polisi watakupigia simu." Nikawaza, *Je Biblia ni kweli?* Na polisi walinitafuta siku iliyofuata na walitumia masaa mawili wakijaribu kunihoji.

Unaona ninacho kisema? Kunapokuwa na wahalifu huko mtaani, polisi walipoteza masaa yao mawili. Kwa nini? Kwa ajili ya Yesu kristo, kwa ajili ya Injili. Je Neno la Mungu ni kweli? Kama ukisimamia kwenye Neno la Mungu, kama una ujasiri wa kushuhudia, kama una ujasiri wa kumtangaza Yesu, kama una ujasiri wa kuishi maisha ya haki mbele ya wanadamu, lazima kutakuwa na upinzani. Kuna nguvu za mwovu, na kuna nguvu za mema, Yesu alitaka wanafunzi wake wajiandae.

Yesu alisema katika Mathayo 10:19, *"Lakini hapo watakapo wapeleka, msifikiri fikiri* [msiwe na mashaka] *mtakavyosema maana mtapewa saa ile mtakavyosema."* Kwa uwepo wa Roho wa Mungu mtakuwa na hekima kama Stephano. Watu hawakuweza kuelewa hekima aliyokuwa akiitumia kuzungumza. Yesu anasema katika mistari ya 22-23, *"Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu lakini mwenye kuvumilia hata mwisho ndiye atakaye okoka. Lakini watakapo wafukuza katika mji huu kimbilieni mwingine."* Upinzani dhidi ya haki, dhidi ya madhumuni la Yesu Kristo, ni uhalisi ikiwa kama wewe ni mtendaji wa Neno na si tu msikilizaji.

Nilikua nimekaa kwenye bustani ya kupumzikia siku moja, nikamwona mwanamke mmoja mtu mzima kiumri ameketi kwenye bembea na nikajiambia ndani ya moyo wangu Ni mtu mzuri, hawezi kunidhuru! Nika muuliza kama ningeweza kukaa naye kwenye bembea, na nikaketi chini na kuanzisha mazungumzo naye. Nikafahamu kuwa jina lake alikuwa anaitwa Jane, na nikasema, "Hivi Jane, unafanya kazi gani?" Akajibu, "Oh, mimi ni mwanamke mzee;

sifanyi kazi tena. Nimestaafu" halafu akasema, "Na wewe unafanya kazi gani?" Nikamjibu kuwa, "Ninafanya kazi katika huduma ya Kanisa", Ghafla sura yake alibadilika. Akasema, "Kamwe usianiambie kuhusu Mungu! Wala usiniambie kuhusu Kristo!" Nikasema "Oh, Jane hupaswi kuzungumza hivyo," na akasema, "Kama Yesu Kristo angekuwa mbele yangu, ningemtemea mate usoni Mwake!" Nikasema, "Jane! Hupaswi kusema vitu kama hivyo! Lazima utakuwa umeumizwa na watu wengi sana katika makanisa kwa wewe kusema maneno kama hayo. Hutakiwi kusema hivyo! Acha nikueleze kuhusu familia yangu" Akasema, "Hapana! Huwezi kuongea na mimi utakwenda kunieleza kuhusu Yesu Kristo na kile ambacho Mungu amekifanya kwenye familia yako, na mimi wala sitakuruhusu ufanye hivyo. Huwezi kuzungumza." Nikasema, "Jane, tafadhali. Ni lazima nikuambie kuhusu Yesu." Akasema, "Hapana! Nina kwambia NYAMAZA!"

Alikua na mbwa mdogo pembeni yake, na alimvuta yule mbwa hadi akatoka pale alipokua amemfungia, na kuondoka pale nilipokua. Huyu alikua ni mwanamke ambaye amepoteza dira ya maisha yake kwa kuwa roho iliinuka ndani yake, roho ya kutokutii. Alikuwa akitawaliwa na adui. NIkawaza nafsini mwangu, *Sijazoea kuwa na watu wakinikaripia na wala sijazoea kwa watu kunipandishia sauti.* lakini sikua na cha kusema zaidi ya kumhurumia, hakuna kingine zaidi ya upendo kwa Jane. Alikua amepoteza mwelekeo, na mimi nilikua katika njia sahihi. Nilirudi nyumbani na kusema, "Bwana Unajua nini? muujiza mkubwa ni kwamba nilikua katika njia iliyo sahihi. Pale mtu alipokua akinijilia juu, sikuwa na chochote isipokuwa upendo na huruma."

Upinzani na mateso vitakuja pale tutakapotoka katika Jina la Yesu. Lakini Roho yule yule wa Mungu atupaye ujasiri wa kumtangaza Yesu hata kama tukikataliwa kwa sababu Yake, Roho huyo huyo atatupa faraja na nguvu katika hali yoyote ile.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma 2 Timotheo 3:12. Wale wanaoishi maisha ya kimungu watapitia nini?
   ______________________________
   ______________________________

2. Unaweza kuelezea vipi mateso"?
   ______________________________
   ______________________________

3. Soma Marko 4:16-17. Mateso na kukataliwa kunakuja kwa sababu ipi?
   ______________________________
   ______________________________

4. Soma Matendo 8:1, 4. Mateso kule Yerusalemu yalisababisha nini? __________
   ______________________________
   ________________________

5. Soma Mathayo 5:10-12. Kuna Baraka kwa wale wanoteswa kwa ajili: ____________
   ______________________________
   ______________________

6. Soma Mathayo 5:12. Waumini wanapopitia mateso kwa sababu ya haki, wanaweza kutegemea nini katika siku zijazo?
   ______________________________
   __________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### 2 Timotheo 3:12

"Naam,na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa."

### Marko 4 :16-17

"[16] Kadhalika hawa ndio wapandwao kwenye miamba, ambao kwamba kasha wakiisha kulisikia neno, mara hulipokea kwa furaha [17] Ila hawana mzizi ndani yao, bali hudumu muda mchache kasha ikitokea dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno mara hujikwaa."

### Matendo 8:1, 4

"[1] Siku ile kutakua adha kuu ya kanisa lililokua katika Yerusalemu, wote watatawanyika katika nchi ya uyahudi na samaria isipokua hao mitume. [4] Lakini wale waliotawanyika wakaenda huko nahuko wakilihubiri neno."

### Mathayo 5:10-12

"[10] Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki maana ufalme wa mbinguni ni wao. [11] Heri ninyi watakapo washutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo kwa ajili yangu. [12] Furahini na kushangilia kwa kuwa dhawabu yenu ni kubwa mbinguni kwa maana ndivyo walivyo waudhi manabii waliokuwa kabla yenu."

### Mathayo 5:12

"Furahini na kushangilia kwa kuwa dhawabu yeni ni kubwa mbinguni kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

7. Soma Matendo 9:4-5. Sauli alikua akimtesa nani? ______________________________ ____________________

8. Soma Matendo 9:1. Katika uhalisia ni nani ambaye Sauli alikuwa akimsulubisha? ____ ____________________________________ __________________________________

9. Soma Wagalatia 6:12. Wayahudi katika kitabu cha Wagalatia walijaribu kuongeza kwenye Injili kushika Sheria za dini. Katika kufanya hivyo, walikuwa wanaepuka nini? ____________________________________ ____________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Matendo 9:4-5

"Akaanguka chini akasikia sauti ikimwambia sauli, sauli mbona waniudhi? [5] Akasema u nani wewe Bwana naye akasema mimi ndimi yesu unayeniudhi wewe"

### Matendo 9:1

"Lakini Sauli akizidi kutisha na kuwaza kuwaua wanafunzi wa Bwana, akamwendea kuahani mkuu.."

### Wagalatia 6:12

"Wote watakao kuonekana ni wazuri kwa mambo ya mwili, ndio wanawashurutisha kutahiriwa, makusudi wasiudhiwe kwa ajili ya msalaba wa Kristo."

## UFUNGUO WA MAJIBU

1. Soma 2 Timotheo 3:12. Wale wanaoishi maisha ya kiungu watapitia nini? **Mateso.**

2. Unawezaje kuelezea vipi mateso"? **kunyanyaswa na kuteswa kwa sababu ya imani.**

3. Soma Marko 4:16-17. Mateso na kukataliwa kunakuja kwa sababu ipi? **Kwa ajili ya Neno la Mungu; yaani kwa ajili ya kuliondoa Neno.**

4. Soma Matendo 8:1, 4. Mateso kule Yerusalemu yalisababisha nini? **Watu waliekwenda kila mahali kuhubiri Neno.**

5. Soma Mathayo 5:10-12. Kuna Baraka katika wale wanaoteswa kwa ajili; **Ya Haki.**

6. Soma Mathayo 5:12. Waumini wanapopitia mateso kwa sababu ya haki, wanaweza kutegemea nini katika siku zijazo? **Thawabu kubwa kutoka kwa Mungu.**

7. Soma Matendo 9:4-5. Sauli alikua akimtesa nani? **Yesu.**

8. Soma katika matendo 9:1. Katika uhalisia ni nani ambaye Sauli alikuwa akimsulubisha? **Wanafunzi wa Yesu.**

9. Soma wagalatia 6:12. Wayahudi katika kitabu cha Wagalatia walijaribu kuongeza kwenye Injili kushika Sheria za dini. Katika kufanya hivyo, walikuwa wanaepuka nini? **Kupitia mateso kwa ajili ya msalabani wa Kristo. Kwa maneno mengine, waliepuka mateso yaliyokuja kutokana na mahubiri kuhusus wokovu huja kwa neema kupitia Imani katika Kristo pekee.**

DARAJA 3

# SOMO 6
# MFALME NA UFALME WAKE

*Na, Don Krow*

Katika Agano la Kale, kilichotofautisha taifa la Israeli na mataifa mengine ni kuwa ilikuwa ni mfumo wa utawala ambapo Makuhani walikuwa wakitawala katika jina la Mungu. Kwa maneno mengine lilikua linaongozwa na Mungu mwenyewe moja kwa moja (Isaya. 43:15). Baadaye katika historia ya Israeli, walitaka kuwa kama mataifa mengine duniani watawaliwe na mfalme wa kidunia.

(1 Samweli 8:5-19). Hivyo Mungu akawapatia kile walichokuwa wakiomba na kuwachagulia mfalme aliyeitwa Sauli

(1Samweli 10:24-25). Baadae kwa sababu kutokutii kwa Sauli. Mungu akamwinua Daudi awe mfalme, mtu aliyeupendeza katika moyo Wake (Matendo 13:21-22 na 1 Wafalme 15:3).

Mfalme alitakiwa kuwa mwakilishi anayeonekana anayemwakilisha Mungu asiyeonekana (Kumbu kumbu ya Torati 17:14-20). Mfalme alipomfuata Bwana, yeye na ufalme wake walifanikiwa. Lakini mfalme aliposhidwa kumfuata Bwana. Yeye na ufalme wake wangepelekwa utekani na kuangamizwa ( 1 Samweli 15:22-23).

Mungu alipochagua mfalme, alimtuma nabii kwenda kumpaka mafuta. Hii iliashiria Roho Mtakatifu akija juu ya mfalme huyo ili kumuwezesha na kumpaka mafuta aweze kutawala. Kwa wakati huu Roho wa Mungu anakuja ndani yake na kubadilisha moyo wake ili kutawala katika haki, kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye (1 Samweli 10:1, 6-7, na 9). Upako huu wa kutawala (au wa kuwa mfalme) ndipo wazo la Mesihi lilipoanzia. Neno “Mpakawa mafuta” katika Kiebrania ni *Mashiac* (Mesihi) na linatafsiriwa kama *christos* (Kristo) kwa Kiyunani. Manabii wa Agano la Kale walitabiri ya kuwa katika siku zijazo, Mesihi (au Mpakwa Mafuta) atakuja, na Mungu wa mbinguni ataweka ufalme ambao hautavunjika kamwe (Danieli. 2:44, 7:14, na 27). Katika maandiko, kama umegundua, Yesu hakuwahi kuwaelezea Wayahudi alimaanisha nini alipokuwa akizungumza kuhusu ufalme. Ilikua ni dhana ya Agano la Kale (Isaya. 9:6-7, 11:1-6; Danieli. 2:44, 7:13-14, 18, na 27).

Ni vigumu kuweza kuelewa ujumbe wa Yesu bila kuwa na uelewa wa msingi wa ufalme. Ufalme ulikuwa ndiyo ujumbe pekee Yesu aliyouzungumzia na pekee Aliyowaagiza wanafunzi Wake kuuhubiri, (Marko 1:14-15, Luke 9:1-2, na 28:23-31, Luka 16:16, na Mathayo. 24:14). Ujumbe huu pia ulimaanisha kuwa ni "wokovu" au fursa iliyotolewa ya "uzima wa milele" (Waebrania. 2:3; Mathayo. 19:16, 19:23; Matendo 28:23-24, 28, na 30-31). Ndani ya kauli "ufalme wa Mungu" ni wazo la kundi la watu ambao wangetawaliwa na Mungu. Ili kuweza kuingia katika ufalme wa Mungu, masharti ilibidi yafikiwe. Kubadilishwa moyo kuli hitajika. Kubadilika huku kwa moyo ndiko Biblia inakuita toba. Ilikuwa ni kubadilika kwa moyo kumuelekea Mungu; yaani, ilikuwa ni kugeuka mbali na Shetani, dhambi na njia zake, kumuelekea Mungu, Kristo na njia Zake. Mtu anapogeuka, Mungu anatoa (kama zawadi kupitia kumwagika kwa damu ya Yesu) msamaha wa dhambi na uzima wa milele. (Warumi 6:23). "Habari hii njema" inafahamika kama "Injili ya neema" au kuhubiriwa kwa "ufalme wa Mungu" (Matendo 20:24-25). Ufalme wa Mungu, unajulikana kwa Neema. (Mathayo. 20:1-16) na umekuja kwa ukimya na kwa siri katika huduma ya Yesu. (Mathayo. 13:33). Siku moja katika siku zijazo utakuja kwenye utimilifu uliyo na utukufu na wenye kuonekana (Mathayo. 13:36-43).

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Danieli 2:44. Manabii wa Agano la Kale walitabiri ya kuwa katika siku zijazo, Mesihi (au Mpakwa Mafuta) angekuja, na Mungu wa mbinguni atasimamisha ufalme wake?

   A. utadumu kwa miaka 1,000.

   B. Kamwe hautaangamizwa.

   C. Utakuwa si wa kudumu.

2. Soma Mathayo 4:17, 23. Ujumbe wa Yesu ulikuwa ni nini? ______________________ ____________________________________ ______________

3. Soma Marko 1:14-15. Yesu alihubiri injili ya __________________________________ ___________________________________.

4. Soma Luka 4:43. Sababu ya Yesu kutumwa kutoka kwa  Mungu ilikuwa ni. _________ ____________________________________ ___________________________.

5. Soma Yohana 4:25. Kwenye maandiko, Yesu hakuwahi kuwaelezea Wayahudi alichokua akimaanisha anapozungumza kuhusu ufalme. Ilikua ni dhana ya Agano la Kale ambayo?

   A. waliijua kidogo kuhusu  hiyo?

   B. walifikiri ya kuwa usingewahi kuja?

   C. tayari walikua wanautarajia.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Danieli 2:44

“Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ualme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawata achiwa enzi yake, bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele.”

### Mathayo 4:17, 23

“[17] Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema, tubuni, kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia. [23] Naye alikua akizunguka katika Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, na kuubiri habari njema ya ufalme, na kuponya wagonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu.”

### Marko 1:14-15

“[14] Hata baada ya yohana kutiwa gerzani, Yesu akaenda Galilaya, akihubiri habari njema ya Mungu. [15] Akisema wakati umetimia,na ufalme wa Mungu umekaribia, tubuni na kuamini Injili..”

### Luka 4:43

Akawaambia, imenipasa kuhubiri habari njema ya ufalme wa MUNGU katika miji mingine pia, maana kwa sababu hiyo nalitumwa.”

### Yohana  4:25

“Na huyo mwanamkwe akamwambia najua ya kua yuaja Masihi, (aitwaye Kristo)naye atakapokuja, yeye atatufunulia mambo yote.”

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

6. Soma Luka 9:1-2. Ni mambo gani matatu ambayo wanafunzi kumi na mbili waliyafanya? ______________________________________________________

7. Soma Luka 10:1-2, 8-9. Ni ujumbe gani Yesu aliwambia wale sabini wautangaze? ______________________________________________________

8. Soma Luka 23:2. Kufuatana na tafsiri ya Wayahudi, neno "Kristo" lina maanisha yule ambaye ni. ______________________________________________________.

9. Soma Matendo 17:7. Kinyume na sharia ya Warumi,Wayahudi walisema kuwa Mtume Paulo alifundisha kuwa kulikuwa na ____________________ mmoja ____________________.

10. Soma Matendo 19:8-10. Paulo alizungumza ujasiri katika Efeso akipinga na kuwashawishi wengine kuhusu ______________________________________.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Luka 9:1-2

"[1] Akawaita wale thenashara, akawapa uwezo na mamlaka juu ya pepo wote na kuponya maradhi, [2] Akawatuma wautangaze ufalme wa Mungu, na kupooza wagonjwa."

### Luka 10:1-2, 8-9

"[1] Basi baada ya hayo Bwana aliweka na wengine, sabini, akawatuma wawili wawili wamtangulie kwenda kila mji na kila mahali alipokusudia kwenda mwenyewe. [2] Akwaambia, mavuno ni mengi lakini watenda kazi ni wachache basi muombeni Bwana wa mavuno apeleke watenda kazi katika mavuno yake. [8] Na mji wowote mtakapo ingia wakiwakaribisha, vileni vyakula viwekwavyo mbele yenu,. [9] Waponyeni wagonjwa waliomo, waambieni ufalme wa Mungu umewakaribia."

### Luka 23:2

"Wakaanza kumshtaki wakisema tumemuona huyu akipotosha taifa letu na kuwazuia watu wasimpe kaisari kodi, akasema kwamba yeye mwenyewe ni Kristo, mfalme."

### Matendo 17:7

"na Yasoni amewakaribisha; na hawa wote wanatenda mambo yaliyo kinyume cha amri za Kaisari, wakisema na kwamba yupo mfalme mwingine, aitwaye Yesu."

### Matendo 19:8-10

"[8] Akaingia ndani ya sinagogi akanena kwa ushujaa kwa muda wa miezi mitatu, akihojiana na watu, na kuwavuta katika mambo ya ufalme wa Mungu. [9] Lakini wengine walikaidi wakakataa kuamini

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

11. Soma Matendo 28:23-31. Katika mstari wa 31, ni nini ambacho mtume Paulo alikuwa akikihubiri? ____________________________________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

wakitukana ile njia mbele ya makutano, basi akaondoka akawaacha, akawatenga wanafunzi, akahojiana na watu kila siku katika darasa ya mtu mmoja jina lake Tirano [10] Mambo haya yakaendelea kwa muda wa miaka miwili hata wote waliokaa Asia wakalisikia neno la Bwana, Wayahudi kwa Wayunani."

### Matendo 28:23-31

"[23] Wakiisha kuagana naye siku, wakamjia katika nyumba aliyokaa, watu wengi sana, akawaeleza kwa taratibu na kuushuhudia ufalme wa Mungu, akiwaonya mambo yake Yesu, kwa maneno ya sheria ya Musa na ya manabii, tangu asubuhi hata jioni. [24] Wengine waliamini yale yaliyonenwa, wengine hawakuyaamini. [25] Na walipokuwa hawapatani wao kwa wao, wakaenda zao, Paulo alipokwisha kusema neno hili moja, ya kwamba, Roho Mtakatifu alinena vema na baba zetu, kwa kinywa cha nabii Isaya, [26] Akisema, Enenda kwa watu hawa, ukawaambie, Kusikia, mtasikia wala hamtafahamu; Na kuona, mtaona wala hamtatambua;[27] Kwa maana mioyo ya watu hawa imepumbaa, Na masikio yao ni mazito ya kusikia, Na macho yao wameyafumba; Wasije wakaona kwa macho yao, Na kusikia kwa masikio yao, Na kufahamu kwa mioyo yao, Na kubadili nia zao, nikawaponya. [28] Basi ijulikane kwenu ya kwamba wokovu huu wa Mungu umepelekwa kwa Mataifa, nao watasikia! [29] Alipokwisha kusema hayo, Wayahudi wakaenda zao, wakiulizana mengi wao kwa wao. [30] Akakaa muda wa miaka miwili mizima katika nyumba yake aliyokuwa ameipanga, akawakaribisha watu wote waliokuwa wakimwendea, [31]Ahabari

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

12. Soma Mathayo 24:14. Ni ujumbe gani ambao untakiwa kuhubiriwa duniani kote?

_______________________________________

_______________________________________

13. Soma Matendo 20:24-25. Mara nyengine Injili ya ufalme inajulikana kama injili ya?

_______________________________________

_____________________________________.

14. Soma Luka 16:16. Ni vigumu kuelewa ujumbe wa Yesu bila kuwa na uelewa wa msingi wa ufalme. Ufalme wa ulikuwa ndiyo ujumbe ambao Yesu aliuzungumza na wa pekee ambao Aliwaelekeza Wanafunzi wake

    A. kuhubiri.

    B. kupuuza.

    C. tafakari.

15. Soma Mathayo 6:10. Kimsingi, ufalme wa Mungu ndiyo sharia ya Mungu. Unaelezewaje katika mstari huu?

_______________________________________

________________

16. Soma Wakolosai 1:13-14 na Warumi 14:9. Katika kauli hii "ufalme wa Mungu" ni dhana ya kundi la watu ambao wata

    A. mwalika Yesu katika mioyo yao?.

    B. kubali sheria ya Mungu (na kumkataa Shetani) na kupokea msamaha Wake.

    C. Kujiunga na kanisa.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

za ufalme wa Mungu, na kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri mwingi, asikatazwe na mtu.

### Mathayo 24:14

"Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa kaika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote, hapo ndipo ule mwisho utakapokuja."

### Matendo 20:24-25

"[24] Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa kitu cha thamani kwangu kama kuumaliza mwendo wangu na huduma ile niliyopokea kwa Bwana Yesu, kuishuhudia habari njema ya neema ya Mungu, [25] Na sasa, tazameni, mimi najua ya kuwa ninyi nyote niliowahubiria ufalme wa Mungu, Nikienda huko na huko, hamtaniona uso tena."

### Luka 16:16

"Torati na manabii vilikuwapo mpaka Yohana, tangu wakati huo habari njema ya ufalme wa Mungu hutangazwa, na kila mtu hujiingiza kwa nguvu."

### Mathayo 6:10

"Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni."

### Wakolosai 1:13-14

"[13] Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake. [14] Ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi"

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

17. Soma Mathayo 4:17. Ili kuingia katika ufalme wa Mungu kukubali kubadilishwa moyo wako. Haya mabadiliko kibiblia ni?

    A. Kuungama.

    B. Kazi ya sheria.

    C. Kutubu.

18. Soma Matendo 26:18. Je? Umegeuka kutoka ______________________ kugeukia nuru, kutoka kwenye _________________ ya Shetani _____________ ili kupokea msamaha wa dhambi zako? _______________________ ____________________________________ ________

19. Soma Ezekieli 36:26-27 na Matendo 11:15-18. Je? umepewa moyo mpya na roho mpya inayokusababisha kutembea katika njia za Mungu? ______________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Warumi 14:9

"Maana kristo alikufa akawa hai tena kwa sababu hii, awamiliki walio hai na waliokufa.

### Mathayo 4:17

"Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri, na kusema, tubuni, maana ufalme wa Mungu, umewakaribia."

### Matendo 26:18

"Uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi."

### Ezekieli 36:26-27

"[26] Nami nitawapa ninyi moyo mpya, na nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliyomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama. [27] Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazikisha hukumu zangu,na kuzitenda.

### Matendo 11:15-18

[15] "Ikawa nilipoanza kunena, Roho Mtakatifu akawashukia kama alivyotushukia sisi mwanzo. [16] Nikalikumbuka Neno lile la Bwana, jinsi alivyosema, Yohana alibatiza kwa maji kweli, bali ninyi mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu. [17] Basi ikiwa mwenyezi Mungu amewapa wao karama ile ile aliyotupa sisi tulimwamini Bwana Yesu Kristo, mimi ni nani niweze kumpinga Mungu. [18] Waliposikia maneno haya wakanyamaza, wakamtukuza Mungu,

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

20. Soma Luka 18:13-14. Je? Umemuita Mungu kwa ajili ya msamaha wa dhambi zako? ______________________________ ____________________________________ _________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

wakisema basi, Mungu, amewajalia hata mataifa nao toba iletayo uzima."

### Luka 18:13-14

"[13] Lakini yule mtoza ushuru alisimama mbali, wala hakudhubutu wala hata kuinua macho yake mbinguni, bali alipiga piga kifua akisema ee Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhambi. [14] Nakwambia, huyu alishuka kwenda nyumbani kwake amehesabiwa haki kuliko yule, kwa maana kila ajikwezaye atadhiliwa, naye ajidhilie atakwezwa."

# MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Danieli 2:44. Manabii wa Agano la Kale walitabiri ya kuwa katika siku zijazo, Mesihi (au Mpakwa Mafuta) angekuja, na Mungu wa mbinguni atasimamisha ufalme wake? **Kamwe hautaangamizwa.**

2. Soma Mathayo 4:17, 23. Ujumbe wa Yesu ulikuwa ni nini? **Tubuni, kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.**

3. Soma Marko 1:14-15. Yesu alihubiri injili ya **uafalme wa Mungu**

4. Soma katika Luka 4:43. Sababu ya Yesu kutumwa kutoka kwa Mungu ilikuwa ni **kuhubiri ufalme wa Mungu.**

5. Soma Yohana 4:25. Kwenye maandiko, Yesu hakuwahi kuwaelezea Wayahudi alichokua akimaanisha anapozungumza kuhusu ufalme. Ilikua ni dhana ya Agano la Kale ambayo? **C. tayari walikua wanautarajia.**

6. Soma Luka 9:1-2. Ni mambo gani matatu ambayo wanafunzi kumi na mbili waliyafanya? **Kutoa mapepo, kuponya wagonjwa, na kuhubiri ufalme wa Mungu.**

7. Soma Luka 10:1-2, 8-9. Ni ujumbe gani Yesu aliwambia wale sabini wautangaze? **Ufalme wa Mungu.**

8. Soma Luka 23:2. Kufuatana na tafsiri ya Wayahudi, neno "Kristo" lina maanisha yule ambaye ni. **Mfalme.**

9. Soma Matendo 17:7. Kinyume na sharia ya Warumi,Wayahudi walisema kuwa Mtume Paulo alifundisha kuwa kulikuwa na. **Mfalme**. Mmoja **Yesu**

10. Soma Matendo 19:8-10. Paulo alizungumza ujasiri katika Efeso akipinga na kuwashawishi wengine **kuhusu Ufalme wa Mungu**.

11. Soma Matendo 28:23-31. Katika mstari wa 31, ni nini ambacho mtume Paulo alikuwa akikihubiri? **Ufalme wa Mungu na kuwafundisha mambo yale yahusuyo Bwana Yesu Kristo.**

12. Soma Mathayo 24:14. Ni ujumbe gani ambao unatakiwa kuhubiriwa duniani kote? **Injili ya ufalme.**

13. Soma Matendo 20:24-25. Mara nyengine Injili ya ufalme inajulikana kama injili ya? **neema ya Mungu.**

14. Soma Luka 16:16. Ni vigumu kuelewa ujumbe wa Yesu bila kuwa na uelewa wa msingi wa ufalme. Ufalme wa ulikuwa ndiyo ujumbe ambao Yesu aliuzungumza na wa pekee ambao Aliwaelekeza Wanafunzi wake. **kuhubiri.**

15. Soma Mathayo 6:10. Kimsingi, ufalme wa Mungu ndiyo sharia ya Mungu. Unaelezewaje katika mstari huu? **Mapenzi ya Mungu yafanyike duniani kama ambavyo mapenzi yake yatakavyofanyika mbiguni.**

16. Soma Wakolosai 1:13-14 na Warumi 14:9. Katika kauli hii "ufalme wa Mungu" ni dhana ya kundi la watu ambao wata? **kubali sheria ya Mungu (na kumkataa Shetani) na kupokea msamaha Wake.**

17. Soma Mathayo 4:17. Ili kuingia katika ufalme wa Mungu kukubali kubadilishwa moyo wako. Haya mabadiliko kibiblia ni? **Kutubu**

18. Soma Matendo 26:18. Je? Umegeuka kutoka **gizani** kugeukia nuru, kutoka kwenye **nguvu** ya Shetani **kumuelekea Mungu** ili kupokea msamaha wa dhambi zako?

19. Soma Ezekieli 36:26-27 na Matendo 11:15-18. Je? umepewa moyo mpya na roho mpya inayokusababisha kutembea katika njia za Mungu?.

20. Soma Luka 18:13-14. Je? Umemuita Mungu kwa ajili ya msamaha wa dhambi zako?

DARAJA 3

# SOMO 7
# KITU CHA MSINGI CHA IMANI IOKOAYO

*Na, Don Krow*

Kwa mfano siku ya harusi ya mtu mmoja, anaposimama mbele ya mchungaji, mchungaji ghafla akaanza kusema maneno haya, "Unamchukua mwanamke huyu awe mpishi wako binafsi, asafishe nyumba yako, na vyombo vyako? Unamchukua kuanzia leo na kuendelea asafishe sakafu yako na kutoa vumbi kwenye samani ulizo nazo kwa kadri ninyi wawili mtakapokuwa mkiishi pamoja?" Ghafla mke wake mtarajiwa anasema "Acha! Kama unanitaka mimi kuwa tu mtu anayefanya vitu kwa ajili yako, unaweza kumwajiri mfanya kazi za ndani, nina taka wewe unipende na kunichukulia kama jinsi nilivyo, na nitafanya vitu vyote hivyo kwa ajili yako, lakini nina taka wewe unichukue,! Mimi jinsi nilivyo mzima sitaki uchukue tu faida zangu na kuniacha mimi."

A.W. Tozer alisema hivi, "Sasa, inashangaza kuona badhi ya waalimu wameshidwa kugundua kitu pekee cha kweli cha imani inayookoa si kingine bali ni Kristo Mwenyewe; si 'uwezo wa kuokoa' wa Kristo wala si 'ubwana' wa Kristo, bali ni Kristo Mwenyewe. Mungu hatoi wokovu kwa yule ambaye ataamini kwenye moja ya ofisi za Kristo, wala ofisi ya Kristo imeshawahi kuwasilishwa kama kitu cha msingi cha imani. Wala hatu hamasishwi kuamini kwenye msamaha, wala kwenye msalaba, wala kwenye ukuhani wa Mwokozi. Haya yote yame jumuishwa katika nafsi ya Kristo, lakini kamwe havi tenganishwi wala hakuna hata kimoja kinacho tenganishwa kutoka kwenye nyengine. Chini ya hapo tunaruhusiwa kukubali moja ya ofisi ya Kristo na kuikataa nyengine. Dhana kuwa tumeruhusiwa ni mafundisho potofu ya kileo, imekuwa na matokeo yenye uovu kati ya Wakristo (Mzizi wa Mwenye Haki, Uk. 84 -86)

Je umepata kile nilichotaka ukielewe? Kwa nini tunasisitiza sehemu ya Kristo (Faida zake), ofisi ya Kristo, na si Kristo? Hiyo ni kama kumchukua mke katika ndoa kama mpishi wako binafsi na si kama alivyo.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Yohana 1:12. “Bali wote waliyompokea:

   A. Yeye (Bwana Yesu Kristo),

   B. Yesu kama Mwokozi,

   C. Yesu kama Bwana,

   D. Yesu kama kuhani,

   aliwapa uwezo wa kufanyika wana (watoto) wa Mungu.

2. Soma Matendo 16:31. Tunatakiwa kuamini (yaani kuamini au kumtegemea) sisi wenyewe kwa nani?

   ______________________________________
   ______________________________________

3. Soma Luka 6:46. Neno “Bwana” lina maanisha nini? ______________________
   ______________________________________
   _______________

4. Soma Mathayo 1:21. Neno “Yesu” lina maanisha nini? ______________________
   ______________________________________
   ________________

5. Soma Luka 23:2. Neno “Kristo” lina maansha nini? ______________________
   ______________________________________
   ______________

6. Soma Warumi 1:16.kutokana na mstari huu, Injili au habari njema ni? ___________
   ______________________________________
   ____________________________.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Yohana 1:12

“Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake.”

### Matendo 16:31

“Wakamwambia mwamini Bwana Yesu nawe utaokoka pamoja na nyumba yako.”

### Luka 6:46

“Na kwa nini mnaniita Bwana, Bwana, walakini hamyatendi nisemayo?”

### Mathayo 1:21

“Naye atazaa mwana, nawe utamuita jina lake YESU, maana yeye ndiye atakaye waokoa watu wote na dhambi zao.”

### Luka 23:2

“Wakaanza kumshitaki wakisema, tumemuona huyu kipotosha taifa letu,na kuwazuia watu wasimpe kaisari kodi, akisema kwamba yeye mwenyewe ni Kristo Mfalme.”

### Warumi 1:16

“Kwa maana siionei haya injili, kwa sababu ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye kwa Myahudi kwanza na Mynai pia.”

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

7. Soma Warumi 1:1-3. Injili ya Mungu iko katika msingi wa, au inahusiana na nini? ____________________ ________. Sehemu ya Mwanawe au Sehemu yote ya Mwanawe?

8. Soma Yohana 6:54. Unapokula kitu, hiyo ina maanisha nini? ____________________ ____________________ ____________________

9. Soma Wagalatia 3:27. Mtu anapobatizwa katika Kristo, anamvaa____________________. Ni sehemu gani ya Kristo wanayovaa ____________________.

10. Soma Matendo 9:5-6. Sauli alipobadilishwa ni maswali gani mawili aliyomuuliza Yesu? ____________________ ____________________

11. Soma Warumi 7:4. Tunatakiwa kuolewa na nani? ____________________ Tunaolewa kwenye sehemu Yake ipi? ______________ ____________________.

12. Je? Unafurahia ndoa nzuri na Kristo? ____________________. Je mnaongea? mnawasiliana, mnapendana, na kumwabudu Yeye? ____________________ ____________________.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Warumi 1:1-3

"[1] Paulo mtumwa wa Kristo Yesu aliyeitwa kuwa mtume, na kutegwa aihuburi injili ya Mungu. [2] (Ambayo Mungu amekwisha kuiahidi kwa kinywa cha manabii wake katika maandiko matakatifu). [3] Yaani, habari za Mwanawe, aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili,

### Yohana 6:54

"Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele nami nitamfufua siku ya mwisho."

### Wagalatia 3:27

"Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo."

### Matendo 9:5-6

[5] "Akasema, u nani wewe Bwana, naye akasema, mimi ndimi Yesu unayeniudhi wewe, [6] Lakini simama uingie mjini nawe utaambiwa ya kupasavyo kwenda."

### Warumi 7:4

"Kadhalika, ndugu zangu, ninyi pia mmeifia torati, kwa njia ya mwili wa Kristo, mpate kuwa mali ya wengine yeye aliyefufuka katika wafu kusudi tumzalie Mungu matunda.

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma 1:12. Yohana “Bali wote waliompokea: **A. Yeye ( Bwana Yesu Kristo)**
2. Soma Matendo 16:31. Tunatakiwa kuamini (yaani kuamini au kumtegemea) sisi wenyewe kwa nani? **Bwana Yesu Kristo**
3. Soma Luka 6:46. Neno “Bwana” lina maanisha nini”? **Bwana, mtawala, bosi, Yeye mwenye mamlaka ya kuendesha maisha yetu. Neno hili pia lina maanisha Uungu**
4. Soma Mathayo 1:21. Neno “Yesu” lina maanisha nini? **Yesu kama Mwokozi.**
5. Soma luka 23:2. Neno “Kristo” lina maanisha nini? Y**esu kama Mfalme wetu na Mesihi**
6. Soma Warumi 1:16. Kutokana na mstari huu, injili au habari njema ni?
**Kristo Mwenyewe, ambao inajumuisha faida zake zote.**
7. Warumi 1:1-3. Injili ya Mungu iko katika msingi wa, au inahusiana na nini?
**Mwana wa Mungu Yesu Kristo Bwana wetu. Sehemu ya Mwanawe au Sehemu yote ya Mwanawe, Sehemu Yake yote.**
8. Soma Yohana 6:54. Unapokula kitu, hiyo ina maanisha nini?
**Kwamba unakubali kuingiza vyote ndani, kiasi kwamba kile unachokula kinakuwa sehemu ya maisha yako na nguvu zako.**
9. Soma Wagalatia 3:27. Mtu anapobatizwa katika Kristo anamvaa **Kristo**. ni sehemu gani ya mwili wa yesu wanaivaa? Mwili mzima wa yesu
10. Soma Matendo 9:5-6. Sauli alipobadilishwa ni maswali gani mawili aliyomuuliza Yesu? Wewe ni nani? **Na unataka nifanye nini.**
11. Soma warumi 7:4. Tunatakiwa kuolewa na nani? Na Bwana Yesu Kristo. Tunaolewa kwenye sehemu Yake ipi? **Mwili mzima wa Yesu.**
12. Je? Unafurahia ndoa nzuri na Kristo Je mnaongea? **mnawasiliana, mnapendana, na kumwabudu Yeye?**

DARAJA 3

# SOMO 8

# MATUMIZI SAHIHI YA SHERIA YA MUNGU

*Na Don Krow*

Siku moja Mimi na Joe tulikuwa tunaongea na Bill na Steve tukiwa katika eneo la ziwa. Swali liliulizwa, "Inawezekanaje watu wawajibike mbele za Mungu wakati hawajasikia kuhusu Mungu au Yesu Kristo?" Nikasema, "Bill, kama ungalienda kumtembelea Steve nyumbani kwake, ukakuta hayupo bali mkewe yupo. Kama unkiingia kwenye mahusiano ya uzinzi na mkewe, je ungalijisikia hatia ya kulala na mke wa rafiki yako? Hata kama hukuwahi kusikia amri kumi au kusoma Biblia? Hiyo hisia ya hatia na kuwajibika inatoka wapi?"

Unaona, Mungu amempa kila mtu, kupitia sheria na nafsi yako uwezo wa kutambua makosa na kuhisi hatia. Sheria na nafsi ni hukumu binafsi zinazofanya kazi kuhukumu au kusamehe kutegemneana na tabia za mtu binafsi (Warumi. 2:14-15).

Bill alikuwa ananiambia hadi wakati huu kuhusu jinsi yeye alivyo mtu mzuri. Alikuwa hajaona umuhimu wa kumpokea mwokozi. Nikaenda kwenye Kutoka 20 na nikaanza kumsomea Bill amri kumi. "Bill, je Mungu amekuwa na umuhimu wa kwanza maishani mwako,na je unampenda Mungu zaidi ya kitu chochote duniani? Kama sivyo, umevunja amri ya kwanza"

(Kutoka. 20:3). "Je umewahi kuinua kitu chochote juu zaidi ya Mungu? Kama ndivyo, umevunja amri ya pili " (Kutoka. 20:4). "Je umewahi kutumia jina la Yesu kama neno lenye herufi nne? Umevunja amri ya tatu." (Kutoka. 20:7) "Je umewahi kutunza siku kwa ajili ya kumheshimu na kumuabudu Mungu? Umevunja amri ya nne"

(Kutoka. 20:8). "Je mara zote katika ujana wako uliwaheshimu baba na mama yako? Umevunja amri ya tano" (Kutoka. 20:12). "Je umewahi kuwa na hasira na mtu yeyote? Umevunja amri ya sita " (fananisha Kutoka. 20:13 na Mathayo . 5:21-22). "Je umewahi kumwangalia mwanamke na kumtamani? Umevunja amri ya saba" (fananisha Kut. 20:14 na Mathayo. 5:27-28). "Je umewahi kuchukua kitu ambacho si cha kwako? Umevunja amri ya nane" (Kut. 20:15). "Je mar azote umekuwa ukisema kweli? Kama

sivyo, umevunja amri ya tisa ” (Kut. 20:16). “Je umewahi kutamani mali ya mtu mwingine? umevunja amri ya kumi ” (Kut. 20:17). “Je umeona kwanini Yesu anasema kwamba alikuja kuokoa waliona dhambi?” (Marko 2:16-17).

Tatizo la sisi kujifikiria kwamba ni wema sana, au kujaribu kuwa wema wa kutosha kwenda Mbinguni, ukweli ni kwamba wote tumevunja amri kumi. Yakobo 2:10 inatuambia kwamba yeyote atakaye shika amri zote ila akavunja moja wapo ana HATIA ya kuvunga sheria. Sheria haikuwekwa ili kukufanya wewe kuhesabiwa haki bali kuweka wazi dhambi yako (Warumi. 3:19-20).

Wote tunamuhitaji mwokozi ! neno “Mwokozi ” linamaana mtu anayeweza kukuokoa kutokana na adhabu ya dhambi. Yesu anaokoa wale waliopotea ili wapate uzima wa milele (Matt. 1:21).

Kuwa mwema wa kutosha kwenda mbinguni, lazima tuwe na haki iliyo sawa na ya Mungu (2 Kor. 5:21). Habari njema ya injili si tu je, Yesu atatusamehe dhambi zetu, bali anatoa – bure – haki yake mwenyewe kama zawadi kwetu (Warumi. 5:17: *“Kwa maana ikiwa kwa kukosa mtu mmoja mauti ilitawala kwa sababu ya yule mmoja, zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo*”).

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Warumi 2:16-17. Yesu alikuja kumuokoa nani?

   ___________________________

2. Soma Warumi 2:1. Wakati tunapohukumu wengine, tunajifanyia nini sisi wenyewe?

   ___________________________

   ___________________________Kwanini?

   ___________________________

   ___________________________

3. Soma Yakobo 2:10. Kama tukishika amri za Mungu bali tukakosa kuenenda inavyopasa katika mambo Fulani, tunahatia ya? _____

   ___________________________

4. Soma Galatia 3:10. Kama tunahitaji kuwa wenye haki kwa kushika sheria za Mungu tunaweza kushika kwa kiasi gani? ________________________ Kwa muda gani tunatakiwa kushika amri hizi? ___

   ___________________________

   Je unaona ni kwanini hatuwezi kuokoka kwa kujaribu kuwa wema vya kutosha?

   ___________________________

5. Soma Wagalatia 2:16. Kuhesabiwa haki ni karama ya haki, iliyotokana na Mungu, ambayo inamleta Mtu kuweza kusimama katika sehemu sahihi na kuwa na mahusiano na Mungu. Kuhesabiwa haki kwa watenda dhambi limetolewa kupitia Imani kwa Jina la Yesu Kristo na inakamilika mara moja na kwa wote kupitia kifo chake na ufufuo wake (1 Wakor. 15:3-4 na Warumi. 4:25). Mtu hahesabiwi haki kwa kipi? ___________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Marko 2:16-17

"[16] Na waandishi na Mafarisayo walipomwona anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi, waliwaambia wanafunzi wake, Mbona anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi? 17 Yesu aliposikia aliwaambia, Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi; sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi."

### Warumi 2:1

"Kwa hiyo, wewe mtu uwaye yote uhukumuye, huna udhuru; kwa maana katika hayo umhukumuyo mwingine wajihukumu mwenyewe kuwa na hatia; kwa maana wewe uhukumuye unafanya yale yale."

### Yakobo 2:10

"Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote.."

### Wagalatia 3:10

"Kwa maana wale wote walio wa matendo ya sheria, wako chini ya laana; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu asiyedumu katika yote yaliyoandikwa katika kitabu cha torati, ayafanye."

### Wagalatia 2:16

"hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu; sisi tulimwamini Kristo Yesu ili tuhesabiwe haki kwa imani ya Kristo, wala si kwa matendo ya sheria; maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

______________________________
________ Mtu anaokokaje? __________
____________________________ Watu wangapi watahesabiwa haki kwa sheria? __
________________________________
__________

6. Soma Warumi 6:14. Kama Mkristo, wewe uko:

   A. chini ya sheria.

   B. chini ya neema.

7. Soma Ezekiel 18:20. Kama ungalikuwa chini ya sheria, adhabu ya dhambi zako ingekuwa ni nini? ___________________
________________________________
_________

8. Soma Warumi 4:6-8. Chini ya Neema, ni mambo gani matatu Mungu anafanya na dhambi zako? ______________________
________________________________
______________

9. Soma Warumi 5:1. Sasa ambavyo tumefanywa wenye haki, ni faida gani tunayofurahia? ______________________
________________________________
______________

10. Soma Warumi 5:9. Sasa ambavyo tumeokolewa na damu ya Yesu, tunaokolewa kutokana na nini? _________
________________________________
_________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Warumi 6:14

"Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi, kwa sababu hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema."

### Ezekieli 18:20

"Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa; mwana hatauchukua uovu wa baba yake, wala baba hatauchukua uovu wa mwanawe, haki yake mwenye haki itakuwa juu yake, na uovu wake mwenye uovu utakuwa juu yake."

### Warumi 4:6-8

"[6] Kama vile Daudi aunenavyo uheri wake mtu yule ambaye Mungu amhesabia kuwa na haki pasipo matendo, [7] Heri waliosamehewa makosa yao, Na waliositiriwa dhambi zao. 8 Heri mtu yule ambaye Bwana hamhesabii dhambi.."

### Warumi 5:1

"Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo,."

### Warumi 5:9

"Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye.."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

11. Soma Warumi 10:4. Kristo aliimalizia sheria kama njia ya kupata ______________ ________________________________________ ________________ mbele za Mungu.

12. Soma 1 Wakor 1:30. Mungu alimfanya Yesu Kristo awe ________________________, ____________ ______________________, ______________ ____________________________, na ________ ________________________________________ ____________________________.

13. Soma Wafilipi 3:9. Wakati unapokuwa chini ya sheria ya Musa, unajaribu kujipatia ____________________________ _________________________________yako mwenye.

14. Soma1 Wakor 11:1. Kama Wakristo, tunaishi chini ya sharia ya Kristo. Sheria ya Kristo si mlolongo wa kanuni za kutii ; ni kuishi maisha kwa mwitikio kwa mtu. Mtu huyo ni nani ___________________________ ________________________________________.

15. Soma Warumi 8:3. Sheria haikuweza kutuiokoa, si kwa sababu sheria ni mbaya, bali kwasababu ya udhafu wetu katika ____________________________, Hatuwezi kuishika.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Warumi 10:4

"Kwa maana Kristo ni mwisho wa sheria, ili kila aaminiye ahesabiwe haki.."

### 1 Wakor 1:30

"Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi;."

### Filipi 3:9

"tena nionekane katika yeye, nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani."

### 1 Wakor 11:1

"Mnifuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo.."

### Warumi 8:3 –

"Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili;.

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Warumi 2:16-17. Yesu alikuja kumuokoa nani? **Watenda Dhambi**.
2. Soma Warumi 2:1. Wakati tunapohukumu wengine, tunajifanyia nini sisi wenyewe? **Kujihukumu wenyewe; kujitamkia hukumu sisi wenyewe.** Kwanini? **Kwasababu ingawa tunawahukumu wengine, tunafanya hay ohayo wanayoyafanya**.
3. Soma Yakobo 2:10. Kama tukishika amri za Mungu bali tukakosa kuenenda inavyopasa katika mambo Fulani, tunahatia ya? **tunahatia ya zote**.
4. Soma Galatia 3:10. Kama tunahitaji kuwa wenye haki kwa kushika sheria za Mungu tunaweza kushika kwa kiasi gani? **Zote** Kwa muda gani tunatakiwa kushika amri hizi? **Wakati wote pasipo kukosa.** Je unaona ni kwanini hatuwezi kuokoka kwa kujaribu kuwa wema vya kutosha? **Ndiyo**
5. Soma Wagalatia 2:16. Kuhesabiwa haki ni karama ya haki, iliyotokana na Mungu, ambayo inamleta Mtu kuweza kusimama katika sehemu sahihi na kuwa na mahusiano na Mungu. Kuhesabiwa haki kwa watenda dhambi limetolewa kupitia Imani kwa Jina la Yesu Kristo na inakamilika mara moja na kwa wote kupitia kifo chake na ufufuo wake (1 Wakor. 15:3-4 na Warumi. 4:25). Mtu hahesabiwi haki kwa kipi? **Kazi yake binafsi, kazi za sheria**. Mtu anaokokaje? **Kupitia Imani kwa kumuamini Yesu Kristo**. Watu wangapi watahesabiwa haki kwa Sheria? **Hakuna**.
6. Soma Warumi 6:14. Kama Mkristo, wewe uko: **B. chini ya neema**.
7. Soma Ezekiel 18:20. Kama ungalikuwa chini ya sheria, adhabu ya dhambi zako ingekuwa ni nini? **Mauti**.
8. Soma Warumi 4:6-8. Chini ya Neema, ni mambo gani matatu Mungu anafanya na dhambi zako? **Anasamehe, anazifunika, na anihesabii hatia**.
9. Soma Warumi 5:1. Sasa ambavyo tumefanywa wenye haki, ni faida gani tunayofurahia? **Amani na Mungu (Hajatukasirikia)**.
10. Soma Warumi 5:9. Sasa ambavyo tumeokolewa na damu ya Yesu, tunaokolewa kutokana na nini? **Hasira (hukumu ya dhambi )**.
11. Soma Warumi 10:4. Kristo aliimalizia sheria kama njia ya kupata **haki** Mbele za Mungu.
12. Soma 1 Wakor 1:30. Mungu alimfanya Yesu Kristo awe **hekima, haki, utakaso, na ukombozi**.
13. Soma Wafilipi 3:9. Wakati unapokuwa chini ya sheria ya Musa, unajaribu kujipatia **haki**.

14. Soma1 Wakor 11:1. Kama Wakristo, tunaishi chini ya sharia ya Kristo. Sheria ya Kristo si mlolongo wa kanuni za kutii; ni kuishi maisha kwa mwitikio kwa mtu. Mtu huyo ni nani **Kristo**.

15. Soma Warumi 8:3. Sheria haikuweza kutuiokoa, si kwa sababu sheria ni mbaya, bali kwasababu ya udhafu wetu katika **Mwili**, hatuwezi kushika.

# SOMO 9

# SI CHINI YA SHERIA, BALI CHINI YA NEEMA

*Na Don Krow*

Jana usiku niliota kuhusu mwanamke aliyelipia adhabu ya makossa yake yote (dhambi zake ). Mtu alimfuata, na mara zote yule mama alipofanya makosa, alitingisha kichwa chake kwa kutoridhishwa, na kutoa mshipi wake, na kumpiga yule. Kama mama yule angelisema neno ambalo si sawa au kufanya kitu kisicho sawa, yule mtu angemuadhibu. Alikuwa ana rukaruka huku akitabasamu na akawa na mtazamo chana, bali alijikuta bado anafanya vitu vilivyomsababisha kukosea na kuingia kwenye shida. havikuwa vitu vikubwa, bali vitu vidogo ambavyo mtu huyu alimuona akivifanya kwa makosa na kumpiga. Ilikuwa hali ya kukatisha tamaa.Alishindwa kuacha kufanya vitu ambavyo vilikuwa vinamuingiza kwenye Shida. Nakumbuka nilimuhurumia . Nilitaka nimuondoe mbali na yule mtu mkatili ambaye alikuwa nampiga kila wakati. Halafu nikashtuka toka usingizini.

Nikaanza kutafakari kuhusu Neema ya Mungu, tusiolipia, kibali tusichostahili na uwezo wa Mungu. Wakati moyo unapokuwa umeimarishwa kwa Neema, hatutafuti tena kukubalika na Mungu kwa matendo yetu au kwa kujaribu kushika amri zake kwa kujaribu kushika sharia kwa nguvu au uweza wetu. Mwishowe tunaweza kuepuka vipigo tunavyopokea kwa kuvunja sheria ya Mungu. Yesu ndiye aliyetuokoa.

Fikiri kuhusu Kibali. Hii inamaanisha kupata kibali mbele za mtu, msaada, au baraka. Wakati unapohitaji kibali toka kwa mtu, unafanya nini? Unajaribu kufanya na kusema kila kitu kinachoweza kumpendeza yule mtu, na kutofanya kitakacho wasikitisha. Ni kuwa na tabia njema kila wakati. Je hili ni rahisi kulitimiza? Ni kama kuwakinyume na msukumo unaovuta chini. Unaweza kufanya kw amuda mfupi, bali mwishowe, utashindwa. maana nguvu hiyo inanguvu zaidi yako.

Nilioanisha hili na yule mwanamke niliyemuota. Mara zote nimejihisi hivyo nilipojaribu kufanya vitu kwa uangalifu na usahihi, bali nikajikuta nimekosea kitu kidogo. Nilijifikia hivi inawezekana kwa siku nzima nisikosee kitu chochote, ingelikuwa hivi ningekamilisha kitu.

Bali hakuna, makossa yangu mar azote yalinifanya nisiwe mkamilifu. Nilifiki kwamba si tu kwamba nimemsikitisha baba yangu wa Mbinguni, bali ningejihukumu mimi mwenyewe na kujipiga mwenyewe. Nilijikuta nimeshindwa mimi mwenyewe. Nikiwa nalengo uwezo wangu na madhaifu yangu. Mara zote sikutimiza kiwango, mar azote sikuwa mzuri wa kutosha wa kufikia kiwango, nilihitaji mtu wa kunikomboa !

Mungu katika rehema zake akatutumia msaada; Jina lake Yesu. Mungu alimtuma ili atukomboe kutokana na sisi wenyewe na kujaribu kwetu kusiko na matokeo ya kutimiza sheria. Yesu alichukua adhabu ya sheria ambayo hatukuweza kushika, ili tusife, bali tuwe huru na kupata uzima wa milele pamoja naye. Yesu alitupa karama ya Haki ili tuwe wenye haki na watakatifu mbele za Mungu Baba na kutimiza mahitaji yote ya sheria. Tunaamani na Mungu kupitia kile alichotufanyia kupitia kifo chake, kuzikwa na kufufuka. Tunakibali mbele za Mungu, pasipo kulipia wa kustahili. Hii ni Neema.

Amini hili, moyo wako unapaswa kutulia na hili pasipo wasiwasi, kufahamu kwamba alifanya hivi kwa sababu anakupenda. Moyo wako udhibitike, uwe na usalama, msimamo na wenye ujasiri katika hii Neema; Uwe na uhakika pasipo maswali au tashwishi kwamba ametupa kila kitu tunachohitaji ili kuishi maisha tele na kupitia Yesu.

Tunaendelea kuangalia na kulenga kwenye madhaifu yetu, makossa, na dhambi, badala ya yesu mwanzilishi na mkamilishaji wa Imani yetu, mioyo yetu itasikitika na kukosa nguvu kuamini tunaweza kupokea kitu chochote toka kwa Mungu. Ni kwa moyo mtu huamini na kupokea haki na Neema. Miyo yetu iwe yake kikamilifu. Hapa ndipo tutakuwa katika utulivu.

“Linda moyo wako kuliko yote uyalindayo; Maana ndiko zitokako chemchemi za uzima” (Methali.4:23).

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. "Neema" imeelezewaje kwenye somo lililopita? ______________________________ ______________________________

2. Wakati moyo umethibitika katika Neema, hatutafuti tena Kukubalika na Mungu kupitia ______________________________ ______________________________.

3. Soma Waebrania 10:14. Madhaifu ya Don mara zote yalimsababisha kutokuwa mkamilifu. Tunafanyikaje kuwa wakamilifu, Kutegemeana na maandiko haya? ______________________________ ______________________________

4. Soma Warumi 5:17. Yesu alitupa ______________ ya haki ili tuhesabiwe haki na watakatifu mbele za Mungu baba na kutekeleza mahitaji yote ya Sheria.

5. Soma Isaya 26:3. Tukiendelea kuangalia na kulenga madhaifu yetu, makosa, na dhambi zetu, badala ya kumuangalia Yesu mwanzilishi na mmkamilishaji wa Imani yetu, mioyo yetu itasikitishwa na kukosa nguvu na uwezo wa kuamini ili kupokea kitu chochote toka kwa Mungu. Tunapaswa kulenga nia zetu kwenye nini? ______________________________ ______________________________

6. Soma Waefeso 3:17. Mioyo yetu lazima iwe mikamilifu. Ambapo tutakuwa ________ ______________________________ ______________________________.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Waebrania 10:14

"Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa"

### Warumi 5:17

"Kwa maana ikiwa kwa kukosa mtu mmoja mauti ilitawala kwa sababu ya yule mmoja, zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo."

### Isaiya 26:3

"Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea Katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini."

### Waefeso 3:17

"Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo;."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

7. Soma Warumi 4:5. Je Wokovu ni dhawabu tunayoifanyia kazi? au dhawabu ambayo ni bure inatolewa kwa Neema ya Mungu? ___
_______________________________________
_______________________________________

8. Soma Warumi 5:17. Haki (kuwa sawa na Mungu ) ni Karama. Je inabidi uifanyie kazi? Unapataje haki ya kupata Zawadi? __
_______________________________________
_______________________________________

9. Soma Warumi 6:23. Ni nini Karama ya bure ya Neema ya Mungu ilioko kwenye maandiko haya? _______________________
_______________________________________

10. Soma Warumi 3:5. Ni matendo yapi au kazi zipi njema ulizofanya zilizochangia kwenye wokovu wako? ________________
_______________________________________

11. Soma Warumi 6:14. Elezea kwa maneno yako inamaana gani luwa chini ya Neema ya Mungu. ___________________________
_______________________________________

12. Soma Warumi 11:6. Kama Baraka za Mungu zinakuja kwetu kwa neema, si kwa ajili ya ______________________________
_______________________________________

13. Soma Warumi 3:24. Elezea kwa maneno yako maana ya mstari huu. _____________
_______________________________________
_______________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Warumi 4:5
"Lakini kwa mtu asiyefanya kazi, bali anamwamini yeye ambaye amhesabia haki asiyekuwa mtauwa, imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki."

### Warumi 6:23
"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.."

### Tito 3:5
"si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu;."

### Waebrania 6:14
"Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi, kwa sababu hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema.."

### Waebrania 11:6
"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.."

### Warumi 3:24
"wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu;."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

14. Soma Waefeso 1:7. Msamaha wa dhambi zetu ni kutegemeana na ______________ ____________________________________ ______________________.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

Waefeso 1:7

“Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake.”

# MUONGOZO WA MAJIBU

1. "Neema" imeelezewaje kwenye somo lililopita? **Pasipo kulipia, kiali usichostahili na uwezo wa Mungu.**

2. Wakati moyo umethibitika katika Neema, hatutafuti tena Kukubalika na Mungu kupitia **Matendo**.

3. Soma Waebrania 10:14. Madhaifu ya Don mara zote yalimsababisha kutokuwa mkamilifu. Tunafanyikaje kuwa wakamilifu, Kutegemeana na maandiko haya? Kwa **Yesu' kujitoa, ametukamilisha milele**.

4. Soma Warumi 5:17. Yesu alitupa **Zawadi** ya haki ili tuhesabiwe haki na watakatifu mbele za Mungu baba na kutekeleza mahitaji yote ya Sheria

5. Soma Isaya 26:3. Tukiendelea kuangalia na kulenga madhaifu yetu, makosa, na dhambi zetu, badala ya kumuangalia Yesu mwanzilishi na mmkamilishaji wa Imani yetu, mioyo yetu itasikitishwa na kukosa nguvu na uwezo wa kuamini ili kupokea kitu chochote toka kwa Mungu. Tunapaswa kulenga nia zetu kwenye nini? **Nia zetu lazima zimuangalie Mungu tu.**

6. Soma Waefeso 3:17. Mioyo yetu lazima iwe mikamilifu. Ambapo tutakuwa **Tumeridhika na kuwa katika utulivu**.

7. Soma Warumi 4:5. Je Wokovu ni dhawabu tunayoifanyia kazi? au dhawabu ambayo ni bure inatolewa kwa Neema ya Mungu? **Zawadi ya bure ya neema ya Mungu**.

8. Soma Warumi 5:17. Haki (kuwa sawa na Mungu ) ni Karama. Je inabidi uifanyie kazi? Unapataje haki ya kupata Zawadi? **Kwa kuifikia na kuipokea**.

9. Soma Warumi 6:23. Ni nini Karama ya bure ya Neema ya Mungu ilioko kwenye maandiko haya? **Uzima wa milele (badala ya mauti ya milele)**.

10. Soma Warumi 3:5. Ni matendo yapi au kazi zipi njema ulizofanya zilizochangia kwenye wokovu wako? **Hakuna**.

11. Soma Warumi 6:14. Elezea kwa maneno yako inamaana gani luwa chini ya Neema ya Mungu. **Dhambi zetu haziadhibiwi inavyostahili bali kilicho bora cha Mungu kupitia Kristo. Haki, kukubali, msamaha ni vyetu (kama zawadi ya Rehema za Mungu).**

12. Soma Warumi 11:6. Kama Baraka za Mungu zinakuja kwetu kwa neema, si kwa ajili ya **kazi yetu**

13. Soma Warumi 3:24. Elezea kwa maneno yako maana ya mstari huu.
**Haki (kuhesabiwa haki ) ni karama ya Mungu ya Neema iliyotolewa kwa muumini kwa sababu ya kazi ya ukombozi iliyofanyika na Kritsto msalabani**

.14. Soma Waefeso 1:7. Msamaha wa dhambi zetu ni kutegemeana na **Utajiri wa Neema ya Mungu.**

# SOMO 10
# HAKUNA TENA HATIA YA DHAMBI

*Na Don Krow*

Siku Moja mtu mlevi aliingia katika gari lake, halafu akaanza kuendesha akielekea Mwelekeo usio sahihi, na akagongana macho kwa macho na gari linguine. Katika ajali hii, binti mwenye umri wa miaka 18 alifariki dunia. Familia ya yule binti ikamshitaki muhusika na kupata hela £1.5 kama fidia ya kesi.

Badala ya kuchukua hela yote familia ile ikachukua kiasi cha £936. Sababu ikiwa walitaka mtu huyu alipe fedha hizi kwa jinsi Fulani kimahususi. Walitaka mtu aliyekuwa amelewa akumbuke alichokifanya. Alitakiwa andike hundi kwa jina la yule binti aliyemuua katika ajali, ya £1 kila wiki na kuituma kwa familia ile. Ungeweza kufikiria kwamba malipo ya £936 ni afadhali kuliko yale aliyopaswa kulipa ya milioni £1.5. Mwanzoni kulipa £1 kwa juma ilikuwa rahisi sana, bali baada ya muda, kuandika hundi hiyo kwa jina la yule Binti aliyemuua kwenye ajali lilianza kutawala mawazo yake. Kila wiki aliingia katika msongo wa mawazo, akififikiri kuhusu yule binti aliye muua.

Baada ya miaka ya hili, mwishowe aliacha kulipa malipo haya. Familia ikamrejesha mahakamani na akapewa amri ya kuendelea kulipa malipo hayo. Katika miaka ya kwanza sita au saba, akaacha kulipa tena mara nne au tano. Hatahivyo, kila mara aliporudishwa mahakamani alianza kuendelea kulipa tena.

Ile familia ikasema hawana hasira tena, bali walitaka tu wamkumbushe mtu huyu kuhusu kile alichokuwa amekitenda.

Ukitafakari kuhusu hili, familia na mtu huyu pia aliyekuwa akilipa wote walikuwa katika kifungo. Kila juma wanapata hundi inayowakumbusha kufiwa kwao, kwa hiyo, walikuwa hawawezi kutupilia kufiwa kwa binti yao nyuma.

Mtu huyu sasa anaishitaki familia hiyo kwa kile alichokiita "Adhabu ya kikatili." Anasema, "hili ni sawa nakuniua ! kina haribu maisha yangu ! siwezi kutuppilia yaliopiota nyuma yangu na kusonga mbele na maisha."

Kutegemeana na stori hii, nimekutana na Wakristo wengi walio kwenye hisia kama hizo hujihisi hukumu kama hiyo. Waliambiwa "Yesu amelipia yote," bali wanajisikia kama vile wanapaswa wafanya malipo kila juma kwa kufanya huduma za kidini, lasivyo Mungu hatawakubali.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Ni mahusiano ya aina gani mtu huyu atakuwa nayo na familia yake wakati mambo kama haya yanaendelea? _______ ___________________________________ ________

2. Soma Waebrania 10:1.
   Sheria yaweza kufanya nini?
   __________________________

3. Soma Waebrania 10:1. Mstari huu unasema nini ambalo linatupa kiashiria kwamba dhabihu za agano la kale hazikutosha kutufanya wakamilifu? _____ ___________________________________ ________________________________

4. Soma Waebrania 10:2. Kama dhabihu ilikuja ili kukabiliana na dhambi, itafanya nini kwa wale wanaoabudu? ___________ ___________________________________

5. Yule driva mlevi alilazimika kufanya nini? ___________________________________

6. Soma Waebrania 10:14. Mungu huwakamilisha watu wake kwa:
   A. matendo mema.
   B. kwenda kanisani.
   C. kutii amri kumi.
   D. sadaka dhabihu ya Yesu Kristo.

7. Soma Waebrania 10:14. Yesu ' sadaka yake (ikipokelewa kwa Imani ) hukamilisha wale wanaoamini :
   A. hadi watakapo tend adhambi tena.
   B. toka kwenye dhambi zao za kale.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

Waebrania 10:1 – "Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wo wote kuwakamilisha wakaribiao."

Hebrews 10:2 – "Kama ndivyo, je! Dhabihu hazingekoma kutolewa; kwa maana waabuduo, wakiisha kusafishwa mara moja, wasingejiona tena kuwa na dhambi?."

Hebrews 10:14 – "Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.."

Mwanzo 20:1-18 – "[1] Ibrahimu akaondoka huko kwenda nchi ya kusini, akakaa kati ya Kadeshi na Shuri, naye akatembea katika Gerari. [2] Ibrahimu akamnena Sara mkewe, Huyu ni ndugu yangu. Basi Abimeleki mfalme wa Gerari akapeleka watu akamtwaa Sara. [3] Lakini Mungu akamjia Abimeleki katika ndoto ya usiku, akamwambia, Umekuwa mfu wewe kwa sababu ya mwanamke huyu uliyemtwaa, maana ni mkewe mtu. [4] Basi Abimeleki alikuwa hakumkaribia, akasema, Ee Bwana, Je! Utaua hata taifa lenye haki? [5] Je! Hakuniambia mwenyewe, Huyu ni ndugu yangu? Na mwanamke mwenyewe naye alisema, Huyu ni ndugu yangu. Kwa ukamilifu wa moyo wangu, na kwa kuwa safi mikono yangu, nimefanya hivi. [6] Mungu akamwambia katika ndoto, Nami nimejua ya kwamba kwa ukamilifu wa moyo wako umefanya hivi, ndipo nami nikakuzuia usinitendee dhambi, kwa hiyo sikukuacha umguse. [7]Basi sasa umrudishe mwanamke kwa mtu huyo, maana yeye ni nabii, naye atakuombea,

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

C. Milele.

8. Soma Mwanzo 20:1-18. Ni watu gani wawili walio tajwa katika simulizi hii? ___
______________________________
______________________________

9. Soma Mwanzo 20:2, 5. Ni mtu gani aliyemdanganya mwingine katika simulizi hii? ______________________________
______________________________

10. Soma Mwanzo 20:7. Naamini Mungu hakudhibitisha matendo ya Abraham. Bali Mungu alisimama na nani, Abraham au Abimelech? ____________________ Kwa nini? Soma Mwanzo 15:1, 18 na Yakobo 2:23
______________________________

11. Soma Mwanzo 20:7, 17-18. Hata kama Abraham alikuwa katika hatia, ni nani Mungu alimwambia amuombee mwingine?
    A. Abraham amuombee Abimelech.
    B. Abimelek amuombee Abraham.
    C. Wote waombeane.

12. Soma Warumi 8:31. Hata kama wakati mwingine tunashindwa, nanai yuko upande wetu? ______________________________
______________________________

13. Soma Warumi 4:8. Hata kama tunafanya makosa, Mungu alisema hatafanya nini?
______________________________
______________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

upate kuishi. Bali usipomrudisha, fahamu ya kwamba kwa hakika utakufa wewe na watu wote ulio nao.[ 8] Abimeleki akaamka asubuhi na mapema, akawaita watumwa wake wote, akawaambia maneno hayo yote masikioni mwao, nao watu hao wakaogopa sana. [9] Kisha Abimeleki akamwita Ibrahimu, akamwambia, Umetutenda nini? Nimekukosa nini, hata ukaleta juu yangu na juu ya ufalme wangu dhambi kuu? Umenitenda matendo yasiyotendeka. [10] Abimeleki akamwambia Ibrahimu, Umeona nini hata ukatenda jambo hili? [11] Ibrahimu akasema, Kwa sababu naliona, Yakini hapana hofu ya Mungu mahali hapa, nao wataniua kwa ajili ya mke wangu. [12] Naye kweli ni ndugu yangu, binti wa baba yangu ila siye mwana wa mama yangu, ndipo akawa mke wangu. [13] Ikawa hapo Mungu aliponisafirisha kutoka nyumba ya baba yangu, nikamwambia, Hii ndiyo fadhili yako, utakayonifanyia. Kila mahali tuingiapo, useme, Huyu ni ndugu yangu. [14] Basi Abimeleki akatwaa kondoo, na ng'ombe, na watumwa, na wajakazi, akampa Ibrahimu, akamrudishia Sara mkewe. [15] Abimeleki akasema, Nchi yangu iko mbele yako, kaa upendapo. [16] Naye akamwambia Sara, Tazama! Nimempa ndugu yako fedha elfu, itakuwa kifunika macho kwako mbele ya wote walio pamoja nawe, nawe utakuwa na haki mbele ya watu wote. [17] Ibrahimu akamwomba Mungu, Mungu akamponya Abimeleki, na mkewe, na wajakazi wake, nao wakazaa wana. [18]Maana Bwana alikuwa ameyafunga matumbo ya watu wa nyumbani mwa Abimeleki, wasizae, kwa ajili ya Sara mkewe Ibrahimu.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

14. Soma Waebrania 8:12-13. Katika agano jipya, Mungu aliahidi hatafanya nini?
    ______________________________
    ______________________________

15. Soma Waefeso 2:5, 8-9. Tunaokolewaje?
    ______________________________
    ______________________________

16. Soma Tito 3:5. Hatuokolewi kwa? ________ ______________________________ Bali tunaokolewa kwa? ____________________
    ______________________________

17. Soma Waefeso 1:6. Tutamsifu Mungu wakati wote katika umilele kwa kutuokoa kwa ________________. Maana ametufanya _______________ katika mwanawe mpendwa (Yesu Kristo ).

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Mwanzo 20:2, 5

"[2] Ibrahimu akamnena Sara mkewe, Huyu ni ndugu yangu. Basi Abimeleki mfalme wa Gerari akapeleka watu akamtwaa Sar [5] Je! Hakuniambia mwenyewe, Huyu ni ndugu yangu? Na mwanamke mwenyewe naye alisema, Huyu ni ndugu yangu. Kwa ukamilifu wa moyo wangu, na kwa kuwa safi mikono yangu, nimefanya hivi.."

### Mwanzo 20:7

"Basi sasa umrudishe mwanamke kwa mtu huyo, maana yeye ni nabii, naye atakuombea, upate kuishi. Bali usipomrudisha, fahamu ya kwamba kwa hakika utakufa wewe na watu wote ulio nao."

### Mwanzo 15:1, 18

"[1] Baada ya mambo hayo neno la Bwana likamjia Abramu katika njozi, likinena, Usiogope, Abramu, Mimi ni ngao yako, na thawabu yako kubwa sana [18] Siku ile Bwana akafanya agano na Abramu, akasema, Uzao wako nimewapa nchi hii, kutoka mto wa Misri mpaka huo mto mkubwa, mto Frati,."

### Yakobo 2:23

"Maandiko yale yakatimizwa yaliyonena, Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki; naye aliitwa rafiki wa Mungu.."

# MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

## Mwanzo 20:7, 17-18

"[7] Basi sasa umrudishe mwanamke kwa mtu huyo, maana yeye ni nabii, naye atakuombea, upate kuishi. Bali usipomrudisha, fahamu ya kwamba kwa hakika utakufa wewe na watu wote ulio nao.. [17] Ibrahimu akamwomba Mungu, Mungu akamponya Abimeleki, na mkewe, na wajakazi wake, nao wakazaa wana. [18] Maana Bwana alikuwa ameyafunga matumbo ya watu wa nyumbani mwa Abimeleki, wasizae, kwa ajili ya Sara mkewe Ibrahimu.."

## Warumi 8:31

"Basi, tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu??"

## Warumi 4:8

"Heri mtu yule ambaye Bwana hamhesabii dhambi.."

## Waebrania 8:12-13

"[12] Kwa sababu nitawasamehe maovu yao, Na dhambi zao sitazikumbuka tena. [13] Kwa kule kusema, Agano jipya, amelifanya lile la kwanza kuwa kuukuu. Lakini kitu kianzacho kuwa kikuukuu na kuchakaa ki karibu na kutoweka."

## Waefeso 2:5, 8-9

"[5] hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema;) [8] Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; [9] wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."

## Tito 3:5

"si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu;."

## Waefeso 1:6

"Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha katika huyo Mpendwa."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Ni mahusiano ya aina gani mtu huyu atakuwa nayo na familia yake wakati mambo kama haya yanaendelea? **Mahusiano yasiyo na msamaha, yenye uchungu na hasira**.
2. Soma Waebrania 10:1. Sheria yaweza kufanya nini? **Kuwafanya wanaoabudu kuwa wakamilifu (wasiyo na mawaa** ).
3. Soma Waebrania 10:1. Mstari huu unasema nini ambalo linatupa kiashiria kwamba dhabihu za agano la kale hazikutosha kutufanya wakamilifu? **Waliendelea, – kila siku, kila juma, kila mwezi. Ukweli kwamba zilikuwa zinatolewa kila wakati unatuambia kwamba hazikuweza kukabili tatizo la dhambi.**
4. Soma Waebrania 10:2. Kama dhabihu ilikuja ili kukabiliana na dhambi, itafanya nini kwa wale wanaoabudu? **Ingeweza kusababisha wao kutokuwa na moyo wa kuwa na hatia tena ya dhambi (mar azote wanaangushwa chini na kushindwa).**
5. Yule dereva mlevi alilazimika kufanya nini? **Kufikiri kuhusu dhambi mar azote.**
6. Soma Waebrania 10:14. Mungu huwakamilisha watu wake kwa:
   **D. sadaka (dhabihu) ya Yesu.**
7. Soma Waebrania 10:14. Yesu' sadaka yake (ikipokelewa kwa Imani) hukamilisha wale wanaoamini: **C. Milele**
8. Soma Mwanzo 20:1-18. Ni watu gani wawili walio tajwa katika simulizi hii?
   **Abraham na Abimelech.**
9. Soma Mwanzo 20:2, 5. Ni mtu gani aliyemdanganya mwingine katika simulizi hii?
   **Abraham**
10. Soma Mwanzo 20:7. Naamini Mungu hakudhibitisha matendo ya Abraham. Bali Mungu alisimama na nani, Abraham au Abimelech? **Abraham** Kwanini? Soma Mwanzo 5:1, 18 na Yakobo 2:23. **Kwa sababu Abraham alikuw ana agano na Mungu na alikuwa rafiki wa Mungu.**
11. Soma Mwanzo 20:7, 17-18. Hata kama Abraham alikuwa katika hatia, ni nani Mungu alimwambia amuombee mwingine? **A. Abraham amuombee Abimelek**
12. Soma Warumi 8:31. Hata kama wakati mwingine tunashindwa, nanai yuko upande wetu?
    **Mungu**
13. Soma Warumi 4:8. Hata kama tunafanya makosa, Mungu alisema hatafanya nini?
    **Kutuhesabia dhambi.**

14. Soma Waebrania 8:12-13. Katika agano jipya, Mungu aliahidi hatafanya nini?
**Mungu hatakumbuka dhambi zetu au kutuhesabia hatia**

15. Soma Waefeso 2:5, 8-9. Tunaokolewaje? **Kwa Imani. Kwa neema yake tusiostahili**

16. Soma Tito 3:5. Hatuokolewi kwa? **kwa kazi za haki tulizofanya** Bali tunaokolewa kwa? **Kutegemeana na rehema zake,alituosha kwa kuzaliwa upya, na kutufanya upya kwa Roho wake Mtakatifu.**

17. Soma Waefeso 1:6. Tutamsifu Mungu wakati wote katika umilele kwa kutuokoa kwa **Neema**. Maana ametufanya **Kukubalika** kupitia mwanawe mpendwa (Yesu Kristo ). .

# SOMO 11
# MIMI NAPENDWA, MIMI NI MZURI

*Na Don Krow*

Siku moja, Michael alikuja ofisini kwangu ili aniambie habari za siri sana kuhusu mmoja wapo wa wanafunzi wenzake. Wakati nafundisha kwenye kipindi katika chuo cha Biblia cha Charis, inaonekana kwamba Patricia alikuwa anaandika muhtasari katika daftari lake. Muhtasari huu ulikuwa na maandishi haya: "Mimi Napendwa, Mimi ni Mzuri," n.k. Patricia alikuwa aina ya mtu ambaye aanavaa nguo ambazo zinasababisha watu kumuangalia. Sababu kuu iliosababisha Patricia aandike maneno haya ilikuwa kwamba alijihisi yey ni mtu asiyependwa na hakujihisi yeye ni mzuri, bali alijisikia kutopendwa na kwamba yeye si mzuri.

Kama wanadamu, wote tunamahitaji ya msingi yanayofanana – Matamanio ya kupendwa, kukubalika, na kuthaminiwa, na pia hali ya kuwa na thamani na kujua kwamba tuko sawa na Mungu. Dini nyingi leo zinafanya tujisikie hatupendwi, hatuthaminiki, na pia hatukubaliki. Moja ya ngome kubwa ya Shetani anayotumia ni kutufanya tuwe na hatia na kuhukumiwa, Wakati wote tunajisikia wakiroho kuhusu hili.

Swali ni Hili: Wangapi kati yenu, mlipokuja kwa Yesu kwa mara ya kwanza mliambiwa kwamba si tu anawapenda, bali kwa kumkubali, atakufanya kuwa mwenye haki mkamilifu? Kiuhalisi, Haki ambayo angeiachilia itakuwa haki yote ambayo utaihitaji (1 Wakor. 1:30 inasema, *"Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi;")*. Hii ni habari njema ya Injili: (Warumi 1:16-17). *"Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia. [17] Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa, Mwenye haki ataishi kwa imani."* (Warumi. 4:5). Mungu hakutuita tuwe na imnai katika imnai au Imani ya vitu, bali ujasiri, wa kumtegemea na kumuamini Yeye.

Mungu hawezi kukupenda zaidi ya jinsi ambavyo anakupenda tayari. Yeye ni Pendo (1 Yohana 4:8). Bali unaweza kupokea zaidi, kuuhisi zaidi, na uwepo wa upendo zaidi. Kadri ya jinsi unavyoamini, ndivyo utakavyo jikuta unampenda Mungu zaidi. Maandiko yanasema, *"Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza."* (1 Yoh 4:19). Fikiri kuhusu hili, lianmini, na ulipokee!

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Mtume Paulo alikuwa ameshawishika kuhusu ? ______________________________
____________________________________

2. Wakati nilikuwa chuo cha Biblia , nilikuwa na mkufunzi ambaye aliwahi kutugawia makaratasi yenye matamko haya : "Haki ni kitendo cha kisheria ambacho Mungu anatamka haki kwa yeyote aaminiye si humfanya mwenye Haki." Wakati najifunza maandiko mwenyewe , nilishawishika kwamba kuhesabiwa Haki ni karama inayokufanya kuwa mwenye haki mbele za Mungu . Soma Warumi 5:19. Kupitia Utii wa Yesu (kwa kutii sheria na kwenda msalabani ), wengi wata:

   A. tamkwa wenye haki

   B. watafikiriwa kuwa wenye haki

   C. watafanywa wenye haki

3. Soma 2 Wakorintho 5:21. "Kwa kuwa yeye [Mungu] amemfanya [Yesu Kristo] kuwa dhambi kwa ajili yetu, ambaye hakujua dhambi [Hakuwahi kufanya dhambi]; ili tuwe ________________________________
____________________________".

4. Soma Wakolosai 1:21-22. Yesu alikuja duniani na kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Kwa sababu ya hili , tunasimama katika uwepo wa Mungu kama watu ambao ni watakatifu , pasipo makossa wala hatia katika :

   A. Mbele za mwenzi wako

   B. Mbele za marafiki

   C. Mbele za Mungu

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Warumi 8:38-39

"[38] Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, 39 wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.."

### Warumi 5:19

"Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki.."

### 2 Wakorintho 5:21

"ili kwamba, kama vile dhambi ilivyotawala katika mauti, vivyo hivyo kwa njia ya haki neema itawale hata uzima wa milele kwa Yesu Kristo Bwana wetu.

### Wakolosai 1:21-22

"[21] Na ninyi, mliokuwa hapo kwanza mmefarikishwa, tena adui katika nia zenu, kwa matendo yenu mabaya, amewapatanisha sasa; [22]katika mwili wa nyama yake, kwa kufa kwake, ili awalete ninyi mbele zake, watakatifu, wasio na mawaa wala lawama"

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

5. Soma Waefeso1:6. Tutamsifu Mungu katika umilele kwa Neema maana ametufanya __________________________ __________________________.

6. Soma Waebrania 10:14. Kupitia Kristo na dhabihu alioitoa msalabani , tumefanywa wakamilifu kwa muda gani?

   A. Hadi ufanye dhambi tena

   B. Hadi uende kanisani

   C. Milele

7. Soma Waebrania 10:15-17. Katika agano jipya , Mungu anaahidi kukumbuka dhambi zetu:

   A. kila wakati tunapotenda dhambi

   B. wakati hatulipi zaka zetu

   C. hakumbuki tena

8. Soma Warumi 6:1-2. Neema ya Mungu ni kuu zaidi ya dhambi zetu. Je tuendelee kwenye dhambi ili Neema ya Mungu ionekane zaidi kwetu ?

   ______________________________

9. Soma Waebrani 9:12. Ni ukombozi wa Aina gani (uhuru kutokana na adhabu ya dhambi zetu ) ambao Yesu alitupatia ?

   A. Wa muda mfupi

   B. Wa sehemu tu

   C. Wa milele

10. Soma Warumi 8:33. Taja mtu ambaye anaweza kuhukumu wateule wa Mungu .

    ____________________________________

    __________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Waefeso 1:6

"Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha katika huyo Mpendwa."

### Waebrania 10:14

"Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.."

### Waebrania 10:15-17

"[15] Na Roho Mtakatifu naye amshuhudia; kwa maana, baada ya kusema, [16] Hili ni agano nitakaloagana nao baada ya siku zile, anena Bwana, Nitatia sheria zangu mioyoni mwao, Na katika nia zao nitaziandika; ndipo anenapo, [17] Dhambi zao na uasi wao sitaukumbuka tena kabisa.."

### Warumi 6:1-2

"[1] Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? [2] Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi??"

### Waebrania 9:12

"wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika Patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele.."

### Warumi 8:33

"Ni nani atakayewashitaki wateule wa Mungu? Mungu ndiye mwenye kuwahesabia haki.."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

11. Soma Warumi 8:34. Taja mtu ambaye anaweza kuhukumu (maana yake, kuleta hukumuni ) watu wa Mungu . ______________________________________________

12. Soma Warumi 8:35. Taja mtu ambaye anayeweza kutenganisha Wakristo toka kwenye Upendo wa Mungu . ______________________________________________

13. Soma Warumi 8:31. Hitimisho la somo hili la uanafunzi ni nini? ______________________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Warumi 8:34

"Ni nani atakayewahukumia adhabu? Kristo Yesu ndiye aliyekufa; naam, na zaidi ya hayo, amefufuka katika wafu, naye yuko mkono wa kuume wa Mungu; tena ndiye anayetuombea.."

### Warumi 8:35

"Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je! Ni dhiki au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga?"

### Warumi 8:31

"Basi, tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?"

# MWONGOZO WA MAJIBU

1. Mtume Paulo alikuwa ameshawishika kuhusu? Alishawishika kwamba hakuna kinachoweza kututenganisha na upendo wa Mungu – si uzima wala mauti, malaika au roho , wakati ulioko wala ujao , mamlaka iliyo juu wala chini . Hakuna kinachoweza kututenga na upendo wa Mungu unaopatikana katika Kristo Yesu Bwana wetu.

2. Wakati nilikuwa chuo cha Biblia , nilikuwa na mkufunzi ambaye aliwahi kutugawia makaratasi yenye matamko haya : "Haki ni kitendo cha kisheria ambacho Mungu anatamka Haki kwa yeyote aaminiye  si humfanya mwenye Haki." Wakati najifunza maandiko mwenyewe , nilishawishika kwamba kuhesabiwa" Haki ni karama inayokufanya kuwa mwenye haki mbele za Mungu . Soma Warumi 5:19. Kupitia Utii wa Yesu (kwa kutii sheria na kwenda msalabani ), wengi wata: C. fanywa wenye haki.

3. Soma 2 Wakorintho 5:21. "Kwa kuwa yeye [Mungu] amemfanya [Yesu Kristo] kuwa dhambi kwa ajili yetu, ambaye hakujua dhambi [Hakuwahi kufanya dhambi]; ili tufanyike wenye haki mbele za Mungu katika Kristo" .

4. Soma Wakolosai 1:21-22. Yesu alikuja duniani na kufa kwa ajili ya dhambi zetu . Kwa sababu ya hili , tunasimama katika uwepo wa Mungu kama watu ambao ni watakatifu , pasipo makossa wala hatia katika :C. Mbele za Mungu.

5. Soma Waefeso1:6. Tutamsifu Mungu katika umilele kwa Neema maana ametufanya tunakubalika katika mwana mpendwa (ambaye ni, Kristo).

6. Soma Waebrania 10:14. Kupitia Kristo na dhabihu alioitoa msalabani , tumefanywa wakamilifu kwa muda gani?C. Milele

7. Soma Waebrania 10:15-17. Katika agano jipya , Mungu anaahidi kukumbuka dhambi zetu:: C. hakumbuki tena.

8. Soma Warumi 6:1-2. Neema ya Mungu ni kuu zaidi ya dhambi zetu. Je tuendelee kwenye dhambi ili Neema ya Mungu ionekane zaidi kwetu ? Mungu epusha . Hapana!

9. Soma Waebrani 9:12. Ni ukombozi wa Aina gani (uhuru kutokana na adhabu ya dhambi zetu ) ambao Yesu alitupatia? C. wa Milele

10. Soma Warumi 8:33. Taja mtu ambaye anaweza kuhukumu wateule wa Mungu :Hakuna.

11. Soma Warumi 8:34. Taja mtu ambaye anaweza kuhukumu (maana yake , kuleta hukumuni ) watu wa Mungu . Hakuna.

12. Soma Warumi 8:35. Taja mtu ambaye anayeweza kutenganisha Wakristo toka kwenye Upendo wa Mungu Hakuna.

13. Soma Warumi 8:31. Hitimisho la somo hili la uanafunzi ni nini?? Mungu yuko upande wetu hakuna anayeweza kuwa kinyume nasi

DARAJA 3

# SOMO 12
# TUNDA LA WOKOVU (Sehemu 1)

*na Don Krow*

Je kitendo kimoja cha Imani "kinaokoa" kama haiendelei ? Je kinaweza kukoma nab ado kikafikia kupokea ahadi ? Abraham alimwamini Mungu na ikahesabiwa kwake kama haki (Mwanzo. 15:6). Kama Imani ya Abrahamu ingalikoma (ikaisha), je ile haki aliohesabiwa ingekoma?

Kutoka katika maandiko , tunajua kwamba "Imani " huanza na kitendo kikamilifu (aorist tense) bali huendelea katika maisha ya mkristo kama inavyoelezewa katika kiyunani wakati uliopo. Amri zinazotolewa katika wakati ulioko zinategemewa kuwa na kisifa cha muendelezo , au cha kurudia , utendaji. Wakati unatumia sifa za wakati uliopo , kama tungalitoa maneno yafuatayo au matamko kwa msomaji wa Biblia , bila shaka tungaliongeza uelewa wake kuhusu hayo maandiko katika Biblia . Maneno haya ni : kwa kurudia ; maana yake,tene na tena , kwa muendelezo, daima, isiobadilika ,kikawaida ,kama tabia au mazoea, au pasipo kuingilia .

Rejea maandiko yafuatayo na jinsi lugha ya kuyunani ilivyo yaathiri kwa ajili ya visifa vya hali ilioko:

Yohana 3:16 – Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye (hali ilioko: anaamini na kuendelea kuamini ) asipotee, bali awe na uzima wa milele .

Waebrania 10:14 – Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa (Wakati uliopo: wale walio tengwa na kuendelea kutengwa , kwamba dhabihu moja imeendelea kukamilisha milele. Toleo la New King James Version linasema "Kutakaswa." Toleo la New International Version linasema "kufanywa watakatifu .").

1 Yohana 3:9 – Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake;. (wakati uliopo: asiyeendelea kufanya dhambi na kuwa ndiyo sehemu ya maisha , kuonyesha hali ya kutokuwa na toba) wakati ulioko : mbegu ya Mungu inadumu na

kuendelea ) wala hawezi kutenda dhambi (wakati ulioko: kama mwenendo wa maisha yake ) kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu .

Marko 1:15 – akisema, Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na. (wakati uliopo: tubu na kuendelea kutubu kila wakati ) (wakati uliopo: amini na uendelee kuamini ) kuiamini Injili .

Yohana 5:24 – Amin, amin, nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani. (wakati uliopo: na kuendelea kuamini ).

Luka 15:7 – Nawaambia, Vivyo hivyo kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye, kuliko kwa ajili ya wenye haki tisini na kenda ambao hawana haja ya kutubu (wakati uliopo : na kuendelea katika toba ),

Matendo 17:30 – Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza (Wakati uliopo : na kuendelea kutoa amri ) watu wote wa kila mahali watubu. (wakati uliopo : na kuendelea katika toba ).

Yohana 6:47 – Amin, amin, nawaambia, Yeye aaminiye yuna uzima wa milele. (wakati uliopo: na kuendelea kuamini .

Warumi 4:5 – Lakini kwa mtu asiyefanya kazi, bali anamwamini (wakati uliopo : na kuendelea kuamini ) yeye ambaye amhesabia haki asiyekuwa mtauwa, imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki .

Matendo 26:20 – bali kwanza niliwahubiri wale wa Dameski na Yerusalemu, na katika nchi yote ya Uyahudi, na watu wa Mataifa, kwamba watubu na,. (wakati uliopo : na kuendelea kutubu ) (wakati ulioko : na kuendelea kugeuka ) kumwelekea Mungu (wakati uliopo :na kuendelea kufanya matendo ,yanayo thibitisha toba yako) wakiyatenda matendo yanayopatana na kutubu kwao .

Uhitimisho: Kisifa cha wakati uliopop kimetumika mara mamia kwenye Biblia.Si nia yangu kuonyesha mambo yote yanayohusiana na mjadala huu.ukweli kuhusu Imani inayookoa ni kwamba ni yenye kuendelea na hufundishwa na wote wawili kwenye theologia ya Waarmani na Kalvari.

Ukalvari, ambao unakiri usalmawa nje , hufundisha kwamba waumini wanaweza kujikwa ana kuanguka , bali bado watahifadhiwa katika Imani ya Kristo (1 wakor. 1:8). To Wale wanaoamini katika usalama wa milele huamini kwamba wa kristo wa kweli wamepitia kifo kitokanacho na dhambi na hawaendelei katika hiyo (Warumi. 6:1-3). Wale ambao baadaye

wangegeuka kinyume na Kristo ,wanaonyesha kwamba hawakuwa wameokoka kikamilifu (1 Yohana 2:19).

Teknolojia ya waarminia inatufundisha kwamba waumini wa kweli wanaweza kuasi Imnai ya Kikristo . Wanaamini na kufundisha kwamba wale walioanguka katika Imani, au wanaoasi , wokovu wao. Mfumo wao hauachi nafasi kwa ajili ya Ukristo (wale wa jina) kuishi katika uasi au dhabi kwa makusudi pasipo matunda yanayothibitisha toba yao.

Mtume Yohana anasema "Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu." (1 Yohana 1:8), bali pia alisema , "Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu."

(1 Yoh 3:9). Hapa tuna fumbo , bali lisilo na mwendelezo wa kimaandiko. Wakristo wote hutenda dhambi (1 Yoh 1:8), bali Wakristo pia hutii (1 Yoh 2:3). Dhambi na ubinadamu bado upo katikati ya Wakristo , bali haiwezi kuwatawala au tabia ya kuwatofautisha (1 Yoh 3:9). Toba ya kweli na imani inahitaji nia iliobadilika , moyo uliobadilika, mwelekeo uliobadilika , hata kama si utimilifu (Matendo 26:18 na 1 Yoh 1:8). "Tunda" bado ni jaribu la uhalisi wa Imani na uhalisi . Imani ni ushawishi wa kimungu unaaoongoza tabia za waumini wa kweli na kuleta matokeo katika matendo yatokanayo . Hili linaonekana katika mifano ya Imani katika kiebrania , Sura 11, iletayo matokeo ya matendo yatokanayo. Kwa maneno mengine , tunachofanya ni matokeo ya kile tunachoamini. Kityabu cha Yakobo 2:18 kinasema, "Lakini mtu atasema, Wewe unayo imani, nami ninayo matendo. Nionyeshe imani yako pasipo matendo, nami nitakuonyesha imani yangu kwa njia ya matendo yangu.."

Wakati mitume wanaongea katika njia hasi kuhusu njia za kimaisha , wanarejea "kazi za sharia "; ni kwamba , chochote ambacho mtu anafanya ili kupata , au kufanyia kazi , wokovu wao.

Maandiko pia yanaongelea kuhusu tunda la wokovu , ambalo ni kazi njema , au kazi ya Imani . Hizo ni kazi , au matendo , ambayo yanatokana na toba na Imani (Matendo 26:20, Math 3:7-10, 1 Wathesa. 1:3, na Yakobo 2:14-26), wanaonyesha uthibitisho wa wokovu. Umoja unaoonekana kwenye dhambi na Imani ni kwamba vyote vina Tunda swa au uthibitisho sawa. Hatuokolewi kwa matendo mema , bali twaokolewa ili tuwe na matendo mema (Waefeso. 2:8-10 kwa ajili ya kutofautisha kuokoka kwa na ili tuwe ). Kazi ni jaribu la uhalisi wa Imani , na neema ambayo hatimaye haigusi maisha ya muhusika na matendo hayawezi kueleweka kama neema ya kweli ya Mungu (Tito 2:11-12). Yesu anafundisha hilo kuhusu matunda, waumini wa kweli watajulikana (Math. 3:8, 7:16-20, 25:34-40; Yoh 13:35, 14:23; Matendo 26:20; Warumi. 2:6-11; Yakobo 2:14-18; na 1Yohana 3:10).

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Amri zinazotolewa katika kisisfa cha wakati uliopo zinatarajiwa kuwa na ______ ________________________________ ______________________________.

2. Soma Yohana 3:16. Kutegemeana na kisifa cha wakati ulipo katika lugha ya kuyunani , Yohana 3:16 inasemaje? _______________ ________________________________ ______________

3. Soma 1 Yohana 3:9. Yeyote aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi. Hili linamaana gani? ______________________________ ________________________________

4. Soma Luka 15:7. Kuna furaha mbinguni mtu mmoja mwenye dhambi akitubu kwamba ____________________________ ________________________________.

5. Soma Matendo 17:30. Mungu ana amrisha watu wote kila mahali ________________ ________________________________ __________________.

6. Soma Matendo 26:20. Andiko hili linasema nini ? ______________________________ ________________________________

7. Soma 1 Yoh 2:3. Ni nini matokeo ya kuwa na mahusiano binafsi na Mungu , ni kusema , kumjua Mungu ? ____________ ________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Yohana 3:16

"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.."

### 1 Yohana 3:9

"Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake wakaa ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu."

### Luka 15:7

"Nawaambia, Vivyo hivyo kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye, kuliko kwa ajili ya wenye haki tisini na kenda ambao hawana haja ya kutubu."

### Matendo 17:30

"Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu."

### Matendo 26:20

"Bali kwanza niliwahubiri wale wa Dameski na Yerusalemu, na katika nchi yote ya Uyahudi, na watu wa Mataifa, kwamba watubu na kumwelekea Mungu, wakiyatenda matendo yanayopatana na kutubu kwao."

### 1 Yohana 2:3

"Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake.."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

8. Soma Yakobo 2:18. Yakobo anasema, "Nionyeshe Imani yako pasipo matendo (haiwezekani), na mimi ni takuonyesha imani kwa ______________________________."

9. Soma 1 Wathessalonike 1:3. Kazi au Matendo, yanayotokana na Imnai yanajulikana kama ______________________ ________________________________________ ______________.

10. Soma Wagalatia 2:16, 21. Kazi ya sharia ni kazi watu wanazofanya ili kujaribu kupata wokovu au ________________________ (mstari 21). Haziwezi kuokoa , hazina nguvu ya kuleta wokovu .

11. Soma Warumi 2:7-10. Mistari hii inaelezea matunda toka kwa makundi mawili ya watu? __________________________________ ______________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Yakobo 2:18

"Lakini mtu atasema, Wewe unayo imani, nami ninayo matendo. Nionyeshe imani yako pasipo matendo, nami nitakuonyesha imani yangu kwa njia ya matendo yangu.."

### 1 Wathesalinike 1:3

"Wala hatuachi kuikumbuka kazi yenu ya imani, na taabu yenu ya upendo, na saburi yenu ya tumaini lililo katika Bwana wetu Yesu Kristo, mbele za Mungu Baba yetu."

### Wagalatia 2:16, 21

"[16] hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu; sisi tulimwamini Kristo Yesu ili tuhesabiwe haki kwa imani ya Kristo, wala si kwa matendo ya sheria; maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki. [21] Siibatili neema ya Mungu; maana, ikiwa haki hupatikana kwa njia ya sheria, basi Kristo alikufa bure.."

### Warumi 2:7-10

"[7] wale ambao kwa saburi katika kutenda mema wanatafuta utukufu na heshima na kutokuharibika, watapewa uzima wa milele; [8] na wale wenye fitina, wasioitii kweli, bali wakubalio dhuluma, watapata hasira na ghadhabu; [9] dhiki na shida juu ya kila nafsi ya mwanadamu atendaye uovu, Myahudi kwanza na Myunani pia; [10] bali utukufu na heshima na amani kwa kila mtu atendaye mema, Myahudi kwanza na Myunani pia."

# MWONGOZO WA MAJIBU

1. Amri zinazotolewa katika kisifa cha wakati uliopo zinatarajiwa kuwa na muendelezo, au marudio, zenye kutumika .

2. Soma Yohana 3:16. Kutegemeana na kisifa cha wakati ulipo katika lugha ya kuyunani , Yoh 3:16 inasemaje? Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanawe wa pekee , ili kila amuaminiye (wakati uliopo ;anayeamini na kuendelea kuanmini )asipotee bali awe na uzima wa milele .

3. Soma 1 Yoh 3:9. Yeyote aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi. Hili linamaana gani? Yeyote aliyezaliwa na Mungu (wakati uliopo : haendelei kutenda dhambi kama mwenendo wa maisha , kuonyesha moyo usio na toba ) hatendi dhamibi.

4. Soma Luka 15:7. Kuna furaha mbinguni mtu mmoja mwenye dhambi akitubu na kuendelea kutubu.

5. Soma Matendo 17:30. Mungu ana amrisha watu wote kila mahali watubu na kuendelea kutubu.

6. Soma matendo 26:20. Andiko hili linasema nini ? bali kwanza niliwahubiri wale wa Dameski na Yerusalemu, na katika nchi yote ya Uyahudi, na watu wa Mataifa, kwamba watubu na kumwelekea Mungu, (wakati ulioko: na kuendelea kugeuka ) , wakiyatenda (Wakati ulioko : na kuendelea kufanya kazi au matendo yanayo thibitisha toba yako) matendo yanayopatana na kutubu kwao. .

7. Soma 1 Yoh 2:3. Ni nini matokeo ya kuwa na mahusiano binafsi na Mungu , ni kusema , kumjua Mungu ? Kufanya kile anacho agiza , na kutii amri zake

8. Soma Yakobo 2:18. Yakobo anasema, “Nionyeshe Imani yako pasipo matendo (haiwezekani), na mimi ni takuonyesha imani kwa, kazi, au katika yale nayoyafanya”

9. Soma 1 Wathessalonike 1:3. Kazi au Matendo, yanayotokana na Imani yanajulikana kama kazi zinazofanyika kwa imani

10. Soma Wagalatia 2:16, 21. Kazi ya sharia ni kazi watu wanazofanya ili kujaribu kupata wokovu au haki (mstari 21). Haziwezi kuokoa , hazina nguvu ya kuleta wokovu .

11. Soma Warumi 2:7-10. Mistari hii inaelezea matunda toka kwa makundi mawili ya watu? Waumini na wasio amini

# SOMO 13
# TUNDA LA WOKOVU (Sehemu 2)

*Na Don Krow*

Tambua maandiko haya: "Katika hili watoto wa Mungu ni dhahiri, na watoto wa Ibilisi nao. Mtu ye yote asiyetenda haki hatokani na Mungu, wala yeye asiyempenda ndugu" (1 Yoh 3:10, New International Version). hakusema, "Hivi ndivyo tunavyojiokoa." inasema, "Katika hili watoto wa Mungu ni dhahiri …" (1 Yoh 3:10, msisitizo ).

Yesu alisema hivi, "Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua" (Mathayo. 7:20, msisitizo).

Katika Maandiko , Mungu huongelea wokovu kwa njia mbili: (1) wokovu ni kwa neema kwa njia ya Imani (Waefeso. 2:8-9) na (2) kutegemeana na kazi njema ambazo kila mtu aliyeokoka anafanya (Waefeso. 2:10). Kwanini tunaogopa kuongea kuhu Tunda la muumini? Biblia haijajifunika kuhusiana na mada hii .Hivi ndivyo tunavyoweza kujua tuko kwenye ufalme wa Mungu na chini ya utawala wa Mungu:

1 Yohana 2:3-5 – [3] Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake. [4] Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake. [5] Lakini yeye alishikaye neno lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli. Katika hili twajua ya kuwa tumo ndani yake.

Kama mkijua ya kuwa yeye ni mwenye haki, jueni ya kuwa kila atendaye haki amezaliwa na yeye. (1 Yoh 2:29). (Je hili linaleta maana? Asili ya Mungu na kristo ni haki, na kila anayefanya haki anatoa uthibitisho wa ushiriki wa asili ya Mungu au, kama Yohana asemavyo , amezaliwa katika yeye).

1 Yohana 3:5-10 – [5] Nanyi mnajua ya kuwa yeye alidhihirishwa, ili aziondoe dhambi; na dhambi haimo ndani yake. [6] Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi; kila atendaye dhambi hakumwona yeye, wala hakumtambua. [7] Watoto wadogo, mtu na asiwadanganye; atendaye haki yuna haki, kama yeye alivyo na haki; [8] atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi. [9] Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wake

wakaa ndani yake; wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa kutokana na Mungu. [10] Katika hili watoto wa Mungu ni dhahiri, na watoto wa Ibilisi nao. Mtu ye yote asiyetenda haki hatokani na Mungu, wala yeye asiyempenda ndugu yake.. (Yohana anasema, "Hivi ndivyo jinsi tujuavyo nani ni mtoto wa Mungu na mtoto wa yule mwovu." Wale ambao hawatendi haki na kuwa na upendo wanaonyesha kuwa hawana asili yay a Baba. Je uthibitisho wa kuzaliwa mara ya pili si muhimu ?)

1 Yohana 3:14 – Sisi tunajua ya kuwa tumepita toka mautini kuingia uzimani, kwa maana twawapenda ndugu. Yeye asiyependa, akaa katika mauti..

1 Yohana 4:6 – Sisi twatokana na Mungu. Yeye amjuaye Mungu atusikia; yeye asiyetokana na Mungu hatusikii. Katika hili twamjua Roho wa kweli, na roho ya upotevu.

1 Yohana 4:8 – Yeye asiyependa, hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni upendo. (Upendo ni alama ya tabia ,kwa kuwa asili ya Mungu ni upendo.)

1 Yohana 5:2 – Katika hili twajua kwamba twawapenda watoto wa Mungu, tumpendapo Mungu, na kuzishika amri zake (wakati uliopo: na kuendelea kumpenda ) na kuendelea kufanya (wakati uliopo: na kuendelea kutii) amri zake .

1 Yohana 5:18-19 – Twajua ya kuwa kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi; bali yeye aliyezaliwa na Mungu hujilinda, wala yule mwovu hamgusi. [19] Twajua ya kuwa sisi tu wa Mungu; na dunia yote pia hukaa katika yule mwovu..

KWA NINI MTUME YOHANA ALITUSHIRIKISHA SISI HAYA YOTE ? "Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu" (1 Yohana 5:13).

Hitimisho: Haki, Utakatifu, Upendo, tunda la Roho wa Mungu ni uthibitisho wa kuzaliwa mara ya pili (upya). Wewe mwenyewe hauna ujasiri kwamba wewe ni wa Mungu wakati unapoishi maisha yasio na utauwa. Nafsi uhukumu , na hakuna ujasiri mbele za Mungu . Mtume Petro anashauri ujitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwako na uteule wako (2 Petro. 1:10); maana yake uthibitishe moyoni mwako kwamba wewe ni wa kwake kwa kuishi maisha ambayo yanaendana na injili yenye utukufu ,sikusema "Hivi ndivyo tunavyo okolewa"; nimesema , "Hivi ndivyo tutajua kwamba sisi ni wa Mungu ."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Matendo 8:13, 18-22. Kwanza Yohana anazungumzia "tunda," au uthibitisho, wa muumini wa kweli. Haya ni maswala yanayotokana na maswala ya moyoni . Wakati moyo wa Muumini unapokuwa hauko sawa (kama Simeoni), wanapaswa kufanya nini? ______________ ______________________________________ __________________________

2. Soma 2 Petro 1:5-11. Ni Vithibitisho vipi , vitakavyo onyesha kwamba mtu ameitwa au kuteuliwa na Mungu ? ______________ ______________________________________ _________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Matendo 8:13, 18-22

"[13] Na yeye Simoni mwenyewe aliamini akabatizwa, akashikamana na Filipo; akashangaa alipoziona ishara na miujiza mikubwa inayotendeka. [18] Hata Simoni alipoona ya kuwa watu wanapewa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya mitume, akataka kuwapa fedha akisema, [19] Nipeni na mimi uwezo huu, ili kila mtu nitakayemweka mikono yangu, apokee Roho Mtakatifu. [20] Lakini Petro akamwambia, Fedha yako na ipotelee mbali pamoja nawe, kwa kuwa umedhania ya kuwa karama ya Mungu yapatikana kwa mali. [21] Huna fungu wala huna sehemu katika jambo hili, kwa kuwa moyo wako si mnyofu mbele za Mungu. [22] Basi, tubia uovu wako huu, ukamwombe Bwana, ili kama yamkini, usamehewe fikira hii ya moyo wako."

### 2 Petro 1:5-11

Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa, [6] na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa, [7] na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, upendo. [8] Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo. [9] Maana yeye asiyekuwa na hayo ni kipofu, hawezi kuona vitu vilivyo mbali, amesahau kule kutakaswa dhambi zake za zamani. [10] Kwa hiyo ndugu, jitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu; maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe. [11] Maana hivi mtaruzukiwa kwa

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

3. Soma Mathayo 25:34-40. Ni sifa zipi zimeonyeshwa na hali ya mtu kuwa muumini katika maandiko haya ? ________
____________________________________
__________________

4. Soma Yohana 13:35. Wanafunzi wa Yesu wanatambulika kwa sifa gani? __________
____________________________________
____________________________

5. Soma Mathayo 7:21-23. Kwanini watu hawa wamekataliwa kwenye ufalme wa Mungu ? ____________________________
____________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo.."

### Mathayo 25:34-40

Kisha Mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; [35] kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; [36] nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia. [37] Ndipo wenye haki watakapomjibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona una njaa, tukakulisha, au una kiu tukakunywesha? [38] Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha, au u uchi, tukakuvika? [39] Ni lini tena tulipokuona u mgonjwa, au kifungoni, tukakujia? [40] Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi.."

### Yohana 13:35

"Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.."

### Mathayo 7:21-23

"[21] Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. [22] Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi?

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

6. Soma Yohana 14:23. Kama mtu anampenda Yesu atafanya nini? ____________________________________________________________

7. Soma Matendo 26:20. Maandiko haya yanasemaje? ____________________________________________________________

8. Soma Yakobo 2:17. Kama Imani yako haina matendo mema, basi unaimani ya aina gani? ____________________________________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

[23] Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.."

### Yohana 14:23

"Yesu akajibu, akamwambia, Mtu akinipenda, atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake."

### Matendo 26:20

"bali kwanza niliwahubiri wale wa Dameski na Yerusalemu, na katika nchi yote ya Uyahudi, na watu wa Mataifa, kwamba watubu na kumwelekea Mungu, wakiyatenda matendo yanayopatana na kutubu kwao."

### Yakobo 2:17

"Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake.."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Matendo 8:13, 18-22. Kwanza Yohana anazungumzia "tunda," au uthibitisho, wa muumini wa kweli. Haya ni maswala yanayotokana na maswala ya moyoni . Wakati moyo wa Muumini unapokuwa hauko sawa (kama Simeoni), wanapaswa kufanya nini? **Tubuni kwa ajili ya dhambi zenu (uovu) na muombe kwa Mungu kwamba mawazo ya mioyo yenu yasamehewe .**

2. Soma 2 Petro 1:5-11. Ni Vithibitisho vipi , vitakavyo onyesha kwamba mtu ameitwa au kuteuliwa na Mungu? **Wanaongeza kwenye Imani yao sifa zote za Roho, sifa za hali yao ya kuwa wapya.**

3. Soma Mathayo 25:34-40. Ni sifa zipi zimeonyeshwa na hali ya mtu kuwa muumini katika maandiko haya ? **Matendo yanayotokana na Imani – Kuwapa wenye njaa chakula , ukarimu kwa wengine, kuwavika wasio na nguo, kuwajali wanao umwa, kuwafikia walioko jela n.k.**

4. Soma Yohana 13:35. Wanafunzi wa Yesu wanafahamika kwa sifa gani? **Upendo wanao onyesha moja kwa mwingine .**

5. Soma Mathayo 7:21-23. Kwanini hawa watu walikataliwa kuingia kwenye ufalme wa Mungu ? **Walikuwa watenda kazi wa uovu . Katika kiyunani , Wakati ulioko umetumika, ambalo linaonyesha haya ndio maisha yao , asili ya kwao. Yesu alisema hakuwajua . Walikuwa wanadini waliopotea ambao hawakuwahi kuw ana mabadiliko ya moyo .**

6. Soma Yohana 14:23. Kama mtu anampenda Yesu , wanatakiwa wafanye nini? **Shika maneno yake , au fanya anachosema.**

7. Soma Matendo 26:20. Andiko hili linasemaje? **Thibitisha toba yako kwa matendo yako.**

8. Soma Yakobo 2:17. Kama Imani yako haina matendo mema , inamaana una Imani ya aina gani? **Imani iliokufa, Ambayo haiwezi kuokoa (Yakobo 2:14).**

DARAJA 3

# SOMO 14
# WITO WA KUWA MFUASI WA YESU

*na Andrew Wommack*

Leo tutaongelea kuhusu kuwa mfuasi wa Yesu na jinsi ya kuwafanye wengine kuwa wanafunzi wa Yesu . Nataka nikukumbushe kwamba Bwana alitupa agizo si tu kuwafanya watu kuokoka au kuwafanya wamkiri Yesu na kupokea msamahawa Dhambi pekee hapana ,Bali kuwafanya watu kuwa wanafunzi wa Yesu. Ingawa hayo mawili ni ya muhimu ,sijaribu kudharau haya kabisa, madhumuni yanatakiwa kwenda zaidi ya kuokoka na kuelekea kwenye kukomaa. Lengo la mkristo , ambaye ni mwanafunzi wa Yesu , linatakiwa kuwa ni kwenda na kuwafanya watu kuwa wanafunzi wa Yesu .

Yesu alituambia tufanye watu kuwa wanafunzi wake, kuwaleta watu katika hali ya kukomaa na wawe na uwezo wa kuzaa. Dunia ya Kanisa letu leo haijafanya hivi. Tumeweka jukumu hili la kuwafanya watu waokoke kwa watumishi wachache . Tuna wainjilisti wanaosafiri huku na kule, na kuwa na mikutano mikubwa ya injili , na kuona maelfu ya watu wakifanya uamuzi wa kumpokea Bwana. Ingawa baadhi yao wanakuwa hawajaokoka kiuhalisi bali wanakuwa wamepatwa na hisia tu, Ninauhakika kuna watu ambao wameokoka kweli na wanamahusinao na Bwana. Mara nyingi , hatahivyo , hakuna msisitizo wakuendelea na kuwa mwanafunzi wa Yesu , na si njia ambayo Mungu alitamani iwe.

Nafananisha hili na mtu anayependa watoto . Itakuwa hali ya kutokuwa muwajibikaji kwa kuwa na mtoto , na kumfurahia , bali kwa kumuona tu amezaliwa. Unapokuwa na mtoto , lazima ukubali mtoto na majukumu yake ya kumkuza na kumlea. Tunawaambia watu , “Swala la msingi ni kuokoka , kumkiri Yesu kama bwana .” Wakati hilo linatokea , tunawapapasa mgongoni na kuwaambia , “Sasa wewe ni Mkristo. Mwamini Mungu , jifunze biblia, na kila kitu kitakuwa sawa .” Huu si msisitizo wa Yesu .

Kwa sababu ya hili , tumezalisha watu, wengi wamefanya makubaliano ya kweli na Bwana , bali wameshindwa kukoma kiroho. Wameshindwa kuzaa matunda ya Imani yao kwa sababu hakuna nyenzo za kuwasaidia kufanya hivyo. Badala ya kuwa wanao shuhudia Imani ya Kristo chanya, wanakuwa mashuhuda hasi. Anatamani tutoke na kuwafikia watu kwa njia

ambayo wanakuwa wafuasi wa moja kwa moja wa Yesu na wanaoweza kuendelea kuzaa wafuasi wengine katika Imani .

Kama ukimuongoza mtu mmoja kwa Kristo kila baada ya miezi sita, ukajitenga na kuwafundisha kuwa wafuasi wa Yesu kwa kiasi ambacho wakawa wakristo waliokomaa ambao wanaweza kuendelea kuzaa wengine katika Imani , mwisho wa miezi sita kutakuwa na wakristo wawili tu. Halafu , kama kila mmoja wenu angemuongoza mtu mmoja kwa Kristo, mkajitenga mkawafundisha kuwa wafuasi wa Yesu kwa miezi sita inamaana mwisho wa Mwaka kutakuwa na wakristo wane waliokomaa. Hili haliwezi kufananishwa na mtu anayeweza kuongoza maelfu ya watu kumpokea Kristo kwenye mkutano. Watu wengi husema , "njia hii ya kuwafundisha wafuasi wa Yesu huzaa watu wane tu katika mwaka wa kwanza, wakati hiyo njia nyingine inazaa watu elfu moja . Bora tufanye hiyo njia nyingine." Mtu ambaye anaweza kuwaongoza watu 1000 wamjue Kristo huenda akaweza kuongoza watu 35,000 kwa Bwana . Hilo ni jema , hakuna atakaye weza kukosoa hilo; bali hili ni kama tone katika ndoo ukilinganisha na idadi ya watu duniani. Kimsingi , hivi ndivyo kanisa lkimekuwa likifanya kazi.

Kama tukisisitiza uwanafunzi , Mtu anayemuongoza mtu kwa Kristo katika kila miezi sita na wale wawili walioongozwa wakafanya hivyo, katika miaka 12 na nusu watakuwa wamefanya uinjilisti zaidi ya idadi ya watu duniani .Watu wengine hawaamini kama ndivyo ilivyo bali nakutia changamoto ulifanyie kazi. Nimelifanyia hesabu na katika miaka 12 na zaidi kidogo , mtu mmoja akiwa namfundisha ufuasi wa Yesu mtu mwingine mmoja kila miezi sita , huku wakiwafanya na wenyewe kuendelea kuzaa watu katika mwili wa Kristo , itawezekana kufanya uinjilisti kwa watu Bilion tano na nusu katika miaka 12 na nusu kwa kutumia njia hii.

Kama tunaweza kukufikisha mahali ambapo si tu kwamba utapata uzoefu wa ushindi na kukomaa bali utatamani kutoka nje na kuendelea kuzaa kwa watu wengine, kama utakuwa mfundishaji na si mwanafunzi, mambo yafuatayo yatatokea kama mtu mmoja tu atapata dhana hii na kuishika , akamfuata Bwana hadi kiwango cha kukoma , na kuanza kumfanya mtu mwingine kuwa mwanafunzi wa Yesu. Kama ukifanya hili na mtu mmoja kwa mwaka , Mwisho wa mwaka mmoja , kutakuwa pamoja na yule uliomfundisha watu wawili. Mwisho wa miaka miwili , wangekuwa wanne . Bali , kama utaendelea na kuwafundisha watu na kufuata hili , mwisho wa miaka kumi kutakuwa na watu 1,024 ambao wamefanywa wanafunzi wa Yesu na wao pia wanaendelea kuzaa watu wengine katika mwili wa Kristo. Mkiendelea , na mtu mmoja tu aliyepokea hili, mwisho wa miaka 20 kutakuwa na zaidi ya watu milioni. Hili linashangaza . Hii ni njia ya muongezeko ambayo Bwana aliiunda– kwenda na kuwafanya wanafunzi , si kwenda na kuwafanya walokole. Hii ni njia nzuri ya kupanua ufalme wa Mungu kwa kuwafikia watu , bali nia zetu zisiangalie suluhisho la haraka .

Watu wangapi huenda kwenye mikutano mikubwa , wakajitoa kikamilifu kuwa wakristo, lakini bado wanahasira , uchungu, na wivu, na wanakuwa mashuhuda hasi? Kama tunataka

kuhesabu takwimu , watu wangapi wamegeuzwa kinyume na injili ya kweli kwa sababu tu walimuona mtu akiukiri ukristo na wakadhania, Mimi ni bora zaidi ya hawa wanafiki kanisani . sihitaji ziada.

Kimsingi ni kwamba njia ya kuwafanya watu wanafunzi ndio aliyoiunda Mungu kwa ajili ya kuufikia ulimwengu na injili . Ukweli haukuweki huru endelea katika neno (Yoh 8:31-32). Hili ndilo Mungu analotaka kwa ajili ya kila mtu binafsi ili wapate utele wake, bali ni njia pia ya uinjilisti ambayo ameipanga. Haijalishi ni nani aliamua kwamba hii si njia sahihi aliamua , akafanyia njia mbadala ambayo haijafanikiwa

Naomba leo kwamba Bwana azungumze na Moyo wako kukuonyesha thamani ya uanafunzi wa Yesu. Nakutia moyo kuendelea mbele ili uwe mwanafunzi na anayefanya wengine kuwa wanafunzi wa Yesu.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Inaweza kukushangaza kwamba Yesu hakuwahi kumwita mtu yeyote kuwa “Mkristo,” badala yake wito wake ulikuwa kuwa fanya watu wawe “wanafunzi wa Yesu.” angalia kupitia injili (Mathayo, Marko, Luka, na Yohana), na katika karatasi ya pembeni, tafuta na kuorodhesha maandiko mengi uwezavyo yanayoonyesha wito wa Yesu ulikuwa kuhusu watu kufanywa wanafunzi wake.

2. Katika kitabu cha Matendo , watu hawakukaribishwa wawee “Wakristo,” Badala yake wito wao ulikuwa wafanyike“wanafunzi .” Angalia katika kitabu cha Matendo, na katika karatasi ya pembeni andika orodha ya maanidko yanayoonyesha watu wameitwa kuwa wanafunzi wa Yesu.

3. Katika maandiko , Neno “uwanafunzi wa Yesu” limetumika mara 273 . Katika Biblia Neno “Mkristo limetumika mara tatu , Andika orodha kwenye karatasi ya pembeni Ambapo linatumika.

4. Soma Mathayo 10:25. Mwanafunzi ni nani, Kutegemeana na andiko hili ?

5. Soma Luka 14:26. Hali ya kuwa”Mwanafunzi wa Yesu’ inamaanisha kutoa maisha yako pasipo masharti kwa ajili ya maisha ya mwingine. Kweli au Si kweli.

6. Soma Luka 14:33. Katika hali Fulani , kuwa mwanafunzi wa Yesu kunamaanisha

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Mathayo 10:25

“Yamtosha mwanafunzi kuwa kama mwalimu wake, na mtumwa kuwa kama bwana wake. Ikiwa wamemwita mwenye nyumba Beelzebuli, je! Si zaidi wale walio wa nyumbani mwake?”

### Luka 14:26

“If any man come to me, and hate not his father, and mother, and wife, and children, and brethren, and sisters, yea, and his own life also, he cannot be my disciple.”

### Luke 14:33

“Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, na mama yake, na mke wake, na wanawe, na ndugu zake waume na wake; naam, na hata nafsi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu..”

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

kuacha kila kitu , na kuweka madai ya Yesu juu ya kila kitu . Kweli au Si kweli.

7. Soma Mathayo 19:29. Kila mtu aliyeacha nyumba , ndugu, baba m mama , mke na watoto, au hata ardhi kwa ajili ya Yesu, atapokea zaidi ya hayo mara mia , na piaataurithi uzima wa milelel . Kweli au Si kweli.

8. Soma Matendo 14:22. Wanafunzi wa Yesu wanahitaji kuendelea katika imani . Kweli Si Kweli.

9. Soma Waebrania 10:14. Kipingamizi ambacho watu wengine wanacho katika maandiko yanayo sisitiza kuwa mwanafunzi wa Yesu ni kuwa , kuwa“Mkristo” hakuhitaji kuhangaika kokote (ni kwa neema tu), bali kuwa “Mwanafunzi wa Yesu ” kunahitaji kujitoa kikamilifu. Ukweli ni kwamba kwa ajili ya ukombozi wa Kristo hatuhitaji kutumia nguvu kama sisi ; Kristo amekamilisha na hatuhitaji kutumia nguvu yeyote , bali ni wito wa Kristo kwa ajili ya maisha yetu wakati wote. Kweli Si kweli.

10. Soma Matendo 11:26. Wito wa Kristo haukuwa kwa ajili ya Wakristo (waumini) wa aina mbili aina ya kwanza wabaki mwilini na iana nyingine wafanyike wanafunzi wa Yesu . Katika uhalisi, Wakristo wote ni Wanafunzi wa Yesu na wote wanapaswa wawe sawa . Kweli Si kweli.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Mathayo 19:29

“Na kila mtu aliyeacha nyumba, au ndugu wa kiume au wa kike, au baba, au mama, au watoto, au mashamba, kwa ajili ya jina langu, atapokea mara mia, na kuurithi uzima wa milele”

### Matendo 14:22

“wakifanya imara roho za wanafunzi na kuwaonya wakae katika ile Imani, na ya kwamba imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi.”

### Waebrania 10:14

“Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa.”

### Matendo 11:26

“hata alipokwisha kumwona akamleta Antiokia. Ikawa kwa muda wa mwaka mzima wakakusanyika pamoja na kanisa na kuwafundisha watu wengi. Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia.”

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

11. Soma Mathayo 28:19. Agizo la Yesu ’ kwa waumini yalikuwa ni kwenda na kuwafanya mataifa yote kuwa : A. wanafunzi. B. walokole.

12. Soma Mathayo 28:20. Waumini wanapaswa kuwafundisha wengine kutii kila kitu ambacho Yesu ameagiza. Kweli au Si kweli.

13. Soma Yohana 1:12. Yesu alielezea faida (msamaha, kuhesabiwa haki, n.k.), bali hili haliwezekani pasipo kumfuata alivyo. Kweli au Si kweli.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Mathayo 28:19

“Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu.”

### Mathayo 28:20

“na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari..”

### Yohana 1:12

“Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake; .”

# MWONGOZO WA MAJIBU

1. Inaweza kukushangaza kwamba Yesu hakuwahi kumwita mtu kuwa "Mkristo," badala yake wito wake ulikuwa watu wawe "wanafunzi wake" Angalia katika injili zote (Mathayo, Marko, Luka, na Yohana), na katika karatasi ya pembeni, tafuta na kuorodhesha maandiko mengi iwezekanavyo yanayoonyesha wito wa Yesu' ulikuwa kuwafanye watu kuwa wanafunzi .

2. Katika Kitabu cha Matendo , watu hawajaalikwa kuwa "Wakristo," badala yake wameitwa kuwa "wanafunzi ." angalia katika kitabu cha Matendo, na weka kwenye karatasi ya pembeni , tafuta na kuorodhesha maandiko mengi uwezavyo yanaoonyesha watu wameitiwa kuwa Wanafunzi wa Yesu .

3. Katika maandiko neno "mwanafunzi wa Yesu " limetumika takriban mara 273 . Katika Biblia nzima , Neno "Wakristo" limetumika mara tatu . Orodhesha na kuandika katika karatasi ya pembeni mara hizo tatu ambazo "Wakristo" imetumika kwenye maandiko . Matendo 11:26, Mataendo 26:28, na 1 Petero 4:16.

4. Soma Mathayo 10:25. Uwanafunzi wa Kristo ni nini kiutegemeanana andiko hili? Mwanafunzi ni yule anayekuwa kama mwalimu wake.

5. Soma Luka 14:26. Hali ya kuwa "Mwanafunzi wa Yesu' inamaanisha kutoa maisha yako pasipo masharti kwa ajili ya maisha ya mwingine. Kweli.

6. Soma Luka 14:33. Katika hali Fulani, kuwa mwanafunzi wa Yesu kunamaanisha kuacha kila kitu, na kuweka madai ya Yesu juu ya kila kitu. Kweli.

7. Soma Mathayo 19:29. Kila mtu aliyeacha nyumba, ndungu, baba m mama, mke na watoto, au hata ardhi kwa ajili ya Yesu, atapokea zaidi ya hayo mara mia, na piaataurithi uzima wa milelel. Kweli.

8. Soma Matendo 14:22. Wanafunzi wa Yesu wanahitaji kuendelea katika Imani . Kweli.

9. Soma Waebrania 10:14. Kipingamizi ambacho watu wengine wanacho katika maandiko yanayo sisitiza kuwa mwanafunzi wa Yesu ni kuwa, kuwa "Mkristo" hakuhitaji kuhangaika kokote (ni kwa neema tu), bali kuwa "Mwanafunzi wa Yesu" kunahitaji kujitoa kikamilifu. Ukweli ni kwamba kwa ajili ya ukombozi wa Kristo hatuhitaji kutumia nguvu kama sisi; Kristo amekamilisha na hatuhitaji kutumia nguvu yeyote, bali ni wito wa Kristo kwa ajili ya maisha yetu wakati wote. Kweli.

10. Soma Matendo 11:26. Wito wa Kristo haukuwa kwa ajili ya Wakristo (waumini ) wa aina mbili aina ya kwanza wabaki mwilini na iana nyingine wafanyike wanafunzi wa Yesu.

Katika uhalisi, Wakristo wote ni Wanafunzi wa Yesu na wote wanapaswa wawe sawa . Kweli.

11. Soma Mathayo 28:19. Agizo la Yesu' kwa waumini yalikuwa ni kwenda na kuwafanya mataifa yote kuwa : A. wanafunzi..
12. Soma Mathayo 28:20. Waumini wanapaswa kuwafundisha wengine kutii kila kitu ambacho Yesu ameagiza. Kweli.
13. Soma Yohana 1:12. Yesu alielezea faida (msamaha, kuhesabiwa haki, n.k.), bali hili haliwezekani pasipo kumfuata alivyo. Kweli.

DARAJA 3

# SOMO 15
# JINSI YA KUTUMIA USHUHUDA WAKO

*Na Don Krow*

Leo nataka nionge na wewe kuhusu kuutumia ushuhuda wako binafsi. Matendo 5:42 Inasema, "Na kila siku, ndani ya hekalu na kutoka nyumba hadi nyumba, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo." (Tafsiri ya New American Standard). Tambua kwamba wanafunzi wa kanisa la awali walikutanika hekaluni kila siku, na toka nyumba hadi nyumba, Waliendelea kufundisha na kuhubiri kuhusu Yesu kama Kristo. Watu wengi wanahisi mtazamo wa nyumba kwa nyumba au mlango kwa mlango si wa asili au haufai. Nataka kuwashirikisha mambo machache tuliyojifunza wakati wa kufanya huduma za nje, milango kwa ajili ya wafuasi wa Kristo kuwa wazi, na kuwaona watu wakiwa wameokolewa na kumgeukia Yesu Kristo.

Si ngumu kama ambavyo umeambiwa, na moja ya vitu nilichokigundua katika maandiko ni kwamba Mtume Paul alitumia shuhuda zake binafsi mara tatu wakati anaongea na mtu ambaye alikuwa hajaokoka. Katika matendo 9, 22,na 26, alitoa ushuhuda wake, uzoefu wake , na kilichomtokea alipokuwa akiongea na watu wasioamini. Moja ya njia ambayo ni nzuri tuliiyona ya kuleta injili ya Yesu Kristo kwa watu wengine ni kile tunachokiita "maombi ya kutembea." Tunaenda kwenye mlango na kugonga halafu tunawaambia, "Tuko katika eneo la kwao tunawaombea watu wa eneo hilo. Tunamwamini Mungu ana masikio na anasikia maombi, na kama unashida yeyote katika familia yako –ya kiafya au hata nyingine – na ungependa tuweze kukuombea." Wakati mwingine wanasema "Ndiyo nina shida" na anataka tuombe; wakati mwingine wanakosa raha moyoni na utulivu kwa hiyo wanaamua kusema, "Hapana hatuna maombi yeyote kwa wakati huu." Halafu tunaanza kuwaambia shuhuda zetu binafsi.

Nasema, "Nimegundua una watoto . Ninao watoto watatu. Desemba 14, 1981, Mabinti zangu ambao ni mapacha walizaliwa. Wapili alizaliwa akiwa marehemu." Wanajibu , "Oh, pole sana kwa hayo." Halafu nasema, "hauna haja ya kusikitika. Ngoja nikwambie nini kilitokea." Naanza kutoa hadithi. Kwa pacha wa pili kuzaliwa ili kuwa si jambo la kawaida; ni kwamba

, alizaliwa akiwa mzima kwanza halafu. Oksijeni ilikatika ghafla wakati wa mchakato wa kuzaliwa. Alizaliwa amekufa; ni kwamba alizaliwa amekufa.

Mzalishaji alimchukua, akampiga kofi (akampiga kwa nguvu iwezekanavyo), Akavuta hewa kwenye mapafu yake akifikiria alikuwa na maji kwenye mapafu, alifanya lolote awezalo na mwisho akakata tamaa. Nilikuwa kama baba mwingine yeyote. Nilikuwa nimempoteza binti yangu – ni fanye nini? Wakati huu, nikasema kwa watu waliokuwa wako mlangoni, "Naomba kuwauliza, je ninyi ni wasomaji wazuri wa Biblia?" Wanasema "Ah nimesoma kidogo" au wakati mwingine "Hapana si sana." Naeleza, "Sababu inayonifanya niulize ni kwamba Biblia inasema katika Matendo 10:38 kwamba Yesu aliendа huku na kule akitenda mema, kuwaponya wote waliokuwa wamekandamizwa na ibilisi, kwa kuwa Bwana alikuwa pamoja naye. Ntakwambia nini kilitokea . Unaweza kuamini au kutoamini kutegemeana na unavyoelewa , bali mtoto alikuwa amefariki, na nilikuwa nafikiri kwa siku chache, tutamzika ." nilitafakari mwenyewe, Nilitaka kumkumbatia tu . Nilipoenda kumchukua, kulikuwa na uwepo wa kiovu uliomzunguka, Biblia inaita roho hiyo mapepo. Kimwili roho hiyo ilinivamia na kunifanya nipooze kwa muda mfupi. Ghafla wakati hilo lilipotokea, nikasema, "Kwa Jina la Yesu Kristo, nakuamuru, ewe roho mchafu, kutoka kwa huyu mtoto, na kuamuru uzima juu ya mtoto kwa Jina la Yesu." Mtoto yule mdogo ambaye hakuwahi kupumua, akaweza kupumua mara moja, na akaacha tena kupumua. Nikasema tena, "Katika Jina la Yesu Kristo, ewe roho mchafu, nakuamuru utoke kwa huyu mtoto sasa hivi, na uzima umuingie!" Wakati huu akapumua mara kadha, akapumua na kuendelea kupumua.

Namwita mtu nayeongea naye kwa jina na kusema, "unajua baada ya muda wa dakika tatu, mtu ambaye hana oksigen inayoenda kwenye ubongo huaharibikiwa ubongo. Binti yangu yuko mkamilifu katika kila namna . tunamwita Vita, Ambalo kwa lugha ya ki Latino ina maana "Uzima," kwa sababu tulitaka kutoa ushuhuda kuhusu kile alichokifanya Mungu kwa ajili yake. Alimrejeshea uzima. Toka wakati huo, nimekuwa nikijifunza Biblia sana, na hiki ndicho nilichokigundua: Kama vile tu ile roho ya uovu juu ya mwanangu, kuna ufalme wa giza , mamlaka ya Shetani na utawala wake , na kuna ufalme wa Mungu na Mwanawe mpendwa.

"Wakati Yesu alipokuja Duniani, Alianza kuwaita watu kuingia kwenye ufalme Wake toka kwenye ufalme wa giza kupitia toba na kumuamini – kupokea msamaha wa dhambi na kugeuka kumfuata. Sijui unaamini nini, bali nakwambia nini kilichotokea katika familia yangu. Nataka nikwambie sababu halisi kwa nini tuko mlangoni kwako. Yesu alituambia na tuwafanye watu kuwa wafuasi wake. Nimegundua watu wengi wanashughuli nyingi na hawawezi kwenda kanisani au hawataki. Kama una swali unaweza kuinua mkono wako na kusema, 'Mchungaji (au kuhani), Ulichosema sasa hivi kina maana gani?' Kwa hiyo hii ndiyo sababu inayofanya tuje mlangoni kwako. Kwa dakika kumi tunakuwa na mafundisho yenye mwelekeo toka kwenye Neno la Mungu. Halafu tunaenda kwenye maandiko kuhakikisha wote tumeelewa

maandiko. Ni mazungumzo yanayoendelea mbele na nyuma. Hatukuwa tunawahubiria watu au kuwaeleza Biblia inasema nini bali tunajaribu kuwafanya watu wagundue inasema nini kwa kuuliza maswali machache.

"Je hili limekusisimua? Tutapanga wakati mwingine ukiwa na nafasi, na kuja kwako hapa nyumbani, na kuongea na wewe na kukupa masomo. Kama hujapata kitu toka kwenye masomo ya kwanza kabisa, kama haijasaidia kutia moyo , na kukujenga, hautaona nyuso zetu tena . Hatuko hapa kukusumbua, ili kukufanya ujiunge na kanisa au shirika, au chochote cha aina hii. Tulikuja kukuambia kuhusu Yesu Kristo alichokifanya kwa ajili yako binafsi na kukusaidia ili uelewe neno la Mungu wewe mwenyewe. Kuna mambo mengi katika Biblia hatuvyajui wala kuyaelewa kikamilifu, bali tuko hapa kukupatia mafunzo mafupi. Unaweza kuwa na nia ya swala hili?"watu wengi wanasema "Ndiyo , nina nia" tunatenga muda wa kwenda nyumbani kwao na kuanza masomo haya ya ufuasi wa Yesu . hatupo kwa ajili ya kufanya "uinjilisti wa mikrowevu," kupinda mikono yao , na kuwafanya waombe maombi mafupi wakati hata hawaelewi wanachofanya. Tunafuatailia masomo ya ufuasi wa Yesu na kuwasaidia kumuelewa Kristo na kusulubiwa kwake.

Nilimwambia mchungaji kuhusu mafunzo yetu ya ufuasi halafu akasema, "Don, nini hutokea baada ya masomo ya awali?" Baada ya masomo ya awali, mtu huelewa anachohitaji kufanya ili kuwa na mwitikio kwa Kristo na kupokea rehema na msamaha alioutoa. Sisi si wauzaji wa bidhaa wenye msisimuko na haraka. Huo si mtazamo wetu, bali kwa kupitia somo la kwanza , wafuasi watafikia ufahamu wa kile kinachowapasa kufanya toka moyoni mwao. Halafu akauliza , "nini kinatokea baada ya somo la 15?" nikasema, "Baada ya somo la 15, kama mtu akiendelea kuwa na sisi, watakuwa tayari wametubu dhambi zao na amebatizwa kwa maji mengi na pia kwa Roho Mtakatifu . Tunaona kitu cha aina hii kikitokea, si baada ya somo la 15, bali baada ya somo la 6."

Katika Mathayo 28, Yesu alisema enendeni ulimwenguni na kuwafanya wanafuasi wangu, wakiamini wabatizeni kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Katikati ya kufundisha wafuasi wa Yesu, tunamleta Yesu Kristo na kusulubiwa kwake kwa asiyeamini. Katika kuleta ufahamu huo wiki baada ya wiki, tunajenga mahusiano na wao, Urafiki . Wanatokea kutupenda na kutuamini. Tunawaletea Neno la Mungu, si kuwahubiria .Tunasoma maandiko, Kuwafanya na wao wasome maneno ya Mungu , na kuuliza maswali kwa njia mabayo wanaona majibu toka kwenye Neno la Mungu wao wenyewe. Wiki baada ya wiki , Tunaona watu wanafika kwenye uamuzi wa hiari kumkiri Kristo wazi kwa sababu wamejua ina maana gani kumpokea Krisyo na kumfuata, na kujitoa kwake. Ni tofauti sana na njia nyingi za uinjilisti siku hizi.

Njia tunayotumia mara nyingi kuwafikia waliopotea ni kuwa elezea ushuhuda wetu binafsi kwanza, na kila mmoja wetu ana ushuhuda binafsi. Mara nyingi tunaandika vipeperushi

vyetu wenyewe. Niliandika kimoja kinaitwa "Kifo cha Binti yangu," ambacho huwa naacha kwenye milango ya watu mara nyingi. Watu wengine katika kikundi chetu cha uinjilisti wa wafuasi wa Yesu wameandika vipeperushi kama vile "Mtumwa kuwekwa huru," na Joe Rose, alikuwa amefungwa na pombe na madawa na "Kifo cha mihadarati," na Rocky Forry, Aliyekuwa amefungwa na mihadarati tangu akiwa umri wa miaka 15 na Yesu amemuweka huru. Tunatoa shuhuda hizi milangoni kwa watu.

Watu wengine wanasema, "Bali mimi sina ushuhuda wa nguvu. Sikumuona mtoto wangu akifufuliwa baada ya dakika nane." Nagundua watu wengi hawana aina hii ya shuhuda. Huenda una ushuhuda kama wa Andrew Wommack ambaye nguvu za Mungu ziliyahifathi maisha yake, ambapo, wakati wote wa udogo wake, alikingwa na kutenda dhambi, uchafu, na kuwa na utauwa vitu ambavyo wengi hupambana navyo. Kila mmoja wetu ana ushuhuda, na kama unafikiri ushuhuda wako si wa nguvu sana tumia wa kwangu. Wakati tulipoanza huduma ya timu za uinjilisti wa wafuasi wa Yesu na kuanza kuwafikia watu wengine, Joe Rose alitumia ushuhuda wangu. Baaada ya muda, Alikuwa anautoa hata kwa ubora zaidi ya mimi na mimi ningeweza kusema tu, "Joe, endelea na kusema kile kilichonipata."

Kama mtume Paulo alitumia ushuhuda wake binafsi mara tatu katika Agano Jipya katika kuwafikia waliyo potea, unaweza kufanya hivyo pia. Tunazo Kompyuta leo zenye programu za aina mbalimbali: Word Perfect, Microsoft Word, au yeyote ile. Ni rahisi kutengeneza kipeperushi cha ushuhuda wako binafsi. Ni sawa zaidi kusema, "Hiki siyo kitu nime nunua kwenye duka la kuuza Biblia. Ni kilichonitokea na ndicho ninacho washirikisha

Ningependa ukae chini na kuanza kuandika ushuhuda wako binafsi– nini kilichokutokea – jinsi ulivyompokea Yesu Kristo. Halafu toa ushuhuda wako kwa mtu mwengine kama vile una uwasilisha mlangoni kwa mtu fulani.

Kama unahitaji taarifa zaidi kuhusu somo hili, nenda katika tovuti yangu: www.krowtracts.com na uangalie taarifa katika "Vidokezo Kuhusu Kushirikisha Wengine Imani Yako." Andika ushuhuda wako binafsi, fanyia mazoezi jinsi ya kuuwasilisha na jifunze "Vidokezo Kuhusu Kushirikisha Wengine Imani Yako." Ni muhimu ujifunze – usisome tu – unapoenda na kufanya unjilisti kwa mataifa, Mtu mmoja kwa wakati . Mungu Akubariki.

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

1. Soma Marko 16:15. Injili inatakiwa ihubiriwe kwa nani? ___________________
_________________________________________
____________________

2. Soma Matthayo 28:19-20. Nani anatakiwa kufanywa kuwa Mfuasi wa Yesu? _________
_________________________________________
_____________________________

3. Soma Matendo 8:5, 26, 16:13-15, 23, 20:20-21. Uinjilisti ulifanyika wapi? __________
_________________________________________
___________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Marko 16:15

"Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe."

### Matthayo 28:19-20

"[19] Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; [20] na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."

### Matendo 8:5, 26

"[5] Filipo akatelemka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo [26] Malaika wa Bwana akasema na Filipo, akamwambia, Ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza; nayo ni jangwa."

### Matendo 16:13-15, 23

"[13] Hata siku ya sabato tukatoka nje ya lango, tukaenda kando ya mto, ambapo tukadhani ya kuwa pana mahali pa kusali; tukaketi, tukasema na wanawake waliokutana pale. [14] Mwanamke mmoja, jina lake Lidia, mwenye kuuza rangi ya zambarau, mwenyeji wa Thiatira, mcha Mungu, akatusikiliza, ambaye moyo wake ulifunguliwa na Bwana, ayatunze maneno yaliyonenwa na Paulo. [15] Hata alipokwisha kubatizwa, yeye na nyumba yake, akatusihi, akisema, Kama mmeniona kuwa mwaminifu kwa Bwana, ingieni nyumbani mwangu mkakae. Akatushurutisha. [23] Na walipokwisha kuwapiga mapigo mengi, wakawatupa gerezani, wakamwamuru mlinzi wa gereza awalinde sana."

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

4. Soma Marko 4:11-12. Kabla ya kubadilika kabisa hakujafanyika, mtu lazima :

   A. aone

   B. atambue

   C. asikie

   D. aelewe

   E. yote hapo juu

5. Soma Matendo 28:23-24. Wakati Paulo alipoelezea na kushuhudia kuhusu Injili, alifanya hilo kwa muda gani ili kuwashawishi watu kuhusu aliyoyasema Yesu?

   ___________________________________

   ________________________________

6. Soma Matendo 16:14. Wakati mtu hakika anapo mgeukia Kristo, nini kinatakiwa kufunguka?

   ___________________________________

   _________________________________

7. Soma Matendo 2:37. Nini kinatokea wakati moyo wa mtu umefunguka na wana jisikia hatia?

   ___________________________________

   _________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Matendo 20:20-21

[20] Ya kuwa sikujiepusha katika kuwatangazia neno lo lote liwezalo kuwafaa bali naliwafundisha waziwazi, na nyumba kwa nyumba, [21] Nikiwashuhudia Wayahudi na Wayunani wamtubie Mungu, na kumwamini Bwana wetu Yesu Kristo."

### Marko 4:11-12

[11] Akawaambia, Ninyi mmejaliwa kuijua siri ya ufalme wa Mungu, bali kwa wale walio nje yote hufanywa kwa mifano, [12] Ili wakitazama watazame, wasione; Na wakisikia wasikie, wasielewe; Wasije wakaongoka, na kusamehewa."

### Matendo 28:23-24

"[23] Wakiisha kuagana naye siku, wakamjia katika nyumba aliyokaa, watu wengi sana, akawaeleza kwa taratibu na kuushuhudia ufalme wa Mungu, akiwaonya mambo yake Yesu, kwa maneno ya sheria ya Musa na ya manabii, tangu asubuhi hata jioni. [24] Wengine waliamini yale yaliyonenwa, wengine hawakuyaamini."

### Matendo 16:14 –

"Mwanamke mmoja, jina lake Lidia, mwenye kuuza rangi ya zambarau, mwenyeji wa Thiatira, mcha Mungu, akatusikiliza, ambaye moyo wake ulifunguliwa na Bwana, ayatunze maneno yaliyonenwa na Paulo."

### Matendo 2:37

"Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu?"

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

8. Somo Matendo 16:31, 2:38. Mtu anatakiwa kufanya nini?

 ___________________________________

 ___________________________________

9. Somo Matendo 2:42 na Yohana 8:31-32. Na halafu mtu anapaswa afanye nini? _______

 ___________________________________

 ___________________________________

10. Soma Warumi 10:14-15. Kwa mtiririko wa kinyume (katika maandiko haya), mtu anakujaje kwa Kristo?

 ___________________________________

 ___________________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Matendo 16:31

"Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako."

### Matendo 2:38

"Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."

### Matendo 2:42

"Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali."

### Yohana 8:31-32

"[31]Huko nyuma wanafunzi wakamsihi wakisema, Rabi, ule. [32] Akawaambia, Mimi ninacho chakula msichokijua ninyi."

### Warumi 10:14-15

"[14] Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri? [15] Tena wahubirije, wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa, Ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema!"

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Soma Marko 16:15. Injili ilitakiwa ihubiriwe kwa nani ? Kila kiumbe, kila mtu.
2. Soma Mathayo 28:19-20. Nani anatakiwa kufanywa kuwa mfuasi wa Yesu? Watu wa mataifa yote.
3. Soma Matendo 8:5, 26, 16:13-15, 23, 20:20-21. Unjilisti ulifanyika wapi? katika miji , jangwani, pembezoni mwa mito, jela, hadharani, na toka nyumba hadi nyumba .
4. Soma Marko 4:11-12. Kabla ya kubadilika kabisa hakujafanyika, mtu lazima : E. Yote yaliyotajwa hapo juu
5. Soma Matendo 28:23-24. Wakati Paulo alipoelezea na kushuhudia kuhusu Injili, alifanya hilo kwa muda gani ili kuwashawishi watu kuhusu aliyoyasema Yesu? Toka asubuhi hadi jioni, takriban masaa sita hadi nane.
6. Soma Matendo 16:14. Wakati mtu hakika anapo mgeukia Kristo, nini kinatakiwa kufunguka? Moyo, kiini cha utu wa mtu.
7. Soma Matendo 2:37. Nini hutokea wakati moyo wa mtu unapokuwa umefunguka na wanajisikia hatia? Wakiwa na mwitikio sahihi, watauliza, "Ni fanye nini?"
8. Soma Matendo 16:31, 2:38. Na mtu anapaswa afanye nini? Kutubu na kuamini katika Bwana Yesu Kristo, na kubatizwa.
9. Soma Matendo 2:42 and John 8:31-32. Na halafu mtu anapaswa afanye nini? Aendelee katika mafundisho ya mitume. Aendelee kujifunza na kufanyia kazi maneno ya Yesu.
10. Soma Warumi 10:14-15. Katika mtiririko wa kinyume (kwenye maandiko haya), Mtu anakujaje kwa Kristo? Mtu hutumwa. Mtu huhubiriwa, au kutangaziwa. Kwa sababu wanasikia ujumbe wa Kristo, wanaweza kuamini. Kwa sababu wana amini, wana liitia jina la Bwana kwa ajili ya kupata wokovu.

DARAJA 3

# SOMO 16

# KUTUMIA KARAMA ZA KILA MTU ILI KUFANYA WANAFUNZI

*Na Don Krow*

Leo tunataka kuzungumza kuhusu kutumia karama za kila mtu ili kufundishia wafuasi. Zinawezekana kutumika. Tumekuwa tukifanya kazi katika programu hii ya ufuasi kwa miezi mingi kwa mafanikio makubwa, kuona maisha ya watu yamebadilika kwa kuokoka, kujazwa Roho Mtakatifu, na kubatizwa kwa maji. Siku moja nilikuwa naongea na rafiki yangu na nikasema, "Tunapungukiwa na vitu fulani – vina anguka kupitia nyufa." Akasema , "Nilifikiria kila kitu kilikuwa kinaenda vizuri. Una maanisha nini?"

Ninacho enda kushirikiana na wewe ni jinsi ya kuleta kanisa la ndani – pale ambapo watu wanakaa, wakimsikiliza mchungaji, na kuenda nyumbani – ili liwe kanisa la nje ambapo wanafikia zaidi ya kuta nne za jengo la kanisa. Hizi ni takwimu halisi: asilimia 95 ya Wakristo hawajawahi kumuongoza mtu yeyote kumpokea Bwana na asilimia 90 ya uinjilisti inaelekezwa kwa Wakristo. Jengo la kanisa ni sehemu inayofanyiwa injilisti zaidi duniani. Tunafanya uinjilisti katika vyumba vya shule ya Jumapili, na tunafanya uinjilisti katika hekalu. JInis unafanya uinjilisti kwenye jengo, utafikiri kanisa linahitaji kuokoka.

Ni hadi karne ya tatu chini ya Constantine ndipo majengo ya kanisa yalianza kujengwa. Tangu wakati huo, kwa kadri kuwafikia waliyopotea kunavyohusika, kanisa limekuwa ndani na kujificha nyuma ya kuta za jingo. Tunataka kuongelea kuhusu kuwafikia wengine zaidi ya kuta hizo ili kubadili kanisa la ndani kuwa kanisa la nje. Kitarakimu, kuna asilimia 0.5 pekee (chini ya asilimia 1) ya programu zinazofikia zaidi ya kuta nne za majengo yetu. Hii ni kusema kuwa hakuna dhehebu Marekani leo lenye mpango wa kuwafikia waliopotea. Kuwafikia watu na kuwafanya kuwa wafuasi wale waliyo nje ya majengo ya kanisa ni sehemu ya Ukristo unaohitaji kugundulika.

Kupitia mageuzi, Martin Luther alileta mafunuo ya kuhesabiwa haki kupitia imani kwenye kanisa. Miaka ya 1800, uinjilisti kwa watu wengi ulikuja kupitia John Wesley. Bali inaonekana uinjilisti na kuandaa wafuasi wa mtu mmoja mmoja haujagundulika tena tangu

Mitume. Unaweza kusema sijui ni kwa vipi, "Sijui kwa vipi." Kupitia programu hii, Kwa hakika tutakuonyesha ni kwa vipi – ni rahisi sana. Tutakuonyesha jinsi ilivyo rahisi kufanya kazi na watu na kukutana na watu wapya mlangoni kwa kupitia kutumia ushuhuda wako Hili ndilo ninalotaka kulilenga kwa sasa. Hii ni habari njema.

Ni kwa jinsi gani ungelipenda kufanya unachotaka kufanya, si ambacho mtu mwingine anachotaka ufanye, (ambacho hakika hutaki kukifanya) bali haswa kile ambacho unataka kukifanya? Hilo ndilo tunaloliongelea. Ninapo waonyesha watu jinsi uinjilisti na ufuasi unavyofanya kazi, nikisema , "Angalia hiki ndicho tunachokifanya: Tunagusa maisha ya watu. Wanaokolewa, kuzaliwa mara ya pili, wanajazwa na Roho Mtakatifu, na wanabatizwa kwa maji." Watu wanasema, "Hivi ni vyema!" Bali nikisema "Sasa, wangapi wenu wanataka kwenda na mimi," huenda wakawa watu watatu kati ya mia mbili, kwa sababu waliobaki wanaogopa au hawajui jinsi ya kufanya. au, nikisema , "Sasa sahauni kuhusu hili. Usihofu kuhusu hili; hautakiwi kuogopa. Tutaenda nje na kuwa na somo la Biblia na kupanga mafunzo ya kuwafanya wafuasi wa Yesu kwa ajili yenu." Wangapi wangepend a kufundisha? Hapa wengi wangejitokeza – angalau kumi au kumi na mbili – wakisema, "Ndiyo, nataka kufindisha." Lakini isingeenda zaidi ya hapo.

Tunachotaka kukuonyesha ni jinsi kila karama katika mwili wa Kristo inavyoweza kutumika ili kufikia waliopotea, kuwapenda na kuwafanya wafuasi . Inahitaji kila karama na karama hizo zinapatikana kwenye mwili wa Kristo tu, Kanisa. Wengine wenu mnasema, "Napenda kuomba kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, uponyaji, na vitu kama hivyo." Vyema, Kuna wakati katika kufanya kazi ya ufuasi wetu tunapoweza kukukaribisha kwa ajili tu ya kusudi hili. Watu wengine husema, "mimi sina utulivu na hili," bali je waweza kuoka pai? Waweza kutuma kadi? Waweza kupiga simu ? Je waweza kupaka rangi uzio? Je waweza kumlea mtoto wa mama asiye na ndoa tuliye mshuhudia ili aweze kupata hata muda wa lisaa akafanya shughuli zake nyingine? Je waweza kufanya mambo ya kiuhalisia? Vipi kuhusu maombezi? Wengine wenu mmeitwa kuwa wanamaombezi, kuomba. Tutakuonyesha watu tunaowashuhudia, na kukupa majina yao , kwahiyo unaweza kuwa unawaombea na kuwafanyia maombezi, peke yako au katika makundi, kwa ajili yao na kwa ajili ya timu za Kuwafanya wengine kuwa wanafunzi w Yesu na Uinjilisti tunazoenda nazo nje kila wiki.

Kuna fursa ya kila mtu kuwafikia wengine, na kuwafanya wanafunzi wao. Tuna programu ambapo kila karama inaweza kutumika. Tunaunda timu za waalimu na wasaidizi wa walimu ambao wanaenda kufanya huduma ya kufundisha wafuasi. Watu wawili toka kwenye huduma ya usaidizi hufuatana nao ili kufanya shughuli mbali mbali, mfano kugawa chakula, kuoka pai, au kupiga simu ili kujua nini kuendelea. Tuna watu ambao wanaendelea na maombezi kwa ajili yetu na wale tunaowahudumia .

Je unafahamu unachoona? Tunamuona Mungu akibadilisha maisha ya watu kwa sababu wanachungwa na kujaliwa, kwa sababu upendo Wake unaonyeshwa kwao. Je unajua nani anafanya kazi ya huduma? Inafanyika na wale wanaopaswa kufanya hivyo – watu. Waefeso 4:11 inasema mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji, na waalimu wamepewa kuwakamilisha watakatifu ili waweze kufanya kazi ya huduma. Kanisa inafanya kazi ya huduma, siyo tu mtu asimamaye mbele anayeitwa "Mchungaji." Wakati mchungaji anafundisha na kuimarisha kanisa kwa ajili ya huduma na wanaenda na kufanya, haya ni mafanikio ya kweli.

Ngoja nielezee mfano. Kama tukitangaza vita dhidi ya taifa jegine na raisi wetu akasema, "tunawapoteza watu wengi kwenye vita, nimeamua kuachana na askari wa jeshi na kutuma majenerali tu vitani." Dunia nzima itatucheka, na hakika hilo ndilo linalofanyika. Shetani anatucheka kwa sababu tumetuma majenerali, zile huduma tano, wafanye kila kitu. "Acha wafanye – tunawalipa ili wafanye hiyo kazi." Tumeshindwa kuunda jeshi. Mungu anataka kuunda jeshi hilo, na kila karama inaweza kutumika katika uinjilisti na mafunzo ya uanafunzi.

Tunahitaji kusaidia kuunda jeshi, liloimarishwa na nyenzo za nguvu za kufundishia wanafunzi – si tu hapa katika mji wetu – bali kufikia ulimwenguni kote. Hili linaweza kufanyika kupitia nyenzo tulizoounda, mafunzo ya ufuasi na mikakati yote Mungu aliyotupatia.

Mungu akubariki wakati kila mtu anapokusanyika kutumia karama ili kuhudumu kwa walio potea, waumini wapya, na kushika alichosema Yesu' Enendeni ulimwenguni na kuwafanya watu wanafunzi wangu.

Maswali ya Uanafunzi wa Yesu

1. Yanayofuata ni maelezo mafupi kwa njia ambazo tuna andaa timu pamoja kwa ajili ya kufanya uinjilisti, kufundisha Ufuasi, na kuwafikia walio potea. Bodi ya kanisa lenu inaweza kujiunga kwenye timu yoyote katika timu hizi. Mkiendelea na ufuatiliaji, kwa kutumia karama zote katika kuhududmu, mnaweza kumleta mtu kwenye ufalme na lakini pia anaweza kukomaa haraka. Kifuatacho ni kidadisi ambacho unatakiwa kuwapa washirika wa kanisani kwako. Halafu andaa timu kwa ajili ya ufuatiliaji

   Hiki ndicho nina penda kukifanya: (weka alama ya pata kwenye eneo husika)
   _____ Kuwasiliana na watu wapya milangoni kwao.
   _____ Kuwafundisha wafuasi masomo
   _____Maombezi: Kuwaombea waliopotea na timu za kuwafanya watu kuwa wafuasi na timu za Uinjilisti.
   _____ Kugawa chakula au vitu vyengine kwenye familia zenye uhitaji.
   _____ Kuwasiliana na wengine kwa simu au kuwatembelea.
   _____ Unjilisti wa ukarimu: Kuwapikia chakula wengine, kutuma kadi, kusaidia kwa njia yeyote unayoweza.
   _____ Kufanya kazi na wamama wasiyo na waume na wenye watoto.
   _____ Kutoa usafiri wa kwenda kanisani, n.k.
   _____ Mengine: Ninataka ku_______________________________________________

2. Inayofuata ni mfano wa fomu ya ufuatiliaji ya wafuasi wa Yesu ambayo inatakiwa itumike baada mafunzo ya ufuasi wa Yesu. Fomu hii itamuonyesha Mchungaji au aliye kwenye mamlaka ni masomo mangapi yamefundishwa na matokeo yake kwenye kila masomo.

## FOMU YA KUFUATILIA MATOKEO YA WAFUASI WALIOPATA MAFUNZO

Tarehe ya kutembelea/Somo : _______________________________________

Mtu(watu) aliyefundisha Somo: _______________________________________

Jina (Ma) la aliyetembelewa na kufundishwa :______________________________

Sehemu uwezeshaji ulipofanyika:_______________________________________

Mada ya Somo: _______________________________________________

Mafunzo haya yalikuwaje? ____________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

3. Soma Yakob 1:22. Kama tutasikia Neno la Mungu na tusilifanyie kazi, tutakuwa tumefanya nini? ______________________________

4. Soma Mathayo 7:24-27. Ili uwe mwenye hakima, lazima tusiishie tu kusikia misemo ya Yesu, bali tufanye nini? ______________________________

5. Soma Waefeso 4:11-12. Nani anapaswa afanye kazi ya huduma? ______________________________

6. Soma Matendo 8: 1, 4. Nani alikwenda kila mahali akihubiri Neno? ______________________________

7. Soma Matendo 8:1, 4. Nani hakwenda kila mahali kuhubiri Neno? ______________________________

8. Soma Matendo 11:19 katika kanisa la mwanzo kwenye Agano Jipya, waumini walifanya kazi ya huduma, na ikafuatiwa uongozi wa kitume na maagizo. Katika makanisa yetu leo, ni uongozi ndiyo unaoanza vitu halafu waumini wanafuata. Matendo 11:19-22 inathibitisha tamko hili vipi? ______________________________

9. Soma 1 Wakoritho 12:14-18. Kila kiungo cha mwili wa Kristo ni cha muhimu. Tusifananishane sisi kati yetu. Bali, tujitoe kikamilifu kwa Kristo si kufanya kila kitu bali kufanya kile ambacho Mungu alicho kuwezesha kukifanya. Utafanya nini na taarifa ulizopokea kwenye masomo haya? ______________________________

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Yakobo 1:22

"Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu."

### Mathayo 7:24-27

"[24] Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba;[25] Mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba. [26] Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga; [27] Mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa."

### Waefeso 4:11-12

[11] Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; [12] Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe."

### Matendo 8:1, 4

"[1] Siku ile kukatukia adha kuu ya kanisa lililokuwa katika Yerusalemu; wote wakatawanyika katika nchi ya Uyahudi na Samaria, isipokuwa hao mitume.[2] Watu watauwa wakamzika Stefano, wakamfanyia maombolezo makuu.[3] Sauli akaliharibu kanisa, akiingia kila nyumba, na kuwaburuta wanaume na wanawake na kuwatupa gerezani.[4] Lakini wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri neno.

### Matendo 11:19-22

[19] Basi wale waliotawanyika kwa sababu ya ile dhiki iliyotukia kwa habari ya Stefano, wakasafiri hata Foinike na Kipro na Antiokia, wasililihubiri lile neno ila kwa Wayahudi peke yao. [20] Lakini baadhi ya hao walikuwa watu wa Kipro na Kirene, nao walipofika Antiokia wakasema na Wayahudi wa Kiyunani, wakihubiri habari njema za Bwana Yesu. [21] Mkono wa Bwana ukawa pamoja nao, watu wengi wakaamini, wakamwelekea Bwana. [22] Habari hizo za watu hao zikafika masikioni mwa kanisa lililokuwako katika Yerusalemu; wakamtuma Barnaba, aende hata Antiokia."

### 1 Wakorintho 12:14-18

"[14] Kwa maana mwili si kiungo kimoja, bali ni vingi. [15] Mguu ukisema, Kwa kuwa mimi si mkono, mimi si wa mwili; je! Si wa mwili kwa sababu hiyo? [16] Na sikio likisema, Kwa kuwa mimi si jicho, mimi si la mwili; je! Si la mwili kwa sababu hiyo? [17] Kama mwili wote ukiwa jicho, ku wapi kusikia? Kama wote ni sikio ku wapi kunusa? [18] Bali Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Yanayofuata ni maelezo mafupi kwa njia ambazo tunaanda timu pamoja kwa ajili ya kufanya uinjilisti, Kufundisha Ufuasi, na kuwafikia waliopotea. Bodi ya kanisa lenu inaweza kujiunga kwenye timu yeyote kati ya hizi. Mkiendelea na ufuatiliji, kwa kutumia karama zote katika kuhudumu, mnaweza kumleta mtu kwenye ufalme na kukomaa kwake haraka. Kifutacho ni kidadisi unachotakiwa kuwapa washirika wa kanisani lako. Halafu andaa timu kwa ajili ya ufuatiliaji.

   Hiki ndicho ninachopenda kukifanya: (Weka alama ya pata kwenye kitu kimoja au zaidi).
   Hiki ndicho nina penda kukifanya: (weka alama ya pata kwenye eneo husika)

   ____ Kuwasiliana na watu wapya milangoni kwao.

____ Kuwafundisha wafuasi masomo
____ Maombezi: Kuwaombea waliopotea na timu za kuwafanya watu kuwa wafuasi na timu za Uinjilisti.
____ Kugawa chakula au vitu vyengine kwenye familia zenye uhitaji.
____ Kuwasiliana na wengine kwa simu au kuwatembelea.
____ Unjilisti wa ukarimu: Kuwapikia chakula wengine, kutuma kadi, kusaidia kwa njia yeyote unayoweza.
____ Kufanya kazi na wamama wasiyo na waume na wenye watoto.
____ Kutoa usafiri wa kwenda kanisani, n.k.
____ Mengine: Ninataka ku ____________________________________________

2. Inayofuata ni mfano wa fomu ya ufuatiliaji ya wafuasi wa Yesu ambayo inatakiwa itumike baada mafunzo ya ufuasi wa Yesu. Fomu hii itamuonyesha Mchungaji au aliye kwenye mamlaka ni masomo mangapi yamefundishwa na matokeo yake kwenye kila masomo.

## FOMU YA KUFUATILIA MATOKEO YA WAFUASI WALIOPATA MAFUNZO

Tarehe ya kutembelea/Somo: ____________________________________________
Mtu (watu) aliyefundisha Somo: ____________________________________________
Jina(Ma) la aliyetembelewa na kufundishwa: ________________________________
Sehemu uwezeshaji ulipofanyika: ____________________________________________
Mada ya Somo: ____________________________________________
Mafunzo haya yalikuwaje? ____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________
____________________________________________

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

3. Soma Yakobo 1:22. Kama tutasikia Neno la Mungu na tusilifanyie kazi, tutakuwa tumefanya nini? Tumejidanganya wenyewe.

4. Soma Mathayo 7:24-27. Ili kuwa mtu mwenye hekima, , lazima tusiishie tu kusikia misemo ya Yesu, bali tufanye nini? Lazima tuyafanye.

5. Soma Waefeso 4:11-12. Nani anatakiwa afanye kazi ya huduma ? Wateule, na si daraja fulani la watu ambao ni watenda kazi ya kanisa .

6. Soma Matendo 8: 1, 4.Nani alienda kila mahali akihubiri Neno ? Waumini waliotawanyika kila mahali.

7. Soma Matendo 8:1, 4. Nani hakwenda kila mahali kuhubiri Neno? Mitume. Tunaona toka kwenye haya maandiko kwamba kanisa la kwanza la Agano Jipya walikuwa ndiyo waliokuwa na jukumu la kufanya uinjilisti na ufuasi wa Yesu

8. Soma Matendo 11:19-22. katika kanisa la mwanzo kwenye Agano Jipya, waumini walifanya kazi ya huduma, na ikafuatiwa uongozi wa kitume na maagizo . Katika makanisa yetu leo, ni uongozi ndiyo unaoanza vitu halafu waumini wanafuata. Matendo 11:19-22 inathibitisha tamko hili vipi. Matendo 11:19-22 inathibitisha tamko hili vipi? Kanisa lilisikia majadiliano ya waumini wapya na wakamtuma Barnabas aende akawasaidie (mstari 22).

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

### Yakobo 1:22

“Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu.”

### Mathayo 7:24-27

“[24] Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba; [25] Mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba. [26] Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga; [27] Mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa.”

### Waefeso 4:11-12

[11] Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; [12] Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe.”

### Matendo 8:1, 4

“[1] Siku ile kukatukia adha kuu ya kanisa lililokuwa katika Yerusalemu; wote wakatawanyika katika nchi ya Uyahudi na Samaria, isipokuwa hao mitume.[2] Watu watauwa wakamzika Stefano, wakamfanyia maombolezo makuu. [3] Sauli akaliharibu kanisa, akiingia kila nyumba, na kuwaburuta wanaume na wanawake na kuwatupa gerezani. [4] Lakini wale

## MASWALI KUHUSU UANAFUNZI WA YESU

9. Soma 1 Wakorintho 12:14-18. Kila kiungo cha mwili wa Kristo ni cha muhimu. Tusifananishane sisi kati yetu. Bali, tujitoe kikamilifu kwa Kristo si kufanya kila kitu bali kufanya kile ambacho Mungu alicho kuwezesha kukifanya. Utafanya nini na taarifa ulizopokea kwenye masomo haya? Matumaini, ni kuyaweka katika matendo kwa kutoka nje na kutumia karama yangu ili kuwasaidia wengine.

## MAANDIKO YA KUTUMIA KUJIBIA MASWALI

waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri neno.

### Matendo 11:19-22

[19] Basi wale waliotawanyika kwa sababu ya ile dhiki iliyotukia kwa habari ya Stefano, wakasafiri hata Foinike na Kipro na Antiokia, wasilihubiri lile neno ila kwa Wayahudi peke yao. [20] Lakini baadhi ya hao walikuwa watu wa Kipro na Kirene, nao walipofika Antiokia wakasema na Wayahudi wa Kiyunani, wakihubiri habari njema za Bwana Yesu. [21] Mkono wa Bwana ukawa pamoja nao, watu wengi wakaamini, wakamwelekea Bwana. [22] Habari hizo za watu hao zikafika masikioni mwa kanisa lililokuwako katika Yerusalemu; wakamtuma Barnaba, aende hata Antiokia."

### 1 Wakorintho 12:14-18

"[14] Kwa maana mwili si kiungo kimoja, bali ni vingi. [15] Mguu ukisema, Kwa kuwa mimi si mkono, mimi si wa mwili; je! Si wa mwili kwa sababu hiyo? [16] Na sikio likisema, Kwa kuwa mimi si jicho, mimi si la mwili; je! Si la mwili kwa sababu hiyo? [17] Kama mwili wote ukiwa jicho, ku wapi kusikia? Kama wote ni sikio ku wapi kunusa? [18] Bali Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka."

## MWONGOZO WA MAJIBU

1. Yanayofuata ni maelezo mafupi kwa njia ambazo tunaanda timu pamoja kwa ajili ya kufanya uinjilisti, Kufundisha Ufuasi, na kuwafikia waliopotea. Bodi ya kanisa lenu inaweza kujiunga kwenye timu yeyote kati ya hizi. Mkiendelea na ufuatiliji, kwa kutumia karama zote katika kuhudumu, mnaweza kumleta mtu kwenye ufalme na kukomaa kwake haraka. Kifutacho ni kidadisi unachotakiwa kuwapa washirika wa kanisani lako. Halafu andaa timu kwa ajili ya ufuatiliaji.

## HIKI NDICHO NINACHOPENDA KUKIFANYA: (WEKA ALAMA YA PATA KWENYE KITU KIMOJA AU ZAIDI)

Hiki ndicho nina penda kukifanya: (weka alama ya pata kwenye eneo husika)

____ Kuwasiliana na watu wapya milangoni kwao.
____ Kuwafundisha wafuasi masomo
____ Maombezi: Kuwaombea waliopotea na timu za kuwafanya watu kuwa wafuasi na timu za Uinjilisti.
____ Kugawa chakula au vitu vyengine kwenye familia zenye uhitaji.
____ Kuwasiliana na wengine kwa simu au kuwatembelea.
____ Unjilisti wa ukarimu: Kuwapikia chakula wengine, kutuma kadi, kusaidia kwa njia yeyote unayoweza.
____ Kufanya kazi na wamama wasiyo na waume na wenye watoto.
____ Kutoa usafiri wa kwenda kanisani, n.k.
____ Mengine: Ninataka ku ____________________

2. Inayofuata ni mfano wa fomu ya ufuatiliaji ya wafuasi wa Yesu ambayo inatakiwa itumike baada mafunzo ya ufuasi wa Yesu. Fomu hii itamuonyesha Mchungaji au aliye kwenye mamlaka ni masomo mangapi yamefundishwa na matokeo yake kwenye kila masomo.

   Fomu ya Kufuatilia Matokeo ya Wafuasi Waliopata Mafunzo
   Tarehe ya kutembelea/Somo: ____________________
   Mtu (watu) aliyefundisha Somo: ____________________
   Jina(Ma) la aliyetembelewa na kufundishwa: ____________________
   Sehemu uwezeshaji ulipofanyika: ____________________
   Mada ya Somo: ____________________
   Mafunzo haya yalikuwaje? ____________________
   ____________________
   ____________________
   ____________________

3. Soma Yakobo 1:22. Kama tutasikia Neno la Mungu na tusilifanyie kazi, tutakuwa tumefanya nini? Tumejidanganya wenyewe.

4. Soma Mathayo 7:24-27. Ili kuwa mtu mwenye hekima, , lazima tusiishie tu kusikia misemo ya Yesu, bali tufanye nini? Lazima tuyafanye.

5. Soma Waefeso 4:11-12. Nani anatakiwa afanye kazi ya huduma ? Wateule, na si daraja fulani la watu ambao ni watenda kazi ya kanisa .

6. Soma Matendo 8: 1, 4.Nani alienda kila mahali akihubiri Neno ? Waumini waliotawanyika kila mahali.

7. Soma Matendo 8:1, 4. Nani hakwenda kila mahali kuhubiri Neno? Mitume. Tunaona toka kwenye haya maandiko kwamba kanisa la kwanza la Agano Jipya walikuwa ndiyo waliokuwa na jukumu la kufanya uinjilisti na ufuasi wa Yesu

8. Soma Matendo 11:19-22. katika kanisa la mwanzo kwenye Agano Jipya, waumini walifanya kazi ya huduma, na ikafuatiwa uongozi wa kitume na maagizo . Katika makanisa yetu leo, ni uongozi ndiyo unaoanza vitu halafu waumini wanafuata. Matendo 11:19-22 inathibitisha tamko hili vipi. Matendo 11:19-22 inathibitisha tamko hili vipi? Kanisa lilisikia majadiliano ya waumini wapya na wakamtuma Barnabas aende akawasaidie (mstari 22).

9. Soma 1 Wakorintho 12:14-18. Kila kiungo cha mwili wa Kristo ni cha muhimu. Tusifananishane sisi kati yetu. Bali, tujitoe kikamilifu kwa Kristo si kufanya kila kitu bali kufanya kile ambacho Mungu alicho kuwezesha kukifanya. Utafanya nini na taarifa ulizopokea kwenye masomo haya? Matumaini, ni kuyaweka katika matendo kwa kutoka nje na kutumia karama yangu ili kuwasaidia wengine.

# FOMU YA MATOKEO YA UFUATILIAJI WA WAFUASI YA CHUO CHA BIBLIA CHA CHARIS

Tarehe ya kutembelea: ________________________________

Jina la Mkufunzi: ________________________________

Jina(Ma) ya/la watu/mtu wanao hudhuria mufunzo: ________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

Sehemu ambayo mafunzo yanafanyika: ________________________________

Rika ya umri: Watu wazima__________ Kijana ____________ Mtoto ______________

Habari za ndoa: ____ Sina ndoa ____Nina ndoa ____ Talaka ____ Haijulikani

Watoto nyumbani: ________________________________

Kazi: ________________________________

Kanisa Shirikishi: ________________________________

Namba ya Somo: ________________ Mada ya Somo: ___________________

Mafunzo yaliendaje? ________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

(Tumia nyuma ya ukurasa kama itahitajika.)

Miadi iliofanyika kwa ajili ya mafunzo yanayofuata? Ndiyo Hapana
Tarehe ya miadi na Muda ________________________________